Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Thelathini na Nane - Tarehe 4 Agosti, 2003**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:**

Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwa mwaka wa Fedha 2003/2004.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. ABDISALAAM ISSA KHATIBU):**

Hotuba ya Waziri wa Fedha kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

**MHE. NJELU E. M. KASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:**

Taarifa Kamati ya Fedha na Uchumi kuhusu utekelezaji wa Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Wizara ya Fedha katika mwaka uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka 2003/2004.

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 369

**Kuondolewa Vizuizi Barabarani**

**MHE. EDSON M. HALINGA** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imepiga marufuku kuweka vizuizi vyote vinavyohusiana na kuzuia mazao yasitoroshwe bila kulipia ushuru na kuzifanya Halmashauri za Wilaya zisifikie malengo yake ya ukusanyaji wa mapato:-

(a) Je, Serikali itakuwa tayari kufidia upungufu unaotokana na kutoroshwa kwa mazao ya Wilaya hizo?

(b) Je, tangazo hilo halizipunguzii nguvu Halmashauri na kuzifanya sheria za Halmashauri zisiwe na maana?

(c) Je, Serikali itakuwa tayari kuzipatia Halmashauri uwezo wa kuajiri Askari wake watakaosaidia kusimamia Sheria za Halmashauri kiutekelezaji?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Edson Halinga, Mbunge wa Mbozi Mashariki, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Halmashauri zimeelekezwa kuandaa magulio ambapo wakazi wake watakusanyika na kuuza mazao yao na wanunuzi watatakiwa kulipa ushuru wa mazao palepale. Aidha, Halmashauri zimetakiwa kuwaelimisha wananchi umuhimu wa kuuza mazao yao kwenye magulio na kuacha tabia ya kuwauzia wafanyabiashara wakiwa majumbani kwani mazao hayo hununuliwa kwa bei ndogo na wanazinyima Halmashauri zao mapato. Kwa msingi huo, Serikali haioni sababu za kuzifidia Halmashauri. Halmashauri zikijiwekea utaratibu mzuri zinaweza kukusanya ushuru zaidi kuliko wakati wa vizuizi vya barabarani.

(b) Mheshimiwa Spika, sikubaliani na Mheshimiwa Mbunge kuwa tangazo hili linazipunguzia nguvu Halmashauri na kuzifanya sheria za Halmashauri zisiwe na maana. Sheria za Halmashauri za kukusanya ushuru hazijaondolewa. Kinachobadilika ni utaratibu wa kukusanya ushuru huo.

(c) Mheshimiwa Spika, Halmashauri zina watendaji kuanzia ngazi ya Mtaa/Kitongoji ambao wamepewa jukumu la kusimamia makusanyo ya mapato mbalimbali ya Halmashauri. Wafanyabiashara wanaonunua mazao ndani ya Halmashauri wanatakiwa wajisajili na Halmashauri, kupewa leseni na kupangiwa maeneo. Hivyo ni jukumu la Halmashauri kuhakikisha watendaji wake wanawasimamia ipasavyo wakusanyaji kodi na ushuru wa mazao kwenye maeneo husika na wananchi wanaitikia wito wa kuuzia mazao yao kwenye magulio yaliyopangwa na Halmashauri.

Aidha, Halmashauri zinaruhusiwa kutunga sheria ndogo ambazo zinasaidia katika kusimamia utekelezaji wa majukumu yake. Vile vile vyombo vya dola vilivyopo vinatosheleza kusaidia utekelezaji wa majukumu ya Halmashauri kwani Serikali ni moja. Lakini pale Halmashauri inapoona ni lazima kufanya hivyo kwa gharama zake inaweza kuwasiliana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili iweze kuelekezwa utaratibu.

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, naomba niulize maswali ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa hawa wanunuzi binafsi huzunguka vijiji kwa vijiji na kaya kwa kaya, Halmashauri isipoweza kuwazuia haoni kwamba biashara hii italeta matatizo katika maendeleo ya uchumi wa Halmashauri hizo?

(b) Kama anasema kwamba Halmashauri zisiwe na ajira zake kwa sababu Askari wanafanya kazi ya kuzuia kupitisha mazao vijijini, kwenye *main road* ni sawasawa, lakini vijijini iko haja na Halmashauri kuwa na Mgambo watakaowezesha watu wasipitepite ovyo na kuzunguka kununua mazao bila kufuata utaratibu, haoni hilo ni la msingi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la kwanza, ni kweli anavyosema kwamba inawezekana wapo wafanyabiashara wanaozunguka kaya kwa kaya, kijiji kwa kijiji, lakini tunalosisitiza hapa ni kwamba hakuna mahali katika ngazi yoyote ya chini ambapo hakuna uongozi. Katika ngazi ya Kitongoji yupo Mwenyekiti wa Kitongoji na uongozi wake, katika ngazi ya Kijiji yupo Mwenyekiti Mtendaji wa Kijiji. Kwa hiyo, ni vigumu kuona ni jinsi gani Serikali hizi zinaweza kushindwa kubaini kuwepo kwa mfanyabiashara kama kweli dhamira ipo na kama kweli wamenuia kusikiliza na kutekeleza majukumu ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuajiri Askari katika Serikali, nilichosema ni kwamba katika maeneo mengi bado utaratibu wa kutumia vyombo vya dola vilivyopo unaonekana unatosheleza. Lakini kama iko sehemu ambapo wanaona ni vizuri wakawa na ajira kwa ajili ya Askari wake hakuna tatizo.

Kikubwa ni kuwasiliana na Wizara ya Mambo ya Ndani kwa sababu wao ndio wanaweza kuwasaidieni kujua namna gani zoezi hilo linaweza kufanyika na kukamilika.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri katika kujibu swali hili amesema kwamba lazima kuwe na magulio ya kuuzia mazao. Sasa ili kumkamata mtu hataki kupeleka mazao kwenye magulio anataka kutoroka kwenda mahali popote na vizuizi hataki kuviweka, Halmashauri watumie njia gani ili kukamata watu hawa ambao hawataki kupeleka mazao kwenye magulio?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kama kweli vijiji kama Serikali vitaamua kwa dhati kabisa kutekeleza maagizo ya Serikali ya kuwa na sehemu maalum ya kununua mazao na kuuza, suala la namna mfanyabiashara anavyoweza kukwepa Serikali ya kijiji halipo. Lakini kama itatokea jambo hilo limetokea, tunachoweza kusema ni kwamba Mtendaji wa Kijiji au Mtendaji wa Kata awajibike kwa kitu chochote cha aina hiyo kitakachotokea.

Na. 370

**Matukio ya Ujambazi Kwenye Barabara ya Mombo - Soni**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa ujambazi umekuwa kero kubwa kwa wasafiri katika barabara itokayo Mombo hadi Soni hasa kwenye eneo liitwalo Maili Tano:-

(a) Je, ni matukio mangapi ya ujambazi yametokea katika eneo hilo tangu mwaka 1995 hadi 2002?

(b) Je, matukio ya ujambazi ya kuwavua watu nguo na kuwanyang'anya fedha na mali zao nyingi huwa yanatokea nyakati gani?

(c) Je, ni majambazi wangapi wameshakamatwa na kufikishwa mbele za haki na je, Serikali ina mipango gani kuondoa kero hiyo kabisa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, utekaji nyara wa magari ni kero sio tu kwa wananchi wa Jimbo la Bumbuli, bali kwa wananchi wa Mikoa yote. Katika barabara Mambo - Soni, matukio ya ujambazi yaliyotokea kati ya mwaka 1995 hadi 2002 ni matatu.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho lilitokea tukio moja la kuwavua watu nguo na kuwanyang'anya mali zao. Hili lilitokea eneo la Maili Tano saa mbili na nusu usiku tarehe 20 Novemba, 1997.

(c) Mheshimiwa Spika, jumla ya majambazi watano walikamatwa na kufikishwa mbele ya sheria. Serikali inachukua hatua zifuatazo kukabaliana na kero hii ya ujambazi katika barabara zetu:-

Kwanza, askari Polisi kusindikiza magari ya abiria na mizigo yanapokuwa safarini kwenye maeneo yenye mashaka.

Pili, Polisi hufanya doria za mara kwa mara na kushtukiza kwenye sehemu zinazoshukiwa ni maficho ya majambazi, tatu, Polisi kufanya misako ya kuwakamata majambazi na silaha zinazoingizwa na wakimbizi kutoka nchi jirani na nne, kwa sasa Serikali ipo kwenye maandalizi ya utekelezaji wa Mpango

wa Kimataifa wa kudhibiti kuingia, kuenea na kuzagaa kwa silaha ndogo ndogo nchini. Silaha zilizozagaa ni moja ya chanzo kikubwa cha kero ya ujambazi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, tano, Serikali inaandaa mpango wa Polisi jamii wenye lengo la kuweka utaratibu mzuri zaidi na kuwashirikisha wananchi katika ulinzi wa maisha na mali zao.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inatoa wito kwa raia wema wote washirikiane na Jeshi la Polisi katika mapambano haya dhidi ya majambazi.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa matukio haya mengine yamehusisha wanafunzi hasa wa Shule za Kifungilo na Mazinde Juu ambao wanatoka sehemu mbalimbali na mabasi yao huanzia Dar es Salaam na Moshi na huenda mipango ya wizi inapangwa wakati huo, je, Waziri haoni kwamba kuna haja ya kuwaandikia Waraka Wakuu wa Shule hizo ili washirikishe Polisi wakati mabasi hayo yanapokwenda shule?

(b) Kwa kuwa matukio haya yanatokea nyakati za usiku, je, Waziri atakubaliana nami kwamba kuna haja ya kujenga Kituo Kidogo cha Polisi *(Police Post)* ambacho kingetoa ulinzi wakati wa usiku maana ndio wakati hasa wenye matatizo maana eneo hilo limekaa katika mazingira ya mabonde makubwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, fursa na ruhusa ipo kwa Wakuu wa Shule hizi kuomba msaada wa Jeshi la Polisi wakati wowote wanapoona kuna jambo ambalo linawatia mashaka na si Wakuu wa Shule tu kusema kweli ni Wakuu wa maeneo yote nchini wakiona kuna hatari fulani au mazingira ya kutatanisha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa *Police Post* katika eneo hilo, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba haja hiyo ipo na namwomba kama tunavyowaomba siku zote wananchi wa eneo hilo, viongozi pamoja na Mheshimiwa Mbunge waanze kazi hiyo ya kujenga kituo hicho na sisi Wizara ya Mambo ya Ndani, tutafika kuwaunga mkono.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, ninarufahi kupata nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa ujambazi na hasa katika eneo hili limeonekana limekuwa ni jambo la kawaida na kwa kuwa katika nchi suala la ujambazi wananchi wamefikia hatua ya kufikiria kwamba na Polisi nao wanahusika, je, Serikali itachukua hatua gani kuondoa dhana hii ambayo kwa kweli kwa njia moja au nyingine wananchi wamekata tamaa kuhusu ujambazi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kwanza sio sahihi kabisa kusema kwamba wananchi wamekata tamaa na kwamba nchi hii sasa inatawaliwa na majambazi na wananchi hawana lolote la kufanya, hii picha anayoiweka Mheshimiwa Mbunge sio sahihi.

Mheshimiwa Spika, kwa kiasi kikubwa wananchi katika maeneo mbalimbali wanashirikiana vema na Jeshi la Polisi katika kukabiliana na suala la ujambazi. Si jambo la siri kwamba tukijilinganisha na nchi jirani nyingi hali yetu ni nzuri zaidi kwa sababu wananchi wanashiriki kwa ukamilifu katika kusaidiana na Polisi. Pale ambapo wananchi wanahisi kwamba Polisi wanashirikiana na majambazi, tunachoomba kwa kweli tupate taarifa na hatua zitachukuliwa.

Naomba wananchi popote walipo tuimarishe ulinzi wa Sungusungu, tujenge vituo vidogo vya Polisi ili tusogeze huduma za Polisi katika maeneo hayo ili tukamilishe utaratibu wa kushirikisha wananchi katika kupambana na majambazi.

Na. 371

**Umri wa Kustaafu Miaka 60**

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 1999 Bunge lilipitisha Sheria ya Kustaafu kwa Watumishi wa Serikali kuwa miaka 60 badala ya miaka 55; na kwa kuwa watumishi wa JWTZ na Usalama wa Taifa waliokuwa kwenye likizo ya kustaafu kazi waliitwa tena kazini kuendelea na kazi kwa kuzingatia sheria mpya ya kustaafu:-

(a) Je, kwa nini kwa upande wa Jeshi la Polisi sheria hiyo haikutekelezwa kama ilivyofanyika kwa vikosi vingine wakati uzito wa kazi zao unalingana?

(b) Je, kwa nini sheria hiyo kwa upande wa Jeshi la Polisi haikutekelezwa kuanzia kwenye ngazi ya Askari wa kawaida hadi *Inspector* na kutekelezwa kuanzia cheo cha *ASP* hadi *IGP?*

(c) Je, inawezekana vipi uamuzi uliopitishwa na Bunge kutoka kwa mtu au watu kwa Wizara au Idara kubatilisha uamuzi huo na ni kwa kipengele kipi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mbunge wa Chwaka, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sheria mpya ya kustaafu kazi watumishi wa Serikali ilianza kutumika rasmi tarehe 1 Julai, 1999. Kwa mtumishi wa Jeshi la Polisi ambaye kustaafu kwake kulikuwa tarehe 30 Juni, 1999 au kabla ya hapo basi huyo hakuhusika na sheria hii mpya. Kwa watumishi ambao walitakiwa kustaafu au kuanza likizo ya kustaafu kuanzia tarehe 1 Julai, 1999 hawa walihusika na sheria mpya ya kustaafu kazini na walipewa uhuru wa kuchagua ama kusitisha likizo ya kustaafu na kuendelea na kazi au kustaafu kazi.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa mabadiliko haya ya sheria ya umri wa kustaafu kuwa miaka 60 ya mwaka 1999, hayakuhusisha Askari Polisi wa ngazi zote isipokuwa iliwahusisha Askari wa kuanzia cheo cha Mrakibu Msaidizi wa Polisi *(ASP)* kwenda ngazi za juu, hii ni kutokana na utaratibu wa umri wa kustaafu kwa makundi katika Majeshi yote nchini. Utaratibu huu umewekwa kwa sababu ya tofauti ya majukumu. Askari wa ngazi za mwanzo ni kundi la kiutendaji wa kioperesheni *(operational);* Maafisa wa ngazi za juu ni kundi ambalo majukumu yake ni uongozi *(command).* Utaratibu wa umri wa kustaafu kwa makundi upo katika Sheria ya *Public Service Retirement Benefits Act No.2* ya 1999 na kama ilivyorekebishwa katika Sheria Na.9 ya 2000. Katika sheria hiyo, kifungu Na.1 kinafafanua kwamba Askari wa cheo cha *Constable* wa Polisi umri wake wa kustaafu ni miaka 45, Askari wa ngazi ya Koplo - Sajenti umri wa kustaafu ni miaka 50, Askari wa cheo cha Sajini-Taji *(Staff Sergeant)* hadi Wakaguzi umri wa kustaafu ni miaka 55 na Maafisa wa ngazi ya Mrakibu Msaidizi hadi *IGP* umri wa kustaafu miaka 60.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo, ni wazi kwamba utaratibu wa muda wa kustaafu kwa Askari Polisi kwa makundi haukuwekwa na Wizara yangu bali umewekwa kisheria na Bunge lenyewe kwa kuzingatia hali ya utendaji kazi katika mazingira ya Kijeshi.

**MHE. YAHYA KASSIM ISSA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa katika matumizi ya mwanadamu nguvu zinatumika zaidi katika kufikiria au kubuni na kwa kuwa kasema kwamba kuanzia *ASP* au *IGP* ndio ambao walioongezewa muda wa kustaafu, je, haoni kwamba uwezo wao katika utendaji kazi utakuwa mdogo kuweza kumudu kazi ipasavyo?

(b) Kwa kuwa kuna vyombo vya Serikali ambavyo vina kazi nzito zaidi kuliko ile ya Polisi kama JWTZ na kwa kuwa utendaji wao waliweza kutekeleza hata kwa muda wa miaka miwili hadi mitatu, je, haoni kuwa Askari wa Jeshi la Wananchi kutokufanya hivyo ni kuwanyima haki yao?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, katika sehemu ya kwanza, si kweli kwamba Askari wakifika ngazi za juu uwezo wao unakuwa umepungua. Kusema kweli ni kinyume chake kwa sababu Askari mpaka ufike ngazi ya *IGP, Commissioner* au *Assistant Commissioner* maana yake umeanzia huku chini ukapanda kidogo kidogo mpaka ukafikia ngazi hiyo na jinsi unavyopanda ndivyo ambavyo unajikusanyia ujuzi na uzoefu kwa sababu mpaka ufike huko juu unakwenda kozi mbalimbali.

Kwa hiyo, hii ngazi ya juu ni ngazi ambayo watu wamepitia kozi mbalimbali, wana ujuzi na uzoefu na ndio maana tunasema kwamba tuutumie ujuzi na uzoefu wao walioukusanya kwa miaka mingi angalau mpaka kufikia miaka hiyo 60. Hawa wengine wa ngazi ya chini kwa sababu kama nilivyosema kazi zao ni za kiutendaji kuwatuma kwenda kwenye *operational* mbalimbali kama vile kufukuzana na majambazi ni dhahiri huwezi kumpleka mtu wa miaka 60 katika operesheni kama hizo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba sheria hii inayohusika na Askari kustaafu kwa makundi ni kwa Majeshi yote hata Jeshi la Wananchi ambalo amelitolea mfano na lenyewe utaratibu wao ni huu huu. Kwa hiyo, hakuna sheria mbili katika vyombo vyetu vya ulinzi na usalama na utaratibu ni huu huu wanavyotendewa Polisi ndivyo wanavyotendewa Jeshi la Wananchi na Jeshi la Magereza.

Na. 372

**Tatizo la Maji - Mji wa Sikonge**

**MHE. SAID JUMA NKUMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa Mji wa Sikonge hauna chanzo cha maji cha uhakika kwa wakazi wa Mji huo na taasisi zake; na kwa kuwa Mji huo unaendelea kukua bila kuwa na huduma hiyo muhimu:-

(a) Je, ni lini Serikali itaanzisha utaratibu wa kusaidia utatuzi wa tatizo hilo?

(b) Je, Serikali haioni kwamba Mbiu ya Maji ni Uhai kwa wananchi wa Sikonge ambao hawana huduma ya maji inamaanisha kwamba wanachungulia kaburi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA - MHE. DR. FESTUS B. LIMBU (k.n.y. WAZIRI WA MAJI NA MAENDELEO YA MIFUGO)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Nkumba, Mbunge wa Sikonge, kama ifuatavyo:-

(a) Mji wa Sikonge una idadi ya wakazi wapatao 8,155 na mahitaji yao ya maji ni meta za ujazo 611,600 kwa siku. Vyanzo vitumikavyo ni Bwawa la Utyatya na visima vifupi ambavyo vina uwezo wa kutoa maji meta za ujazo 166,300 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, ni kweli wakazi wa mji wa Sikonge wana uhaba wa maji kwa matumizi yao kutokana na kutokuwepo kwa vyanzo vya kutosheleza upatikanaji wa huduma hiyo. Serikali kwa kutambua tatizo hili, ilifanya utafiti wa maji chini ya ardhi kwa ajili ya kuchimba visima virefu eneo la Mwanankola. Mradi huu utahusisha uchimbaji wa visima, ulazaji wa bomba kubwa kutoka kwenye visima hadi kwenye tanki kubwa lililopo Mlimani - Hospitali, kununua pampu 2 na kujenga nyumba 2 za wahudumu wa mashine.

Mheshimiwa Spika, hadi sasa kazi zilizofanyika ni ujenzi wa visima maeneo ya Zahanati mpya na kufunga pampu za mkono. Pia chujio la maji linajengwa katika chanzo cha maji cha Bwawa la Utyatya ambapo mitambo miwili imenunuliwa kupitia mfuko wa *Tanzania Japan Counterpart Fund.*

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutoa mbiu ya Maji ni Uhai ina lengo la kuboresha afya za wananchi wake wakiwemo wakazi wa Sikonge, kwa kuwapatia maji safi, salama na kuwaondolea adha ya

kutafuta maji mwendo mrefu. Kauli mbiu hiyo ni mwamsho wa kichocheo kwa wananchi kuwa na maji ya kutosha yaliyo salama na safi kwa ajili ya afya zao na mifugo yao na hivyo kuboresha maisha yao.

Na. 373

**Uhusiano wa *TANROADS* na Wizara**

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI** aliuliza:-

Kwa kuwa muundo wa usimamizi wa barabara nchini umebadilika sana kiasi kwamba hali ya uwajibikaji *(chain of command)* imevurugika; na kwa kuwa kabla ya hapo kulikuwa na *Regional Engineer* ambaye ni Mshauri Mkuu wa Mkoa na Katibu wa *Road Board;* na kwa kuwa sasa wapo Wakala wa Barabara *(TANROADS)* ambao uhusiano wao na Wizara sio wa moja kwa moja na kwamba *Regional Engineers* wamehamia kwa Wakala wa Barabara na wanawajibika kwa *MD TANROADS* na Bodi ya *TANROADS;* na kwa kuwa fedha za Serikali zikipelekwa Mkoani zinaingia kwa Wakala wa Barabara wa Mkoa ambako hatuna sauti nazo:-

Je, Serikali inaweza kutueleza kwa kina uhusiano uliopo kati ya Wakala wa Barabara *(TANROADS)* na mtandao wa barabara kuanzia ngazi ya Taifa hadi vijiji?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA UJENZI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, Mbunge wa Peramiho, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, kwamba muundo wa usimamizi wa barabara nchini umebadilika kutokana na kuanzishwa kwa Wakala wa Barabara nchini *(TANROADS).* Lakini si kweli hali ya uwajibikaji *(chain of command)* imevurugika. *TANROADS* ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya *Road Tolls (Amendment) No.2* ya mwaka 1998 pamoja na Sheria Na.30 ya *Executive Agencies* ya mwaka 1997 ili kusimamia shughuli za matengenezo ya barabara zilizoko chini ya Mamlaka ya Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Spika, *TANROADS* ilianzishwa rasmi mwezi Julai, 2000 ili kuchukua majukumu yaliyokuwa yakifanywa na Wizara ya Ujenzi ya kutunza na kukarabati barabara kuu na barabara za Mikoa zenye jumla ya kilometa 35,000.

Mheshimiwa Spika, *TANROADS* inaongozwa na Mtendaji Mkuu anayewajibika kwa Katibu Mkuu. Aidha, Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* huteuliwa na Waziri wa Ujenzi. Wapo Mameneja wa Mkoa wa kila Mkoa wa Tanzania Bara ambao wanawajibika kwa Mtendaji Mkuu wa *TANROADS.* Katika kutekeleza kazi za matengenezo ya barabara, *TANROADS* kila mwaka huingia mikataba ya utekelezaji kati yake na Bodi ya Mfuko wa Barabara kwa miradi ya matengenezo ya barabara na Wizara ya Ujenzi kwa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, fedha za Serikali kwa ajili ya matengenezo ya barabara hutokana zaidi na tozo katika ushuru wa mafuta na hutunzwa na Bodi ya Mfuko wa Barabara. Katika mgawanyo wa fedha hizi, *TANROADS* hupewa asilimia 70 na Serikali za Mitaa za Mitaa hupewa asilimia 30 kwa ajili ya matengenezo ya barabara husika.

Mheshimiwa Spika, napenda kumkumbusha Mheshimiwa Mbunge kwamba haya mabadiliko ni kutokana na Sera ya Serikali yetu ya kujiondoa katika usimamizi wa moja kwa moja na kukasimu majukumu hayo kwa taasisi nyingine pamoja na sekta binafsi. Lengo kubwa la mabadiliko haya ni kuboresha na kuleta ufanisi katika utunzaji wa barabara zetu ili ziwe kichocheo cha kukua kwa uchumi wa nchi yetu.

Waheshimiwa Wabunge mtakubaliana na mimi kwamba kutokana na kuanzishwa kwa *TANROADS* na Bodi ya Mfuko wa Barabara, matengenezo ya barabara yanafanyika kwa kiwango cha kuridhisha. Aidha, katika kuhakikisha kwamba kunakuwepo uhusiano na mawasiliano ya kutosha kati ya Wizara na Idara ama Taasisi nyingine za Serikali zilizopo Mikoani, Wizara imemteua mmojawapo wa Wahandisi wake waliopo Mikoani kutoka aidha Wakala wa Majengo, Idara ya Ufundi na Umeme ama *TANROADS* kuwa Mwakilishi wake huko Mikoani.

Hata hivyo, uteuzi huo hauwaondolei majukumu yao waliyokwishapangiwa kulingana na muundo wa Wizara ama taasisi husika bali unawaongezea jukumu la kuratibu shughuli za Wizara huko Mikoani na ndio maana vikao vya *Regional Road Board* vinaendelea kutambulika na *Regional Engineers* wameendelea kuwa Makatibu wa vikao hivyo vilivyo chini ya *Regional Commissioners.*

Baada ya kusema hayo, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba uhusiano wa *TANROADS* na Mikoa husika haujabadilika kwani Mameneja ni wale wale na kazi ni zile zile ila tu wanafanya kazi kulingana na mikataba wanayopewa na Wizara pamoja na *Road Fund Board. TANROADS* inawajibika moja kwa moja kwa Wizara ya Ujenzi.

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali ya nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri.

(a) Bado kuna utata katika uwajibikaji wa yule aliyekuwa *Regional Engineer* siku hizo akiwajibika kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi siku hizi *Regional Engineer* anawajibika kwanza kwa *Managing Director* wa *TANROADS* sijui kama *Managing Director* ndiye anayewajibika kwa Katibu Mkuu yaani wameongeza ngazi hapo.

(a) Mara nyingi kuna ubishi katika ngazi ya chini kati ya *District Engineer* na *Regional Engineer, Regional Engineer* anasema barabara hii ni ya *Regional* hiyo ni ya *District* siku hizi ndio kuna sehemu tatu hiyo ni ya *District,* hiyo ni *Regional* na hii ni *TANROADS* ingawa *TANROADS* ilikuwa ni *Regional Engineer* hakuna uhakika wa vitu hivyo, mara nyingi ni vigumu.

**SPIKA:** Mbona huulizi swali unatoa maelezo tu? Uliza swali. *(Kicheko)*

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Ninauliza swali la nyongeza lini Wizara ya Ujenzi itakuwa na chombo kimoja tu toka juu mpaka chini?

Mheshimiwa Spika, hakuna utata kwa sababu wakati Meneja wa Mkoa anawajibika moja kwa moja kwa Mtendaji Mkuu, huyu Mtendaji Mkuu wa *TANROADS* anawajibika kwa Bodi ya Ushauri ya Wizara *(Ministerial Advisory Board)* ambayo yenyewe ipo chini ya Wizara na Mwenyekiti wake ni Katibu Mkuu wa Ujenzi.

Kwa hiyo, hapa hakuna utata hata kidogo kwa sababu kadri itakavyokuwa lazima Katibu Mkuu wa Wizara anatoa maelekezo moja kwa moja kwa *TANROADS* ambayo ndiyo inammiliki yule Meneja wa Mkoa. Lakini bado pale tunaye *Engineer* kutoka kwenye umeme au kutoka kwenye ujenzi ambaye yeye ndiye anakuwa mwakilishi wa shughuli hizi za barabara kati ya Wizara na Mkoa unaohusika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la kwamba kuna utata kati ya barabara za Mikoa, Wilaya na Manispaa. Huu utata haupo, kwa sababu kwa mujibu wa taratibu zetu za barabara tumezigawa hizi barabara. Zipo barabara kuu na zile za Mikoa ambazo tunajua urefu wake ni kilomita 35,000. Zipo barabara za Wilaya na zile *feeder roads* ambazo tunajua urefu wake ni kilometa 47,550. Lakini zipo barabara za Manispaa na Miji ambazo tunajua urefu wake ni kilomita 2,450. Kwa hiyo, kila daraja lina barabara zake na urefu wake na wanazifahamu, kwa hiyo hakuna utata. *(Makofi)*

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa fedha zinazotengwa kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Vijijini yaani fedha ambazo zinapewa Serikali za Mitaa kutokana na mfuko wa barabara ni 30% na Wizara inabaki na asilimia 70.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana nami kwamba ipo haja ya kuongeza fedha angalau asilimia arobaini ili tuweze kutengeneza barabara zetu Vijijini?

Pili, kwa kuwa Wahandisi wa Ujenzi hawamo .....

**MBUNGE FULANI:** Swali moja tu.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Ahaa, Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Wahandisi......

**SPIKA:** Hapana, unakumbuka Kanuni inasema kwamba kama wewe huna swali la msingi unauliza swali moja tu la nyongeza siyo mawili.

Mheshimiwa Naibu Waziri lijibiwe hilo la kwanza.

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA UJENZI):** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniokoa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, uamuzi wa Wizara ya Ujenzi kupewa asilimia 70 na Halmashauri zetu kupewa asilimia 30, umetokana na nia yetu ya kuhakikisha kwamba barabara kuu na zinazounganisha Mkoa hadi Mkoa zinajengwa. Tukimaliza hapo tutatilia nguvu zetu sasa katika barabara za Wilaya, Miji na zile *Feeder Roads* za Vijijini. Kwa hiyo, huu ni uamuzi wetu wenyewe kwamba itakapofikia mwaka 2005 angalau kila Mkoa uwe unaunganishwa na Mkoa mwingine. Kwa hiyo, tukimaliza kazi hiyo tutapunguza huku tuongeze upande mwingine. *(Makofi)*

Na. 374

**Ujenzi wa Barabara ya Dar es Salaam - Kibiti**

**MHE. BAKARI M. MBONDE** aliuliza:-

Kwa kuwa ujenzi wa barabara kati ya Dar es Salaam na Kibiti, unaenda pole pole sana:-

(a) Je, ni sababu zipi za msingi zinazosababisha kasi ndogo ya ujenzi wa barabara hiyo?

(b) Je, ni miujiza gani Serikali itatumia kuhakikisha kuwa, ujenzi wa barabara hiyo unakamilika kabla ya mwaka 2005 kama ambavyo Serikali imeahidi?

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA UJENZI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Mbonde, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa napenda kukiri kuwa ni kweli kwamba kasi ya ujenzi wa barabara hii ilikuwa ni ndogo kwa kipindi kilichopita. Ucheleweshaji huu umesababishwa na kutopatikana fedha ya kutosha kwa ajili ya mradi huu. Wakati Serikali ilipokuwa ikisubiri hatua za kupata fedha toka kwa wafadhili kati ya mwezi Januari, 2001 na Desemba, 2002, Serikali kwa kutumia fedha za ndani iliweza kukarabati jumla ya kilomita 22 kati ya kilomita 79 zilizokuwa zimebaki kati ya Kitonga na Kibiti.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa zimebaki kilometa 57 kati ya Kimanzichana na Kibiti ambazo zilianza kujengwa kuanzia mwezi huu wa Julai, 2003 baada ya mfadhili *(Kuwait Fund)* kutoa mkopo mwezi Machi, 2003. Kazi hii ambayo inakadiriwa kuchukua muda wa miezi 20 inatarajiwa kukamilika mwezi Februari, 2005. Mradi huu utagharamiwa kwa pamoja chini ya ufadhili wa *Kuwait Fund* na *OPEC Fund* pamoja na mchango wa Serikali ya Tanzania. Kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 9.5 kutoka

katika mikopo ya *Kuwait Fund* na *OPEC Fund* zitaelekezwa katika ukarabati wa sehemu ya Kimanzichana hadi Kibiti yenye urefu wa kilometa 57.

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza tunaipongeza Serikali kwa kutekeleza ahadi zake kwamba barabara kati ya Kimanzichana na Kibiti itajengwa na hivi karibuni juzi tu tumefungua daraja la Mkapa pale Rufiji na tuna uhakika kwamba barabara kuanzia Somanga hadi Lindi-Mingoyo sasa wakandarasi wapo kwenye *site* na tuna imani kwamba barabara hii itaisha.

Je, sehemu pekee iliyobakia ya barabara kati ya Nyamwage kupitia Vijiji vya Chumbi, Muhoro, Kiwanga katika Wilaya ya Rufiji hadi Somanga itaanza lini ili tuweze kuwasiliana kwa karibu zaidi na watoto wetu Wamakonde na Wamakuwa? *(Makofi)*

Pili, barabara ya Kibiti kupitia Utete hadi Nyamwage ni kiungo muhimu kati ya Makao Makuu ya Wilaya ya Utete na hii barabara kubwa ya Dar es Salaam-Kibiti-Lindi na kwa kuwa Waziri alikubali na akatoa fedha kwa ajili ya kujenga sehemu ya Nyamwage hadi Utete tunamshukuru. Je, mgogoro uliopo kati ya Serikali na Kandarasi Piru kwa kipande cha barabara kuanzia Kibiti hadi Utete utaisha lini ili nayo barabara hii iweze kuimarishwa? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KAZI, MAENDELEO YA VIJANA NA MICHEZO (k.n.y. WAZIRI WA UJENZI):** Mheshimiwa Spika, kwanza napenda kupokea shukrani zake kwa Serikali juu ya jitihada kubwa zinazoonyeshwa katika kukamilisha barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipande cha barabara kati ya Nyamwage, Chumbi, Muhoro, Kimanga, Malendegu mpaka Somanga ili Mheshimiwa Bakari Mbonde, aweze kuwasiliana vizuri na baba zake Wamwera na Wamakonde, kipande hiki Serikali sasa hivi inaendelea kufanya mashauriano na Mfuko wa Kuwait na pindi mambo yakikamilika tunatarajia barabara hii itaanza.

Mheshimiwa Spika, lakini kama tulivyosema wakati tunasubiri mikopo hatukai tu tunahakikisha kwamba tunatumia fedha zetu za ndani ambazo Serikali inatenga bilioni 1.84 kila mwezi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba barabara hii ya kutoka Mnazi Mmoja-Lindi-Mchinga-Kibiti-Dar es Salaam mpaka Mwanza kwamba itakapofika mwaka 2005 basi Kisukuma tunasema *Taxi,* lakini Kiswahili safi kwamba gari ndogo inaweza ikapita mpaka huko.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, tunahangaika kuhakikisha kwamba tunapata fedha lakini wakati tunasubiri fedha, la msingi tunalolifanya katika Wizara yetu ni kuhakikisha kwamba barabara hiyo inapitika katika vipindi vyote vya jua kali na mvua. Namwomba Mheshimiwa Bakari Mbonde, avute subira pamoja na Wandengereko wote. *(Kicheko)*

Na. 375

**Wasichana Wanaopata Mimba Mashuleni**

**MHE. JOHN L. MWAKIPESILE** aliuliza:-

Kwa kuwa Elimu ya Msingi na ya Sekondari ni haki ya vijana wetu wote wa Tanzania na kwa kuwa vijana wanafunzi wengi wa kike katika Shule za Msingi na za Sekondari wanabeba mimba na kulazimika kuacha kusoma na baadaye kuwa mzigo mkubwa kwa jamii na Taifa:-

(a) Je, Serikali haioni kuwa kitakuwa ni kitendo cha hekima na busara na cha manufaa kwa Taifa kuwaruhusu hao kuendelea na masomo baada ya kuzaa watoto wao?

(b) Kama kufukuzwa kwa wanafunzi wanaopata mimba shuleni ni kwa mujibu wa Sheria. Je, Serikali itakuwa tayari kuleta Sheria hiyo Bungeni ili irekebishwe na kuwatendea haki ya msingi wanafunzi wa kike?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Mwakipesile, Mbunge wa Kyela, lenye sehemu (a) na (b) kuanza na maelezo ya kiujumla yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, wanafunzi wasichana huacha au huachishwa shule kwa sababu mbalimbali. Kufukuzwa shule au kuacha shule kwa sababu ya mimba ni sababu mojawapo. Kwa mfano, takwimu za mwaka 2001 zimeonyesha kuwa jumla ya wanafunzi 62,659, sawa na asilimia 1.29 ya wanafunzi wa shule za msingi walikatisha masomo kwa sababu mbalimbali. Waliokatisha masomo kwa sababu ya mimba walikuwa wanafunzi 2,666, sawa na asilimia 0.05 ya wanafunzi wote wa mwaka huo. Kwa misingi ya takwimu hizo, wasichana wanaokatisha masomo kwa ajili ya mimba siyo wengi kama alivyoiweka Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kujibu sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali haijawa na uhakika kuwa tumefikia muafaka wa Kitaifa kuwaruhusu wanafunzi wasichana wanaopata mimba kuruhusiwa kuendelea na masomo baada ya kujifungua, tunahitaji kwanza kutathmini athari zinazoweza kutokana na uamuzi huo.

Aidha, inafaa ieleweke kuwa zipo athari zinazoweza kutokea kutokana na umauzi wa kuwaruhusu watoto hawa wachache kuendelea na masomo katika mfumo rasmi baada ya kujifungua ambazo ni lazima zizingatiwe kabla ya kufikia uamuzi huu. Inabidi tuzingatie kuwa lengo mojawapo la kutoa elimu ni kujenga maadili mema ambayo watoto wetu wanapaswa kuyafuata.

Baada ya Serikali kuridhika kuwa tunao muafaka juu ya jambo hili, tunapaswa kuwa na maandalizi yenye lengo la kuweka utaratibu unaofaa wa kuwarudisha shuleni wasichana hao baada ya kujifungua. Masuala ya kuzingatiwa ni pamoja na kuandaa shule watakazoweza kupelekwa, utaratibu wa kuachishwa na kuwarejesha kwa mfano muda kati ya kujifungua na kurejeshwa shuleni na malezi ya watoto waliozaliwa lazima yazingatiwe kwa makini.

(b) Mheshimiwa Spika, sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 10 ya Mwaka 1995, imempa Waziri wa Elimu uwezo wa kutunga sheria ndogo zinazohusu suala la kufukuzwa au kuachishwa shule kwa mwanafunzi yeyote kwa ukosefu na utovu wa nidhamu au kwa misingi ya kutokuwa na hali ya afya inayoridhisha. Mwaka 2002 kwa uwezo niliopewa chini ya sheria hiyo katika kifungu namba 60(0) nilitunga sheria ndogo iitwayo *The education (Expulsion and Exclusion of Pupils from Schools) Regulations 2002 (GN No. 295 of 2002).*

Mheshimiwa Spika, Kanuni hiyo imeweka vigezo na utaratibu unaopaswa kutumika katika kumwachisha na kumfukuza mwanafunzi shuleni likiwemo suala la la kumfukuza mtoto wa kike anayepata mimba shuleni kwa kosa la kujihusisha katika kitendo ambacho ni kinyume cha maadili *(Immoral)* ya mwanafunzi. Kutokana na maelezo hayo, suala hili haliko katika Sheria ya Elimu bali liko ndani ya sheria ndogo iitwayo kanuni ambayo marekebisho yake yako ndani ya uwezo wa Waziri. Muafaka utakapofikiwa marekebisho yatafanywa katika kanuni hiyo ikiwa ni pamoja na kuweka utaratibu unaofaa wa kuwarejesha wanafunzi husika.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kutumika kwa kanuni hiyo, Wizara yangu imekuwa ikielekeza kila shule iwe na kitengo cha ushauri nasaha kwa vijana wetu wa kike na wa kiume ili kuweza kuwasaidia kujua athari za tabia ya uasherati.

Napenda kuchukua fursa hii kuwaasa wazazi, walezi na Watanzania wote kuwa hata kama kanuni hii ikibadilishwa, ni lazima waendelee kwa juhudi kubwa kuwalea vijana katika malezi ya tabia njema kwani faida ya maadili mema kwa vijana ni kubwa na muhimu zaidi kwa kijana na kwa Taifa. Mlezi wa kwanza wa mtoto ni mzazi na jamii inayomzunguka mtoto huyo. *(Makofi)*

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa tatizo la msingi ni watoto wa kike kukosa muda wa kusoma kwa ajili ya kupata mimba. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja sasa hivi kutenga shule chache ili watoto hao wapate nafasi za kuendelea kusoma na wakati huo huo wapate maadili wakati wanasoma? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, napenda tu kusisitiza kwamba suala hili tunaweza tukaliboresha kama tutakuza ushirikiano, si suala la kuachia shule peke yake, ni suala la kukuza ushirikiano kati ya walimu, wazazi na wanafunzi. Huo ndiyo utatu ulio muhimu ili tuweze kujenga tabia njema lakini pia tuhakikishe kwamba watoto wavulana na wasichana wote wanapewa muda wa kutosha wa kujifunza wakiwa shuleni na hata majumbani wanakotoka. *(Makofi)*

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri inaonekana kuna mpango ambao wameupata, mtu anajifungua anarudi shuleni. Je, kama huyo mwanafunzi atapata mimba ya pili tena huko shuleni ataruhusiwa kurudi tena na huyo aliyempa mimba atachukuliwa hatua gani?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa nadhani kama mwalimu katazama mbele zaidi kwamba hili jambo siyo rahisi kama wanavyofikiria wengine. Kwa sababu ukisema tu kwamba anayepata mimba arudi shuleni lazima pia uzungumzie suala la je, akipata tena mnaendelea kufanya hivyo.

Kwa hiyo, hayo ni baadhi ya mambo ambayo kwa kweli tunahitaji kuyazingatia kabla hatujafanya uamuzi. Kwa hiyo, napenda kurudia tu kusema kwamba endapo tutakuwa na muafaka juu ya jambo hili tutalikamilisha kwa kuweka utaratibu ambao tutaridhika kwamba unafaa na upo sahihi kutokana na makubaliano yatakayokuwepo.

Na. 376

**Matatizo ya Upungufu wa Walimu Nchini**

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA** aliuliza:-

Kwa kuwa Shule nyingi za Sekondari hapa nchini zina tatizo la upungufu wa walimu wa masomo mbalimbali na kwa kuwa upungufu huo huongezeka kila mwaka kutokana na sababu za uhamisho, vifo, kustaafu au kuacha kazi jambo linalopelekea Serikali kuendelea kupata malalamiko ya upungufu wa walimu wa mara kwa mara:-

(a) Je, ni kwa nini Serikali haichukui tahadhari kubwa katika zoezi zima la uhamisho wa walimu kila mwaka ambalo linasababisha upungufu wa walimu kwenye maeneo mbalimbali ya nchi na kusababisha malalamiko juu ya tatizo hilo kuendelea dhidi ya Serikali?

(b) Kwa kuwa kumekuwa na upungufu wa walimu katika shule ya sekondari Matai na kwa kuwa mwaka 2002 nimeilalamikia Serikali juu ya tatizo hilo ndipo Serikali ilipopeleka walimu kwenye shule hiyo ambapo wengine wameripoti na wengine kati yao hawakuripoti, lakini ilipofikia mwishoni mwa mwaka huo wamehamishwa walimu wengine kutoka hapo na tatizo likabakia. Je, ni lini tatizo hilo litatatuliwa kwa shule za pembezoni kama vile sekondari za Matai na Mambwe?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mbunge wa Kalambo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mwalimu huhamishwa kutoka kwenye kituo chake cha kazi kwa sababu mbalimbali zikiwemo za mke kumfuata mume wake, afya ya mwalimu kwa ushauri wa daktari, kwenda masomoni Chuo Kikuu na baada ya kuhitimu kupangiwa shule ya Sekondari ya juu kufundisha masomo ya

ngazi ya A *(A Level)* na kufunguliwa kwa shule mpya hasa zile zinazojengwa na wananchi ambazo zinakuwa hazina walimu kabisa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikichukua tahadhari hasa wakati wa kuanzisha shule mpya kwa kutoa maelekezo ya mara kwa mara kwa wananchi wanaotaka kufungua shule kuwasilishwa Wizarani maombi yao mwaka mmoja kabla ya kufungua shule hizo, ili utaratibu wa kuipatia walimu shule inayofunguliwa uweze kufanywa mapema.

Pia Serikali imeweka masharti ya msingi kabla ya kusajili shule, mojawapo ikiwa ni kukamilisha ujenzi wa angalau nyumba nane za walimu ili walimu wakipangwa kwenye shule hizo waweze kuwa na mahali pa kuishi.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa shule za sekondari za Matai na Mabwe kama ilivyo katika shule nyingi za sekondari hapa nchini, zina tatizo la upungufu wa walimu. Upungufu wa walimu katika shule hizi, haukusababishwa na uhamisho tu bali pia lipo tatizo la msingi la kutokuwa kwa muda mrefu na mpango wa mafunzo ya walimu unaoendeana na mfumuko mkubwa wa shule za sekondari zinazojengwa kwa nguvu za wananchi.

Mheshimiwa Spika, shule ya sekondari ya Matai ilikuwa na jumla ya walimu 14, walimu sita kati ya hao walihamishwa kutokana na sababu za afya zao na wengine kuolewa. Shule ya sekondari Mabwe ilikuwa na walimu tisa, mwalimu mmoja alihamishwa kwa sababu ya afya na mapendekezo ya daktari. Aidha, katika ajira ya walimu inayoendelea hivi sasa mwalimu mmoja amepangwa sekondari ya Matai angalau kupunguza kidogo tatizo.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea na juhudi za kuajiri walimu wapya na kuwapanga katika shule zote kwa kuzingatia mahitaji. Aidha, mpango wa maendeleo ya sekondari wa miaka mitano 2004 hadi 2009 unaandaliwa ili kuboresha elimu ya sekondari. Mpango huo utafuatiwa na mpango kamambe wa mafunzo ya ualimu yaani *Teacher Education Masterplan (TEMP),* utakaohakikisha kuwepo kwa walimu wa kutosha wa ngazi zote kwa ajili ya shule zetu.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekubali tatizo hili la upungufu wa walimu na kweli anajitahidi sana ili kuweza kutatua tatizo hili.

Sasa swali je, Waziri haoni kwa sababu ya upembezoni wa Mkoa huu wa Rukwa Chuo cha Ualimu kilichopo Sumbawanga kiweze kufanya kazi ya kuongeza idadi ya walimu wanafunzi wanaopokelewa katika Chuo kile ili kuweza kutosheleza mahitaji ya walimu wa shule za msingi katika Mkoa ule wa Rukwa?

Pili, je, si busara kwa Wizara ikaangalia uwezekano wa kuanzisha Chuo kitakachofundisha walimu wa Diploma katika Chuo hicho hicho cha Sumbawanga ili walimu wale waweze kusambazwa katika shule za sekondari za Mikoa ya Rukwa, Kigoma pengine na Mbeya ambayo ipo karibu pale? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, nakubali kwamba Mkoa wa Rukwa ni kweli upo pembezoni na nakubali pia kwamba hali yake ya elimu ni mbaya sana. Pia napenda kukiri kwamba nimepata mapendekezo mazuri sana kutoka kwa Mheshimiwa Mwananzila ameniandikia na tumeongea kidogo na pia Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kuhusu namna ya kuingiza wanafunzi wa kutosha katika Chuo cha *TCC* kilichopo Mpanda pamoja na mawazo kwamba kwa vile watu wengine huwa wanakataa kwenda huko Mpanda na Mkoa wa Rukwa tujaribu kujaza wanafunzi wanaomaliza katika sekondari zilizopo huko kwa sababu wamezoea mazingira ya kule Rukwa na hawatakuwa na sababu ya kukataa kufanya kazi ya ualimu miongoni mwa Vijiji wanakotoka. Kwa hiyo, mapendekezo hayo nimeyakubali na tunayafanyia kazi Wizarani na nadhani yatachangia kuondoa hilo tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili, jambo hili tutaliangalia wakati tunakamilisha huu mpango wa maendeleo wa elimu ya sekondari na ule mpango utakaofuatia wa *Teacher Education Masteplan* baadhi ya Vyuo vitafanyiwa *up grading.*

Napenda niseme ni mapema mno sasa hivi kabla ya kuangalia hali halisi ilivyo katika vyuo vyetu kuweza kutamka hivyo, kama kitabahatika kikawa ni kimojawapo itakuwa ni bahati. Lakini tutajitahidi tuwe na walimu wa kutosha katika vyuo vyetu, tufundishe walimu wa kutosha ili kutosheleza mahitaji ya nchi nzima Mkoa wa Rukwa ukiwa miongoni mwake.

Na. 377

**Huduma ya Umeme**

**MHE. JOEL N. BENDERA** aliuliza:-

Kwa kuwa kwa miaka mingi sasa wananchi wa Vijiji vya Kwagunda, *Gereza East,* Mkwakwani na Kwemzindawa, waliahidi kupatiwa umeme kutokana na majibu yenye matumaini ya mara kwa mara Bungeni na kwa kuwa wananchi wamehamasika na kuanza kufanya *wiring* majumbani mwao tayari kusubiri umeme:-

(a) Je, Serikali ina maelezo gani kwa wananchi wa Vijiji hivyo?
(b) Je, Serikali haioni kuwa sasa ndiyo muda muafaka wa kuvipatia umeme Vijiji hivyo ambavyo vipo karibu na umeme ili kutimiza ahadi yake ya muda mrefu?

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joel Bendera, Mbunge wa Korogwe Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Serikali hutekeleza ahadi zake za kupeleka umeme Vijijini kupitia *TANESCO.* Mara nyingi kwa Vijiji vilivyo karibu na njia za umeme hupatiwa huduma hii kupitia miradi inayopangwa na kutengewa fungu la fedha la utekelezaji na ofisi za *TANESCO* za Mikoa na Wilaya husika au mafungu kutoka Serikalini.

(a) Kijiji cha Kwagunda tayari kimepata umeme tangu Januari, 2002 na jumla ya wateja sita wameunganishiwa umeme. Hata hivyo, kwa bahati mbaya sana wimbi la wizi wa nyaya za umeme limeathiri upatikanaji wa umeme kwa wateja hao. Kwani nyaya za umeme kutoka kwenye laini kubwa zimeibiwa na kwa sasa hivi wateja hao hawana umeme.

(b) Mheshimiwa Spika, ili kuvipatia umeme Vijiji vya *Gereza East,* Mkwajuni na Kwemzindawa inakadiriwa kuwa itagharimu jumla ya shilingi milioni 84. Ni matarajio ya Serikali kuwa pindi fedha zitakapopatikana Vijiji hivyo vitapelekewa huduma ya umeme kwa haraka.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza niishukuru Wizara kwa kukipatia umeme Kijiji cha Kwagunda na kwa kuwa mradi huu wa Kwagunda, Kwemzindawa ni wa muda mrefu na Mheshimiwa Waziri amesema zinatakiwa shilingi milioni 84 na kwa kuwa mradi ule ni wa muda mrefu na una kero. Je, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kutembelea maeneo hayo ili ajionee mwenyewe jinsi wananchi walivyokuwa wanakerwa na umeme?

Pili, kwa kuwa kwa muda mrefu *TANESCO* wamekuwa wakipitisha umeme na nguzo za umeme porini kiasi ambacho inakuwa si rahisi kuulinda umeme unapofika katika maeneo hayo. Je, *TANESCO* ipo tayari sasa kubadilisha mwelekeo kwamba nguzo wanazoziweka katika awamu hizi za sasa katika nchi nzima zipitie kwenye Vijiji ili iwe rahisi kwa wananchi katika Vijiji kupata umeme? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kutembelea Vijiji vile ambavyo vimetajwa katika swali la msingi nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Mbunge kwamba tukimaliza Bunge hili tupange mimi na yeye ili tuweze kutembelea huko na kuona ni kitu gani kinatokea.

Mheshimiwa Spika, kuhusu swali la pili la kwamba nguzo zipitie sehemu ambazo siyo porini sana na zipitie kwenye Vijiji nadhani nia yake ni kwamba zikipitia kwenye Vijiji basi Vijiji vingi vitapata umeme. Lakini ukweli ni kwamba kitaalam umeme kwa sababu ni gharama sana kuutoa sehemu moja kwenda nyingine unachukua hatua ambazo wale waliojifunza hesabu wanaita *the shortest distance between two points in the straight line.*

Kwa hiyo, unajaribu sana kuunganisha sehemu moja kwa mstari ulionyooka ikiwa inawezekana hakuna milima au mabonde makubwa sana ili umbali huo uwe mfupi na nyaya na gharama za kuutoa umeme sehemu moja kwenda nyingine ziwe za nafuu sana. Lakini kwa kusema kwamba tupitie Vijijini tu ili mradi Vijiji vingi viguswe na nyaya hizo kwa kweli itategemeana na gharama ambazo wataalam watatuambia wakati wakitathmini ni kiasi gani kitahitajika kupeleka umeme kutoka sehemu moja kwenda nyingine.

**MHE. BALOZI GETRUDE I. MONGELLA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na majibu mazuri ya Waziri ya kusema umeme mara nyingi unakwenda *shortest distance,* je, atakubaliana na mimi ya kwamba sasa ni wakati wa kupeleka umeme Ukerewe kwa sababu hatuna milima wala mabonde, ni mserereko tu ndani ya maji, atachukua *shortest distance* kwenda Ukalla, Gana, Kamafi, Buyubi na Ilugwa? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, ushauri wake huo kama kweli sehemu hizo ndiyo *the shortest distance between two points* basi nitaupeleka *TANESCO* ili wataalam nao wahakikishe kwamba kweli ni hivyo na panapitika bila kuongeza gharama za mradi.

**SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, swali la Mheshimiwa Ernest Mabina, ameliondoa mwenyewe kwa kusema kwamba, limepitwa na wakati.

Kwa hiyo, maswali yamekwisha na muda wa maswali umekwisha. Kuna tangazo moja tu la kikao cha Kamati leo nayo ni Kamati ya Hesabu za Serikali, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, anaomba wajumbe wa Kamati ya *PAC* wakutane saa 7.00 mchana chumba Na. 56.

Mwisho wa matangazo, tunaendelea na *Order Paper,* Katibu.

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

*(Kusomwa Mara ya Kwanza)*

### Muswada wa Sheria ya Sekta ya Uvuvi wa Mwaka 2003
### *(The Fisheries Bill, 2003)*

**SPIKA:** Muswada umesomwa Mara ya Kwanza, kwa utaratibu ule ule kwamba utajadiliwa katika Mikutano ijayo.

*(Muswada uliotajwa hapo juu ulisomwa Bungeni Mara ya Kwanza)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2003/2004
### Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama nilivyowaeleza siku ya Ijumaa kwamba ratiba imebadilika kidogo. Kwa hiyo, leo kuna Wizara mbili ambazo zitawasilisha hoja zake moja baada ya nyingine. Halafu zitajadiliwa kwa pamoja. Kama tulivyofanya mwanzoni wakati wa Bajeti tutafanya hivyo hivyo zitajadiliwa kwa pamoja. Halafu zitaamuliwa moja baada ya nyingine mwishoni mwa mjadala. Sasa namwita mtoa hoja wa kwanza.

Ukitaka mwongozo wa Spika, mwambie mapema ili akuone. Sasa wewe unasimama tu mimi nitajuaje unataka nini. Nafikiri unatoka nje kwenda kwenye chai. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi iliyochambua Bajeti ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwa mwaka wa fedha 2003/2004, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa lipokee na kujadili mapitio ya utekelezaji wa mwaka 2002/2003 na kukubali kupitisha Makadirio ya fedha za Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji pamoja na asasi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha wa 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutumia fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati ya Fedha na Uchumi, wakiongozwa na Mwenyekiti wao Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, kwa uchambuzi wao wa kina na makini wa makadirio haya. Aidha, ningependa kukupongeza wewe mwenyewe pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa uvumilivu na umakini mliouonyesha hadi sasa katika kazi hii nzito ya kujadili na kupitisha Makadirio ya Wizara mbalimbali tangu kuanza kwa kipindi hiki cha Bunge la Bajeti.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji pamoja na asasi zake yanajumuisha kusimamia uendeshaji wa uchumi, kuongoza maandalizi na kusimamia utekelezaji wa mipango ya maendeleo kwa kuzingatia mabadiliko makubwa katika uchumi hasa ya kuweka mazingira mazuri na kuipa Sekta binafsi nafasi kubwa ya kuchangia katika maendeleo ya nchi yetu. Katika kufanikisha azma hii, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji inatekeleza majukumu yafuatayo:-

Kuendeleza utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 pamoja na sera mbali mbali za kupambana na umaskini na kukuza uchumi, kuimarisha mfumo wa mipango na usimamizi wa uchumi, kuendeleza na kuimarisha taaluma ya ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa takwimu na taaluma ya mipango ya maendeleo vijijini, kuchambua sera na kuainisha masuala muhimu katika mipango na uendelezaji utafiti, kusimamia shughuli za ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma na kuratibu uwekezaji wa raslimali, kupanga mipango ya maendeleo ya rasilimali watu na kukamilisha zoezi la sensa ya kuhesabu Watu na Makazi.

Pia kusimamia uimarishaji wa tija katika uchumi wa Taifa, kubuni mwongozo na shughuli za sekta ya nje na kupanga matumizi ya mikopo na misaada toka nje na kuimarisha Tovuti ya Taifa ili iweze kutumika vizuri katika usambazaji wa takwimu vizuri katika usambazaji wa takwimu, habari umuhimu na taarifa mbalimbali za uchumi na maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, katika kipindi cha 2002/2003 utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji yaliyotajwa hapo juu ulikuwa ni wa kuridhisha. Maeneo muhimu yafuatayo yalishghulikiwa na kutekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji ilikarabati jengo na kupata samani mpya pamoja na kompyuta. Ofisi iliajiri wachumi na maofisa mipango 44 ambao walisambazwa katika Wizara na Mikoa mbalimbali na baadhi yao tayari wamepatiwa mafunzo kazini. Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini kilichoko Dodoma na Chuo cha Takwimu cha Mashariki mwa Afrika, vimeendelea kuimarishwa kwa kuajiri walimu zaidi na kuvipatia vitendea kazi ili viweze kutoa Maafisa Mipango na Maafisa Takwimu wa kutosha kitaaluma kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya sekta mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kushughulikia Idadi ya Watu *(UNFPA)* tumetoa kompyuta na vifaa kwa Wilaya 26 ili kuboresha uwezo wa kuandaa mipango katika ngazi ya Wilaya. Maafisa Mipango kutoka Wilaya hizo wamepewa taaluma ya kutumia vifaa hivyo katika kuchambua na kutumia takwimu katika kuandaa Mipango ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, tutaendelea kuboresha utendaji kwa kutoa mafunzo kazini, tutaajiri wataalam zaidi pamoja na kuwapatia vitendea kazi na kuendelea kuboresha mazingira ya kazi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji inalo jukumu la kusimamia Tovuti ya Taifa *(National Website).* Katika kipindi cha 2002/2003, Tovuti imetumiwa na wastani wa watu 10,000 kwa siku, kati ya hao, wastani wa watu 5,000 ndio walioitumia kikamilifu. Ofisi imeendelea kuboresha huduma hiyo kwa kuainisha na kupitia taarifa muhimu zikiwemo sera za sekta mbalimbali, hotuba za viongozi wetu wakuu, matokeo ya uchambuzi wa takwimu za Sensa ya Watu na Makazi na kadhalika.

Katika mwaka 2003/2004, tutaendelea na uboreshaji wa Tovuti hii pamoja na kutangaza fursa na vivutio tulivyonavyo vya utalii na uwekezaji kwa watu wengi zaidi na kwa gharama ndogo. Mikoa na Wilaya itaendelea kuhamasishwa pia kutumia Tovuti hii.

Mheshimiwa Spika, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ilianza kutekelezwa miaka minne iliyopita kwa kutekeleza sera za kuimarisha na kutengemaza vigezo muhimu vya uchumi jumla na Mkakati wa Kupunguza Umaskini, kurekebisha sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza uchumi, kuboresha mfumo wa Serikali za Mitaa, kuhuisha sera za Sekta mbalimbali na kutayarisha Mkakati wa Kukuza Sekta ya Kilimo na wa kuleta Maendeleo Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Wizara, Mikoa na Wilaya vimeendelea kubaini fursa na vikwazo vya maendeleo vilivyoko katika maeneo yao kwa lengo la kutayarisha Mpango wa Muda wa Kati wa kutekeleza Dira. Kwa mwaka 2002/2003, kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kiuchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, tumetayarisha rasimu ya Mpango wa Kwanza wa Taifa wa Muda wa Kati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini. Rasimu ya Mpango huu ilisambazwa kwa wadau mwezi Oktoba, 2002 ili iweze kutolewa maoni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Ofisi ya Taifa ya Takwimu iliendelea kukusanya na kuimarisha ubora wa twakimu nchini. Taasisi hii imeweza kuboresha shughuli zake katika maeneo ya kukusanya takwimu za fahirisi ya bei ili kutoa kigezo cha kasi ya upandaji bei, uzalishaji viwandani na zile za ukadiriaji wa Pato la Taifa na kuchambua takwimu za biashara na nchi za nje.

Mheahimiwa Spika, aidha, tafiti za Ajira na Mapato, hali ya utalii na uzalishaji katika mashamba makubwa na za uzalishaji wa Sekta ya Viwanda kwa mwaka na robo mwaka zilifanywa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, iliendelea kusambaza matokeo ya Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi na yale ya Utafiti wa watu wenye Uwezo wa Kufanya kazi na Ajira kwa Watoto. Pia Ofisi hii kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Chakula, Maji na Maendeleo ya Mifugo na Ushirika na Masoko, iliendelea na matayarisho kwa ajili ya kufanya Utafiti wa Kilimo.

Aidha, juhudi za kuboresha takwimu za Pato la Taifa ziliendelea kufanywa katika ukusanyaji wa takwimu kupitia Sensa ya Biashara *(Business Census)* kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kama Wakala wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilifanikiwa kupata kazi *(commissioned work)* zifuatazo:-

Utafiti wa matatizo ya Uzazi katika Wilaya ya Moshi Mjini, utafiti wa Ustawi wa Kaya *(Core Welfare Indicators)* kwa Wilaya ya Singida Mjini, Mtwara- Mikindani na Mbeya Mjini na uutafiti wa Uelewa wa Elimu kwa Walipa Kodi Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Ofisi ya Taifa ya Takwimu kwa niaba ya Tume ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi *(TACAIDS)* itafanya utafiti wa viashirio vya Ukimwi Tanzania *(Tanzania HIV/AIDS Indicators Survey).*

Mheshimiwa Spika, wadau wengine watakaoshiriki katika tafiti hii ni Programu ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi *(NACP)* na Chuo Kikuu Kishiriki cha Tiba, Muhimbili. Lengo la utafiti huu ni kuratibu na kupima mahitaji ya programu za Ukimwi na uhusiano wa maaambukizi ya Ukimwi na magonjwa ya zinaa. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2003/2004, Ofisi hii kwa kushirikiana na Wizara za Kilimo na Chakula, Maji na Maendeleo ya Mifugo na Ushirika na Masoko, pamoja na wadau wengine

itakamilisha utafiti wa kilimo ikijumuisha mifugo, kama shughuli moja muhimu katika Mpango wa Kufuatilia Umaskini Nchini.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji inaendelea kutoa mafunzo ya watakwimu kupitia Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika. Katika mwaka wa fedha 2002/2003, Chuo kiliendelea kutoa mafunzo ya kawaida ya muda mrefu ya Cheti na Stashahada kwa wanafunzi 59 kutoka nchi tano. Kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, Chuo kiliendesha warsha tatu za Kimataifa na mafunzo ya muda mfupi ya kitaifa mara tano. Jumuiya ya Ulaya na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa ziligharamia mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha ukusanyaji na matumizi ya takwimu katika ngazi ya vijijini, Chuo kimeanza kutoa mafunzo ya takwimu kwa wafanyakazi walioteuliwa na Serikali za Mitaa. Jitihada nyingine kama hizo pia zinafanyika chini ya program ya masuala ya idadi ya watu inayofadhiliwa na *UNFPA*. Kwa kushirikiana na TAMISEMI na *UNFPA,* Chuo kitaendesha mafunzo kwa maofisa wa wilaya katika Mikoa ya Kagera na Shinyanga katika kuwapa uwezo wa kufundisha watendaji ngazi za Vijiji, taaluma ya kukusanya, kuchambua na kutumia takwimu za msingi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka mwa fedha 2003/2004, Chuo kinatarajia kuendesha mafunzo ya kawaida ya Cheti na Stashahada, kutayarisha na kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa wazalishaji na watumiaji wa takwimu kulingana na watumiaji wa takwimu kulingana na mahitaji ya wateja, kushiriki katika zoezi la kuboresha mfumo wa kukusanya na kutunza takwimu za kiutawala chini ya Mkakati wa Kupunguza Umaskini, kutangaza shughuli za Chuo na kuhamasisha matumizi sahihi ya takwimu katika maamuzi ya utayarishaji wa Mipango ya Maendeleo katika ngazi mbalimbali na kushughulikia maombi yote ya huduma za Chuo kutoka nchini, nje ya nchi na taasisi mbalimbali pamoja na wateja wengine.

Aidha, kwa kushirikiana na TAMISEMI na *UNFPA,* Chuo kitaendelea kuendesha mafunzo kwa Maofisa wa Wilaya katika Mikoa mingine ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini kiliendelea kuendesha mafunzo ya muda mrefu kwa wanafunzi 280. Chuo kiliendesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu pamoja na kufanya tafiti kwa kushirikiana na Idara za Serikali pamoja na Mashirika yasiyo ya Kiserikali kama ifuatavyo: -

Kwa kushirikiana na TAMISEMI, Chuo kiliendesha mafunzo ya Mbinu Shirikishi ya Upangaji Mipango kwa kutumia Mfumo wa Fursa na Vikwazo, kuendesha mafunzo ya Ukusanyaji Takwimu, Ufuatiliaji wa Tathmini katika ngazi ya Wilaya hadi Kijiji kwa Mikoa ya Tabora, Kigoma, Shinyanga na Kagera kwa kushirikiana na TAMISEMI, kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Upunguzaji Umaskini kupitia Taasisi isiyo ya Kiserikali, inayoitwa *Southern Africa Extension Unit,* Chuo kimeandaa na kuendesha mafunzo ya muda mfupi kwa *Community Based Organizations* na Chuo kimefanya utafiti wa mfumo wa ukusanyaji takwimu kutoka ngazi ya Kijiji hadi Taifa kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Chuo kinatarajia kuendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi, kufanya tafiti na kutoa ushauri kwa Wizara na Idara mbalimbali za Serikali, Mashirika yasiyo ya Kiserikali, pamoja na vikundi mbalimbali kuanzia ngazi ya Kijiji. Aidha, Chuo kitakamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa bweni pamoja na kuanza awamu ya pili ili kuongeza idadi ya wanafunzi hadi kufikia 400 mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji ikishirikiana na Wizara na wadau mbalimbali, iliendelea na juhudi za kuweka mikakati na kuchambua Sera za Kiuchumi na Kijamii ili kuimarisha usimamizi wa uchumi kwa kutekeleza yafuatayo:-

Kuandaa Sera za Uchumi Jumla na Maendeleo ya Jamii kwa kipindi cha mwaka 2003/2004 hadi 2005/2006 na Taarifa ya Hali ya Uchumi katika mwaka 2002, kuandaa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2003/2004, kushiriki katika zoezi la uchambuzi wa mapato na matumizi ya Serikali, kuandaa Mwongozo wa kutayarisha Mpango wa Muda wa Kati na Mfumo wa Bajeti, kukusanya na kuchambua taarifa za Mikoa

na kuandaa hali za uchumi na kijamii za Mikoa mbalimbali *(Regional Profiles),* kwa kushirikiana na Mikoa husika, kuandaa taarifa ya pili ya utekelezaji wa Mkakati wa Kupambana na Umaskini , taarifa ya kwanza ya Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mpango wa Mikopo ya Shirika la Fedha la Kimataifa na Benki ya Dunia na kushiriki katika kuandaa Sera za Mkakati wa Maendeleo ya Ushirika, Sera ya Ujenzi, Sera ya Uchukuzi, Sera na Mkakati wa Kilimo na Maendeleo Vijijini wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, pia kushiriki katika kuandaa Taarifa ya Utekelezaji wa Programu ya Mtandao wa Barabara za Afrika Mashariki, kushirikiana na wadau wengine katika kuendeleza juhudi za kuleta usawa wa kijinsia kwa kuendeleza uingizaji wa masuala ya jinsia katika sera na mipango ya maendeleo, kuandaa programu za ushirikiano wa kiuchumi Kimataifa hasa za *EAC* na *SADC* kwa kushirikiana na wadau wengine ikiwa ni pamoja na sekretarieti za Jumuiya hizo na kuandaa na kushiriki katika kongamano la kwanza la kutathmini maendeleo ya Tanzania katika miaka 40 iliyopita na mikakati thabiti ya kusukuma ukuaji wa uchumi na maendeleo katika miaka ijayo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004 tutaendelea na juhudi za uchambuzi wa sera na mwenendo wa vigezo mbalimbali vya kupima maendeleo ya uchumi ili kubainisha vipaumbele na kuainisha maeneo yanayohitaji marekebisho.

Mheshimiwa Spika, zoezi la Sensa ya watu na makazi lilikamilika tarehe 4 Septemba, 2002. Shughuli ya uingizaji wa takwimu kwenye kompyuta ilifanyika kwa kutumia teknolojia ya *Optical Mark Recognition (OMR),* kazi ambayo ilichukua siku 26 badala ya miaka miwili kama tungelitumia teknolojia ya zamani. Aidha, taarifa ya jumla ilikamilika mwishoni mwa Desemba, 2002 na kusambazwa Wilayani, Mikoani, Wizarani na katika Taasisi mbalimbali na wadau wengine.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, shughuli za Sensa ya watu na makazi zitaelekezwa katika kukamilisha uchambuzi wa takwimu zilizokusanywa, kuchanganua takwimu, kuchapisha taarifa mbalimbali za sensa na kusambaza matokeo ya sensa kwa watu na wadau mbalimbali. Matarajio ni kukamilisha shughuli hizi ifikapo Desemba, 2004.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2002/2003, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kwa kushirikiana na *UNFPA* iliendelea kuratibu, kufuatilia na kutathmini programu ya Taifa kuhusu idadi ya watu na maendeleo ikiwa katika programu ya tano ya utekelezaji 2002/2006.

Katika mwaka 2003/2004 tutaendelea na uratibu wa programu hiyo, pamoja na kuandaa na kukamilisha mfumo wa kusaidia na kuainisha masuala ya idadi ya watu na mipango ya maendeleo. Hii ni katika jitihada za kutekeleza Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu ya mwaka 1992.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, tulikamilisha ukusanyaji wa takwimu za Mikoa kuhusu viwango vya maendeleo ya watu *(Human Development Index - HDI)* na kiwango cha Umaskini wa Watu *(Human Poverty Index - HPI),* pamoja na utayarishaji wa viwango vya maendeleo Kimkoa kwa Mikoa ya Mbeya na Kilimanjaro kwa majaribio. Kiwango cha Maendeleo ya watu Kimkoa huonyesha tofauti za maendeleo baina ya Mikoa husika, ambapo kiwango cha umaskini wa watu huonyesha hali ya umaskini nchini.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, utayarishaji wa viwango vya maendeleo kwa kutumia kiwango cha maendeleo ya Jinsia *(Gender Related Development Index - GDI)* na kipimo kipimo cha kuipa uwezo jinsia *(Gender Empowerment Measure - GEM),* utaendelea. Pia kwa kushirikiana na wadau wengine tutaendelea na ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu za Wilaya mbalimbali ili kubaini viwango vya maendeleo Kiwilaya katika Mikoa mingine.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2002/2003, tuliendelea kushirikiana na *UNICEF* katika kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa programu ya uhai, ulinzi na maendeleo ya mtoto. Hii ni awamu ya nne ya mpango (2002 hadi 2006) wenye lengo la kujenga mazingira ya kutambua na kuheshimu haki za watoto na wajibu wao katika jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2003/2004, tutaendelea kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa programu hii. Aidha, kwa kushirikiana na *UNICEF* na wadau wengine, tutaweka mikakati ya maandalizi ya

kufanya mapitio ya muda wa kati wa utekelezaji wa programu hii *(Mid - Term Review).* Vile vile katika mwaka huu wa fedha, utatayarishwa mfumo wa kufuatilia na kufanya tathmini ya huduma za jamii.

Mheshimiwa Spika, kwa kushirikiana na wadau wengine, katika mwaka 2002/2003, tulichambua na kutoa ushauri katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kubaini mikakati ya kuwezesha Tanzania kushiriki kwa kupitia fursa zilizopo za kibiashara za kimataifa hasa *WTO, EBA, AGOA* na mpango wa *EU/ACP* kwa kuzingatia lengo letu la kujenga uchumi endelevu unaokua.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ushirikiano wa kiuchumi kimataifa, baadhi ya maeneo tuliyoshughulikia katika mwaka 2002/2003 ni kuratibu kitaifa zoezi la mpango wa ushirikiano ili kuleta maendeleo Barani Afrika *(NEPAD)* pamoja na kukamilisha programu za kitaifa za utekelezaji wake kwa kushirikiana na Wizara na wadau mbalimbali nchini. *NEPAD* inaweka mkazo wa kuleta maendeleo kwa kutumia raslimali zetu wenyewe zikisaidiwa na unafuu unaotokana na kufutiwa madeni na nchi zilizoendelea. Umuhimu pia unawekwa katika sekta ya binafsi kwa kuiimarisha na kuongeza juhudi zinazolenga katika upatikanaji wa soko kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika kipindi cha 2002/2003, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji ilishirikiana na wadau nchini na wale wa nchi za *SADC* katika kuandaa rasimu ya mkakati wa maendeleo ambao unatarajiwa kuwa dira ya maendeleo ya nchi za *SADC.* Tanzania imebahatika kuwa mwenyeji wa Mkutano wa Wakuu wa *SADC* ambao utafanyika Dar es Salaam toka tarehe 20 hadi 27 Agosti, 2003.

Napenda kutumia fursa hii kuwaomba na kuwahamasisha Waheshimiwa Wabunge, wafanyabiashara, sekta binafsi na wadau wengine, kuitumia nafasi hiyo ya mkutano kuweza kujifunza kutoka nchi hizo na kuitangaza nchi yetu kwa lengo la kutumia fursa zilizopo kukuza biashara na uwekezaji kati ya Tanzania na nchi hizo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ushirikiano na nchi za Afrika Mashariki kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kiuchumi ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam tulianza zoezi la kuchambua na kutathmini fursa na vikwazo vya ushiriki wetu kwenye Jumuiya hiyo. Aidha, tuliratibu majadiliano ya mikataba ya kukuza na kulinda rasilimali kati ya Serikali yetu na Serikali za Uswisi, Mauritius, India, Afrika ya Kusini, Malawi, Zimbabwe, Ubeligiji, Oman pamoja na *OPEC Fund.*

Mheshimiwa Spika, chini ya Mpango wa *TCDC* kwa kushirikiana na Umoja wa Mataifa, tuliimarisha kitengo cha kuratibu mpango wa *TCDC* kwa kupatiwa vifaa na mafunzo. Aidha, taarifa za awali za Taasisi mbalimbali zinazokusudia kushiriki katika mpango huu zilikamilishwa. Shabaha ya mpango huu ni kuwa na utaratibu utakaoziwezesha nchi zinazoendelea kubadilishana utaalam wa kiufundi kwa gharama ndogo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji itashiriki katika kukamilisha itifaki ya ushuru wa forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, tutakamilisha taarifa ya kutathmini fursa na vikwazo vya ushiriki katika maandalizi ya Mkutano wa Tatu wa Kimataifa wa Tokyo kwa ajili ya maendeleo ya Afrika *(TICAD III)* ambapo Mkutano wa Wakuu wa Nchi za Afrika na Serikali ya Japan umepangwa kufanyika Tokyo, Japan kutoka Septemba, 29 hadi Oktoba 1, 2003. Madhumuni ya mkutano huo ni kuangalia jinsi gani *TICAD III* itaweza kusaidia mpango wa *NEPAD.*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Kituo cha Uwezekezaji *(TIC)* kiliendelea kutekeleza Mkakati wa Muda wa kati wa 2001 hadi 2006. Baadhi ya malengo yaliyotekelezwa ni pamoja na kukamilisha upanuzi wa ofisi, kuandaa jarida maalum lenye makala za kuitangaza Tanzania na vivutio vya uwekezaji, kuanzisha Tovuti ya kituo na pia kuhudhuria semina, makongamano na Mmaonyesha ya Biashara ya Kimataifa ili kutangaza vivutio vya kuwekeza Tanzania.

Vile vile kituo cha Uwekezaji kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu pamoja na Benki Kuu kimeendelea na zoezi la kutayarisha takwimu za uwezekaji wa moja kwa moja kutoka nje *(FDI).*

Mheshimiwa Spika, kituo kiliendelea kuwakutanisha na kuwahamasisha wawezekaji wa ndani ambapo jumla ya miradi 60 kutoka kwa wawekezaji wa ndani ilitangazwa kwa wawekezaji wa nje kwa lengo la kupata mikopo na teknolojia ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, mikutano ya kuhamasisha wawekezaji wa ndani ilifanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Kilimanjaro, Kigoma, Rukwa, Mbeya, Pwani na Dodoma kwa lengo la kutoa taarifa zinazohusiana na mazingira ya uwekezaji nchini. Pia, kituo kilitembelea miradi 300 iliyoko Mikoani kwa lengo la kubaini na kutafuta ufumbuzi wa matatizo yanayowakabili wawekezaji wa ndani. Ili kuboresha mazingira ya uwekezaji nchini, Hazina ya Ardhi *(Land Bank)* ilianzishwa kwa ajili ya kuainisha ardhi inayofaa kwa kuwekeza.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, *TIC* itaendelea na mikakati ya kuwahamasisha na kutoa huduma bora kwa wawekezaji wa ndani na nje. Mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea na juhudi za kukusanya na kusambaza taarifa za maeneo yanayohitaji wawekezaji ikiwa ni pamoja na kuwaunganisha wawekezaji wa ndani na wa nje kwa lengo la kuingia ubia, kuitangaza Tanzania kama eneo bora kwa ajili ya uwekezaji kwa kushiriki katika mikutano, warsha na maonyesho ya biashara ya Kimataifa, kuwahamasisha na kutoa elimu kwa wafanyabiashara ndogo na za kati jinsi ya kuendesha na kuimarisha biashara zao na kuandaa taarifa zitakazowawezesha kupata mikopo na kufanya uchambuzi na kuboresha taratibu za mfumo wa Hazina ya Ardhi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Baraza liliandaa mkutano wa pili wa Wawekezaji wa Nje *(International Investors Round Table)* uliofanyika Zanzibar kwa lengo la kuhamasisha uwekezaji na kuainisha kero mbalimbali zinazohusiana na biashara na uwekezaji nchini. Kutokana na mapendekezo ya mkutano huo, Serikali inaandaa marekebisho ya Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999 ili ardhi itumike kama dhamana katika utoaji wa mikopo kwa lengo la kukuza uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2003/2004, *TNBC* itaendelea na shughuli zake za kuimarisha mawasiliano baina ya sekta binafsi na Serikali katika masuala ya sera, mfumo wa kodi, sheria, taratibu na kanuni mbalimbali za biashara na uwekezaji nchini. Jitihada pia zitawekwa katika kuhamasisha uimarishaji wa vyombo mbalimbali vinavyounganisha sekta binafsi nchini ili viweze kuchangia zaidi katika jitihada za kukuza uchumi. Aidha, Baraza litaendelea kuimarisha ufuatiliaji wa makubaliano yaliyofikiwa katika mikutano na vikao mbalimbali vilivyofanyika hususan Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji uliofanyika mwezi Mei, 2003 Mjini Zanzibar na vikao vya *Smart Partnership* ili kuhakikisha utekelezaji wa maamuzi yaliyofikiwa kwenye mikutano na vikao hivyo.

Mheshimiwa Spika, katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na biashara nchini, Serikali imeanzisha programu ya *BEST.* Programu hii ni ya miaka mitano ambayo itaanza kutekelezwa katika mwaka huu wa fedha. Programu hii itaendeshwa na Serikali ikishirikiana na Serikali za Denmark, Uholanzi, Sweden na Uingereza na utekelezaji wake utakuwa katika awamu tatu.

Mheshimiwa Spika, shughuli za awamu ya kwanza ambazo zitatekelezwa katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, ni pamoja na kuanzisha na kuendesha kitengo cha *Better Regulation Unit (BRU)* katika Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na kukijengea uwezo imara wa kufanya kazi pamoja na kufanya tafiti mbalimbali zitakazolenga katika kuondoa vikwazo vya uendeshaji biashara na uwekezaji nchini.

Mheshimiwa Spika, lengo la programu ya *BEST* ni uboreshaji wa sera, sheria, taratibu, utawala bora na kuimarisha vyombo na taasisi mbalimbali hususan kituo cha Uwekezaji *(TIC), (BRELA)* na Mahakama ya Biashara. Programu hii itabainisha na kuchambua sheria, taratibu na biashara zilizopitwa wakati na kuzihuisha ili zitungwe upya au kufanyiwa marekebisho. Shughuli nyingine ni kuongeza ufanisi katika utatuzi wa migogoro ya kibiashara na kuboresha utendaji na utoaji huduma za Serikali katika sekta binafsi. Nia ni kuondoa vikwazo na kasoro ambazo ni kero kwa wawekezaji na wafanyabiashara hapa nchini na kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma za Serikali na kujenga uwezo wa sekta binafsi kubainisha matatizo yake, kuyachambua na kutafuta ufumbuzi wa haraka.

Mheshimiwa Spika, zoezi la kurekebisha na kubinafsisha Mashirika ya Umma katika kipindi cha miaka 10 iliyopita linaendelea vizuri kwa kubinafsisha jumla ya Mashirika 266 yakijumuisha Mashirika 47

yaliyopelekwa kitengo cha kukusanya madeni *(LART).* Juhudi kubwa katika zoezi hili zimeelekezwa zaidi katika kukamilisha awamu ya pili ya ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma ifikapo Desemba, 2004 ambapo mkazo mkubwa umeelekezwa katika ubinafishaji kwa njia ya ukodishaji na urekebishaji wa Mashirika ya miundombinu na huduma.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002/2003, Mashirika makubwa yaliyoweza kupata wawekezaji ni *DAWASA* kwa njia ya kukodisha, Shirika la Ndege la Tanzania *(ATC)* kwa kuuza hisa asilimia 49 na Mashirika mengine madogo 9 yaliyobinafishwa kwa njia ya kuuza hisa au mali. Hivyo hivyo, jitihada zilielekezwa katika kuandaa mikakati ya kuweza kuwapata wawekezaji katika Mashirika makubwa yakiwemo *TANESCO,* Shirika la Bima la Taifa *(NIC), National Microfinance Bank (NMB)* na *Tanzania Harbours Authority (THA)* kwa vitengo vilivyosalia na Shirika la Reli la Tanzania *(TRC)* baada ya kushindwa kupata mkodishaji katika kipindi cha mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, katika kuweka mazingira mazuri ya kupata wawekezaji na kulinda maslahi ya Taifa na walaji katika Mashirika ya huduma na ya miundombinu, Serikali imechukua hatua ya kuanzisha mamlaka nne za udhibiti *(Regulatory Authorities)* ambazo zitasimamia sekta za Usafiri wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA),* Nishati na Maji *(EWURA),* Mawasiliano na Utangazaji *(TCRA)* na Usafiri wa Anga *(TCAA).*

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubinafsishaji wa mashamba makubwa ya kilimo na mifugo na Ranchi za Taifa, kazi ya awali imeshaanza katika kushirikisha viongozi na wataalam wa Mikoa na Wilaya husika katika Mikoa ya Rukwa, Mbeya na Kagera. Aidha, kazi ya kupima upya mashamba mbalimbali yaliyopo Mikoani inaendelea kwa kishirikiana na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi ili kuwasaidia wakulima na wafugaji wadogo wadogo waweze kupata ardhi kwa lengo la kuitumia kwa faida na kuleta maendeleo kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, katika kufuatilia Mashirika yaliyobinafsishwa mbali na ufuatiliaji uliofanywa na vitengo vya Wizara husika, Waheshimiwa Wabunge ambao ni wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi na Kamati ya Mitaji na Mashirika ya Umma waliweza kutembelea Mashirika ya Umma katika Mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Morogoro, Iringa na Mbeya na kuona mafanikio na matatizo yaliyopo katika Mashirika hayo na kutoa ushauri wa kushirikiana na wawekezaji waliopo ili kuongeza ufanisi zaidi kwa Mashirika hayo. Tutaendelea kuzingatia ushauri na maoni wa Waheshimiwa Wabunge, katika kutekeleza sera na kusimamia zoezi la ubinafsishaji na urekebishaji wa Mashirika ya Umma pamoja na ufuatiliaji wa Mashirika yaliyobinafsishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2003/2004, kwa kushirikiana na wadau mbalimbali tutaendelea na urekebishaji na ubinafsishaji wa Mashirika makubwa ya huduma na miundombinu, mashamba makubwa ya kilimo na mifugo pamoja na ufuatiliaji wa mwenendo wa utekelezaji wa Mashirika yaliyokwisha binafsishwa ili kuhakikisha wawekezaji wanazingatia masharti ya mikataba ya ubinafsishaji kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi kwa Mashirika hayo. Katika jitihada za kuwaendeleza watumishi zoezi la kuhuisha mpango wa mafunzo ya muda mfupi na mrefu wa kuinua viwango vya ujuzi na kuboresha utendaji wa kazi wa watumishi lilikamilika. Watumishi 15 walipata nafasi za kuhudhuria mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi yaliyowawezesha kujiongezea ujuzi katika fani zao.

Kwa upande mwingine, Ofisi kwa kushirikiana na Taasisi ya Kuzuia Rushwa nchini *(PCB)* pamoja na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, iliendesha semina nne kuhusu mapambano ya kuzuia rushwa ambapo washiriki 302 wote wakiwa ni watumishi wa Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji pamoja na asasi zilizo chini yake walihudhuria. Pia, Ofisi kwa kushirikiana na Tume ya Kudhibiti Ukimwi *(TACAIDS)* iliendesha semina moja iliyohudhuriwa na watumishi 104 ambapo walipata fursa ya kujifunza mbinu mbalimbali za kupambana na janga la Ukimwi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2003/2004, jitihada zitaelekezwa katika kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi, kusimamia na kulinda haki za watumishi ili waweze kufanya kazi kwa juhudi na maarifa kwa kuzingatia uwezo mkubwa walionao.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya utekelezaji wa mwaka 2002/2003 pamoja na mwelekeo kwa mwaka 2003/2004, sasa ningependa kuchukua fursa hii kuainisha kwa muhtasari maeneo ambayo

Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, pamoja na asasi zake itayapa kipaumbele katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, kuendelea kuboresha shughuli za ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa takwimu na taarifa za masuala ya kiuchumi na kijamii, kukamilisha maandalizi ya Mpango wa Muda wa Kati *(Medium Term Plan)* pamoja na kuratibu matayarisho ya ratiba ya utekelezaji *(Medium Term Action Plan),*kuendelea na juhudi za kuelimisha wananchi kuhusu Dira ya Maendeleo ya Taifa, 2025, kuendelea na zoezi la Urekebishaji na ubinafishaji wa Mashirika yaliyobaki na kuboresha ufuatiliaji wa utendaji wa Mashirika yaliyobinafsisha, ili kubaini mafanikio na matatizo wanayoyapata wawekezaji na wadau wengine katika Mashirika hayo na kutoa ushauri pamoja na kubuni au kuboresha mikakati na kuendelea na uchambuzi wa takwimu za sensa na kusambaza matokeo kwa wadau na wananchi kwa jumla kupitia vyombo mbalimbali vya habari pamoja na kutumia Tovuti ya Taifa.

Pia kubaini na kuchambua fursa za kukuza uchumi katika sekta mbalimbali na kupendekeza vipaumbele katika matumizi ya raslimali za taifa, pamoja na kuendelea kutoa ushauri kwa Serikali juu ya mikakati ya kukuza uchumi na kuweka vigezo vya kupima mafanikio ya kila sekta, kuendelea kuboresha na kuimarisha ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu na taarifa mbalimbali ambazo hutumika katika kuandaa Pato la Taifa na Fahirisi ya Bei, kuendelea kushirikiana na Mikoa na Wilaya katika kubaini fursa na vivutio na kuandaa taarifa za hali ya uchumi na kijamii kwa Mikoa na Wilaya kwa lengo la kutoa taarifa na takwimu za kusaidia katika kuwavutia wawekezaji, kuendelea na juhudi za kutathmini fursa na changamoto zinazokabili sekta ya nje kwa lengo la kuboresha mikakati ya kiuchumi na biashara ya nje na ushirikishwaji wa kiuchumi wa Kimataifa na kuendelea kushirikiana na wadau wengine katika kuendeleza uingizaji wa masuala ya jinsia katika sera na mipango ya maendeleo.

Baada ya maelezo hayo, naomba sasa Bunge lako liidhinishe jumla ya shilingi 24,881,718,700/= ambazo zinaombwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji pamoja na asasi mbalimbali zilizo chini yake. Kati ya fedha hizo shilingi 8,181,637,000/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 16,700,081,700/= kwa Matumizi ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2003/2004**
**Wizara ya Fedha**

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Fedha na Uchumi iliyowasilishwa hapa Bungeni, leo, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako sasa likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya kawaida na ya maendeleo ya Wizara ya Fedha kwa mwaka wa Fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati zote za Kudumu za Bunge kwa uchambuzi wao wa kina wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara, Idara na Mikoa kwa mwaka 2003/2004. Napenda kuwathibitishia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa Wizara ya Fedha itazingatia ushauri wao, ili kuboresha usimamizi wa mapato na matumizi ya Wizara na Serikali kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)* na ile ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* zinategemewa kuendelea kupitia Hesabu za mwaka 2000/2001 mara baada ya kikao hiki cha Bunge. Wizara yangu itaendelea kusaidia Kamati hizi ili ziweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Fedha kama Wizara kiungo, inalo jukumu la kusimamia ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali kulingana na sheria, kanuni na taratibu za fedha. Kwa hiyo, Wizara imeendelea kuimarisha kazi ya kukusanya mapato chini ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* pamoja na yale yanayokusanywa na Wizara na Idara.

Aidha, mfumo wa Bajeti na uhasibu umeimarishwa kwa kuelimisha wadau wote kuhusu mtandao wa kompyuta pamoja na Sheria za Fedha na Ununuzi. Kwa kuzinagatia majukumu hayo, ninaomba sasa kutoa taarifa ya utekelezaji kwa mwaka 2002/2003, pamoja na malengo ya mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Mikoa yote imeanza kuandaa Bajeti zao kwa mfumo wa *MTEF* kuanzia mwaka 2003/2004.

Wizara yangu ilichukua hatua mbalimbali kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa lengo la kuhakikisha kuwa miradi hiyo inatekelezwa kama ilivyokusudiwa. Hatua hizo ni pamoja na kukagua miradi inayotekelezwa na Wizara, Mikoa na Halmashauri katika sekta muhimu za afya, elimu, kilimo, maji na barabara pamoja na ile iliyoko chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto na Idara za Polisi na Magereza.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendelea kufuatilia matumizi ya fedha za Serikali *(Expenditure Tracking)* katika mwaka wa 2003/2004 ili kuhakikisha kuwa fedha zinatumika kwa madhumuni yaliyoidhinishwa tu.

Aidha, Wizara itaaandaa vigezo vya kupima utekelezaji wa Bajeti *(Performance Indicators)* kwa Wizara, Idara na Mikoa. Hatua hii itasaidia kufanya tathmini ya utekelezaji wa Bajeti. Vile vile, Wizara itaendelea kutoa taarifa kwenye vyombo vya habari kuhusu fedha zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya kutekeleza miradi na kutoa huduma mbalimbali kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, hatua hii inalenga kuongeza uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma. Napenda kusisitiza umuhimu wa Wizara, Mikoa, Wilaya na Halmashauri kutangaza mgao wa fedha hizo kwa wananchi katika maeneo yao kama Waraka wa Hazina unavyohitaji.

Mheshimiwa Spika, sera na mikakati ya kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Serikali zimeelezwa kwenye Hotuba ya Bajeti ya Serikali niliyowasilisha tarehe 12 Juni, 2003. Kwa ujumla, ukusanyaji wa mapato kwa mwaka wa 2002/2003 unaridhisha. Hadi tarehe 30 Juni, 2003 kiasi cha mapato yaliyokusanywa kilifikia shilingi bilioni 1,217.5, ikiwa ni zaidi ya lengo kwa asilimia 4.

Mheshimiwa Spika, aidha, kiasi kilichokusanywa kinazidi makusanyo ya mwaka 2001/2002 kwa kiasi cha shilingi bilioni 174.57. Vyanzo vya mapato ambavyo vimevuka malengo ni pamoja na kodi ya mapato ya ongezeko la thamani na mapato yasiyokuwa ya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2003/2004, Serikali inalenga kukusanya jumla ya shilingi bilioni 1,393. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 1,280.7 ni mapato ya kodi yatakayokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania, shilingi bilioni 24.9 ni mapato yasiyo ya kodi yatakayokusanywa na Wizara ya Fedha na kiasi kilichobaki cha shilingi bilioni 87. 4 kitakusanywa na Wizara na Idara za Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* imetayarisha Mpango wa miaka mitano ambao unasisitiza mambo yafuatayo:-

(a) Kutoa huduma zote za kodi kwa walipakodi katika Ofisi zote za Mamlaka Wilayani. Chini ya mpango huu utakaokamilika ifikapo Januari 2004, Ofisi zote za Mamlaka za Wilaya zitakuwa ni *One-Stop-Centres* zenye kutoa huduma zote za kodi isipokuwa za Forodha, tofauti na hivi sasa ambapo ni Wilaya chache tu zinapata huduma hizo.

(b) Kuimarisha Idara ya Walipa kodi wakubwa kwa lengo la kuboresha taaluma, mifumo na taratibu za kazi na uwajibikaji. Aidha, idadi ya walipakodi wakubwa wanaohudumiwa na Idara hii inategemewa kuongezeka kutoka 100 wa sasa hadi 200 ifikapo Julai, 2004.

(c) Kuandaa na kutangaza Mkataba wa huduma kwa walipakodi *(Taxpayers' Charter)*. Kwa kupitia mkataba huo, walipakodi watafahamishwa haki na wajibu wao na pia haki na wajibu wa Mamlaka

kutokana na Sheria za Kodi. Lengo la Mamlaka katika kuandaa mkataba huu ni kuweka wazi matarajio ya kila mmoja.

(d) Kupitia kwa kina Sheria zote za kodi kwa lengo la kuainisha mapungufu yaliyopo na kuzifanyia marekebisho.

Mheshimiwa Spika, kutokana na utekelezaji wa sera nzuri za kusimamia uchumi pamoja na za mapato na matumizi ya Serikali, Tanzania imeendelea kupata misaada na mikopo kutoka nchi wahisani na asasi za fedha za Kimataifa.

Katika mwaka 2002/2003, Serikali imepata misaada na mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1,179.6 ikiwa ni zaidi ya lengo kwa asilimia 19. Kwa kutumia Mkakati wa Misaada Tanzania *(Tanzania Assistance Strategy - TAS),* Wizara ya Fedha inaendelea kujadiliana na wahisani wetu ili watumie mfumo wa uhasibu na malipo wa Serikali *(Exchequer System).* Hadi sasa, karibu misaada yote ya Bajeti *(Programme/Budget Support* na *Basket Funds)* inatolewa kwa kutumia mfumo wa Bajeti na uhasibu wa Serikali, wakati ni asilimia 50 tu ya misaada ya miradi inatolewa kupitia mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, 2002 hadi Juni, 2003, hatua kadhaa zimetekelezwa katika mkakati wa madeni. Sheria Na. 30 ya 1974 ya Mikopo, Dhamana na Misaada *(The Government Loans, Guarantees and Grants Act No. 30 of 1974)* imerekebishwa na Muswada wa Marekebisho ya Sheria hiyo umepitishwa na Bunge la mwezi Aprili, 2003. Pamoja na mambo mengine muhimu katika marekebisho ya Sheria hiyo ni yale yanayompa Waziri wa Fedha pekee mamlaka ya kukopa, kutoa dhamana na kupokea misaada. Marekebisho pia yanazingatia Sheria mpya ya Fedha *(Public Finance Act)* pamoja na Sheria nyingine za Asasi za Umma ambazo zingeweza kugongana ili kuondoa mianya ya kukopa kiholela.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Usimamiaji Mikopo, Dhamana na Misaada *(National Debt Management Committee - NDMC)* imeundwa kutokana na marekebisho ya Sheria Na. 30 ya mwaka 1974 kuhusu Mikopo, Dhamana na Misaada. Wajumbe wa Kamati ni Katibu Mkuu Hazina (Mwenyekiti), Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Uchumi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais (Mipango na Ubinafsishaji), Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Katibu Mkuu Mambo ya Nchi za Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, majukumu makubwa ya Kamati ya Udhibiti Madeni, yatakuwa ni kumshauri Waziri wa Fedha juu ya masuala yote yanayohusiana na mikopo, dhamana na misaada. Chini ya Kamati hiyo, ipo Kamati ya Wataalam *(Technical Debt Management Committee - TDMC),* ambayo imepewa uwezo Kisheria wa kutoa ushauri wa kitaalam kwa Kamati ya Kudhibiti Madeni. Ili kufikia malengo ya utekelezaji wa Sheria hii, Kanuni zimetayarishwa. Kutokana na marekebisho ya sheria hii, utaratibu wa kuomba mikopo, dhamana na misaada umebadilika na maombi yote yatawasilishwa kwa Katibu Mkuu wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, Mtandao wa Usimamizi wa Fedha na Malipo *(IFMS)* utaendelea kuimarishwa ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wadau wote. Maafisa Wahasibu wote tayari wamepatiwa mafunzo ya awali kuhusu mtandao huo. Aidha, Wizara yangu tayari imekwishaweka mtandao wa *IFMS* kwa Maafisa Wahasibu wote katika Wizara na Idara zinazojitegemea. Tunategemea kufanya hivyo hivyo kwa Makatibu Tawala wa Mikoa ili kuimarisha usimamizi wa fedha wanazopewa.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Usimamizi wa Fedha na Malipo kwa kutumia Kompyuta umekuwa maarufu siyo hapa nchini tu bali hata nchi za nje. Wizara ya Fedha imekuwa ikipata maombi kutoka nchi na asasi mbalimbali kutaka kufahamu na kujifunza jinsi tulivyoweza kumudu na kusimamia kwa umakini mtandao huo. Nchi kadhaa zimetuma Wajumbe kuja kujifunza namna ya kuendesha mfumo huo wa malipo.

Mheshimiwa Spika, nchi hizo ni pamoja na Kenya, Eritrea, Ethiopia, Malawi, Msumbiji, Namibia na Zambia. Pia, tumepata maombi mengine toka nchi za Ghana, Lesotho na Swaziland ambazo Wajumbe wake wanatarajia kuja hivi karibuni. Matumizi ya *IFMS* yameisaidia Serikali kuandaa

hesabu kwa wakati, kutayarisha Bajeti na kufichua kwa haraka njama zinazotumiwa na Wahasibu wasio waaminifu kuiba fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Wizara itatayarisha sehemu maalum ya mtandao huo kwa ajili ya tahadhari *(Disaster Recovery Site)* ili kuepukana na majanga yanayoweza kuathiri mtandao wa malipo na kumbukumbu husika. Aidha, Ofisi za Hazina Ndogo zitapatiwa jenereta ili kupunguza adha kwa watumiaji pale matatizo ya umeme yatakapojitokeza.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa kunakuwa na uwajibikaji katika matumizi na mapato ya fedha za Serikali, Wizara yangu imeandaa na kukamilisha miongozo ya Uhasibu na Ukaguzi wa Ndani Serikalini *(Government Accounting and Audit Manuals).* Miongozo hiyo inahusu Wizara na Idara za Serikali, Hazina Ndogo na Ukaguzi wa Ndani. Wizara itaendesha mafunzo mwaka 2003/2004 ili kuhakikisha kuwa walengwa wanaielewa vizuri miongozo hiyo kwa nia ya kuboresha uhasibu na ukaguzi wa ndani.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeanza kuboresha Sheria ya Fedha ya mwaka 2001 kwa lengo la kuondoa vipengele vya kanuni vinavyosababisha kero kiutekelezaji. Katika mwaka wa fedha 2002/2003 Wizara katika azma yake ya kuhakikisha ufanisi katika kutunza Hesabu za Serikali, imeandaa na kukamilisha Mwongozo wa Utayarishaji wa Hesabu za Serikali, ambao unawaelekeza Maafisa Wahasibu namna bora ya utunzaji wa hesabu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kutoa miongozo na nyaraka mbalimbali kwa Maafisa Wahasibu wa Wizara, Mikoa na Idara za Serikali. Kufuatia hatua hizo, pamoja na matumizi ya hati za kuagizia vifaa *(LPO)* itolewayo na Mtandao wa Kompyuta, Serikali imeweza kwa kiasi kikubwa, kudhibiti deni la wazabuni hasa wa ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla kazi za ununuzi zimeendelea kuathiriwa na uwezo mdogo wa kutekeleza Sheria Na. 3 ya 2001 ya Ununuzi katika Sekta ya Umma.

Katika mwaka wa fedha 2002/2003, Halmashauri Kuu ya *Tender* iliidhinisha zabuni 51 zenye thamani ya shilingi bilioni 1,245.4. Aidha, Halmashauri Kuu ya *Tender* imetayarisha nyaraka mbalimbali za zabuni *(Standard Bidding Documents)* ili kufanikisha kazi za ununuzi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki ya Dunia na Serikali ya Uingereza imefanya tathmini ya kitaalam juu ya mfumo wa Ununuzi katika Sekta ya Umma *(Public Procurement)* mwaka 2002/2003. Kwa ujumla, tathmini hii inaonyesha kuwa Sheria Na. 3 ya mwaka 2001 ya Ununuzi katika Sekta ya Umma inakidhi vigezo muhimu vya Kimataifa isipokuwa katika maeneo yafuatayo:-

(a) Halmashauri Kuu ya *Tender (Central Tender Board)* kuwa na majukumu ya kiutendaji (kuidhinisha zabuni) na usimamizi wa Sheria. Hali hii inapingana na dhana ya utawala bora na uwajibikaji.

(b) Baadhi ya Asasi zinazotumia fedha za Umma kutohusishwa na Sheria hii.

(c) Sheria haiko wazi katika ushirikishwaji wa sekta binafsi katika Mamlaka ya Rufaa za Zabuni.

Mheshimiwa Spika, tathmini iliyofanywa imeainisha pia mapungufu ya utekelezaji yanayotokana na ukosefu wa wataalam wenye elimu, ujuzi na uzoefu wa kutekeleza kazi za ununuzi kwa kuzingatia Sheria Na. 3 ya 2001. Upungufu huo unaathiri sana kazi za ununuzi na hatimaye utekelezaji wa miradi na utoaji wa huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kuongeza ufanisi kwenye ununuzi katika Sekta ya Umma, katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu imepanga kuanza kutekeleza baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa kwenye tathmini iliyofanywa mwaka 2002/2003. Baadhi ya hatua zitakazochukliwa ni pamoja na:-

(a) Kuendelea kutoa mafunzo *(Capacity Building)* kwa watumishi wanaofanya kazi ya ununuzi.

(b) Kufuatilia na kukagua kazi za ununuzi.

(c) Kuongeza mamlaka za bodi za zabuni za Wizara, Idara, Mikoa na Asasi katika kufanya maamuzi ya zabuni. Hatua hii itapunguza idadi ya zabuni zinazofanyiwa maamuzi na Halmashauri Kuu ya *Tender* na hivyo kuongeza ufanisi na uwajibikaji.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali yameainishwa katika Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Na. 6 ya 2001. Majukumu hayo ni pamoja na kukagua hesabu za Wilaya, Idara za Serikali, Mikoa, Halmashauri za Wilaya, Jiji na Miji, Ofisi za Ubalozi za Tanzania, Wakala wa Serikali, Mamlaka ya Mapato Tanzania pamoja na Miradi inayogharamiwa na wafadhili na kutoa taarifa za ukaguzi huo Bungeni. Katika mwaka 2002/2003 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iliweza kukagua hesabu 47 za Wizara na Idara za Serikali, 20 za Mikoa, 117 za Halmashauri, 10 za Ofisi za Balozi za Tanzania pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Aidha, Ofisi hiyo ilidhamini mafunzo katika fani mbalimbali kwa watumishi wake 168 ili kuwaongezea ujuzi na uwezo wa kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Ofisi hii imepanga kukagua hesabu 47 za Wizara na Idara za Serikali, 21 za Mikoa na 117 za Halmashauri, 10 za Ofisi za Balozi pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania. Ofisi pia, itaendelea kudhamini mafunzo kwa watumishi 49 katika vyuo mbalimbali hapa nchini na nje ya nchi na kuendesha mafunzo ya ndani kwa watumishi wa ngazi mbalimbali ili kuboresha utendaji. Kwa msaada kutoka Serikali ya Sweden, Ofisi hiyo itaendesha mafunzo kwa vitendo na nadharia kwa watumishi wake. Lengo ni kuanzisha mfumo wa ukaguzi wa hesabu kwa kutumia kompyuta *(computerised audits)* katika Ofisi hiyo na kufanya kaguzi za *value for money.*

Mheshimiwa Spika, ili kuharakisha uanzishaji wa kaguzi hizo, vitengo maalum vitaanzishwa chini ya usimamizi wa wataalam watakaoajiriwa chini ya msaada huo. Aidha, kitaanzishwa kitengo cha ushauri na utafiti ili Ofisi iweze kwenda na mabadiliko ya ukaguzi, teknolojia na utendaji kazi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara yangu iliendelea na majukumu ya kuhakiki Bohari; kusimamia uundaji wa Bodi za Ukaguzi *(Annual Boards of Survey),* kushiriki katika kufuta au kuuza mali na vifaa chakavu na sinzia na kuendesha zoezi la uthamini wa mali ya Serikali. Hadi Juni, 2003 jumla ya bohari 400 za Serikali zilikuwa zimehakikiwa na taarifa za ukaguzi kutolewa. Katika kipindi hicho, Wizara yangu ilisimamia kuundwa kwa Bodi za Ukaguzi 37 zikijumuisha 19 za Wizara, 3 za Idara na 15 za Mikoa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Wizara yangu inalenga kuhakiki bohari 500 za Wizara, Idara na Mikoa, uondoshaji wa vifaa sinzia na chakavu ambapo magari, pikipiki na mitambo chakavu itafutwa au kuuzwa, kuthamini mali za Serikali katika Wizara za Afya, Elimu na Utamaduni, Mambo ya Ndani, Maliasili na Utalii na Wizara ya Fedha. Kazi ya kuorodhesha mali hizo imekamilika katika Wizara 4 na taratibu za kuitisha zabuni ya kumpata mthamini zimekamilika, kusimamia uundaji wa Bodi za Mwaka za Ukaguzi wa Bohari *(Annual Boards of Survey)* kwa mafungu yote kabla ya Desemba, 2003 na kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya Bodi za Ukaguzi *(Boards of Survey)* zilizoteuliwa mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara yangu kwa kushirikiana na Idara Kuu ya Utumishi iliendelea kuboresha mfumo na huduma za kompyuta. Hatua hii imesaidia Serikali kulipa mishahara ya watumishi wake kwa wakati. Aidha, katika mwaka wa fedha wa 2003/2004, Wizara yangu kwa kushirikiana na wadau wengine itaweka mkazo katika kutumia kompyuta ili kutunza kumbukumbu za watumishi, kulipa mishahara ya watumishi kwa wakati na kupunguza kero.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Bodi ya Rufani za Kodi ilipokea rufaa 46 za Kodi ya Mapato na kati ya hizo 39 zilisikilizwa na kutolewa maamuzi. Rufaa 14 za Kodi ya Ushuru wa Forodha zilifunguliwa na kati ya hizo 11 zilisikilizwa na kutolewa maamuzi. Rufaa 15 za Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* zilifunguliwa na kati ya hizo 13 zilisilikilizwa na kutolewa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Bodi itaendelea kusikiliza rufaa zote pamoja na maombi ambayo yatakuwa yamefunguliwa. Zoezi la kuelimisha wadau kuhusu majukumu ya Bodi katika Mikoa na Wilaya litaendelea. Kwa upande wa Baraza la Rufani za Kodi, mwaka 2002/2003, rufaa 15 zilipokelewa ambapo 10 zilisikilizwa na kutolewa maamuzi. Serikali itaendelea kuchukua hatua za kuimarisha Bodi na Baraza ili viweze kutoa huduma hiyo kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara yangu iliendelea kushughulikia maslahi ya watumishi ili kuhakikisha kuwepo watumishi wenye sifa zinazotakiwa, wenye ari na uwezo wa kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Katika kufanikisha lengo hilo, watumishi 355 walipatiwa mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi; watumishi 270 walipandishwa vyeo, 40 walithibitishwa kazini na 144 waliajiriwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inaendelea kuimarisha utendaji kazi wa kada za Uhasibu na Ukaguzi wa Ndani wa Hesabu. Hadi kufikia mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara yangu ilikuwa imetoa mafunzo kwa watumishi 192, kati yao watumishi 74 walipata mafunzo ya Shahada ya Juu ya Uhasibu *(CPA)* na watumishi 118 wanaendelea kupata mafunzo ya Stashahada ya Uhasibu.

Katika mwaka 2003/2004, Wizara inatarajia kudhamini mafunzo kwa watumishi 419 wa Serikali za Mitaa na Serikali Kuu. Kati ya watumishi hao, watumishi 184 wanatarajia kupata mafunzo ya Shahada ya Juu ya Uhasibu *(CPA),* 200 Stashahada ya Uhasibu na 27 Teknolojia ya Habari. Aidha, watumishi 6 wanatarajiwa kuchukua mafunzo ya Uboharia na watumishi 2 Shahada ya Pili ya Fedha *(Master in Finance).*

Kwa ufupi, hadi mwisho wa mwaka huu wa fedha Wizara yangu itakuwa imegharamia mafunzo kwa watumishi 611: Kati ya hao 117 ni wanawake na 494 ni wanaume. Wizara pia, inaendelea kutoa mafunzo ya kompyuta kwa watumishi wake wote ili waweze kutumia teknolojia hiyo ya kisasa. Juhudi hizi zinalenga kuboresha hali ya utunzaji wa fedha na uhasibu Serikalini. Mategemeo yetu ni kuwa wale watumishi walioko vyuoni ambao watamaliza mafunzo yao mwishoni mwa mwaka 2003/2004 watakaporejea kazini, hali ya utendaji kazi itabadilika na kuwa bora zaidi. Hata hivyo, Wizara yangu inatambua tatizo la mishahara duni ambalo linaathiri sana utendaji kazi wa wahasibu na wakaguzi. Serikali itaendelea kulifanyia kazi tatizo hili ili kuongeza tija na ufanisi.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kuathirika kiutendaji na ugonjwa hatari wa Ukimwi na hivyo kuathiri utendaji wa kazi kutokana na kuugua na vifo. Kwa kuzingatia hilo, kwa mwaka 2003/2004, Wizara yangu inakusudia kufanya tathmini ili kujua wastani wa watumishi wanaoishi na virusi vya Ukimwi, ili kuweka mkakati wa kupambana na usambaaji wa virusi hivi hatari. Tathmini hiyo pia italenga katika kuwasaidia watumishi kuweza kuishi kwa matumaini kwa kuwapa misaada itakayowasaidia kudumisha afya zao kadri hali ya fedha itakavyoruhusu.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kuboresha huduma za pensheni kwa Wastaafu kwa kuimarisha uwekaji wa kumbukumbu za wastaafu zilizo sahihi na timilifu. Pamoja na jitihada hizo, Wizara inatambua kuwa matatizo yanayowakabili wastaafu yanayotokana na viwango vidogo vya pensheni wanazolipwa kila mwezi au baada ya miezi sita. Hali yetu ya uchumi kwa sasa hairuhusu kukidhi matarajio na mahitaji halisi ya pensheni za wastaafu.

Hata hivyo, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Serikali imeongeza kima cha chini cha pensheni kutoka shilingi 13,385 hadi kufikia shilingi 20,077. Aidha, kutokana na ongezeko hilo, kuanzia mwaka wa fedha 2003/2004 malipo ya pensheni ya mkupuo, ambayo hutolewa kwa wale wapatao chini ya shilingi 20,000 haitakuwepo. Wakati huo huo, Serikali inayafanyia kazi maombi ya wastaafu waliolipwa pensheni zao kwa mkupuo kwa lengo la kuangalia uwezekano wa kuwarejesha kwenye malipo wakati muafaka.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Wizara yangu imelipa wastaafu mbalimbali wakiwemo wanajeshi 1,094, walimu 40 na watumishi wengine 790 kwa jumla ya shilingi bilioni 12.36. Wizara imelipa madai ya mirathi 1,606 yenye thamani ya shilingi bilioni 4.99. Pia, wastaafu 173 waliomba na kulipwa pensheni zao kwa mkupuo zenye thamani ya shilingi bilioni 2.75. Aidha, wastaafu 34,764 wamelipwa pensheni za mwezi zenye thamani ya shilingi bilioni 10.67 kwa utaratibu wa malipo ya kila baada ya miezi sita.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma *(PSPF)* unaendelea na zoezi la kusajili, kuhakiki na kuingiza kumbukumbu za wanachama kwenye mtandao wa kompyuta ili kurahisisha malipo ya wastaafu katika muda mfupo. Idadi ya wanachama waliosajiliwa hadi mwezi Juni, 2003 imefikia 140,330 sawa na asilimia 72 ya wanachama wote wa mfuko. Zoezi hili linatarajiwa kumalizika mwaka huu wa fedha. Aidha, zoezi la kuingiza kumbukumbu za wanachama kwenye mtandao wa kompyuta za wanachama kwenye mtandao wa kompyuta unaolenga kurahisisha rejea linaendelea vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza malengo ya Mfuko kwa mwaka 2002/2003, kiasi cha shilingi bilioni 60.1 zilikusanywa kutokana na vyanzo mbalimbali. Kiasi hicho kinajumuisha shilingi bilioni 51.68 za michango ya wanachama na shilingi bilioni 8.42 mapato kutokana na vitega uchumi mbalimbali. Thamani ya Mfuko imeongezeka kutoka shilingi bilioni 134.4 mwaka 2001/2002 hadi kufikia shilingi bilioni 192.6 mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2003/2004, Mfuko unatarajiwa kuendelea kuelimisha wanachama wake kuhusu kazi za Mfuko, kufanya maandalizi muhimu kwa ajili ya kuanza malipo ya wastaafu kwa mwaka 2004/2005, kukamilisha zoezi la kutathmini Mfuko kulinganisha na majukumu yake kifedha *(Actuarial Valuation).* Aidha, Mfuko unatarajiwa kukusanya shilingi bilioni 55.89 kutokana na michango ya wanachama ya mapato ya shilingi bilioni 12.14 kutokana na vitega uchumi mbalimbali. Matarajio ya malengo hayo ni kuongeza thamani ya Mfuko kutoka shilingi bilioni 192.6 hadi kufikia shilingi bilioni 257.32 ifikapo Juni, 2004.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma *(PPF)* katika mwaka 2002, uliweza kukusanya shilingi bilioni 45.1. Hili ni ongezeko la asilimia 9 ukilinganisha na makusanyo ya shilingi bilioni 41.5 mwaka 2001. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa michango ya wanachama kutoka shilingi bilioni 31.5 mwaka 2001 hadi shilingi bilioni 35.6 mwaka 2002. Aidha, mapato yatokanayo na uwekezaji yaliongezeka kutoka shilingi bilioni 7.19 mwaka 2001 hadi shilingi bilioni 7.25 mwaka 2002. Mfuko umelipa mafao kiasi cha shilingi bilioni 14.3 mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, thamani ya Mfuko imeongezeka kwa asilimia 20 kutoka shilingi bilioni 107 mwaka 2001 hadi shilingi bilioni 128 mwaka 2002. Ongezeko hilo limesababishwa na kuongezeka kwa michango na faida kutokana na uwekezaji. Katika mwaka 2003, Mfuko unatarajiwa kukusanya shilingi bilioni 44. Mapato yatokanayo na uwekezaji yanatarajiwa kuongezeka kwa asilimia 15 kutoka shilingi bilioni 7.25 mwaka 2002 hadi kufikia shilingi bilioni 8.2 mwaka 2003. Mfuko unategemea kupanua wigo wa wanachama kwa kuandikisha wanachama wapya 5,000 kutoka katika sekta binafsi na ile isiyo rasmi kwa mujibu wa marekebisho ya sheria ya *PPF* yaliyofanywa na Bunge mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2002, Sekta ya fedha na bima ilikuwa kwa asilimia 4.0 ikilinganishwa na asilimia 1.8 mwaka uliopita. Hata hivyo, pamoja na ukuaji wa sekta hii, mchango wake katika Pato la Taifa kwa mwaka 2002 ulipungua kidogo hadi asilimia 10 kutoka asilimia 10.2 mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua matatizo wanayoyapata wafanyabiashara wadogo wadogo katika kupata mtaji kwa ajili ya shughuli zao. Kwa kutambua hilo, Serikali imeanzisha Mfuko wa Udhamini kwa wakopaji wadogo wenye shughuli za kiuchumi na kibiashara.

Mheshimiwa Spika, miaka ya hivi karibuni tumeshuhudia ongezeko la idadi ya Mabenki. Hadi sasa kuna Mabenki 20 yaliyoandikishwa na asasi zisizo za kibenki na maduka ya fedha za kigeni 63. Ukuaji huo kwa mwaka 2002 ulitokana na kufunguliwa kwa Benki mpya za biashara ambazo ni *United Bank of Africa (UBA), CF Union Bank, African Banking Corporation,* pamoja na baadhi ya Mabenki kufungua matawi yake sehemu mbalimbali nchini. Pamoja na ongezeko hilo la Mabenki, Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Benki Kuu imeendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa Mabenki hapa nchini. Idara husika katika Benki Kuu inaimarishwa zaidi kwa kuipa vitendea kazi na mafunzo kwa watumishi wake.

Mheshimiwa Spika, matatizo ambayo yanasababisha kutokuwepo na uwiano wa juu zaidi wa mikopo na amana ni pamoja na kuwepo kwa tofauti kubwa kati ya riba za amana na zile za mikopo. Hali

hii inachangiwa na uduni wa miundombinu ya kiuchumi, mfumo wa sheria usiolinda haki za wanaotoa mikopo na wakopaji kushindwa kutumia hati za ardhi kudhamini mikopo. Hata hivyo, kufuatia jitihada za Serikali katika kuboresha mazingira ya uwekezaji, riba za mikopo kwa ujumla zimekuwa zikishuka kutoka asilimia 18.1 mwezi Desemba, 2001 hadi kufikia asilimia 15.7 mwezi Desemba, 2002 na asilimia 14.1 mwezi Juni 2003.

Aidha, riba za amana zilishuka kutoka asilimia 3.6 mwezi Desemba 2001 na kufikia asilimia 2.7 mwezi Desemba, 2002 na asilimia 2.5 mwezi Juni, 2003. Serikali inakusudia kuleta Muswada Bunge lijalo kwa lengo la kuzifanya Benki zitoe riba nzuri zaidi kwa wakopaji na wawekaji amana.

Mheshimiwa Spika, mpango wa kutoa dhamana kwa mikopo kwa ajili ya ununuzi wa mazao ya kilimo yanayouzwa nje ya nchi *(Export Credit Guarantee Scheme - ECGS)* ulioanza kutekelezwa mwaka 2002/2003, umekuwa na mafanikio ya kuridhisha kutokana na mikopo yote kurejeshwa kwa wakati kwa kutumia dhamana hii. Kiasi cha shilingi bilioni 13.46 zimekopeshwa chini ya mpango huu kwa ajili ya ununuzi wa mazao mbalimbali yanayouzwa nchi za nje.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuboresha huduma kwa wateja wake, Mabenki ya Biashara yameweza kuanzisha huduma mpya za malipo kwa kutumia kadi maalum *(Tembo Card, Automatic Teller Machines - ATM)* zinazowezesha mteja kuchukua fedha Benki wakati wowote kutoka vituo maalum. Kwa kutumia kadi hizo, wateja wanaweza kufanya malipo kwa manunuzi sehemu mbalimbali za biashara zenye vifaa maalum vya kusoma kadi hizo.

Mheshimiwa Spika, Benki ya Rasilimali Tanzania *(TIB)* imeingia katika mwaka wa pili wa utekelezaji wa Mpango wa Urekebishaji wa Benki hii. Rasilimali za *TIB* ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 29.71 mwaka 2002 ikilinganishwa na shilingi bilioni 28.82 mwaka 2001. Amana ziliongezeka kutoka shilingi bilioni 10.00 mwaka 2001 hadi kufikia shilingi bilioni 17.0 mwaka 2002. Mikopo iliyotolewa mwaka 2002 ilikuwa na thamani ya shilingi bilioni 4.57 ikilinganishwa na shilingi bilioni 2.178 mwaka 2001. Benki hii ilipata faida ya shilingi milioni 110 katika mwaka 2002 ikilinganishwa na shilingi milioni 113 mwaka uliopita. Kiwango cha uwezo wa Benki hii bado ni kidogo sana kuweza kuleta mabadiliko katika uchumi. Hivyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki Kuu itaangalia uwezekano wa kuirekebisha zaidi Benki hii ili iwe mhimili wa maendeleo ya kiuchumi katika utoaji wa mikopo kugharamia Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Benki ya Posta *(TPB),* amana za wateja zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 41.47 mwaka 2001 hadi shilingi bilioni 45.13 mwaka 2002. Aidha, vitega uchumi vya Benki hii viliongezeka kutoka shilingi bilioni 39.34 mwaka 2001 hadi shilingi bilioni 41.67 katika kipindi hicho. Ili kupanua wigo wa vitega uchumi katika mwaka 2002, Benki ya Posta ilianza kutoa mikopo midogo midogo ya biashara kwa vikundi na watu binafsi iliyofikia shilingi 2.8 bilioni.

Katika mwaka 2002, Benki hii ilipata faida ya shilingi milioni 346.3 ikilinganishwa na faida ya shilingi milioni 951.1 mwaka 2001. Katika mwaka wa fedha wa 2003, Benki ya Posta imelenga kupanua wigo wa ukopeshaji mikopo midogo midogo kwa vikundi na wafanyakazi na kupanua shughuli za utumiaji wa fedha. Aidha, Benki hii inatarajia kufungua matawi mawili Mwanza na Arusha pamoja na kufungua vituo 48 vya *Western Union Money Transfer.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu *National Bureau de Change (NBDC),* Wizara yangu kwa kushirikiana na Benki Kuu inafanya maandalizi ya kuirekebisha kimuundo na kuimarisha ili iweze kuwa Benki kamili. Katika mwaka 2002, *NBDC* iliongeza amana zake kwa wateja hadi kufikia shilingi bilioni 8.02 kutoka shilingi bilioni 7.71 mwaka 2001 na kutoa mikopo ya shilingi bilioni 4.87 ikilinganishwa na shilingi bilioni 3.26 mwaka 2001. *NBDC* katika mwaka 2002 ilipata mapato ya shilingi bilioni 2.39 na kuingiza faida kabla ya kodi ya shilingi milioni 239.1.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana *(CMSA)* imeendeleza kutekeleza majukumu yake kwa kutoa elimu kwa umma kuhusu dhana ya masoko ya mitaji na faida za uwekezaji kupitia Soko la Hisa la Dar es Salaam *(DSE).* Aidha, Mamlaka iliidhinisha nyaraka mbili za matarajio *(prospectus)* kwa Kampuni ya Saruji Tanga na *DAHACO* ambapo wananchi waliuziwa hisa.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanza kuandikishwa kwa Makampuni katika Soko la Mitaji la Dar es Salaam *(DSE)* mnamo Aprili, 1998, kumekuwa na maendeleo ya kuridhisha katika soko hilo. Kiwango cha mitaji kimeendelea kukua kutoka shilingi bilioni 7 mwezi Julai, 1998 hadi shilingi bilioni 365 sawa na asilimia 4.6 ya Pato la Taifa Desemba 2001 na shilingi bilioni 690 sawa na asilimia 8 ya Pato la Taifa mwezi Machi, 2003. Kiwango hiki cha ukuaji wa soko ni kikubwa ambacho kinakaribia kile cha nchi jirani ya Kenya ambacho ni asilimia 12 ya Pato la Taifa. Kuna kila dalili kwamba umma umeanza kuzielewa shughuli za *DSE.* Hii imedhihirika hivi karibuni ambapo watu waliojitokeza kununua hisa katika Makampuni ya *DAHACO* na *Tanga Cement* walihitaji hisa nyingi zaidi ya zile zilizotengwa kwa ajili hiyo. Aidha, hivi karibuni tumeshuhudia kuanzishwa kwa hatifungani za Benki ya Maendeleo ya Afrika Mashariki *(EADB)* hivyo kuongeza fursa zaidi za kuwekeza kwa asasi na watu binafsi.

Mheshimiwa Spika, kufuatia uamuzi wa Serikali kuidhinisha ushiriki wa wawekezaji wageni katika soko la Hisa, Mamlaka imekamilisha sera, sheria na taratibu za kudhibiti na kusimamia zoezi hili. Aidha, kwa uamuzi huu, tunatarajia Makampuni ya kigeni ambayo yameorodheshwa katika masoko ya hisa ya Kenya na Uganda kujiorodhesha katika Soko la Hisa la Dar es Salaam *(cross-listing). CMSA* kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania itaimarisha usimamizi wa hatua hii ili kuhakikisha maslahi ya nchi yanalindwa.

Mheshimiwa Spika, biashara ya bima katika mwaka wa fedha 2002/2003, iliongezeka kutoka shilingi bilioni 38.21 mwaka 2001/2002 hadi shilingi bilioni 46.18 sawa na asilimia 20.8 ikilinganishwa na lengo la asilimia 10. Ongezeko hili limetokana na kupanuka kwa biashara hii katika miji mikuu ya kibiashara ya Mwanza, Mbeya na Arusha . Aidha, kuanzishwa kwa bima ya matibabu kumechangia sana ongezeko hili. Hata hivyo, bima ya maisha imepungua kutoka shilingi bilioni 8.4 mwaka 2001/2002 hadi shilingi bilioni 7.6 mwaka 2002/2003. Kushuka kwa soko la bima ya maisha kumechangiwa sana na zoezi la ubinafsishaji ambapo wafanyakazi wengi waliokuwa wanachama wamestaafishwa.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kifungu 109 cha sheria ya Bima Na. 18 ya mwaka 1996, Mashirika ya Bima yameweza kulipa madai ya fidia ya shilingi bilioni 18.1 mwaka 2002/2003 ikilinganishwa na shilingi bilioni 15.64 mwaka 2001/2002 ikiwa ni ongezeko la asilimia 15.73. Jitihada hizi ni muhimu katika kufufua na kuimarisha biashara ya bima hapa nchini.

Kuhusu Shirika la Bima la Taifa *(NIC)* ambalo ndilo lenye madai mengi na ya muda mrefu yenye kero kubwa, Wizara yangu kwa kushirikiana na *PSRC* na Idara ya Usimamizi wa Shughuli za Bima imeidhinisha mkakati wa kupunguza madai yake ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za kuuza baadhi ya majengo yake kulipia madai yaliyothibitishwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kukua kwa mapato ya biashara ya bima hapa nchini, thamani ya vitega uchumi vinavyotokana na mapato haya imepungua kwa asilimia 14.4 kutoka shilingi bilioni 119.2 mwaka 2001/2002 hadi shilingi bilioni 102.0 mwaka 2002/2003. Katika mwaka 2003/2004, pato la bima linatarajiwa kukua kwa asilimia 10 kutokana na kuanzishwa kwa Shirika la Bima Mtawanyo *(Tanzania Reinsurance - Tan-Re)* pamoja na juhudi madhubuti za kulipa fidia. Kuwepo kwa *Tan-Re* katika soko la bima hapa nchini kutaimarisha soko na kuvutia biashara ya bima kutoka nje ya nchi *(inward reinsurance).* Aidha, kinga kubwa na bora zaidi *(underwriting capacity)* inavyotokana na bima ya Mtawanyo itawavutia wawekezaji kutoka nje waliokuwa wanasita kuchukua bima hapa nchini kutokana na mitaji midogo.

Mheshimiwa Spika, kufuatia kupitishwa kwa Sheria Na. 4 ya 2003 ya Biashara ya Michezo ya Kubahatisha, Shirika la Bahati Nasibu la Taifa sasa limefutwa na badala yake imeanzishwa Bodi ya Usimamizi wa Michezo ya Kubahatisha *(Gaming Board of Tanzania)* itakayosimamia michezo ya kubahatisha hapa nchini. Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inakamilisha kanuni na taratibu za uendeshaji na udhibiti wa michezo ya kubahatisha hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kusafisha mizania yake kutokana na shughuli za ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma, Serikali iliunda Shirika la *Consolidated Holding Corporation (CHC)* na Mfuko wa Udhamini wa Mikopo na Madeni *(LART). CHC* lilikusanya jumla ya mapato ya shilingi bilioni 4.48

katika mwaka wa 2002 sawa na asilimia 70 ya lengo kutokana na uuzaji wa majengo, magari na vifaa, ukusanyaji madeni na huduma mbalimbali. Aidha, baada ya kuondoa gharama mbalimbali za utekelezaji wa majukumu yake, *CHC* iliweza kuwasilisha Serikalini shilingi bilioni 1.72 kama ilivyopangwa. Tatizo kubwa na sugu limekuwa kasi ndogo ya kuikamilisha idadi kubwa ya kesi zilizoko Mahakamani na mpya zinazojitokeza hivyo kuligharimu Shirika fedha nyingi.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Udhamini wa Mikopo na Madeni *(LART)* ulianzishwa kwa ajili ya kushughulikia madeni sugu ya Benki za biashara za *NBC, CRDB* na *PBZ.* Aidha, *LART* imeendeleza kushughulikia madeni hayo pamoja na mapya yanayojitokeza kutoka Mabenki mengine. Hadi Juni 30, 2003, kiasi cha shilingi bilioni 4.14 kilipatikana ikilinganishwa na lengo la shilingi bilioni 9.36. Kiasi hiki ni kidogo kutokana na baadhi ya wanunuzi kupinga Mahakamani uuzaji mali za Mashirika, hivyo kuendelea kuchelewesha zoezi hilo. *LART* pia imechangia katika utekelezaji wa zoezi la ubinafsishaji wa sekta ya umma kwa kusimamia uuzaji wa baadhi ya Mashirika, kama vile *MWATEX, MUTEX* na kadhalika. Katika mwaka 2003/2004, *LART* imelenga kukamilisha uuzaji wa mali za wadaiwa 12 zinazokadiriwa kuingiza shilingi bilioni 3.7, kukusanya madeni ya shilingi bilioni 1.8 na kukusanya shilingi bilioni 2.9 kutokana na mauzo ya Mashirika ya Umma yanayofilisiwa.

Mheshimiwa Spika, tatizo la fedha haramu limekuwa linaathiri nchi nyingi duniani, kiuchumi na hata kijamii. Fedha haramu ni mojawapo ya njia kuu itumikayo katika kufanikisha vitendo vya uhalifu wa Kimataifa. Katika kudhibiti tatizo la fedha haramu, nchi za Kusini na Mashariki ya Afrika zimeunda Umoja wa Kudhibiti Masuala ya Fedha Haramu (*The Eastern and Southern Africa Anti-Money Laundering Group - ESAAMLG).* Umoja huo ulizunduliwa rasmi mjini Arusha tarehe 27 Agosti, 1999 na makao yake Makuu yapo Dar es Salaam. Chini ya Umoja huo, kila nchi mwanachama huandaa programu za utekelezaji Kitaifa za udhibiti wa fedha haramu katika nyanja za kifedha, kisera na kisheria.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inasimamia vyuo vya Uhasibu vikiwemo Chuo cha Uhasibu Arusha *(IAA),* Chuo cha Usimamizi wa Fedha *(IFM)* na Taasisi ya Uhasibu Tanzania *(TIA)* zamani ikiitwa *Dar es Salaam School of Accountancy.*

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Uhasibu Arusha *(IAA),* katika mwaka wa fedha 2002/2003, kilisajili wanafunzi 437 ikilinganishwa na wanafunzi 402 waliosajiliwa mwaka 2001/2002. Chuo kimeendelea kutoa mafunzo ya Shahada ya Juu ya Uhasibu *(CPA),* Stashahada ya Uzamili ya Uhasibu, Stashahada ya Juu ya Uhasibu, Usimamizi wa Kodi na Teknolojia ya Habari na cheti.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Usimamizi wa Fedha *(IFM)* katika mwaka wa fedha 2002/2003 kilisajili jumla ya wanafunzi 1,335 ikilinganishwa na wanafunzi 1,032 mwaka 2001/2002, ongezeko ambalo ni sawa na asilimia 29. Chuo kinatoa mafunzo ya Stashahada ya Juu ya Uhasibu, Usimamizi wa Bima, Usimamizi wa Benki, Usimamizi wa Kodi, Sayansi ya Kompyuta, Teknolojia ya Habari, Hifadhi ya Jamii, pamoja na Shahada ya Uzamili ya Usimamizi wa Fedha na Biashara za Kimataifa. Katika mwaka wa fedha 2003/2004, Chuo kimelenga kubuni kozi mpya kwa kuzingatia mahitaji ya soko.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Uhasibu Tanzania ilianzishwa tarehe 1 Julai, 2002 kama Wakala wa Serikali na kuzinduliwa rasmi tarehe 24 Januari, 2003. Taasisi hii iliyochukua nafasi ya kilichokuwa Chuo cha Uhasibu cha Dar es Salaam *(DSA)* ina majukumu yafuatayo:-

(a) Kutoa mafunzo bora katika fani za Uhasibu, Ugavi na fani zingine za Kibiashara.

(b) Kutoa huduma za ushauri na utafiti katika fani mbalimbali za Kibiashara na uongozi.

(c) Kujiendesha kwa ufanisi ili kufikia lengo la kuwa Wakala inayojitegemea.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2002/2003, Chuo kilisajili wanafunzi 551 ikilinganishwa na wanafunzi 414 mwaka 2001/2002 ambalo ni ongezeko la asilimia 33.1.

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha viwango vya utaalamu kwa watumishi hususan wa kada za Uhasibu, Uboharia na Teknolojia ya Habari *(IT),* katika mwaka 2003/2004, Wizara yangu imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.2 kwa ajili ya mafunzo. Fedha hizo zitatumika kudhamini wanafunzi wapya 650 kwenye fani hizo pamoja na wale waliopo vyuoni wenye udhamini wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu *(NBAA)* imeendeleza kusimamia na kuratibu shughuli za Uhasibu na Ukaguzi nchini. Katika mwaka wa fedha 2002/2003, Bodi imeboresha Kanuni za Uhasibu na Ukaguzi wa Hesabu. Aidha, Bodi imeanzisha utaratibu wa kutathmini ubora wa kazi za ukaguzi *(Quality Audit Review Scheme).* Vile vile, Bodi imeendelea kuendesha semina na warsha katika ngazi zote za taaluma ili kuongeza ujuzi.

Mheshimiwa Spika, Bodi imepata mafanikio katika utekelezaji wa majukumu iliyopewa chini ya Sheria ambayo ni pamoja na kutahini na kusajili wahitimu wa kozi za Uhasibu na Ukaguzi. Hadi kufikia Desemba, 2002, Bodi imefanikiwa kusajili wataalamu 13,908 katika ngazi mbalimbali ikiwemo ngazi ya Shahada ya Juu ya Uhasibu *(CPA)* 1,352. Wataalamu waliojiandikisha hadi Mei, 2003 ni Wakaguzi wa Hesabu walioidhinishwa 266, Wahasibu walioidhinishwa 641, Wahasibu waliothibitishwa 816, Wahasibu waliohitimu mafunzo lakini bado kusajiliwa 493 na Watunza Vitabu vya Hesabu 111. Vile vile, Bodi imeendelea kushirikiana na Chama cha Kitaifa cha Wahasibu na Chama cha Muungano wa Wahasibu cha Nchi za Mashariki, Kati na Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Spika, ili Wizara iweze kutekeleza majukumu niliyokwishayaeleza na kufikia malengo yaliyopangwa katika mwaka wa fedha 2003/2004, Wizara yangu inaomba Bunge lako liidhinishe jumla ya shilingi 144,685,261,600/= kama ifuatavyo:-

(a) Shilingi 123,540,193,800/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 21,145,067,800/= ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

(b) Kwa upande wa Matumizi ya Kawaida, shilingi 23,426,532,900/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Wizara, shilingi 43,737,975,000/= ni matumizi ya Asasi za Wizara na shilingi 56,375,685,900/= ni Matumizi Maalum.

(c) Kwa upande wa Wizara, shilingi 872,460,500/= ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 22,554,072,400/= ni za matumizi mengineyo.

(d) Kwa upande wa asasi, shilingi 39,092,000,000/= ni kwa ajili ya Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* shilingi 3,803,975,000/= ni kwa ajili ya Vyuo vya Uhasibu *(IFM, IAA* na *TIA)* na Bodi ya Ukaguzi na Uhasibu *(NBAA),* shilingi 817,000,000/= ni kwa ajili ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana na Soko la Hisa *(CMSA/DSE)* na shilingi 25,000,000/= ni kwa ajili ya Idara ya Usimamizi wa Bima.

(e) Shilingi 63,988,463,500/= ni kwa ajili ya Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali - Fungu 23. Kati ya fedha hizo, shilingi 15,362,609,000/= Matumizi ya Kawaida, shilingi 9,000,000,000/= ni za kulipia gharama za huduma za Benki *(Bank Charges),* shilingi 6,616,460,500/=ni za Mfuko wa Bima ya Afya *(National Health Insurance Fund)* shilingi 31,522,000,000/= ni kwa ajili ya kulipia misamaha ya kodi kwa asasi za Kidini na zisizo za Kiserikali *(NGOs)* na shilingi 1,487,394,000/= ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

(f) Shilingi 405,103,791,000 ni kwa ajili ya Deni la Taifa - Fungu 22.

(g) Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi - Fungu 45 inaombewa jumla ya shilingi 5,990,227,700/=. Kati ya fedha hizo, shilingi 4,373,198,400/= ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 1,617,029,300/= ni za Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Fedha na Uchumi imepitia Makadirio ya Wizara na Fedha, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ya mwaka 2003/2004 na kuyakubali. Naomba Bunge lako likubali kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi pamoja na Deni la Taifa kwa mwaka 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, natumia tena nafasi hii kukushukuru wewe na Bunge lako, Kamati ya Fedha na Uchumi na Kamati zote za Bunge katika kupitia mapendekezo ya Bajeti ya Serikali na ya Wizara. Tutaendelea kuzingatia na kuufanyia kazi ushauri wao.

Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru wewe na wasaidizi wako, Manaibu wangu, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatibu, Mbunge wa Makunduchi na Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mbunge wa Magu, kwa ushirikiano mkubwa walionipa wakati wote wa maandalizi ya makadirio haya.

Aidha, nawashukuru wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha chini ya Makatibu Wakuu Bwana Gray Mgonja na Bwana Peniel Lyimo, Manaibu Katibu Wakuu Bwana Ramadhani Khijjah na Bwana Wilfred Nyachia, Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* Benki Kuu ya Tanzania na Asasi nyingine zote zilizofanyikisha maandalizi ya hotuba hii. Nawaomba waendeleze na moyo huo wa kufanya kazi kwa masaa mengi bila kuchoka, ili kuhakikisha kuwa mapendekezo yaliyopitishwa na Bunge lako yanatekelezwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. NJELU E. M. KASAKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA FEDHA NA UCHUMI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kuhusu utekelezaji wa Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Wizara ya Fedha katika mwaka wa fedha uliopita 2002/2003 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio na Matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tunawasilisha kwa muhtasari na baadhi haya haya mambo tuliyowasilisha katika Bajeti Kuu kwa hiyo, baadhi ya mambo tumekwishayataja nadhani wachangiaji watakuwa wanaunganisha na yale ambayo tuliyataja wakati wa Bajeti Kuu.

Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kuwapongeza Mawaziri wa Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafishaji Dr. Abdallah Kigoda na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, kwa kuwasilisha hotuba zao na pia kwa kujibu hoja na maoni mbalimbali yaliyotolewa katika Kamati ya Fedha na Uchumi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kujadili taarifa hizo, Kamati ilipata fursa ya kuzifahamu Idara na Asasi mbalimbali zilizopo chini ya Wizara hizo mbili na kwa kweli kutokana na ukubwa wa Wizara hizo na Idara kuwa nyingi na Taasisi mbalimbali Zilizo chini ya Wizara hizo kuwa nyingi tulishatembelea chache, baadhi bado na tuna mkakati kwa kushirikiana pamoja na Mawaziri kuzitembelea Asasi na Wizara zote na Idara zote katika siku zinazofuata katika vikao vijavyo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kwanza kuwatambua Wajumbe wa Kamati yangu ni hawa wafuatao, Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mwenyekiti, Mheshimiwa Lephy Gembe, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Rostam Aziz, Mheshimiwa Dr. Chegeni Masunga, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Abdullatif Esmail, Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Mwanamkuu Makame Kombo, Mheshimiwa Profesa Simon Mbilinyi, Mheshimiwa Talala Mbise, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mheshimiwa Elisa Mollel, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Felix Mrema, Mheshimiwa Hasnain Murji, Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mheshimiwa John Mwakipesile, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Esther Nyawazwa, Mheshimiwa Omar Juma Omar, Mheshimiwa Suleiman Sadiq, Mheshimiwa Issa Mohammed Salim, Mheshimiwa Iddi Simba na katibu wetu ni Ndugu James Warburg. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa nianze na Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji. Katika mwaka wa 2002/2003 Wizara iliidhinishiwa jumla ya shilingi milioni 400 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ambapo mpaka kufikia mwezi Aprili, 2003 jumla ya shilingi 354,875,917/= ambazo ni sawa na asilimia 89 zilitumika. Kati zilizofanyika ni pamoja na kukarabati jengo la ofisi, ujenzi wa bweni la kulala wanafunzo Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini Dodoma, kujenga uwezo wa kuendeleza utafiti na uchambuzi wa masuala ya kiuchumi na kijamii, kukamilisha na kusambaza

taarifa za utekelezaji wa mikakati ya kupunguza umaskini, Sensa ya watu na makazi, kuendelea kubinafsisha Mashirika ya Huduma na Miundombinu muhimu na ukusanyaji wa takwimu mbalimbali za Hali ya Uchumi na Maendeleo za Mikoa yote *(Regional Social-Economic Profiles).*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2002/2003, Kamati ilitoa maagizo mawili yaliyolenga katika kuboresha taratibu za zoezi la ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma na kuweka misingi imara ya utendaji kwa yale Mashirika ambayo yanaendelea kubaki katika himaya ya umma.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara ilitoa taarifa na maelezo ya kutosha katika kutekeleza maagizo ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa maagizo iliyotoa mwaka jana, ambayo kinadharia yameonyesha mwelekeo mzuri wa kiutendaji. Aidha, pamoja na maelezo mazuri ya kiutendaji Wajumbe bado walisisitiza kuwepo kwa takwimu mbalimbali ambazo zingelitoa picha halisi ya malengo yaliyofikiwa kiutekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 92(2)(v) tarehe 18 hadi 24 Mei, 2003 Kamati yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaii pamoja na Tume ya Rais inayoshughulikia Ubinafishaji Mashirika ya Umma ilifanya ziara katika Mikoa ya Morogoro, Iringa na Mbeya na kukagua Mashirika yaliyobinafsishwa ili kutathmini utekelezaji wa zoezi la ubinafishaji na kubaini mafanikio, matatizo na mwelekeo wa zoezi hili katika siku zijazo. Aidha, tarehe 30 Mei, 2003 Wajumbe wa Kamati yangu na Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara walifanyiwa Semina ya pamoja iliyoandaliwa na Mwenyekiti wa Tume ya Rais ya Kubinafsisha Mashirika ya Umma iliyofanyika *Kunduchi Beach Hotel* kwa lengo la kujielimisha zaidi kuhusu zoezi la ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004 Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafishaji imeandaa kitabu cha mpango maalum ambacho kitakuwa ni dira ya utekelezaji wa mipango ya ofisi katika Idara na Asasi mbalimbali zilizo chini yake. Aidha, mipango ya Wizara italenga katika kuendeleza jitihada za Serikali za kukuza uchumi jumla sambamba na utekelezaji wa malengo ya dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeweka malengo katika kuimarisha ushiriki wa nchi yetu katika nyanja za Biashara na Uwekezaji raslimali nchini kwa kushirikiana na nchi za nje pamoja na Jumuiya za Kimataifa kama vile *EAC, SADC, NEPAD, WTO, AGOA, TICAD* na *EU/ACP.*

Mheshimiwa Spika, Wizara imeweka pia mikakati mbalimbali ya kukuza uchumi, kuboresha huduma za kijamii na kuendeleza Sekta binafsi kwa kuhusisha Kituo cha Uwekezaji Raslimali na Baraza la Taifa la Biashara *(TNBC).*

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine ambayo Wizara inatarajia kuimarisha ni pamoja na upande wa Idara za Maendeleo ya Sera na Habari, Utawala na kusimamia kwa karibu majukumu ya Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini Dodoma. Aidha, Wizara itaendelea kuisimamia Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC)* katika kuendeleza majukumu yake ya kurekebisha Mashirika yanayotoa huduma na ya miundombinu na Mashirika mengine ya kibiashara.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004 Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji imeainisha miradi mbalimbali ya kutekelezwa chini ya mpango wa *Business Environment Strengthening for Tanzania (BEST)* inayohusisha uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji nchini, hususan katika kuimarisha matumizi ya Sera, Sheria na Utawala Bora. Miradi mingine ambayo Ofisi inatarajia kuitekeleza ni pamoja na kuendeleza programu ya utafiti wa kupunguza umaskini, kuendeleza ujenzi wa Bweni la Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini Dodoma, ukarabati wa Jengo la Ofisi ya Taifa ya Takwimu na upanuzi wa Ofisi ya *Tanzania Investment Centre.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia na kujadili taarifa ya utekelezaji wa mipango ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Kamati imebaini kuwa majukumu makubwa ya ofisi hii ni kusimamia uendeshaji wa uchumi wa nchi *(Economic Management),* kutoa miongozo ya kutekeleza Dira ya Taifa

2025 na kusimamia mipango ya maendeleo, kuweka mazingira bora ya uchumi wa soko yatakayowezesha wawekezaji wa ndani na nje kuwekeza Tanzania na kukua kwa Sekta Binafsi na kukusanya, kuandaa na kutawanya takwimu za Kitaifa. Kutokana na majukumu hayo Kamati inatoa maoni na mapendekezo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali ifufue Tume ya Mipango iliyokuwepo na ambayo kisheria haijafutwa. Kamati inaamini, majukumu niliyotaja hapa kwa muhtasari hayawezi kutekelezwa vizuri bila ya kuwa na Tume ya Mipango imara. Tume ya Mipango ndicho Chombo kitakachohakikisha kuwa mipango ya Sekta mbalimbali inaandaliwa kwa lengo la kutekeleza Dira ya Maendeleo 2025.

Aidha, Tume ya Mipango ndicho chombo muhimu cha ushauri kwa Serikali kuhusu masuala ya maendeleo. Watu watakaoteuliwa kwenye Tume wawe na elimu ya kutosha, uwezo na uzoefu katika masuala ya uchumi na maendeleo. Ningependa ieleweke kuwa nchi iliyopania kuleta maendeleo endelevu kwa haraka na kwa uhakika, haiwezi kushindwa kuona umuhimu wa Tume ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, katika Tanzania Sekta zenye uwezo mkubwa wa kuharakisha maendeleo ya Wananchi ni kilimo na viwanda. Kwa bahati mbaya Sekta hizi bado ziko nyuma katika kuchangia Pato la Taifa. Mchango wa Sekta ya Viwanda bado ni 8% tu na mchango wa kilimo ingawa unaonekana mkubwa 48% inatokana na kilimo cha asili *(Traditional Agriculture)* ambacho hakiwezi kuleta mabadiliko makubwa katika uchumi wa kisasa. Kilimo cha Tanzania lazima kibadilike kwa kupanua maeneo, kuongeza uzalishaji kwa eneo, kutumia zana na pembejeo za kisasa na uzalishaji ulenge soko badala ya mahitaji ya familia. Kukua kwa Sekta hizi mbili kunakabiliwa na pamoja na mambo mengine, tatizo la upatikanaji wa mikopo ya Mabenki. Kamati inashauri kuanzishwa kwa Benki za Kilimo na Viwanda ambako kumekubaliwa, kufanyike haraka.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kukiimarisha Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini Dodoma. Chuo hiki ni muhimu sana hasa ikizingatiwa kuwa asilimia 80% ya Watanzania wanaishi Vijijini na azma ya Serikali kupeleka madaraka kwa Wananchi. Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini lazima kihuishwe na mpango wa kilimo wa *Participatory Agriculture Development and Empowerment Project(PADED),* kwa kuwa walengwa wa *PADEP* ni watu wa Vijijini. Aidha, Kamati inaitaka Wizara ikamilishe ujenzi wa mabweni ambao umekuwa ukiendelea hapo chuoni. Fedha zilizotengwa kwa ajili ya mradi huu ni nyingi shilingi milioni 344 kwa 2003/2004 na ni matumaini ya Kamati kuwa mradi utakamilika katika mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, programu ya ubinafsishaji wa Mashirika na Makampuni ya Umma licha ya kupata mafanikio katika baadhi ya maeneo, bado ina mapungufu na kasoro nyingi za kiutekelezaji. Ni kweli Serikali imeondokana na mzigo wa kutoa ruzuku kwa Mashirika ya Umma, inapata kodi nyingi na kwa baadhi ya Mashirika, gawio kutokana na hisa zake. Aidha, uzalishaji wa bidhaa na huduma umeongezeka na ajira imepatikana katika Mashirika na Makampuni yaliyokuwa yamefungwa. Haya ni mafanikio makubwa ambayo lazima tuyatambue.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, baada ya ziara ya Kamati katika Mikoa ya Morogoro, Iringa na Mbeya na kusoma taarifa za *PSRC* yamebainika mambo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, katika Mashirika 192 ambayo *PSRC* imewekeana mikataba ya mauzo na Wawekezaji ni Wawekezaji 39 tu ndio wamelipa asilimia 100 kwa mujibu wa mkataba. Waliobaki hawajamaliza kulipa hadi leo ingawa baadhi walikabidhiwa Mashirika hayo tangu 1996.

Mheshimiwa Spika, Wawekezaji wengi waliouziwa Mashirika wameshindwa kuyaendeleza. Baadhi bado wamefungwa na baadhi wanafanya uzalishaji wa kiwango cha chini, kilicholingana na malengo ya kubinafsisha. Tunashauri malengo ya kubinafisha yazingatiwe.

Mheshimiwa Spika, makubaliano ya mwanzo ya kuuza Kampuni ya Sukari ya Mtibwa yalilenga kuuza hisa asilimia 75 kwa Mwekezaji na asilimia 25 zibaki Serikalini kwa ajili ya kuuziwa Watanzania. Lakini Mwekezaji wa Kampuni aliiarifu Kamati yangu kwamba alishauziwa hisa zote asilimia 100. *PSRC* walikiri kumuuzia Mwekezaji hisa zote isipokuwa kwamba walimwomba baadaye atoe hisa asilimia 5 kwa ajili ya wakulima wadogo wa miwa, jambo ambalo ameonekana hataki. Nafasi ya Watanzania kumiliki

Kampuni ya Sukari ya Mtibwa kwa sasa haipo kabisa. Tunashauri ubinafsishaji ulenge kuwawezesha na kuwashirikisha Watanzania katika kumiliki Mashirika yaliyokuwa ya Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Benki ya *NBC (1997) Limited* iliuzwa kwa Kampuni ya *ABSA Group* ya Afrika Kusini kwa thamani ya shilingi bilioni. 15. Kwa taarifa ya *PSRC* iliyowasilishwa kwenye Kamati ya Fedha na Uchumi ambayo inaishia Juni 30, 2003 inaonyesha kuwa tangu *ABSA* wachukue Benki ya *NBC (1997) Limited,* hakuna malipo yaliyopokelewa na *PSRC* kwa mujibu wa mkataba. Ni vigumu kuamini kuwa *PSRC* wanaweza kusahau kuingiza kwenye kompyuta fedha za mauzo ya Shirika kubwa kama *NBC.* Hali kama hiyo inajitokeza kwenye Kampuni ya *Tanzania Gemstone Industries* iliyouzwa kwa *Euro Africa Investment Corporation* kwa asilimia 100. Panahitajika maelezo jinsi gani Wawekezaji hawa wamekaa muda wote huu bila kulipa.

Aidha, *NBC* pamoja na kubinafsishwa bado ina matatizo ya kiuendeshaji. Serikali inashauriwa kusimamia Benki hii kubwa hapa nchini, kwa karibu sana. Uchumi utaathirika sana Benki hii ikiyumba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kuna matatizo pamoja na migogoro mbalimbali kati ya wafanyakazi na Wawekezaji wa Benki hiyo. Tunaishauri Serikali isiache migogoro kama hiyo ikaendelea. Migogoro kama hii kama itaendelea katika Mashirika mengine itaharibu utulivu ambao tumekuwa nao katika nchi yetu kwa muda mrefu. Tunashauri usimamizi wa Benki hii pamoja na Mabenki mengine uwe wa karibu sana.

Mheshimiwa Spika, kutokana na Wawekezaji wengi kutoheshimu mikataba waliyowekeana na Serikali kwa kulipia Makampuni au Mashirika waliyokabidhiwa, *PSRC* wameamua kuajiri Kampuni ya kukusanya madeni toka kwa Wawekezaji wasiolipa. Kamati inaona hatua hii kuwa itaongeza gharama na hivyo kupunguza faida itakayopatikana kutokana na kuuza Mashirika ya Umma. Kwa kuwa Wawekezaji wengi wameshindwa kulipia kikamilifu Makampuni waliokabidhiwa na kwa kuwa baadhi ya Makampuni yaliyobinafsishwa hayafanyi kazi, basi lengo la kubinafsisha Makampuni hayo halijafikiwa.

Kamati inaishauri Serikali iwabane Wawekezaji hao walipe au wanyang'anywe Makampuni na kuwapatia Wawekezaji wengine wenye uwezo. Aidha, Kamati inashauri ubinafsishaji wa Mashirika yaliyobaki ufanywe kwa uangalifu sana kuepuka matatizo yaliyojitokeza hadi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imegundua udhaifu mkubwa katika ufuatiliaji wa Mashirika yaliyobinafsishwa ama kwa asilimia 100 au kwa asilimia kubwa ya hisa kuliko Serikali. *PSRC* wanasema ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkataba wa Shirika lililobinafsishwa si kazi yake, bali ni wajibu wa Wizara Mama ya Shirika. Lakini sheria iliyoanzisha *PSRC (Public Corporations (Amendment) Act 1993)* Ibara ya 39 (2) (i) inaipa *PSRC* uwezo wa kujadili na kukamilisha mikataba ya kuuza au kukodisha Mashirika.

Aidha, sheria hiyo haitoi uwezo kwa *PSRC* wala kwa Wizara Mama na kufuatilia utekelezaji wa mikataba inayofikiwa kati ya *PSRC* na Wawekezaji. Tunafikiri udhaifu wa ufuatiliaji huenda unatokana na udhaifu katika sheria yenyewe. Kamati inaishauri Serikali kuimarisha eneo hili la ufuatiliaji ili Taifa lifaidike na programu ya ubinafsishaji. Vinginevyo, Wawekezaji wanaonekana kuwa na uhuru usio na mipaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baadhi ya matatizo yaliyojitokeza katika suala zima la ubinafsishaji inaonekana yametokana na Serikali kujipa muda mfupi wa kumaliza kubinafsisha Mashirika na Makampuni ya Umma. Hali hii huenda imesababisha kukubalika kwa Wawekezaji ambao hawako makini na uwezo wao kifedha ni wa mashaka. Pamoja na nia njema ya Serikali kutaka kutimiza masharti ya Benki ya Dunia, kuna haja ya kuangalia tena uamuzi huo kwa faida ya nchi. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kuhakikisha kwamba suala hili linashughulikiwa vizuri.

Mheshimiwa Spika, tunasema hivyo kwa sababu Ripoti ya Shirika la Fedha Duniani ya hivi karibuni inasema kuwa *IMF* kwa mara ya kwanza imekubali kuwa kuzilazimisha nchi zinazoendelea kufungua masoko yao kwa Wawekezaji toka nje kunasababisha uwezekano wa kuongezeka kwa matatizo ya kifedha katika nchi hizo. Mwandishi anasema na ninanukuu: *"In some cases the process of liberalization (imposed on developing countries) has been accompanied by increased vulnerability*

*to crises."* Katika ripoti hiyo *IFM* inaonya: *"Countries to take caution when integrating with the global economy and countries are advised to achieve economic balance by creating strong domestic financial institutions."* Kamati inashauri tahadhari kama hizi zinafaa kuzingatiwa katika programu ya ubinafsishaji na suala zima la mageuzi ya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, mwezi Mei, 2003 Kamati ilifanya ziara kama nilivyoeleza pale awali, katika Mikoa ya Morogoro, Iringa na Mbeya kutathmini hali ya viwanda vilivyobinafsishwa na vile ambavyo Serikali ilivifunga na mpaka sasa havijapata Wawekezaji. Kamati ilitembelea kiwanda cha *SPM* Mgololo ambacho Serikali ilikifunga mwaka 1999 kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo ukosefu wa mtaji wa kufanyia kazi na gharama kubwa za umeme.

Mheshimiwa Spika, kiwandani hapo kuna jumla ya tani 4,200 za kemikali/sumu kali zilizohifadhiwa katika matanki 32. Matanki hayo sasa hivi yanaliwa na kutu, maelezo yaliyotolewa na uongozi wa kiwanda ni kwamba, endapo madawa hayo yatavuja, yatasababisha uharibifu wa mazingira na vifo kwa binadamu, wanyama, wadudu, mimea na viumbe hai katika sehemu za Wilaya ya Mufindi, Ulanga, Njombe na Bonde lote la Mto Ruaha, Kilombero, Rufiji hadi Bahari ya Hindi. Kwa hiyo, Kamati inaishauri Serikali kwa kweli ichukue hatua za haraka za kuhakikisha kwamba suala hili linashughulikiwa. Suala hili lishughulikiwe haraka ili kuondoa madawa hayo au yatumike ili yasije yakaleta madhara kwa watu wetu.

Mheshimiwa Spika, mazingira ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu, ambayo ina majukumu makubwa ya kutafiti kuhusu masuala ya kiuchumi na kijamii, kukusanya, kuchambua na kusambaza takwimu mbalimbali zinazohusu Pato la Taifa, idadi ya watu, ajira, mapato na kadhalika hairidhishi, kuna haja ya Ofisi hii kuwekewa mazingira mazuri ya kazi ili itekeleze majukumu yake vizuri. Kamati inashauri Ofisi za Idara hii zifanyiwe matengenezo na ukarabati katika mwaka huu wa fedha. Aidha, Kamati inashauri mawasiliano kati ya Ofisi Kuu ya Takwimu, Mikoa na Wilaya yaimarishwe ili takwimu zinazotolewa zisitofautiane.

Mheshimiwa Spika, ili kuliwezesha Bunge kutekeleza majukumu yake ya kuidhinisha Bajeti na kuisimamia Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ya Fedha na Uchumi ihusishwe tangu hatua za mwanzo za kuandaa Bajeti *(Budget Framework).* Hatua hii itawezesha ushauri wa Bunge kupatikana na kuzingatiwa tangu hatua za awali za kuandaa bajeti yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, taarifa za Wizara ya Fedha za kila mwaka zimekuwa zikielezea kuwapo kwa ongezeko la makusanyo ya mapato kutokana na kodi mbalimbali. Kamati inaipongeza Wizara ya Fedha kwa jitihada inazozichukua katika kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Serikali ambayo sasa yamefikia shilingi bilioni 110 kwa mwezi. Hata hivyo, Kamati inasisitiza juhudi zaidi zifanyike hasa katika maeneo ya ukwepaji kodi na wizi. Iwapo mianya ya ukwepaji kodi na wizi itazibwa, mapato yataongezeka zaidi. Tunazo taarifa kwamba, huko bandarini hasa katika maeneo ya makontena kuna ukwepaji mkubwa sana wa kodi ambapo mapato ya Serikali yangeweza kupatikana, lakini kutokana na usimamizi au mabadiliko ya kimenejimenti katika maeneo hayo, kodi nyingi hazikusanywi.

Mheshimiwa Spika, suala la usimamizi wa matumizi ya Serikali ni muhimu katika azma ya kuendeleza jitihada za kuondokana na umaskini kwa Wananchi. Kamati inashauri kwamba, Bunge litumike kikamilifu kwa kuwa na vikao vya kufanya medium review ya Bajeti ya Serikali. Aidha, kwa kutumia Kamati zake ufuatiliaji ufanyike kwa kukagua miradi yote ya maendeleo *(Physical Check)* na kubaini kitu kinachoitwa *value for money* na kwa kuainisha kiasi cha fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Wizara ya Fedha kwa kuweka mtandao wa kompyuta unaotumika katika kuimarisha mfumo wa Bajeti, uhasibu na ulipaji wa mishahara *(Integrated Financial Management System IFMS)* na fedha zinazolipwa kwa Wahasibu wa Wizara mbalimbali, Mikoa na Wilaya ambao kwa kiwango kikubwa umeongeza ufanisi na udhibiti wa matumizi ya fedha za Serikali na kubana mianya ya wizi kwa fedha hizo.

Mheshimiwa Spika, Kamati inachozungumza hapa ni kwamba, mpango huu sasa uharakishwe kuenezwa katika Mikoa na Wilaya ili kuhakikisha kwamba angalau mianya mbalimbali inayojitokeza haipo tena kwa kuruhusu watu waweze kuiba fedha.

Hata hivyo, Kamati inatahadharisha kuwepo umakini mkubwa wa matumizi kwa utaratibu huu ili kuepukana na vitendo vya wizi na ubadhilifu unaoweza kufanywa na watumishi ambao siyo waaminifu. Aidha, pongezi za dhati ziende kwa Mhasibu Mkuu wa Serikali, Bibi Blandina Nyoni, kwa umakini wake wa kusimamia na kukiongoza Kitengo hiki kwa ufanisi wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la udhibiti wa matumizi ya fedha za Serikali unaenda sambamba na kuwa na ukaguzi wa uhakika wa Hesabu za Serikali. Hili linaweza kutekelezwa tu kwa kuimarisha Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kamati inashauri jitihada za makusudi zichukuliwe katika kuimarisha Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kuipa nyenzo zote muhimu zinazohitajika ikiwa ni pamoja na kuboresha maslahi ya watumishi wake.

Aidha, taarifa za Mkaguzi Mkuu wa Serikali mara inapotolewa ifanyiwe kazi kwa kulingana na matakwa ya kisheria na kiutawala. Pia, tunampongeza Msimamizi na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa kazi nzuri anayoifanya, ingawa katika mazingira magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kuwepo vitendo vya matukio ya wizi wa fedha za Serikali zinazolipwa kwa Maofisa Wahasibu wa Mikoa na Wilaya mbalimbali unaofanywa na Maofisa katika Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Wahasibu wa Mikoa au Wilaya. Hili suala lilijitokeza katika baadhi ya Wilaya ambapo tulipata taarifa kuwa fedha zikitolewa, zikipelekwa kwenye Wilaya baadaye Maofisa kutoka Wizarani wanazifuata kule kwenda kuchukua fedha hizo kwa ajili ya matumizi yao.

Kwa hiyo, tunaomba kwamba Wizara ya Fedha ilifuatilie suala hili kwa karibu kuhakikisha vitendo kama hivyo havitokei na vinakomeshwa mara moja kama vipo.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu imewahi kutembelea Viwanda vya Mafuta ya Kula vilivyopo Mjini Dar es Salaam na Morogoro. Moja ya malalamiko ya wenye viwanda hivyo ni kuwepo waagizaji wa mafuta ghafi kutoka nje ambao wamekuwa na vitendo vya kukwepa kulipa kodi kwa Serikali kwa kuingiza mafuta yasiyosafishwa na kutozwa kodi ya mafuta ghafi.

Aidha, Kamati imebaini pia kuwa waagizaji hawa pamoja na kuagiza mafuta ghafi, lakini pia hawana viwanda vya kusafisha mafuta hapa nchini. Kamati inashauri Wizara iwafuatilie kwa karibu wafanyabiashara wa aina hii na ikibidi utafiti ufanyike kwa kuhakiki leseni za bishara zao na hatua za kisheria zichukuliwe endapo itagundulika kuwepo kwa vitendo hivyo vya kulihujumu Taifa letu.

Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya fedha kuwapa unafuu wa kodi wenye viwanda waliofunga mitambo ya kusafisha mafuta mpaka ngazi ya mwisho *(refined edible oils).* Kuna baadhi ya viwanda hawajafunga mitambo hiyo, lakini wanajidai kwamba wanasafisha mafuta. Hawa ndio tunaosema kwamba kwa kweli wabanwe na walipe kodi. Lakini kuna baadhi ambao ni kweli wamefunga viwanda na katika ziara ya Kamati yangu tulivikuta viwanda hivyo, basi hawa wangefikiriwa kupewa unafuu *on the selective basis,* kulingana na gharama ambazo wamezifunga. Ni kweli kwamba mbegu za mafuta hapa nchini hazitoshi na haziwezi kupatikana ghafla kwa mara moja, kuna haja ya pande zote mbili, Wawekezaji pamoja na Serikali na Wananchi wenyewe kuongeza uzalishaji wa hapa ndani.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Wizara kuendelea kudhibiti ujazi wa fedha ili ulingane na ukuaji wa uchumi, kuongeza jitihada za kuziba pengo la Bajeti ya matumizi ya kawaida ya Serikali, kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei na kuchukua hatua kuimarisha Shilingi ya Tanzania ambayo inaendelea kushuka thamani siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, napenda niwapongeze Mawaziri wote wawili, Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ndugu Enos Bukuku, Naibu Katibu Mkuu, Ndugu O. M. S. Bendera, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Ndugu Grey Mgonja, Katibu Mkuu Wizara hiyo

tena Ndugu Peniel Lyimo na wasaidizi wao wote, kwa kazi nzuri waliyoifanya hasa walipokuja mbele ya Kamati kwa kujibu maswali yetu na kwa hiyo kuwezesha kazi ya Kamati yangu kuwa nyepesi. *(Makofi)*

.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kutamka kwamba naunga mkono hoja ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na hoja ya Wizara ya Fedha na kuliomba Bunge lako Tukufu lizipitishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kabla sijamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, nawataarifu wale ambao watachangia mara baada yake. Wote hawa wamechangia mara moja tu huko siku za nyuma, nao ni Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Mpeme, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Nazir Karamagi na Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa.

Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, atoe maoni ya kambi hiyo. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI NA WIZARA YA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba mniruhusu niwasilishe maoni ya Kambi ya Upinzani kwa hoja zote mbili zilizowasilishwa na Waziri wa Mipango na Ubinafsishaji pamoja na Waziri wa Fedha.

Awali ya yote, naomba kuwapongeza Mawaziri wote kwa kazi nzuri walizofanya, Makatibu Wakuu wao na wasaidizi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majukumu ya Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji, yameelezwa ndani ya kitabu cha hotuba ya Waziri na hivyo sitapenda kuyarudia.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwaeleza Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji kwamba, hadi sasa Watanzania wamo ndani ya dimbwi la umaskini, hivyo naomba watumie utaalam wao ili kuhakikisha kwamba wanafikia lengo la kuondokana na umaskini walionao.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2002/2003 Waziri alikiri kuwa Mpango wa Muda wa Kati bado haujakamilika na ni wazi kuwa hauwezi kufikia malengo bila ya kuwa na kigezo cha kupimia ambacho ni Mpango wa Muda wa Kati. Ninamwomba Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge hili Tukufu ni lini mpango huo utakamilika?

Mheshimiwa Spika, kwa kutokuwa na Mpango wa Muda wa Kati ni sawa na kutabiri tu kwamba mpango wa muda mrefu utafikiwa.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Muda wa Kati ndiyo unaotoa mwanga wa namna Wilaya, Kata, Tarafa na Vijiji vitakavyoshiriki kikamilifu katika mipango ya nchi, vinginevyo tutabaki na mfumo wa zamani wa *Central Planning* ambapo Wananchi hupokea maagizo tu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri mpango wa muda wa kati uharakishwe ili Wananchi waone kama kweli wanaweza kuondokana na umaskini ifikapo mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tuko ndani ya utandawazi, hivyo mfumo wa mipango yote na usimamizi wa uchumi wetu lazima ulenge katika kuwa na uchumi unaoweza kupenya kwa urahisi ndani ya chumi za nchi nyingine. Uchumi ulio ghali hauwezi kupenya kwenye soko kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, hivyo, Kambi ya Upinzani inashauri Serikali ianze haraka kubainisha maeneo yanayofanya uchumi wetu uwe ghali kwa mfano *VAT* huko Kenya ni 16% wakati yetu ni 20%. Kutoa mizigo bandari ya Mombasa ni saa 48 tu wakati hapa kwetu kwa muda mfupi ni siku 5 na hufikia mpaka siku 21. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili nitalifafanua zaidi wakati nitakapozungumzia bajeti ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, vile vile, viwango vya umeme, mradi wa aina moja kutekelezwa na Taasisi tatu, kwa mfano mradi wa *Fibre Optic Cables* unaotekelezwa na Asasi tatu za *TANESCO, TRC* na *TTCL* ni miongoni mwa mambo yanayoongeza ughali wa uchumi wetu, madeni makubwa yasiyoweza kulipika, hivyo kuwaongezea Wananchi mzigo wa kulipa madeni kama ilivyo kwa *IPTL*. Aidha, gharama za simu kwetu ni ghali hata kuliko *DRC* ambako kumekuwa na vita muda wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inasisitiza tena kuwa hatuwezi kupunguza ughali wa uchumi wetu na mzigo wa madeni bila ya kuwa na *proper coordination* ya uwekezaji na utumiaji wa raslimali zetu.

Mheshimiwa Spika, katika Kitabu cha Utekelezaji wa Ahadi za Serikali Bungeni ukurasa wa 259 juu ya kuratibu shughuli za kisekta, haionyeshi tathmini ya utekelezaji wa uratibu huo na ndiyo maana bado Asasi nyingi zinafanya mipango yake na kutekeleza bila ya Asasi nyingine yenye shughuli kama hiyo kuarifiana. Kwa mfano niliokwisha utoa wa *TRC, TTCL* na *TANESCO*. Hivyo, Kambi ya Upinzani inaomba ipatiwe taarifa ya tathmini ya utekelezaji na siyo ya kupewa maelezo ya jumla jumla tu.

Mheshimiwa Spika, eneo jingine ambalo Wizara na Serikali kwa jumla iliahidi kulifanyia kazi ni misaada na mikopo ya Tanzania. Tanzania tunapata kwa wastani wa 45% ya misaada na mikopo katika Bajeti yetu. Lakini bado hatujafanya tathmini ya kujua kwamba ni kiasi gani cha fedha hizo zinakwenda kwenye utawala wetu, ambao ni mkubwa sana, utawala wa waliotupa misaada na kiasi gani kinakwenda kwenye miradi na ni kiasi gani kinakwenda kwenye semina na warsha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, watalaam wengine tunaoletewa hata uwezo wa kuandika taarifa hawana, licha ya uwezo wa kufanyakazi na mishahara yao ni mara 5 ya watu wetu wenye ujuzi na uwezo kuliko wao.

Kambi ya Upinzani inashauri tathmini ya misaada na mikopo ifanywe ili tusiwe tunakopeshwa fedha, lakini 40% hadi 50% inarudi kwao kwa kulipia *technical assistance,* warsha na semina na sisi tunabaki na deni lenye riba isiyolipika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na ushirikiano wa kiuchumi na nchi za Afrika Mashariki, *SADC* na sasa *NEPAD* ni muhimu kuanza utaratibu wa kuratibisha ushirikiano huo kwa maana ya kuangalia faida na hasara.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, Kamati za Bunge zipatiwe muda wa kutosha ili zipewe uchambuzi wa kina wa hasara na faida ili ziweze kuishauri Serikali ipasavyo. Kwa kuwashirikisha Wabunge, kwa sehemu kubwa tutakuwa tumewashirikisha Wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ubinafsishaji ambao unaambatana na uwekezaji umekuwa ni sera muhimu ya Serikali, hasa tangu 1992, ambapo Serikali ilianzisha Tume ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC)* kupitia uamuzi wa Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania *(Tanzania Investment Centre - TIC)* na Taasisi ya Kutathmini na Kukusanya Madeni ya Mashirika ya Umma *(LART),* ambazo zote ni Taasisi/Asasi zilizoanzishwa na Serikali kupitia mikono yake mbalimbali katika miaka ya 1990 na miaka ya mwanzo ya 2000, zina mchango na nafasi muhimu katika zoezi la ubinafsishaji na uwekezaji Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani kila siku imekuwa mstari wa mbele kuiunga mkono Serikali katika Sera yake ya Ubinafsishaji, kutokana na madhumuni makubwa ya Sera hiyo ya kuongeza Pato la Taifa, kuboresha hali ya wafanyakazi na kuongeza ajira.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Kambi ya Upinzani inaona zoezi zima la ubinafsishaji si shirikishi. Utafiti wa *REDET* unaonyesha kuwa ni asilimia 55 tu ya Wananchi ndio wanaojua umuhimu wa Sera nzima ya Ubinafsishaji, ambao wengi wao wako Mijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, Mashirika yaliyobinafsishwa hadi ngazi ya makubaliano ya awali *(MOU)* mnamo tarehe 30 Juni, 2003 ni 32 yenye thamani ya shilingi bilioni 6.6 na malipo yaliyopokelewa na *PSRC* hadi Juni ni shilingi bilioni. 1.4. Kwa hali hiyo, Serikali imeshapokea asilimia 20.6 ya malipo tu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani ina wasiwasi juu ya malipo ambayo hayawasilishwi Serikalini. Kwa hiyo, inaitaka Serikali itoe tathmini sahihi ya mapokea ya pesa ambazo zimelipwa na Mashirika hayo. Pia, Serikali imeshindwa nini kumuuzia Mwekezaji mwingine kama sera inavyosema?

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kiwanda cha *Morogoro Polyester Mill* kimeuzwa, lakini Mwekezaji *(21st century)* amekuwa akipunguziwa bei kila kukicha kutoka dola milioni 7 hadi dola milioni 3 na kupewa masharti mapya wakati wapo Wawekezaji walio tayari kulipa fedha taslim, lakini hawapewi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kurejea katika muhtasari wa mapato na matumizi ya fedha taslimu zitokanazo na ubinafsishaji wa mashirika ya umma. Bila shaka kila mwananchi anapenda apate mapato ili atumie pato hilo katika kukidhi mahitaji yake mbalimbali. Kwa mfano, mwisho wa mwezi, kila nyumba ya mfanyakazi yenye watoto utaona kuna furaha na watoto wanacheza kwa sababu wana uhakika wa kula, kulala na mavazi. Tunachotaka kusema ni kwamba, Maisha yanaboreshwa iwapo kuna kipato na si vinginevyo. Kwa kuanzia, tangu mwaka 1993/1994 mpaka 2002/2003, mapato ya fedha taslimu yatokanayo na ubinafsishaji ni Sh. 217.2 bilioni. Kati ya fedha hizi, asilimia 42.2 zilihamishiwa Hazina, 42.7 zililipiwa madeni ya mashirika pamoja na mafao ya wafanyakazi, asilimia 5.3 ililipia gharama za *PSRC* na ni kiasi cha asilimia 0.6 tu kilitumika kwa kulipa gharama za Mfuko wa Ubinafsishaji *(PT)*. Salio la fedha taslimu Sh. 19.09 bilioni ambayo ni sawa asilimia 8.78. Kwa mchanganuo huo tumeonelea kwamba, ni budi wananchi wakafahamishwa maana ya kiasi kilichohamishiwa Hazina (Sh.91.81 bilioni) kuhusiana na maswali yafuatayo:-

(a) Je, hii fedha iko wapi na inafanya nini? *(Makofi)*

(b) Kwa nini Mfuko wa Ubinafsishaji ambao ndio uliotegemewa kuwawezesha Watanzania, kumiliki uchumi wao ukawa mdogo kuliko hata ule wa kuendeshea *PSRC. (Makofi)*

(c) Hizi Sh.91.81 bilioni zilizohamishiwa Hazina zilitumika kwa shughuli gani? *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani ilitegemea kwamba, baada ya kupata mapato ya ubinafsishaji, waliokuwa wafanyakazi wa mashirika husika wengelipwa mafao yao haraka iwezekanavyo na siyo vinginevyo, kama tunavyoona sasa hivi kwa *Tanzania Elimu Supplies*. Mheshimiwa Waziri, alieleze Bunge sababu za kutofanyika malipo ya mafao husika kwa wafanyakazi wanaopoteza ajira katika Mashirika yanayobinafsishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mkazo mkubwa wa ubinafsishaji sasa umejichimbia katika Mashirika ya Miundombinu ya Kiuchumi kama *TTCL, ATC, DAWASA* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ni wazi kwamba, taasisi hizi ni nyeti sana hivyo umakini wa hali ya juu unahitajika katika ubinafsishaji wake.

Mheshimiwa Spika, tunasema hivyo baada ya manung'uniko mengi kutoka kwa wananchi na zaidi ni kutokana na taarifa ya *PSRC* kwamba, hadi leo *NBC* haijalipa hata senti moja au taarifa hii si sahihi?.

Mheshimiwa Spika, kulingana na haya machache niliyoyasema, bado suala la ubinafsishaji wa Mashirika linahitaji upembuzi wa kina ili kubainisha matatizo na kasoro zilizopo zinazojitokeza na kutafuta ufumbuzi wa haraka.

Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na *PSRC* lakini Kambi ya Upinzani inasema kwamba, kutokana na utata huo kujitokeza, tunashauri tathmini ya ubinafsishaji na uwekezaji katika Mashirika na Makampuni ufanywe na vyombo binafsi ili ufanisi wake uwe wazi zaidi. Aidha, Mashirika yaliyobinafsishwa, wawekezaji wake wameonekana hawana uwezo wowote. Wanapoteza muda na kuharibu raslimali za nchi.

Mheshimiwa Waziri, awasilishe taarifa kwenye Kamati za Kisekta zinazo husika ili ufumbuzi wa haraka uchukuliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba Serikali ikumbuke kuwa hakuna nchi inayoendelea kiuchumi kwa uchumi huo kumilikiwa na wananchi bila ya kuwa na asasi zake za kifedha, ambazo zina uwezo wa kuwapatia mikopo ya muda mrefu na mfupi wawekezaji wananchi bila ya usumbufu.

Hivyo, Kambi ya Upinzani inaishauri tena Serikali kuwa ifanye utafiti wa kutosha na iwashirikishe Wabunge kikamilifu kabla ya kubinafsishwa *NMB, TIB* na Benki ya Posta, ambazo ndiyo chachu ya kuwawezesha wananchi kumiliki uchumi wa nchi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Nchi yetu kutokana na kuwa kisiwa cha amani na kuwa na vivutio vingi vya uwekezaji, imeweza kupata wawekezaji wengi kwa muda mfupi. Hatuna budi kuipongeza Serikali na asasi ya uwekezaji kwa ushawishi uliofanyika hadi kuwapata wawekezaji hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi hii nzuri iliyofanyika na inayoendelea kufanyika, ni dhahiri kuwa yapo matatizo mengi ya kiutekelezaji na hata ya kisera, ambayo bado yameshindwa kufanyiwa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, kama hatujawa na sera ya kuhakikisha kuwa Watanzania wenyewe wanawezeshwa kumiliki angalau aslimia 40 ya mradi unaotekelezwa nchini, asilimia 60 ya uajiri, ni dhahiri tunapalilia umaskini, tofauti ya walio nacho na wasio nacho, uvunaji holela wa raslimali na kupelekwa nje ya nchi na la hatari zaidi, kuongezeka kwa uhalifu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukiangalia mapato yanayotokana na uwekezaji kwenye madini na ukiangalia mazingira ya ndani ya migodi halafu ukalinganisha na wananchi wanaoishi pembezoni mwa migodi hiyo, ndiyo utajua tunachovuna Watanzania. Ukiacha mrahaba wa 3% na ajira ya vibarua, pato kubwa wanalopata Watanzania wanaoishi pembezoni mwa migodi ni vumbi lililojaa ndani ya hewa wanayovuta kila siku na lililojaa ndani ya nyumba zao za nyasi, jambo ambalo linaashiria hatimaye Ugonjwa wa Kifua Kikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaendelea kuishauri Serikali ifanye uchanguzi wa athari wanazozipata ndugu zetu walioko pembezoni mwa migodi hasa za afya zao ili hatua za haraka ziweze kuchukuliwa. *(Makofi)*

Aidha, Serikali izibane kampuni zilizowekeza kwenye migodi kuchukua kila tahadhari juu ya uchafuzi wa mazingira na hasa afya za raia wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa upande Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji, naomba kumpa ushauri wa jumla kama ifuatavyo:-

Kwanza, Waziri afikirie sana ku-*decentralize* mipango hasa Uwekezaji kuwe na Ofisi za Kanda kama ilivyo Msumbiji.

Pili, Serikali kwa kupitia asasi za mamlaka, iyasimamie kimakini mashirika au makampuni ili yaendeshwe kibiashara na tuwaachie viongozi wataalamu wayaongoze kitaaluma badala ya kupenyeza siasa kama ilivyojitokeza *(NMB)*. *(Makofi)*

Tatu, *PSRC* na *LART*, wawalipe haraka kiinua mgongo na mkono wa kwa heri wafanyakazi wa Shirika la Vifaa vya Elimu *(TES)* badala ya kuwazungusha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waswahili wanasema mcheza kwao hutunzwa, naomba nichukue fursa hii kuipongeza Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji, kwa kukiimarisha Chuo cha Mipango na Maendeleo Vijijini, kilichopo Dodoma kwa kugharamia mradi wa ujenzi wa mabweni, ukarabati wa majengo, ununuzi wa vifaa muhimu kama Kompyuta, mafunzo kwa wanafunzi, ongezeko la wanafunzi na kadhalika. Aidha,

tunaupongeza Uongozi wa Chuo, kwa utunzaji bora wa Mazingira ya Chuo. Namwomba Mheshimiwa Waziri na Wizara yake, itoe udhamini wa asilimia mia moja ya wanafunzi wote waliopo Chuoni.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, Nawapongeza Waziri wa Fedha na timu yake, kwa kazi nzuri wanazozifanya. Pia napenda kuipongeza Idara ya Wakusanya Kodi, kwa kazi nzuri wanayoifanya.

Mheshimiwa Spika, lakini pongezi pekee naomba nizitoe kwa Mama Nyoni, Mhasibu Mkuu wa Serikali, kwa uchapaji kazi na ubunifu mkubwa alionao katika kutekeleza majukumu yake. Ni imani yangu na Kambi ya Upinzani kwamba, Serikali itawatunza watumishi wa aina hii ili Taifa liendelee kujijengea uwezo wa kiutendaji, jambo ambalo hivi sasa ni tatizo kubwa katika nchi yetu na hata katika Bara la Afrika kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila kama sikumshukuru Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, Mheshimiwa Njelu Kasaka na Wajumbe wake wote, kwa mchango wao kwangu kama Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani, lakini pia kwa kunialika katika vikao vyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, moja katika kazi muhimu za Serikali yetu ni kukusanya mapato yanayotokana na vianzio mbalimbali ndani ya Sheria ya Kodi. Hivyo, ukusanyaji wa kodi ni muhimu sana katika kuiwezesha Serikali kutimiza ahadi zake.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali kwa kupitia *TRA* kwa kuweza kuvuka lengo la ukusanyaji wa kodi.

Kuna hili suala la kukwepa kulipa kodi aidha kwa vibali vya Wakuu Serikalini au kwa kukwepa kiujanja, rushwa au mtu anakataa kwa mabavu tu na halipi. Hali hii imekuwa inaikosesha Serikali mapato sana. Kwa mfano, mwaka 2001, kulitokea uingizwaji wa Sukari zaidi ya tani 3,000 kwamba, ni mali ya Jeshi na kama tunavyoelewa, mali ya Serikali hailipiwi kodi wala ushuru, haikuchukua muda mrefu, sukari hiyo ikaonekana kama vile haikuwa mali ya Jeshi na suala hilo haijulikani jinsi lilivyoisha. Hebu tujiulize ni bidhaa ngapi hazilipiwi ushuru? Kama Wizara ya Fedha ingekuwa makini katika ukwepaji na kulipa kodi na kutoza faini *(Royalties)* ya asilimi 30; je mapato yangekuwa kiasi gani? Kwa hali hii, tungependa Serikali itoe takwimu ya bidhaa ambazo hazikulipiwa kodi na thamani yake kodi kama ingelipwa pamoja na *Royalties* iwapo amebainika kukwepa kulipa kodi. Hii itatuonyesha kwamba, Serikali imekuwa ikifuatilia ulipaji na ukwepaji kodi kwa mujibu wa sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mfano mwingine ni makampuni ya wenzetu kutoka nje ambayo kutokana na teknolojia waliyonayo, wanafanya Ofisi za hapa Tanzania kuwa matawi ya kuuzia bidhaa zao tu. Kwa maana hiyo, mahesabu yote hufanyika Makao Makuu, ambayo ni nje ya nchi, *transactions* zote zinarekodiwa nje ya Tanzania, kitu ambacho ni kigumu kwa *TRA* kukusanya mapato barabara. Mfano wa Kampuni kama hizo ni *Stars*, Mabenki na kadhalika. Yaani Maofisa hata wakienda kufanya ukaguzi, hawaoni ndani kwani teknolojia yao ni ya hali ya juu sana.

Kingine ni kuhusu vifaa vya kisasa vinavyoingizwa na makapuni ya wawekezaji ambayo hayatozwi ushuru kulingana na thamani yake na hivyo hutokea kutozwa ama ushuru mkubwa au mdogo, mfano, ni *Data Cabinets.* Hii inatokana na Wataalam wa *TRA* kutofahamu bidhaa hiyo vizuri na hata katika orodha ya *TRA* vifaa kama hivyo havimo kabisa. Hivyo basi, kazi hufanyika kwa kubuni na kukosesha Serikali mapato halali. Kwa hali hii, tunaishauri Serikali kuweka wafanyakazi wenye taaluma hizo au kusomesha wafanyakazi ili waendane na hizi mbinu mpya zinazojitokeza siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, tunapenda kutoa pongezi kwamba, mizigo mingi inayoingizwa bandarini hukaguliwa vizuri sana na mfano mzuri ni yale magogo yaliyokamatwa yakiwa na bhangi ndani yake. Hiyo ilionyesha kwamba, ukaguzi wa mizigo ni jambo la msingi na la kusifia. Ukaguzi huu sio mbaya isipokuwa huchukua muda mrefu na hata wakati mwingine husababisha usumbufu wa nenda rudi kesho. Hali hii imekatisha tamaa sio Watanzania tu bali hata wa kutoka nchi jirani na kuamua kupitisha mizigo yao mathalani nchini Kenya, ambako mzigo unatolewa kwa muda wa saa 48. Lakini uzoefu wetu sisi hapa

unaonyesha kuwa inachukua wiki 3 hadi 4 kutoa mzigo. Hii inatokana na mlolongo mrefu wa ukaguzi, malipo na kadhalika na asasi zinazohusika kuwa nyingi sana. Kwa mfano, utaratibu uliopo na unaotumika ni kwamba, mzigo unapofika bandarini, lazima uanzie *COTECNA,* ambapo huchukua siku 3 na hapo mwagizaji hulipa asilimia 0.2 ya thamani ya *Free on Board*. Baada ya hapo, utachukua fomu zako na kwenda *Long Room*. Hapa *Long Room,* utapata *TIN, Face Vet, Data Input,* utapitia vile vile kwa *Head Declaration Officer* na *ICS* ambao wanafanya tathmini ya mali na kuhakiki thamani yake. Mpaka hapa, utakuwa umemaliza *Long Room* na kuelekea bandani *(wharf).*

Utaratibu huu wa kutoa mzigo ina sehemu takribani 19 na kuna shughuli ambazo zinajirudia au kufanyika na vyombo viwili tofauti. Kwa mfano, kazi inayofanywa na *COTECNA* ni sawa na inayofanywa na *ICS.* Shughuli zinazofanywa na *(Head Declaration Officer)* na za *Wharf,* zimejirudia mara mbili ambazo zinaweza kufanywa mara moja. Kwa hali hii, Kambi ya Upinzani inashauri Serikali iangalie utaratibu wa kutoa mzigo ili kweli uwe saa 48 na siyo kama ilivyo sasa. Mfano mzuri ni Bandari ya Mombasa, ambayo mzigo hutolewa kwa siku mbili tu na wengi wafanyabishara hupenda kupitishia mizigo yao Mombasa Kenya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala hili la usumbufu linatokea vile vile kwa wafanyabiashara kutoka Zanzibar wanapoleta bidhaa zao kupita bandarini au viwanja vya ndege vya Tanzania Bara. Kwa kweli hawa wafanyabiashara wamekuwa wakilalamika sana kuhusu mlolongo mrefu wa wao kutoa mizigo yao hususan Bandari ya Dar es Salaam na Tanga. Tunaishauri Serikali kwamba, Tanzania ni nchi moja na kwa nini tusumbuane? Ni budi utaratibu uwekwe bayana kwa kila mfanyabiashara ili aelewe cha kufanya wakati wote yaani anapotoa au kusafirisha mzigo toka upande mmoja kwenda mwingine wa Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata magari yenye *registration* za Zanzibar yanachukuliwa kama nambari za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kukusanya ni sehemu moja na matumizi ni sehemu ya pili. Serikali katika kudhibiti matumizi imeendelea na utaratibu wa *Cash Budget. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo mazuri ya Serikali juu ya kuendelea na *Cash Budget*, lakini lazima Serikali ikubali kuwa utaratibu huu hauwezi kuwa wa kudumu. Athari za kuendelea na utaratibu huu kwa muda mrefu, upo uwezekanao wa utaratibu wa kawaida wa kuendesha Serikali ukasahauliwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba yetu ya Bajeti, tuligusia suala hili na kuelezea athari zake kwamba, matumizi yanaweza kufanywa bila ya idhini ya Bunge na hatimaye Bunge likatakiwa liidhinishe *Excess Vote.*

Mheshimiwa Spika, mfano ulio hai ni *Excess Vote* ya 2000/2001, ambayo kiasi cha shilingi bilioni 4 zilitumika kwa vifungu 34, 72, 75, 81, 85. Ukichukua *Vote* 34 peke yake, itakuwa imeongezewa katika Bajeti yake ya mwaka 200/2001 Sh. 4.00 bilioni. Lakini la kushangaza zaidi ni kuwa ukiangalia *Sub- vote 2001 Embassy of Addis Ababa* 2000/2001, Bunge liliidhinisha Sh. 242 milioni, *Excess Vote* ni Sh. 224 milioni. Hivyo, fedha zote zilizopelekwa Ubalozini kwa mwaka huo ni 466 milioni. Hii ndiyo hali ya karibu *Embassy* nyingi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa maji yakishamwagika hayazoleki, ndiyo maana Kambi ya Upinzani, inaitaka Serikali iache utaratibu wa *Cash Budget,* utaratibu wa kufanya *re-allocation* ufuate utaratibu wa kanuni za fedha, *Excess Vote* lazima kwanza ipate idhini ya Bunge, uchambuzi wa kina wa mahitaji ya Balozi zetu ufanywe kwani inaonekana kuna ubadhirifu mkubwa wa fedha na utunzaji mbaya wa samani za Serikali. Ili kudhibiti ununuzi wa vifaa kwenye Balozi na Ofisi za Serikali, ni vyema tukawa na *Standard* zinazoeleweka ili kuepuka kununuliwa vifaa vyenye thamani ya chini na malipo yakawa hewa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa pongezi kwa Serikali, kwa kuunda Tume ya pamoja ya Muungano ya Fedha kama ilivyoagiza Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Katiba ya Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miaka yote iliyopita karibu 38 tulikuwa tukifanya makosa makubwa kwa kutokuwa na Tume hii, jambo ambalo lilichangia sana manung'uniko ndani ya Muungano wetu, juu ya mapato na matumizi ya Serikali ya Muungano yatakayochangiwa na Serikali mbili. *(Makofi)*

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano kifungu 133, Serikali ya Jamhuri ya Muungano itatunza akaunti ya Fedha ya pamoja na ambayo itakuwa ni sehemu ya Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, ambayo kutawekwa fedha yote itakayochangwa na Serikali mbili kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume ya pamoja ya fedha. Naomba kurejea kumpongeza Mheshimiwa Shelukindo, kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Tume hii muhimu katika kudumisha Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni matumini ya Kambi ya Upinzani kuwa Bajeti inayokuja, Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, litakuwa limepata Bajeti iliyotokana na ushauri wa Tume hasa katika mchango wa Muungano wa Serikali mbili kuichangia Serikali ya Jamhuri ya Muungano katika kuendesha mambo ya Muungano kwa mujibu wa Katiba. Pamoja na majukumu hayo, Kambi ya Upinzani inaishauri Serikali iitumie Tume hii, kujadili madeni ya Zanzibar na ya Serikali ya Jamhuri ambayo yamekuwa sehemu ya manung'uniko kwa kila upande. *(Makofi)*

Mfano, ulio hai ni huu wa *TANESCO*, ambapo kila mmoja anamtupia lawama mwenzake, lakini naamini uchambuzi wa kina ukifanywa, kwa mfano, Zanzibar wanadai kuwa ndege za kivita na mizinga ya Masafa marefu yalinunuliwa kutokana na Hazina ya Zanzibar. Aidha, Zanzibar wanadai kuwa gharama za mradi mzima wa umeme kupeleka Zanzibar ulilipwa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, hisa zao kwa *BoT* na kadhalika. Hoja zote hizi zinaweza kupatiwa majibu kupitia Tume ya pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la muhimu ni kuwa kama tunaweza kufutiwa madeni na nchi nyingine, je, sisi tulio nchi moja tunashindwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Waziri aipe Tume vitendea kazi ili itusaidie katika kupunguza misuguano ambayo isipodhibitiwa haraka, itaweza kuleta ufa ndani ya Muungano wetu.

Mheshimiwa Spika, kutokana na kigezo cha mapato yaliyopatikana kutokana na misaada na mikopo mwaka wa fedha wa 2002/2003 kwa asilimia 36 kwa miradi ya maendeleo na asilimia 59.6 kwa matumizi ya kawaida, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa kiwango kikubwa cha mikopo na misaada inayopelekwa kwenye matumizi ya kawaida ni hatari kwani, sehemu kubwa haina uzalishaji au kama upo ni wa muda mrefu sana, hivyo ipo hatari hatimaye kushindwa kulipa madeni kutokana na kutumia fedha hizo nyingi kwenye utawala kuliko uzalishaji. Pia, Serikali itashindwa kusimamia maamuzi yake kutokana na kufadhiliwa hata kwa kuendesha Serikali yenyewe. Vile vile Miradi ya Maendeleo itakwama kama ilivyokosa fedha mwaka 2002/2003, makisio ya Bajeti yalikuwa asilimia 34 ya matumizi yote, lakini hadi Julai, 2002 mpaka Machi, 2003 ni asilimi 19 tu iliyopatikana.

Mheshimiwa Spika, kama tulivyotoa ushauri kwa Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji, ni vizuri Wizara hizi zikashirikiana katika kufanya tathmini ya mikopo hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2002/2003, Wizara ilitenga Sh.13 bilioni na matumizi ya *Treasury Vouchers* kawa Sh. 1.5 bilioni, mwaka huu Wizara imetenga Sh. 31.5 bilioni, je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwa kufanya hivyo, kaongeza nakisi kwenye Bajeti bila sababu kwa kupanga matumizi ya fedha ambayo ana hakika hayatotumika; kwa kuwa hata nusu ya kiwango cha mwaka 2002/2003 hakikufikiwa, kwa nini asiweke kile kile cha 2002/2003?

Kambi ya Upinzani inaona haya ni sehemu ya mapungufu ya *Cash Budget,* hivyo inaishauri Wizara iwe na uhakika wa mahitaji yake.

Mheshimiwa Spika Idara ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, iimarishwe kwa kupatikana Wakaguzi wenye ujuzi na uwezo wa kufanya kazi yao, kutengeneza *Financial Regulation Hand Book*, ili

kila mmoja aelewe majukumu yake na kwamba, kosa litakapotokea siyo tu kwamba, aliyetenda kosa, lakini hata yule aliyeteuliwa kwa mujibu wa Kanuni, kusimamia na kumsimamia huyo aliyetenda kosa, naye anachukuliwa hatua, jitihada za makusudi zifanywe za kumaliza ukaguzi kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, tunaomba kuipongeza *Management* ya *BoT*. Kambi ya Upinzani inapenda kuelimishwa juu ya kasi ya kukua kwa uchumi na kuteremka kwa shilingi yetu, jambo ambalo linatupa wasi wasi wa kuwa na bidhaa ghali hasa bidhaa zinazotokana na mafuta, ambazo zikipanda na vitu vingine vyote vinapanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile tunashauri Serikali katika kubinafsisha *NMB, TIB* na Benki ya Posta. Kuna Benki inaitwa *Grameen Bank* ya Bangladesh *(A Bank of the Poor),* ilianzishwa na Serikali, Benki Binafsi na wananchi. Benki hii ilianza na wateja 15,000 mwaka 1980 na hadi 1998 wakawa na wateja 2.34 milioni kati yao 2.24 ni wanawake ambao aslimia 95 wanalipa mikopo yao kati ya asilimia 98 ya walipaji wote.

Mheshimiwa Spika, mbali na Benki hiyo pia tunaomba kuanzishwa kwa haraka Benki ya Kilimo na Viwanda itakayoweza kutoa mikopo ya muda mrefu. *(Makofi)*

Napenda kurejea suala la ushuru katika Tanzania Visiwani. Ni jambo lisilofichika kwamba, ushuru unaotozwa kwa pande zote za Muungano ni mmoja *(Tax Harmonization),* lakini gharama ya usafirishaji wa mizigo toka sehemu mbalimbali nitofauti. Kwa mfano, kusafirisha *container* ya futi 20 toka Ulaya kuja Dar es Salaam inagharimu Dola 1,500 na mzigo huo huo unaposafirishwa kwenda Zanzibar unagharimu dola 2,000. Kwa kusafirisha *container* ya futi 20 kutoka Bankok (Thailand) inagharimu Dola za Marekani 2,500 kuja Dar es Salaam na *container* hiyo hiyo inagharimu dola 3,600 kwenda Zanzibar, kusafirisha gari dogo *(Saloon)* kutoka Dubai kuja Dar es Salaam inagharimu Dola 475 na kwenda Zanzibar. Kwa kuipa upendeleo wa makusudi Zanzibar, kunaweza hata kuondoa mgogoro uliopo katika mgawanyo wa mapato katika Jamhuri ya Muungano. Vile vile Kambi ya Upinzani inaamini kwamba, hali hiyo itaufanya uchumi kukua kirahisi na kwa haraka zaidi. Pamoja na hayo, tunaamini kwamba, Zanzibar ikiwa Bandari Huru, nchi za Afrika Mashariki na Kati watatumia bidhaa zinazopitia Bandari ya Zanzibar. Hali hii siyo tu kupitisha mzigo bali hali ya uchumi wa Tanzania utakuwa ukipanuka mwaka hadi mwaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la *Central Tender Board,* ambao hutoa zabuni na hatimaye Serikali ikabadilisha utaratibu kinyume cha *Central Tender Board*. Kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, atueleze ni nani mwenye uwezo na mamlaka ya kubadilisha uamuzi wa *Central Tender Board?* Kwa mfano, katika *tender* ya mchele iliyotolewa hivi karibuni, Serikali ilipoteza shilingi 208 milioni. Baada ya kupunguza bei ya mchele kutoka Sh. 203 hadi Sh. 190, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, atueleze hizi fedha zilizopotea shilingi milioni 208 zimekwenda wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nahitimisha kwa kuwaomba Waheshimiwa Mawaziri kuwa, kwa kuwa muda niliopewa ni mfupi kutokana na Wizara zote mbili, basi nitawapelekea hotuba hizi kwa maandishi na naomba majibu yote.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja zote mbili za Waziri wa Fedha na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango. *(Makofi)*

**MHE. SHAMSA S. MWANGUNGA:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kutoa shukrani zangu kwako kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuongea katika hoja hizi. Baada ya hapo naomba uniwie radhi kwa sababu sauti yangu kidogo siyo nzuri inakwaruza, nina uhakika kwamba itasikika.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pongezi kwa Serikali yetu kwa kuhitimisha ujenzi wa Daraja la Mto Rufiji, ambalo kwa kweli ni ushindi mkubwa kwa nchi yetu na ni kitu ambacho ni mlango mkuu wa kuweza kufungua biashara na uchumi mkubwa kutoka Mikoa ya Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kutoa pongezi kwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba na Manaibu wake wawili, pamoja na watumishi wote wa Wizara ya Fedha, kwa jinsi ambavyo wametayarisha hotuba nzuri na pia makadirio mazuri ambayo yanaeleweka na ambayo yamekwenda kwa kina kizuri sana. *(Makofi)*

Pia napenda kutoa pongezi kwa Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, pamoja na Watumishi wote wa Wizara yake kwa Bajeti na makadirio mazuri ya Wizara ya Mipango na Ubinafsishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchangia hoja moja tu ambayo nitaigawanya katika sehemu mbili. Hoja hii inahusu mambo ya ushuru na kodi za bidhaa. Itakumbukwa kwamba, Serikali yetu miaka ya nyuma iliweza kupiga marufuku uagizaji wa baadhi ya bidhaa yakiwemo majani ya chai kutoka nchi za nje. Kitu cha kushangaza hadi leo kuna baadhi ya maduka ya rejareja utakuta bidhaa ya majani ya chai yamejaa na siyo majani yetu tu, majani mengine ya kutoka nchi za jirani. Majani haya ya majina mbalimbali mfano kuna majani yanayoitwa Tausi, ambayo yanauzwa kwa bei ndogo sana ukilinganisha na majani ya hapa nchini kwetu.

Mheshimiwa Spika, majani haya yanaingia kwa njia za panya, kwa njia ambazo kwa kweli ukilinganisha bidhaa zetu za majani ya hapa kwetu, kwa kuwa hawa hawalipi kodi, basi kwa vyovyote vile bei inakuwa ni ya chini ukilinganisha na majani ambayo yanatengenezwa na viwanda vyetu. Swali la kujiuliza ni kwamba, haya majani yanayotoka nchi za nje yanaingia kwa njia za panya na bado yanapokelewa na yanauzwa kama bidhaa yoyote madukani bila aibu wala woga.

Mheshimiwa Spika, majani hayo pia yanatumiwa hapa nchini, lakini ukiangalia nchi za jirani yanakotoka haya majani wenyewe hawayatumii. Hii ina maana kwamba, haya majani huenda yanatengenezwa katika hali ambayo siyo nzuri kiafya na hali ambayo siyo safi. Majani haya kwa kuwa hayapitii katika taratibu zinazofuatwa na Serikali yetu, ni majani ambayo yanaingizwa, hayapimwi hayapiti kwenye Idara ya Viwango *(TBS),* kwa hiyo, ni majani ambayo ni ya kienyeji tu ambapo madukani imefikia hatua hata baadhi wanauza kwa kutumia vijiko, wanachota wanatia kwenye karatasi mtu anauziwa na anakwenda kuyatumia.

Mheshimiwa Spika, majani haya yana athari za aina mbili. Ya kwanza, kiafya ambapo tunatumia majani haya na wananchi wetu wanatumia majani haya bila kufahamu kwamba, kiafya yana uwezo gani au kiafya yaathiri mwili kiasi gani. Pia, majani haya kwa sababu yanauzwa bei ndogo sana, kwa hiyo, hapa nchini tuna viwanda saba vya kusindika majani ya chai, viwanda hivi haviwezi kushindana kuuza na hawa wengine, kwa hiyo, wanakata tamaa na wanauza kidogo. Wanavyouza kidogo, Serikali inapata hasara kubwa kwani Serikali inakosa kipato na inakosa kodi ambayo kama viwanda vyetu vingeuza kwa wingi tungenufaika na tungepata kodi kubwa.

Mheshimiwa Spika, pia haishii hapo tu na hawa viwanda vyetu hivi kama hawawezi kuuza majani mengi ina maana hawawezi kununua majani kutoka kwa wakulima wadogo wadogo ambao ni *out-growers.* Hawa wakulima wadogo watashindwa kuuza majani, kipato chao kitapungua, Serikali itakosa kipato na hapo hapo pia umaskini unarudi pale pale ambao tunajitahidi kumkomboa mkulima mdogo mdogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hali hii, ningependa kuiomba na kuishauri Serikali, ichunguze tena chanzo cha haya majani yanayoingia nchini na ndicho chanzo ambacho kinadhoofisha viwanda vyetu vidogo na pia Serikali inakosa mapato. Tungechunguza hicho chanzo na hapo hapo haraka iwezekanavyo waweze kudhibitiwa na kupigwa marufuku.

Mheshimiwa Spika, baada ya hoja ya majani ya chai, pia ningependa kuchangia kuhusu uuzaji wa madini ya *Tanzanite*. Itakumbukwa tu katika Gazeti la jana la Nipashe la tarehe 3 Agosti, 2003 kumeandikwa habari kwamba, kuna utoroshaji wa madini ya *Tanzanite* kwenda nchi za jirani na yanatoroshwa na baadhi ya wafanyabiashara wawekezaji. Hii ni dhahiri kwamba, utoroshaji huu mpaka kufikia hatua ya kugunduliwa na ingawa Serikali ilianza kuchukua baadhi ya taratibu kukomesha hiyo, lakini bado uchumi wetu kwa njia moja au nyingine umeathirika na tumeumia.

Mheshimiwa Spika, madini hayo yanatoroshwa na wawekezaji na baadhi ya wawekezaji ni wale ambao siyo waaminifu na ni wawekezaji ambao baadhi yao tunawaita *foreign investors.*

Mheshimiwa Spika, kuhusu *foreign investors,* ningependa kuelezea kidogo taratibu ninazozifahamu za uuzaji wa *Tanzanite* kwa upande wa *foreign investors* na kwa upande wa *local investors* zinakuwaje.

Mheshimiwa Spika, *local investor* ambaye anashughulika na yeye katika biashara ya *Tanzanite,* anahitajika alipe *VAT*. Hii *VAT* ni kitendo kizuri na ni kipato cha Serikali yetu. Lakini kina usumbufu kiasi fulani kwa *investor* mdogo kama huyu.

Kwa sababu anahitajika kwanza atoe vithibitisho ya kuonyesha kwamba, yeye kweli kasafirisha hiyo *Tanzanite* na pia imepokelewa kule na imeuzwa ndiyo aweze kurejeshewa ile *VAT* ambayo alilipwa.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia *local investor* anapopeleka biashara yake hii ya *Tanzanite, Tanzanite* ni bidhaa ndogo sana, huwezi ukalinganisha na bidhaa kubwa kama kahawa, pamba, katani na kadhalika, ambapo inabebwa kwa wingi katika magunia na kusafirishwa ambapo wenyewe wakifika kule biashara kama hiyo lazima anapata ile *landing certificate* na ambapo pia ni biashara ambayo ni kubwa.

Tukilinganisha biashara ndogo kama ya *Tanzanite* ambapo *local investor* mwenyewe au muuzaji/mfanyabiashara, hahitaji magunia kuibeba. Anaibeba kwenye mfuko au kwenye *briefcase* na anasafiri nayo yeye mwenyewe kwenda kuuza anakotaka. Huko anakokwenda kuuza sio biashara kubwa ya kwenda kwenye *markets* au wapi, ni biashara ambayo anapita kwa masonara, watu binafsi ambapo anauza polepole.

Hali hiyo inawafanya hawa wa *local investors* wanakata tamaa ya kuweza kupata hizo *landing certificate* au kupata vidhibiti mbalimbali vitakavyomwezesha yeye akirudi nyumbani aweze kurejeshewa *VAT* yake na inachukua muda sana mpaka aweze kurejeshewa pesa za *VAT*. Hali hii inakatisha tamaa, pia anakosa fedha za kuweza yeye kuzungusha tena aendelee na biashara yake.

Mheshimiwa Spika, tukija kwa upande wa *foreign investor,* ambaye na yeye anawekeza katika madini ya *Tanzanite, foreign investor* yeye kitu cha kwanza halipi *VAT*, amesamehewa. *Foreign investor* kitu cha pili masharti yake ni madogo sana anatakiwa awe amewekeza.

Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba, wengi wanawekeza ili Serikali yetu iweze kuwapa leseni za kuweza kufanya hiyo biashara, lakini uwekezaji wenyewe unakuta kwamba, *foreign investor* anakuja kutoka kwao anaingiza hela kidogo Benki tuseme labda anaingiza shilingi milioni 30 ili kuthibitisha kwamba yeye ni *investor* na hapo hapo anaweza akanunua *equipment* kidogo sana. Akanunua labda kama kisu cha kukatia madini, akanunua na darubini ya kuangalizia, basi huyu atapata *certificate,* anakubaliwa kama *investor.* Lakini kitu cha kushangaza pesa hii aliyoiweka kama yeye ni *investor* ndio hiyo hiyo anaichukua Benki ananunulia madini haya anaondoka nayo anakwenda kulipa na *VAT* halipi. Pia hivyo vifaa vidogo alivyoonesha havitumii, anakwenda tu ananunua moja kwa moja madini ya *Tanzanite* na kwa kutumia pesa alizoweka Benki kutuhakikishia kwamba, yeye ni *investor,* anatoka nazo anakwenda anauza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hali kama hiyo nina wasiwasi kwamba, je, Serikali yetu inapata nini hapa? Sioni inachonufaika kwa biashara kama hiyo kwani huyu *foreign investor* alichokiingiza anaondoka nacho chote na ambapo *local investor* yeye atasumbuka kwa kungojea taratibu alizopewa na *VAT* na baada ya hapo hawezi ku-*compete* na huyu *foreign investor* kwa sababu *foreign investor* akishabeba yale madini, akiondoka nayo kule, hana cha kodi wala nini, atakwenda kuuza kwa bei anayotaka. Pia hii inafanya hawa *foreign investor* wakashusha bei kiasi ambacho *local investor* akienda kule nje atauza kwa bei ya hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo na kwa sababu nimeshagongewa kengele ya kwanza, ningeiomba Serikali yetu iangalie vizuri mambo haya mawili, uingizaji holela wa majani ya chai ambapo Serikali inakosa mapato na viwanda vyetu vinaathirika na wakulima wanaathirika. Pili, hizi sheria na kanuni zilizowekwa kwa ajili ya *local investors* katika Ukanda wa Madini ya *Tanzanite,* kwa kweli wanaiumiza Serikali na wanamwumiza *local investor. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, napenda kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ALHAJI AHAMADI HASSAN MPEME:** Mheshimiwa Spika, naomba pia na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja zote mbili zilizopo mbele yetu, hoja ya Wizara ya Fedha, pamoja na hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, naomba nianze juu ya suala la kupambana na umaskini. Umaskini upo kila eneo katika nchi yetu. Maeneo yote ya nchi yetu, watu wetu wana umaskini mkubwa. Isipokuwa umaskini huu tunapitana. Yapo maeneo yana umaskini wa nafuu lakini yapo maeneo yameathirika mno na umaskini. Sasa ni bora tathmini ya umaskini inapofanywa, basi ni vyema mipango iwekwe zaidi kuangalia yale maeneo ambayo yana matatizo makubwa ya umaskini. Pia ziangaliwe sababu za umaskini katika maeneo hayo ni zipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa kwamba, kila eneo linayo au lina raslimali za kutosha kuweza kupambana na umaskini. Lakini inawezekana raslimali zipo ila uwezo wa kuweza kuzitumia zile raslimali ili kuweza kuondoa umaskini ndio mushkeli. Inawezekana mushkeli huo unaletwa labda kwa ukosefu wa miundombinu, wakati mwingine inawezekana mushkeli ukaletwa na ukosefu labda wa elimu ya kutosha kuweza kutumia raslimali zilizokuwepo, sasa hayo yote yaangaliwe. Pale penye matatizo ya miundombinu, basi miundombinu ya kutosha ipelekwe ili kuweka chachu kwa wananchi wa pale kuweza kuzalisha na kutumia zile raslimali katika uzalishaji wa kuondoa umaskini na pia kuweka chachu kwa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, hakuna maendeleo ambayo yatakuja au yatapatikana bila miundombinu. Kama sehemu haina barabara, haina umeme, haina viwanda, kutabiri kupambana na umaskini ni kazi kubwa sana. Sasa ningeomba Serikali iangalie kwamba, ni maeneo gani yana nafuu, maeneo gani yana miundombinu sasa ya kutosha na yale ambayo hayana kabisa, basi miundombinu iweze kupelekwa ili kuweza kupambana na umaskini. Lakini pia bado katika kupeleka miundombinu ni vyema basi kuwashirikisha wananchi waweze kujishughulisha katika uzalishaji mali. Inawezekana wakati mwingine sehemu ina miundombinu lakini wananchi hawajishirikishi kwa ukamilifu katika uzalishaji mali. Kwa mfano, ilivyo katika Wilaya ya Rufiji, ndugu zangu Wandengereko hata kama ungewapelekea miundombinu ya namna gani si rahisi! Wao kazi yao ni kulima mpunga, wakipata gunia mbili, basi wanashukuru Mungu, wanasema tumeshapata. Sasa watu wengine wapo wana hamasa ya kuleta maendeleo lakini tatizo ni miundombinu kwamba haipo ya kukamilika. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningeomba uwezekano wa miundombinu, basi Serikali iweze kushirikisha jamii kwa uwezo wake wote ili kuzalisha mali ili kuweza kuongeza kipato cha kila mwananchi kulingana na ongezeko la watu. Umaskini hauwezi kutoka kama mapato ya nchi hayalingani na ongezeko la watu. Sasa hivi ongezeko la watu limefikia asilimia 2.6 kwa mwaka. Sasa kwa hali hiyo, inabidi kupambana vizuri sana katika kuelimisha jamii ili kuweza kuzalisha mali kwa wingi na kukidhi uwezo wa ongezeko la watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo napenda nizungumzie ni juu ya kutoa kipaumbele kwa wawekezaji Wazalendo pamoja na kuwapa mikopo. Hali hiyo itatuwezesha kumiliki zaidi sisi wenyewe uchumi wa nchi yetu kuliko kama tutaweka kipaumbele kwa wawekezaji, kuwapa wawekezaji wa nje, uchumi wa nchi utakuwa unamilikiwa na watu wa nje. Lakini hata hivyo kuwapa uwezo wa kutoa kipaumbele kwa wawekezaji wetu wa ndani, itasaidia kuwapa uwezo wa kujifundisha umilikaji wa raslimali tulizokuwanazo katika kutoa msukumo wa maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kilimo limezungumziwa sana katika Bunge hili kwamba, asilimia kubwa ya wananchi wa Tanzania wanajishughulisha katika masuala ya kilimo. Sasa ni vyema basi katika kupambana na umaskini, suala la kilimo liwekewe mkazo mkubwa sana. Karibu wananchi wetu milioni 13 mpaka 14 wanajishughulisha na kilimo na katika eneo hilo ndilo eneo ambalo maskini wapo wengi sana, yaani katika eneo la wakulima. Sasa ni vyema kujenga mazingira bora katika kilimo ili wakulima iwaletee tija zaidi. Kilimo cha umwagiliaji kipewe mkazo zaidi. Mategemeo ya kutegemea kilimo cha mvua hakitufikishi mbali na wakulima wetu wataendelea kuwa makini siku zote. Mikopo ya Pembejeo itolewe

hasa kwa wakulima wa chini ambao uwezo wao ni mdogo. Lakini pia mikopo ya vikundi vya wakulima itiliwe mkazo. Viwanda vya kusindika mazao ya kilimo viwekewe mkazo mkubwa. Kulima bila kuwa na viwanda vya kusindika mazao ya kilimo hatufiki popote katika kupambana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie juu ya suala la kuweka mipango kamambe katika msukumo wa Elimu ya Msingi, Sekondari na Chuo Kikuu. Katika dunia ya sasa ya utandawazi, tunahitaji sayansi na teknolojia ili kupambana katika uchumi wa dunia. Kwa hiyo, sayansi na teknolojia inahitaji watu wenye elimu kubwa. Tunashukuru mpango wa MMEM kwamba, utawakusanya vijana wengi sana katika kuondoa ujinga. Lakini bado Elimu ya Msingi haitufikishi au haiwezi ikatusaidia sana katika kupambana na umaskini hapa katika karne ya sayansi na teknolojia. Kwa hiyo, sasa ni vizuri basi tujenge mazingira mazuri au tuwe na mipango mizuri ya kuwezesha hawa vijana watakaomaliza Shule ya Msingi kwa mpango huu wa MMEM, waendelee na Shule za Sekondari pamoja na Vyuo Vikuu ili kuweza kujenga uchumi wa kisasa hapo watakapokuwa na elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, naomba nizungumzie suala la ukusanyaji wa kodi. Pamoja na ukusanyaji mzuri sana wa mapato kwamba, sasa mapato yetu yamefikia kukusanywa shilingi bilioni 110 kwa mwezi, lakini bado ipo mianya ya ukwepaji wa ulipaji wa ushuru au kodi. Wafanyabiashara wa rejareja, pamoja na Wafanyabiashara wa jumla, unapokwenda kununua mali katika maduka wanakupa msimamo kwamba, kama hautaki kuchukua risiti, basi bei utapunguziwa itabakia kiasi kidogo. Lakini ukipewa risiti bei itazidi kwa sababu kuna kodi ya *VAT*. Sasa kwa kupunguziwa bei mtu anaona nafuu zaidi akaacha risiti kuliko kupewa risiti halafu kitu kile akanunua ghali zaidi. Sasa hiyo mianya ipo na ipo mianya katika maeneo ya mafuta na kuna mianya katika maeneo ya madini. Naomba hiyo mianya idhibitiwe ili uwezo wa kukusanya mapato mengi zaidi uwepo.

Pamoja na utaratibu wote wa kupambana na umaskini, lakini mipango yetu inaweza kuharibika kama hatukuangalia kwa makini suala la Ukimwi. Ukimwi ni tatizo kubwa kweli katika Taifa hili, lakini ni pamoja na dunia nzima. Ukimwi umewekwa mahali ambapo kukwepa kwake sio rahisi. Ukwepaji wake ni mzito, mazingira ya kukwepa yanahitaji kuelimisha jamii katika kiwango cha juu sana. Sasa kuhusu elimu ya Ukimwi, ningeomba jitihada zifanyike hasa kwa wananchi wa Vijijini. Semina nyingi sana za Ukimwi zinaishia Mijini, lakini hata Vyombo vya Habari vinaelimisha masuala ya Ukimwi, lakini sasa sio wengi waliokuwa na Vyombo vya Habari Vijijini. Kwa hiyo, ni vyema kuundwe Kamati za Kila Kata ili Kamati hizo zifanye kazi za kuwaelimisha wananchi juu ya suala la Ukimwi, kwa sababu sasa Ukimwi umeshamiri sana Vijijini na unamaliza sana nguvukazi yetu. Kwa hiyo, ningeomba Kamati za Ukimwi ziundwe katika Kata ili uwezekano wa kuwafikishia suala la Ukimwi wananchi walio Vijijini, uwe rahisi zaidi kuliko lilivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, niishukuru Serikali kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu, kwa umalizikaji wa ujenzi wa Daraja la Rufiji. Historia ya barabara ya Dar es Salaam - Kibiti - Lindi - Mingoyo, nadhani inajulikana kwa karne nyingi. Matatizo yalikuwa ni mazito, lakini tunaishukuru sana Serikali kwa kutuondolea kero ile na hakuna cha kuipa Serikali isipokuwa ni kura tu. Serikali ya Chama cha Mapinduzi, hakuna cha kuipa isipokuwa ni kura mwaka 2005. Tunaonya Wapinzani wasiingie tena kule! Maana wakati ule pamoja na kuwa daraja lilikuwa halijakwisha lakini hatukuweza kushawishika kupigia kura Upinzani, sasa baada ya kwisha ile barabara ya Dar es Salaam - Kibiti - Lindi, naomba waondoke, wasiwepo tena Wapinzani kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya shukurani hizo, naomba kuunga mkono hoja zote mbili kwa asilimia mia. Ahsanteni sana. *(Kicheko/Makofi)*

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa na mimi nafasi ya kuchangia hii Miswada miwili. Ningependa niwapongeze Mawaziri wote wawili, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji na Waziri wa Fedha, pamoja na Watendaji wao wote, kwa kazi nzuri waliyofanya, kwa kutengeneza hii hotuba nzuri, inayoonyesha juhudi zao katika kupanga maendeleo ya nchi hii na namna ambavyo mipangilio ya fedha inakuwa kwa kipindi cha mwaka 2003/2004.

Zaidi ya yote ningependa nichukue nafasi hii ya pekee kumpongeza Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa, kwa kusimamia Sera za Chama cha Mapinduzi vizuri mpaka tukaweza kufungua milango ya kwenda Kusini. Hii imedhihirishwa na ufunguzi wa Daraja la Benjamin Mkapa, lililofunguliwa katika Mto Rufiji juzi. Daraja hili limejengwa kwa hela ambazo zimekusanywa kutokana na kodi. Inadhihirisha kwamba, Chama cha Mapinduzi na Sera zake zimesimamia vyema ukusanyaji wa kodi mpaka tukaweza kutumia ile bakaa kwa ajili ya kuleta maendeleo ya wananchi wetu. Pia, ningependa nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara ya Fedha na *TRA* kwa sababu bila *TRA* kufanya kazi vizuri, hizi pesa tusingeweza kuzipata. Ningependa niwaase kwamba, waendelee vizuri ili ile ahadi yetu ya Chama cha Mapinduzi ya kumalizia ile barabara, kutoka Dar es Salaam - Lindi mpaka Mingoyo, iweze kumalizika kwa kipindi ambacho tumetoa ahadi. *(Makofi)*

Ningependa baada ya kusema kwamba, *TRA* inafanya kazi nzuri, nirudi kwangu Morogoro. Napenda nimhakikishie Waziri wa Fedha kwamba, *TRA* ya Morogoro siku hizi inafanya kazi nzuri sana. Napenda kwa niaba yangu na wananchi wa Morogoro, niwapongeze, inadhihirisha kwamba siku hizi wananchi wanasema, tukienda madukani Wahindi na Wafanyabiashara wengine wanatuombea risiti, kinyume na ilivyokuwa hapo nyuma. Ilikuwa unakwenda unauziwa mpaka una-*demand receipt,* mpaka unagombana nao ndio unapata *receipt* yako. Kwa hiyo, siku hizi ina maana kwamba, ufuatiliaji ni mzuri sana, kwa hiyo, wale Watendaji wa Mkoa wa Morogoro wanafanya kazi nzuri na ninaomba Wizara isisahau kuangalia namna ya kuwapa motisha kusudi wasibadilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia nichukue nafasi hii nimtume Waziri wa Fedha, akatoe shukurani zetu kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, kwa kuondoa kodi zote za kero hasa kodi za maendeleo. Lakini wananchi wanachokiomba sasa kutoka kwa Wizara hii ni kwamba, iorodheshe bayana kwamba, ni ushuru upi ambao umekatazwa, ni kodi ipi ambayo imeondolewa kwa sababu bado kuna mkanganyiko. Halmashauri nyingine bado zinaendelea kukusanya kabla *enforcement* ya hili agizo haijaanza kutokea. Kwa hiyo, wananchi wengine bado wanapata kero. Kodi ya baiskeli bado inawanyanyasa, *licenses* Vijijini na kule Mjini bado Morogoro kuna matatizo. Ninaomba Wizara iweze kutoa basi orodha iliyo kamili ya kwamba, ni kodi zipi ambazo zimekuwa ni kero na zimeondolewa. Kodi ambayo imekuwa bayana tu ni kodi ya maendeleo na kila mwananchi anasema kodi ya kichwa sitoi labda unikate kichwa kwa sababu tumeisikia na ilifafanuliwa. Naomba hilo liangaliwe.

Ningependa sasa kwenda kwenye utekelezaji wa Sera ya Urekebishaji na Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma. Mheshimiwa Waziri, kwenye hotuba yake ametuandikia ni Mashirika mangapi yamebinafsishwa mpaka sasa hivi na yaliyorekebishwa, lakini ingekuwa ni vizuri kama hizi takwimu zingekuwa zimeonesha kwamba kati ya haya Mashirika ni mangapi yanafanya kazi *hundred percent,* ni Mashirika mangapi, ambayo yanasuasua ni mangapi mpaka sasa hivi pamoja na kwamba yalishauzwa au yamebinafsishwa hayafanyi kazi na sababu moja kubwa ambayo inafanya haya Mashirika yasifanye kazi au kusuasua ni zipi? Ingetusaidia kuweza kuwa na *assessment* kwamba, sasa tumekuwa na mafanikio mazuri au mafanikio ambayo ni ya wastani au sio mazuri.

Mheshimiwa Spika, napenda sasa mimi nirudi kwenye Mashirika na Makampuni ambayo yamebinafsishwa katika Mkoa wa Morogoro. Morogoro tulikuwa na viwanda vingi sana vimebinafsishwa. Vingine vya mwanzoni kabisa kwa mfano, Kiwanda cha *Tannaries*. Kiwanda kinachofanya kazi ni kimoja tu sasa hivi, lakini hata pamoja na kufanya kazi, sisi wananchi wa Morogoro haturidhiki na jinsi ambavyo wafanyakazi wanatendewa mle. Kiwanda cha *Canvas Mill,* angalau kinafanya kazi, lakini Kiwanda cha *Morogoro Shoe Company,* ni aibu kubwa kwa sababu kile kiwanda kilikuwa ni kikubwa kuliko viwanda vyote *Africa South of Sahara.*

Juzi Waziri wa Viwanda na Biashara, alituambia kwamba kiliungua, kulikuwa na hisa za Serikali na za Mwekezaji. Kichekesho ni kwamba, yule Mwekezaji ameondoka na sasa hivi ananeemeka vizuri sana. Bahati mbaya hatukuelezwa kwamba, baada ya kile kiwanda kuungua Serikali imepata nini mle. Baada ya kuonesha kusikitika kwamba hatujajua Serikali imepata nini, kulikuwa na wafanyakazi wengi, bahati mbaya wengi wao ni wanawake na hao wanawake, wengi ni hawa tunaowaita ni *single parents.* Walikuwa wanategemea sana kile kiwanda kutunza familia zao. Sasa kile kiwanda kimeungua, hawajalipwa chochote na wao wapo wanahaha kule Mjini Morogoro. Angalau basi tungepata tamko la Serikali kwamba, hawa hatma yao ni nini? Hatujapata! *(Makofi)*

Kuna wafanyakazi wa viwanda vingine kwa mfano, Kiwanda cha *Tannaries*, kile kiwanda mimi sijui kwa nini kinaendelea kuoza. Tunaomba leo kama inawezekana tuelezwe hatma ya hiki kiwanda ni nini? Kama kile kiwanda hakiwezi kuendelea tuondoe zile mashine zao kama bado zipo na nina hakika mashine nyingine hazipo. Basi ziondolewe tufanye madarasa kwa sababu hatuna Sekondari za kutosha kule Morogoro. Kama kile kiwanda cha *Morogoro Shoe* hakitakuwa kiwanda tena, tuambiwe sisi Wabunge wa Morogoro, tutakaa na wananchi wetu tutatengeneza hata kama ni Chuo Kikuu cha chini ya mti pale, kitakuwepo kwa sababu watoto wengi wameshindwa kuingia Vyuo Vikuu hata wenye *Division One* na *Two,* lakini majengo yanaoza. Yanaoza kwa sababu ya nani? Tunamwogopa nani pale? *(Makofi)*

Ningependa tumsikie huyu mwekezaji wa *Morogoro Shoe,* kama inawezekana aletwe mbele ya Kamati husika aeleze zile Mashine mle zilikwenda wapi na hela za *insurance* zimekwenda wapi. Kulikuwa na *insurance* kule kwenye kile kiwanda zimekwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, kuna kiwanda kingine kidogo kilikuwa na wanawake watupu, kilikuwa kinaitwa *Morogoro Leather Goods.* Mimi leo nitalia kwa niaba ya wale akina mama. Nasema yeleuuuwi!! Wanawake wamedhulumiwa Morogoro!! *(Kicheko/Makofi)*

*No, it is serious* kwa sababu mimi nimemwendea Waziri anayehusika, wale akina mama walinifuata hapa nikawabeba wale akina mama mpaka kwake, akaniambia nilishapata habari zao nitashughulikia. Sasa kwa ustaarabu namsikiliza. Lakini inafika mahali wanawake wa kiafrika tunapoona haki zetu zinaishia ukingoni, basi itafika mahali tuvue nguo tulie na sitaki tufikie hapo kwa sababu wanawake wengi waliofanya kazi kwenye viwanda vya Morogoro wamedhulumiwa. Sasa Mheshimiwa Waziri, anatuambia nini kwa niaba ya hawa akina mama? Sio kutuambia tu, ningependa atoe mipango inayoeleweka na azimio ambalo ni ahadi ya kweli kwamba, wale akina mama watasaidiwaje? Mimi napenda nimjulishe kwamba, wale wanawake walikuwa ni vijana, wengine wameanza kufa kwa Ukimwi. Karibu asilimia tano wale akina mama wameshakufa na hatujui sasa zile haki zao atalipwa nani, watoto wao wamekuwa ni watoto wa Mitaani, sijui haki yao iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nimelalamika, kweli naomba kulalamika. Linakuja suala lingine, vile viwanda vingine ambavyo vinafanya kazi, hakuna mtu anayefuatilia. Kwa nini tunamwogopa mtu anayekuja kuwekeza? Huyu kapiga hodi kwako, kaamua kukodisha duka lako au kulinunua, anafanya kazi pale, sasa kwa nini hatufuatilii haki za Watanzania wanaofanya kazi kwenye hivi viwanda? Mtu anaamka asubuhi anaamua kwamba, mimi nitawalipa Shilingi mbili na hizo Shilingi mbili hazilipiki, nani atawafuatilia? Sasa tuseme pia kwamba, hata ajira ya Watanzania imekuwa ni biashara huria? Nani atakayejibu hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna wawekezaji wengine wanaokuja wanajenga viwanda. Tunashukuru kwamba, wamekuja, lakini naomba niseme ukweli kabisa, sio kama mimi ni mbaguzi wa rangi, hata wenzetu Wahindi, wanajenga viwanda, wanasubiri ile *Tax Holiday* inapopita, *by the time Tax Holiday* inapita miaka mitano, huyu bwana ameshabadilisha sura ya kile kiwanda, amehamisha humo zile mashine, anaanza kwenda kuanzisha kiwanda kingine kwa jina lingine. Kwa nini wanatufanya wajinga? *(Makofi)*

Nani anayetakiwa kuwafuatilia hawa jamaa wasibadilishe, halafu wanakiacha tu hapo kwa sababu ameshatengeneza faida, anabadilisha jina, kama alikuwa anaitwa Ngedere anakwenda anajiita Gorila *this time,* anajiita Gorila kwa sababu he *has earned a lot of money,* sasa anaanza kitu kikubwa zaidi. Ndiyo sababu atajiita Gorila.

Mheshimiwa Spika, naomba wanaohusika waangalie sana hawa watu, siyo vizuri kama tumekuwa wastaarabu tumewakaribisha, basi wasitufanye sisi wajinga, itafika mahali mjinga akiamua kuzinduka basi watavunjika miguu na isifike hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuzungumzia hawa wengine ambao wananunua viwanda, halafu tunakubaliana kwamba, vile viwanda vikafanye ile kazi ambayo imekubalika, lakini huku nyuma anakuja kubadilisha, anafanya shughuli nyingine. Viwanda vinanunuliwa vinafanywa ma-*godown*, kwa sababu gani? Kwa nini tunanyamaza? Yeye kama alinunua kiwanda cha kuzalisha mifugo, azalishe

mifugo. Kama amenunua kiwanda cha kuzalisha mafuta, azalishe mafuta na siyo *godown.* Kama anataka kujenga *godown* basi akaombe eneo la kujenga *godown.*

Nafikiri Watanzania tumekuwa wastaarabu mno, lakini itabidi ifike mahali na sisi tuwe wakali kidogo. Tuangalie pia na hao watu wanaowaleta kufanya kazi. Nafikiri ni mara nyingi nimelalamika kwamba, hawa watu wanakuja kuwekeza, wanaleta wafanyakazi wao kutoka kwenye nchi zao. Hivi kuna sababu mtu anakuja ku-*promote Cocacola* atoke *South Africa?* Kuna sababu ya mtu anakuja ku-*promote Salama Condom* atoke Marekani? Hakuna Watanzania wanaweza wakazungumzia habari hii? Wapo!

Mheshimiwa Spika, naomba Sheria za kazi za nchi hii sasa ziangaliwe upya na *Work Permit* ziangaliwe upya. Mwisho kabisa, ningependa kurudia kusema kwamba, ninaomba haki za Watanzania ambao walikuwa wanafanya kazi kwenye viwanda vilivyobinafsishwa Morogoro ziangaliwe, hususan akina mama. Ama sivyo kuna siku watakuja akina mama wataingia pale getini na mimi nitakuwa mmojawapo kwa sababu ni wapiga kura wangu. Naomba Mheshimiwa Waziri, uangalie hilo, wana haki, walitoka jasho, wengine hawana waume na wengine wanaume waliwazalisha wakawaacha solemba, wale watoto wanatakiwa kusoma shule, hatutaki watoto wa mtu ambaye alikuwa anafanya kazi mtoto wake awe chokoraa. Kwa nini awe chokoraa? Naomba hili liangaliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, baada ya kuzungumza hayo, ninaomba tena nimpongeze Mheshimiwa Rais, kwa kusimamia vema Sera ya Chama Cha Mapinduzi mpaka tunakuwa na makusanyo mazuri ya kodi, tukajenga Daraja la Mto Rufiji na nina hakika kwamba, baada ya muda hata sisi tutaanza kwenda Mikoa ya Kusini tukaombe mashamba tushirikiane na wenzetu kuendeleza lile eneo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. NAZIR M. KARAMAGI:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kutoa mchango kwa hotuba hizi mbili zilizotolewa na Mawaziri wa Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, napenda kuwapongeza Mawaziri wote wawili, Manaibu wao, pamoja na Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu na Watendaji katika hizo Wizara, kwa maandalizi waliyoyatengeneza ambayo hakika yanaonyesha mwelekeo wa nchi yetu kwa mwaka unaokuja kimipango na kifedha. Vile vile ningependa kuzipongeza Idara mbili ambazo ziko chini ya Wizara hizo nazo ni *TRA* kama walivyosema kwa sababu ndiyo inatuwezesha tufanye mipango hii pamoja na *PSRC* kwa kazi ngumu wanaoifanya na yenye lawama kubwa. Lakini toka nifike hapa nafikiri nimepata hisia kwamba, watu wengi wanafikiria vibaya jinsi *PSRC* inavyoendesha mambo yake na wana matatizo na *PSRC* kwa Waheshimiwa Wabunge walio wengi.

Lakini nilivyododosadodosa nikagundua kwamba, *PSRC* wana matatizo ya kuwaelimisha Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwa ujumla, muundo wake jinsi wanavyoutumia katika ubinafsishaji wa Mashirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hilo ningeomba labda Waheshimiwa Mawaziri wanaohusika, waweze kuwaasa Viongozi wa *PSRC,* waandae Semina kwa Waheshimiwa Wabunge, tuweze kujua kwa ujumla miundo ipi inatumika ili na sisi katika hali kama hiyo, tuweze kuchangia labda wakachukua mawazo ya Waheshimiwa Wabunge katika utendaji wa kazi zao. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge vile vile wamekwishazungumzia juu ya tatizo lingine ambalo linajitokeza katika ubinafsishaji kwa ujumla ni juu ya ufuatiliaji baada ya kubinafsishwa. Hapa kweli ni tatizo ambalo ni kubwa, ambalo linaonekana kwamba, hakuna chombo maalum, aidha chombo cha Wizara ama chombo maalum kilichowekwa ili kuweza kufuatilia zile ahadi zinazowekwa, hususan wakati wa kubinafsisha kwa yale mashirika ya umma ambayo yalikuwa ni muhimu.

Mheshimiwa Spika, tumejaribu, nafikiri ni njia sahihi ambayo imewekwa na Serikali ya kuwachagua Wakurugenzi katika hayo Mashirika yaliyobinafsishwa kuwakilisha asilimia ile ya Serikali iliyobaki kwenye yale Mashirika. Lakini sina uhakika wale Wakurugenzi ambao wapo katika Mashirika

hayo huwa wanawajibishwa vipi iwapo lile Shirika ambapo wanakaa kama Wakurugenzi linatokea kwamba, wale wawekezaji wanafanya mambo ambayo hayalingani na mtazamo wa Serikali. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ningependekeza vitu viwili, kwanza chombo lazima kiwepo cha kuweza kufuatilia *on spot basis,* yale mashirika yaliyobinafsishwa hasa ya umma, ambayo ni muhimu na pili wale Wakurugenzi ambao wamo katika mashirika hayo, ikiwa patatokea tatizo na Mkurugenzi alikuwa hajalitoa katika Wizara husika, basi awajibishwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mchango mwingine ni juu ya kurekebisha haya mashirika kabla hayajabinafsishwa. Sote tulioko hapa ni wafanyabiashara kwa njia moja ama nyingine, lakini tunajua kwamba, kama unataka kupata bei nzuri ya kitu chako, lazima kiwe safi. Kikiwa siyo safi, utapata bei mbovu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kuna haya mashirika ya umma ambayo yamebakia, naona *TANESO*, Bandari, Reli na nyingine. *TANESCO* bahati nzuri naona mfumo wa kuirekebisha uliotumika ni sahihi wa kuanza kuiweka *Management* liwe Shirika zuri, ili wakati linabinafsishwa liweze kupata bei ama soko zuri. Lakini kuna kitengo muhimu kabisa cha Reli, kwa miaka miwili toka yaanze mazungumzo ya kubinafsishwa, kilikuwa hakipati raslimali ya kutosha kutoka Serikalini kiasi kwamba hali yake inatisha, tumepoteza masoko ya nje na hata vitengo vyote vingine katika Sekta mbalimbali vinadumaa kwa sababu ya kitengo hicho muhimu kilishindwa kufanya kazi zake kwa sababu hawakupewa raslimali za kutosha.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka huu nimefurahi kuona kwamba, hiyo kasoro imegunduliwa na wametengewa kiasi fulani, lakini msisitizo ni kwamba, mashirika ambayo tunataka kuyabinafsisha hasa ambayo ni muhimu tuwekee umuhimu wa kwanza kuyafanya bora kusudi yawe *attractive* kwa wale wawekezaji na ili tuweze kupata bei nzuri kwa kuyauza hayo mashirika ili tusiweze kuyatupa bure.

Mheshimiwa Spika, kwenye Bunge lako Tukufu na huko nje kuna hisia kwamba, ubinafsishaji kwa ujumla na mashirika ya umma waliofaidika ni wageni kutoka nchi za nje tu, Watanzania wazalendo hawakufaidika na huu ubinafsishaji. Hiyo hisia inaweza kuwa sahihi ama si sahihi na kutokana na takwimu ambazo tulipewa hapo mwanzoni, inaonekana si sahihi lakini hisia hiyo imekwishaota mizizi na inasemekana kote kote. Lakini kuna jawabu ambalo linaweza kuwa rahisi kwetu sisi, kwa Serikali, ili kuweza kuondoa hisia hizo. Nalo ni kuweza kutumia sera zake, Sera za Chama Cha Mapunduzi, za kuwawezesha wananchi kwa kuwahusisha walio wengi katika mashirika hayo tayari yamekwishabinafsishwa.

Mheshimiwa Spika, chombo tayari tunacho, ama vyombo tayari tunavyo, *Dar es Salaam Stock of Exchange* na *UTT*. Hamna haja ya kuchelewa chelewa sana kwenye yale mashirika ambayo yapo tayari kuyaweka ndani ya soko kusudi hata wananchi walio wengi na wenyewe waanze kupata matunda na haya manung'uniko yaanze kupungua. Mfano, tunasikia matatizo mengi ambayo yapo *NBC. NBC* tunapoizungumzia, watu wengi tunafikiri kwamba, imechukuliwa na watu wa nje. Lakini na Serikali bado ina hisa nyingi sana kwenye hiyo Benki.

Mheshimiwa Spika, nafikiri jawabu sahihi kwa Mheshimiwa Waziri ni kuweza kutoa hisa zilizo nyingi za Serikali kupitia *DSE* ili na wananchi walio wengi waweze kumiliki *NBC.* Kwa njia hiyo, Benki na vitengo vingine vilivyobinafsishwa vitakuwa na mtazamo tunaoita *True Partnership*, wawekezaji wa nje na wawekezaji wa ndani.

Kabla sijamaliza nataka kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa kutusaidia sisi Waheshimiwa Wabunge kupata malinganisho ya Bajeti ya kipindi kilichopita na Bajeti ya mwaka huu. Ikiwezekana kabla hatujaondoka tupate *Paper* moja tu ambayo iko *comprehensive* kwa Wizara zote, ambayo inaonyesha Bajeti ilivyo-*move* kulingana na mwaka 2002. Tutaweza kujua Bajeti ya Wizara fulani ilikuwa kiasi gani mwaka uliopita na kiasi gani mwaka huu, ili kwa ujumla na sisi Waheshimiwa Wabunge, tupate tu kuzilinganisha kwa haraka haraka. Ingawa hizo takwimu tunaweza kuzipata kwenye vitabu tulivyopewa hivi vya *Votes,* lakini hiyo itatusaidia kwa haraka haraka kuweza kueleza jinsi Serikali na matumizi yake na mapato yake yalivyo-*move* ukilinganisha na miaka iliyopita na mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache sitapenda kurudia mengine yaliyozungumzwa na wazungumzaji waliokwishapita. Naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani kwa kunipa nafasi halafu pia naomba niwashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri, waliotoa hoja zao hapa Bungeni. Moja kwa moja nitaongelea makusanyo. Ni kweli hivi sasa zinakusanya zaidi ya shilingi bilioni 110 kwa kila mwezi. Hoja kubwa ilikuwa ni kuhusu *VAT*. *VAT* bado ni kubwa ukilinganisha na nchi jirani kama Kenya ambako wanalipa asilimia 16 mpaka 18 na ukichukulia kwamba, hivi sasa tunaingia kwenye Muungano wa *East Africa,* kwa hiyo, kuna haja ya Mheshimiwa Waziri, kuliangalia hili, kupunguza *VAT* ili iendane na nchi nyingine za *East Africa.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine kubwa kuhusu makusanyo ni kwamba, kweli tunakusanya pesa nyingi, shilingi bilioni 110 kwa kila mwezi. Lakini unapotafakari hii shilingi bilioni 110 na mazingira tuliyokuwa nayo tunakusanya shilingi bilioni 40 bado tunaona hakuna mwelekeo wa punguzo au punguzo la maisha ya mwananchi kwa maana ya kwamba, amepata punguzo fulani kutokana na kukabiliana na maisha. Kwa hiyo, nadhani kuna haja ya kuliangalia hili na hili linatokana na mchezo mmoja mbaya sana, ambao mwananchi mmoja aliwahi kuniuliza akasema kwamba, naomba Mheshimiwa Mbunge, unisaidie ni kwa nini mnasema huko Bungeni mnakusanya shilingi bilioni 110 mpaka shilingi trilioni kwa mwaka, lakini hatuoni nafuu ya maisha?

Mheshimiwa Spika, tukakuta kumbe mchezo ni mdogo tu. Tunakusanya ndani, sisi ni familia moja, huyu anatengeneza pombe. Kwa hiyo, mzunguko wa ile pesa yote unakuwa unazunguka ndani ya sisi wenyewe. Kwa hiyo, ni kwamba, tunamkamua mwananchi yule yule halafu zinamrudia yule yule aidha kwa kunywa pombe, ambayo ni wale wakusanya kodi wanaongoza kwa kunywa pombe.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mchezo utabaki ni ule ule. Kwa maana kwamba, tutakusanya sana lakini hakuna tunakokwenda kwa maana ya kwamba, zinawarudia wale wale. Kwa hiyo, nadhani kuna haja ya kuangalia na kutafuta *solution* ya hili ni kwamba, inabidi tuwe na vigezo vya upande wa mipango, tuangalie tumepeleka nini nje na tumeingiza nini. Kibaya zaidi kilichokuja ni kwamba, pamoja na kwamba, tunakunywa mle mle pombe, kuna mwingine tena anazichota zile tunazopeana ambaye anaitwa ni mwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu mwekezaji maana yake ni kwamba, unakuja kuchukua, hakuna mtu anayeleta. Hakuna mtu anayepeleka nchi nyingine pesa ya nchi yake. Bali anaenda kuchukua kule kupeleka kwao. Kwa hiyo, unapomwongeza na huyu ni kwamba, anaongeza tena kukamua. Kamchezo kanabaki kale kale. Sasa namshauri Mheshimiwa Waziri, aliangalie hili aainishe *export* pamoja na matumizi ya ndani.

Mheshimiwa Spika, lingine linalonisumbua kichwani ni hili, sisi tuna vigezo vingi sana kimaisha, kwa maana kwamba, tuna madini. Ukiangalia nchi ya Dubai, Oman wana mafuta. Yale mafuta inakuwa ni nafuu ya mwananchi kwa maana ya kwamba, kodi itapungua kwa sababu tayari wana raslimali ya kufidia na ukienda Dubai wanatoza kodi *four percent,* hakuna cha *importation* wala nini, ni asilimia nne.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, nguo kama imenunuliwa shilingi 3,000/=, Uingereza itauzwa kwa hesabu za haraka haraka *four percent.* Nafikiri mtanisaidia ninyi ni wasomi Wizara ya Fedha. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ukiangalia pale nguo itauzwa kwa Sh. 3,200/= au 3,100/=. Lakini kwa sasa sisi tunaweka zaidi ya *fifty percent,* ni lazima nguo iuzwe zaidi ya Sh. 5,000/=. Tunakuwa hatuna cha kujisikia kwamba, sisi tuna madini, tuna *Tanzanite*, tuna maliasili wanyama. Kwa hiyo, hatuna sababu ya kujisifia kama hatuwapi wananchi wetu punguzo la maisha kwa kupitia maliasili ambayo tumepewa na Mwenyezi Mungu. Tunaomba Waziri wa Mipango uoanishe, kuwepo kwa haya madini, kuwepo kwa hawa wanyama, kuwepo kwa utalii, pamoja na kodi inayotozwa. Kwa maana hiyo, sitashangaa kodi zote zikiwa asilimia 20, *importation, VAT,* kwa sababu zitafidiwa leo hii utalii tunasema unaingiza shilingi bilioni 700, lakini bado kodi ni ile ile, maisha bado ni magumu vile vile. Mambo ni mazito vile vile.

Mheshimiwa Spika, unafuu wa Serikali na uimara wa Serikali na umanufaa wa Serikali ni pesa kuwa kwenye mfuko wa mtu. Siyo Jengo la *Sheraton*. Hilo jengo kwanza siyo letu, kwa sababu limepachikwa pale. Lakini wewe utadanganya utasema tumeendelea, angalia ule Mtaa sasa una *Sheraton,* pale pamejengwa maghorofa. Yale siyo yetu. Ni ya wenzetu. Kwa hiyo, naomba tusijidanganye na majengo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikimaliza hapo, ninaomba pia nisahihishe kune neno moja kidogo linawasumbua Watendaji wetu. Neno Sera ya CCM. Nadhani imefikia wakati kwamba, Sera ya Serikali, nitatoa maelezo kidogo. Unajua tuna mfumo wa Vyama Vingi na watendaji wetu bado hatujawapeleka kuelewa fika kwamba, ni nini maana ya kuwa mwanachama na nini maana ya kuwa Mtendaji wa Serikali. Kwa maana hiyo, wanatumia Sera vibaya. Mtu anakwenda kwa maringo kabisa kwamba, mimi ninatekeleza Sera ya Serikali, hapana! Sera hii kwa sababu ya Chama Tawala tayari, ili tuipe nguvu siyo kwa maana napinga, tunataka kuipa nguvu Sera, itekelezwe na watu wote. Lazima tuite, baada ya chama kupita kikashika utawala kwa kutumia Sera ya CCM kinapokuwa Chama Tawala sasa kiitwe ni Sera ya Serikali ili kila mtu awajibike kuitimiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge hatuko kwenye malumbano ya 2005. Tuko kwenye malumbano ya wananchi tuwatendee nini? Ninavyojua ni kwamba, wananchi wengi wanapata shida sana kutekeleza Sera. Kuna mwingine ni Mpinzani yuko pale, ni Mkuu wa Wilaya bado ni Mpizani. Yupo mwingine ameiva, yaani yupo, ni Waziri, lakini ni Mpinzani. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ili itekelezwe vizuri lazima aite ni Sera ya Serikali, kwa sababu Serikali ni ya jumla. Waheshimiwa Wabunge, nikimaliza hilo ninaomba niende ubinafsishaji. Huwa hainiingii unaponiambia benki inakushinda kuendesha. Hakuna kitu biashara isiyo na kazi kama benki. Wewe unakaa pale, mtu anakuja analeta pesa yake mwenyewe, humtafuti, wewe unaweka halafu unamkata *percent,* halafu unakopesha, pesa inaingia, tunashindwaje kuendesha?

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana mimi nilisikitika sana mliposema kwamba, tumeuza *NBC* kwa shilingi bilioni 15 wakati yale majengo matatu tu waliyochukua ni shilingi bilioni 15. Huwa hainiingii na ilinisumbua sana, nilikuwa mfuatiliaji mzuri sana nikafikia *stage* nikasema hapana, penye wengi wape, lakini bado nitaendelea kusema na kusema kwamba tumefikia, sasa tuyaangalie. Hii ni mali ya wananchi, siyo mali ya Serikali iliyopo, siyo mali ya bwana fulani mwekezaji, wala Mwenyekiti.

Mheshimiwa Spika, nasema hili suala lote la ubinafsishaji, lazima lije Bungeni. Lazima liletwe Bungeni kwa ajili ya wananchi ambao sisi ni waasisi wao tuone kama ndugu zangu wananchi tuliwakata pesa tukatengeneza kiwanda cha pamba, tukawaambia funga mikanda, tunajenga uchumi, tukawapa bei ndogo ya pamba, kwa maana ya kwamba tuwekeze, lakini leo tunauza, mtu mmoja anakaa pale anasema ninauza.

Mheshimiwa Spika, sasa nasema hivi hii hoja ya kurahisisha wanyang'anywe mara moja kama si mara mbili. Nasema wanyang'anywe. Hii hoja ya kubinafsisha shirika lolote iletwe kwanza Bungeni kama siyo Bunge lote basi tukasimu madaraka haya Kamati ya Bunge husika ione, kama kweli hii Benki inakubalika kuuzwa kwa shilingi bilioni 15 au hapana. Kwa hiyo, mimi naliomba hilo mlione Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, halafu bado naendelea, naomba niyapongeze baadhi ya Mabenki ambayo yamefanya vizuri kama Benki ya Posta ni benki yetu, *CRDB.* Posta wanafanya vizuri sana na wanaenda vizuri mno. Ninaomba msiiuze, kama hamjaiuza. Ahsante sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, lingine nakimbia moja kwa moja kuhusu simu za mkononi. Naomba mtuambie, nimeenda juzi, nilikuwa nchi moja inaitwa India. India unaongea na simu kwa muda wa dakika tatu, unalipa rupia 20 ambayo rupia moja ni sawa na shilingi 20. Unaongea *mobile* ambayo ni *local* Sh.20 kwa dakika tatu. Iweje hapa dakika moja unaongea kwa shilingi 400 kwa nchi maskini, *third world* sawa India?

Uingereza kwenyewe unatumia shilingi 200 kuongea dakika moja. Naomba Mheshimiwa Waziri, utuambie ni kwa nini wamekuja kukamua kwa sababu nimepiga hesabu za haraka haraka nikagundua kwamba, hawa jamaa kupitia kwenye simu zinaondoka hela nyingi sana. Ukipiga hesabu ni hela nyingi mno. *(Makofi)*

Kwa kweli inaumiza sana Waheshimiwa Wabunge. Tunashindwa kuongea na simu. Hakuna mtu mwenye anasa ya kuongea na simu, lakini tunashindwa kuongea. Ukipiga tu, halafu mtindo mwingine ambao wanatuibia ni huu mtindo wa kwenda dakika moja moja. Naomba kama unaongea kama sekunde 10 unataka kumpa mtu *information* ya haraka haraka, zihesabiwe kama sekunde 10 isiwe dakika moja. Mwingine ana visenti kidogo anataka kuongea na mtu, anaambiwa ni *one minute.*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba hilo mliangalie mara moja, tufanyie mtindo ule ule. Huo ni wizi, kama India dakika tatu unaongea kwa shilingi 20, wao kwa nini dakika moja unaongea kwa shilingi 400?

Mheshimiwa Spika, lingine ninasikitika kuhusu uondoaji wa UKIMWI. Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilikuona siku moja nikakuambia nimetunga Kitabu cha kusaidia shule za sekondari. Mheshimiwa Waziri Mkuu, naona anaongea. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Elekeza mawazo yako kwa Spika.

**MHE. MUTTAMWEGA B. MGAYWA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, akanishauri niwasiliane na *TACAIDS* ili niwapatie kile Kitabu na nilisema nitakitoa bure. Nimetunga, nimefanya *research,* nime-*spend more than five million shillings,* nikasema kwa kusaidia kama binadamu wenzangu niwasaidie. Kupeleka *TACAIDS* wakasema hawana pesa ya kuweza kuchapa kile Kitabu. Lakini wakasifia ni Kitabu kizuri, kinafaa kabisa kwa Sekondari lakini hatuna pesa. Baada ya miezi miwili, *TACAIDS* inatoa ripoti kwamba, zimerudi *billions of money* nje kwa sababu hawakuwa na kazi ya kuzifanyia!

Mheshimiwa Spika, naomba hilo watujibu. Kama kweli tuna *agenda* ya kweli ya kumaliza UKIMWI nadhani tumepotea, hatuendi. Labda walitaka zitumike kwa Warsha.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ni pesa naunga mkono hoja. *(Kicheko/Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ndiyo tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi. Wachangiaji wa mchana mpaka saa 12 ni Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Mgana Msindai na Mheshimiwa Stephen Kazi.

Baada ya maelezo hayo, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.58 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipatia nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Basil P. Mramba, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Makatibu Wakuu wote, Wakurugenzi na Watendaji wote, kwa jinsi walivyoweza kuandaa taarifa yao vizuri.

Mheshimiwa Spika, ili kazi walizopanga ziweze kutekelezeka kwa kadri walivyopanga, napenda kuiunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba yangu na kwa niaba ya wanawake wote wa Mkoa wa Mtwara, napenda kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa na Serikali yake iliyoko madarakani ya Awamu ya Tatu, kwa jinsi walivyosimama kidete katika kutengeneza daraja lile la Mto Rufiji na kwamba juzi tarehe 2 Agosti, 2003 tumekuwa ni mashahidi wa

kushuhudia lile daraja likifunguliwa. Namtakia kila la kheri, Mwenyezi Mungu, ambariki. Sisi wa Mikoa ya Kusini, hatuna chochote cha kumlipa ila Mwenyezi Mungu wenyewe anajua ni kitu gani amlipe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwapongeza *TRA* kwa jinsi wanavyojitahidi kukusanya mapato. Napenda kuwashauri kwamba, waendelee na jitihada zao za kuweza kusimamia kwa sababu pamoja na mapato mazuri lakini wako wengine pengine kwa kutokuelewa ni kitu gani wanakifanya, wanajaribu kupiga chenga katika ulipaji wa kodi. Kwa hiyo, elimu itolewe kwa wale ambao wako Vijijini, Makao Makuu na kila mahali, kuwaelewesha kwa nini wanapaswa wao kulipa kodi ya *TRA* ili wote kwa pamoja, tupate maendeleo katika kulipa kodi.

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumpongeza Mama Nyoni, kwa kazi nzuri ambazo anazifanya. Namtakia kila kheri na kwamba, aendelee na jitihada zake na Serikali isimwache peke yake. Ninashauri waende sambamba katika kusimamia na kumsaidia pale anapohitaji msaada katika kazi zake ngumu za kupambana na tatizo la wananchi ambao pengine wanakwepa kulipa kodi kwa sababu wanazozijua wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, amezungumzia jinsi gani Serikali itawasaidia wastaafu katika kulipwa pensheni zao. Napenda niwapongeze sana Serikali, sasa hivi kwa kweli imekuwa inasikia kilio cha watu ila tatizo liko kwa Watendaji. Katika watekelezaji, wengi hawatekelezi kwa kadri Serikali inavyotoa maelekezo. Sisi wenyewe ni mashahidi kwa watu wanaofuatilia pensheni zao pale wanavyopata shida, wengine wanakaa mwezi na wengine wanapata matatizo ya kuuguliwa wakati wanadai zile pensheni zao. Kwa hiyo, kinachoonekana ni Serikali na wala haonekani yule Mtendaji ni mbaya. Ninapenda kushauri kwamba, kwa watumishi wale wakorofi ambao hawatekelezi kazi kwa wakati, wasimamiwe na ikiwezekana wahamishwe wapelekwe mahali pengine ili waje wazuri watakaotekeleza azma ya Serikali na kuwaona wananchi au wenye kudai hela za kustaafu, wapewe masurufu yao kwa wakati unaohitajika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika suala la miundombinu ni kwamba, katika nchi yoyote ili iwe na maendeleo ni lazima iwe na miundombinu mizuri ili itekeleze azma yake. Hali kadhalika unapokwenda katika Mikoa na Wilaya, miundombinu ni jambo muhimu sana. Kwa hiyo, utakuta katika Mkoa huu wa Mtwara, pamoja na kwamba nimepongeza juhudi za barabara, lakini hiyo siyo mwisho, yako mengi ambayo tunahitaji Serikali iangalie.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, tatizo la umeme. Makao Makuu ya Mkoa wa Mtwara umeme ni tatizo na Serikali inajua, mashine iliyoko pale iko pale tangu wakati wa *TANU,* sijui ina miaka thelathini na ni mbovu na sijui ni lini itakuja kutolewa ile mashine kwa sababu sasa hivi imekuwa ni kero katika Mkoa ule. Kama haitolewi au kama Serikali haisaidii basi hata miundombinu au uchumi unakuwa ni mgumu na wale watu wanabaki kuwa maskini kulingana na teknolojia ya kisasa ndiyo inayomsaidia mkulima au mfanyabiashara mdogo mdogo kufikia katika malengo. Kwa hiyo, kutokana na ile mashine ambayo ni kero na sijui kama katika Tanzania hii kuna Mikoa mengine ambayo ina mashine iliyokaa kuanzia *TANU* mpaka leo haijatolewa na imechoka, haifanyi kazi. Mimi kwa kilio cha wakulima wa Mkoa wa Mtwara, hasa wanawake, ninapenda kuishauri Serikali kwamba, kama haiwezi kuleta mtambo mpya basi ile mashine itolewe na tukae mpaka hapo Serikali itakapopata mashine nzuri ili wananchi waweze kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu tatizo la simu. Makao Makuu ya Wilaya Tandahimba mpaka leo simu hakuna. Leo wananchi walio wengi wanataka simu zifike labda kwenye Kata au kwenye Vijiji, lakini katika Mkoa ule utakuta Wilaya kwa mfano, kama Tandahimba, Mtwara Vijijini pia kuna Nanyamba, ni Mji Mkuu, hakuna simu. Kutoka kwenye Wilaya hizi kufika Makao Makuu ni kama maili 40, 45, 50 mpaka 60, unapokuwa na shida ya lazima hivi utakimbiaje kuwafikia wale watu? Pia hata kwenye maeneo hayo kuna shule za sekondari, hizi shule za sekondari ni maskini kabisa, hawana maji, shule hizo hazina umeme, wanatumia vibatari na pia kwenye shule hizo hakuna simu na pia hata katika vyuo vyetu katika Mkoa wetu hakuna hivi vyote ambavyo nimevitaja; je, wanawezaje kutekeleza azma hiyo ya maendeleo na pia wanawezaje kufanya mawasiliano kwa wakati wake kwa sababu wanapokuwa katika maeneo ya vyuo

au kwenye Makao Makuu ya Wilaya, kuna kupata ajali, kuna kuumwa na pia kuvamiwa, sasa anaishi katika mazingira magumu? Serikali ilione hilo na ikiwezekana itekeleze kwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, Makao Makuu ya Tandahimba ni Wilaya mpya, wamejitahidi sana mambo mengi wamejitolea wenyewe, wamejenga Jengo la Serikali, wamejenga Jengo la Halmashauri na pia wamejenga Ofisi ya CCM wenyewe kwa njia ya kujitolea, sasa Serikali kwa nini watu hawa wanaojitegemea wenyewe, wanaojihudumia wenyewe isiwaunge mkono, isiwape *support* yoyote? Hili nalo nalizungumza kwa uchungu sana na naliweka mikononi mwa Serikali nikiwa na matumaini kwamba, Serikali yetu ni sikivu kwa mifano mingi ambayo imejionyesha kwamba hata hili linawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili Mikoa iendelee ni pamoja na uchumi. Mimi nimefurahi sana katika Kikao hiki cha Bajeti, niliposikia Mheshimiwa Waziri wa Ushirika na Masoko, akieleza kwamba, katika Mkoa wa Mtwara wanazalisha zao la korosho na linaliletea Taifa Pato kubwa. Sasa hawa ambao wanalima katika mazingira magumu na wanaongeza pato la nchi hii, bado ndio hao niliowazungumza kwamba, Serikali imewasahau, imewaacha, haijawatengenezea mazingira yao, miundombinu siyo mizuri. Kwa sababu ilibidi Serikali iwe makini katika kuwaangalia kama nilivyozungumza huko nyuma. Halafu katika zao hili wanapata matatizo ya upataji wa pembejeo. Pembejeo tumewaachia wenyewe wakulima wahangaike na bado tunazungumza humu kwenye Bunge kwamba, zao hili limeliletea Taifa pato. Pato la Taifa sasa linakuwa kwa faida ya Taifa lakini; je, hali ya huyu mkulima ambaye anaongeza pato kwa nini hatumuwezeshi kwa kumpa pembejeo? Tumsaidie kupata pembejeo kwa sababu ikiwezekana kama pembejeo atazipata kwa wakati wake na uzalishaji wa zao la koroshoutakuwa maradufu au utakuwa mara mbili zaidi na pato litaongezeka maradufu. Ikiwezekana Serikali isione utata wa kuwapatia *sulphur* hata bure wakulima wa Mikoa ile inayolima korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu gani nazungumza wapewe bure? Kuna misimu sasa kama mitatu zao lile limekuwa likiyumba kutokana na uzalishaji mdogo na zao limekuwa linapata ukungu na pia labda uhaba wa mvua umechangia mambo mengi. Kwa hiyo, sasa hivi kwa sababu wamezungukwa na mambo mengi ya kimaendeleo, kama kuwasomesha watoto, kuwapeleka wagonjwa na kadhalika, narudia kusema kwamba, napenda niishauri Serikali ipeleke *sulphur* Mikoa ile ya Kusini ili hawa wananchi waitumie na kuongeza pato. Lazima Serikali ifike mahali iwashukuru wananchi wanaofanya vizuri, hatujafika mahali pa kuwashukuru vizuri na wakati bado wanahangaika wenyewe. Suala hili la pembejeo ambalo nimelizungumza ninaona kwamba, ndio tatizo kubwa linalowasumbua hawa wakulima na wakisaidiwa kwa kweli matatizo yao mengi yatakuwa yamekwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na miundombinu kuwa ndiyo chanzo cha wawekezaji kutokufika katika Mkoa wa Mtwara, kwa sababu Mheshimiwa Waziri mhusika ,alikwishazungumza humu ndani kwamba, wawekezaji hawawezi kufika Mkoa wa Mtwara kwa sababu miundombinu yao siyo mizuri, haipo. Sasa kama wawekezaji hawapo na leo tunazungumza kwamba, ili tujikwamue ni lazima tuwe na wawekezaji, basi fanyeni kila liwezekanalo ili kuhakikisha mnakaa nao kupanga wataalam ili wawekezaji waende katika Mkoa ule wa Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika Wilaya ya Newala kuna viwanda vya ubanguaji korosho. Hivi viwanda vimekaa sasa ni kama mapambo ni kero kwa sababu vimekaa katika barabara kuu, upende usipende utaviangalia na wakati huo huo viwanda kama vingefanya kazi ajira ya wanawake ingeweza kupatikana na ndio wanawake tunaowazungumzia ya kwamba tuwasaidie, sasa tunawasaidiaje?

Tumekuwa mashahidi pale kwenye viwanda kwamba wanawake ndio wanaopata ajira. Kwa hiyo, viwanda vile kwa sababu havifanyi kazi na hata wanawake wanakosa ajira. Tatizo la kusema kwamba, viwanda vile haiwezekani vikachukuliwa na wataalam, mimi sielewi kwa sababu wataalam tunao na wale wawekezaji wapo au wa kununua vile viwanda wanakuja katika nchi yetu, mkae nao, mjadiliane nao na pia mpange nao kwa sababu inawezekana, mimi nasema inawezekana. Suala la kujibu kwamba, viwanda vile *spare* zimepitwa na wakati kwa kweli mimi mnanichanganya wala siwaelewi. La msingi hapa labda ni kusema kwamba, kazi haijafanyika bado. Kazi muifanye kwa kujitoa, kwa kuamini kwamba, viwanda vile ni kero si kwa Wilaya ile tu, hii ni Serikali yetu nzuri, ni Serikali ya Awamu ya Tatu inafanya mambo mengi. Napenda kurudia kusema kwamba, hakikisheni mashine zile zinafanya kazi kabla hata Bunge hili halijamaliza shughuli zake au uchaguzi wa mwaka 2005 haujafika ziwe zimefanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Benki ya Posta wanafanya kazi nzuri sana. Napenda kuwapongeza kutokana na mipango yao jinsi tulivyosoma kwenye taarifa, wako tayari kuendelea kuwasaidia wanawake na vikundi vyao. Ninaomba wajitahidi kufika mpaka Vijijini, kwa sababu sisi tunaohudumiwa tuko huku Makao Makuu ya Wilaya au Mikoani lakini wanaoathirika sana tunaowazungumzia hapa kwenye Bajeti hii ni watu wa Vijijini na Vijijini ndiko waliko wanawake wenye matatizo. Kwa hiyo, Benki ya Posta iwe ndiyo kimbilio kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Benki ya *NMB* imekuwa ikiwasaidia wananchi mikopo midogo midogo. Kwa hiyo, ninachoshauri Mheshimiwa Waziri ni kwamba, kuzielekeza Benki hizi mbili ambazo zimeanza kuonyesha mfano, ziende moja kwa moja mpaka Vijijini waliko wananchi ili kuwapatia mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo kwa heshima na taadhima ninaunga mkono hoja zote mbili kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni hii katika hotuba zote mbili za Mheshimiwa Waziri wa Fedha, pamoja na Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, pia napenda nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, kwa kazi nzuri na mipango mizuri na hasa napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha, kwa jitihada kubwa ambazo amezifanya ili kuhakikisha makusanyo ya Pato la Taifa yanaongezeka kwa kiasi kikubwa. Lakini ningependa kumsisitizia ya kwamba, ajitahidi kuangalia pande zote mbili kwamba, ng'ombe anapokamuliwa ili aendelee kutoa maziwa mengi inabidi vile vile alishwe, anahitaji mashudu, majani na pia chumvi, vinginevyo anaweza akakamuliwa hata ikatoka damu kama hapati lishe ya vitu hivyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, ajue fika kabisa kwamba, anapoona watu wake wanakusanya mapato vile vile ni vizuri akaangalia hali ya hawa watu ambao wanalipa hayo mapato kwamba hali zao ziko vipi, hali ya maisha kiujumla ikoje na *living style* yao ikoje.

Mheshimiwa Spika, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, ukurasa wa 26, kifungu cha 50, ameelezea mambo ambayo Wizara yake itaweza kuyapa kipaumbele kwa mwaka wa fedha 2003/2004. Nimeangalia kwa umakini mkubwa na mojawapo amezungumzia kwamba, wataendelea na zoezi la urekebishaji na ubinafsishaji wa mashirika yaliyobaki na kuboresha ufuatiliaji wa utendaji wa mashirika yaliyobinafsishwa ili kubaini mafanikio na matatizo wanayoyapata wawekezaji na wadau wengine katika mashirika hayo na kutoa ushauri, pamoja na kubuni au kuboresha mikakati. Napenda kumpongeza kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nikitilia maanani michango mbalimbali ya Waheshimiwa Wabunge, waliyoitoa asubuhi hii, mimi napenda kusema kwamba, *trend* ya kubinafsisha, *trend* ya kuuza mashirika kama *outcome* yake ni ile ile ambayo tumeishuhudia, Waheshimiwa Wabunge wameielezea na hasa nikizingatia hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati na pia hotuba ya Waziri wangu Kivuli ni kwamba, huu urekebishaji tusipojaribu kuuangalia kwa makini hata ile dira tuliyonayo na malengo tuliyonayo ya kubinafsisha tunaweza tusifanikiwe na matokeo yake ikawa ni hasara maradufu.

Mheshimiwa Spika, inatia huruma sana tunapozungumza kwamba, baadhi ya mashirika yameuzwa na wakati walioyanunua tangu walilipa ilipobidi na kupata gawio la kuweza kuyanunua hayo mashirika, matokeo yake hawajalipa madeni, kwa kweli inatia wasiwasi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya Waheshimiwa Wabunge, wameelezea baadhi ya mashirika hapa na mimi nina mfano mwingine wa Kiwanda cha *Morogoro CANVAS Limited,* ubinafsishaji ambao ulifanyika mwaka 1998. Huyu bwana aliyenunua, alinunua kiwanda hiki kwa shilingi bilioni 1.872 na akalipa *first installment* ya shilingi milioni 936 na akawa ametakiwa alipe *balance* iliyokuwa inabaki ya shilingi milioni 936 baada ya miezi sita. Sasa inasikitisha kwamba, mpaka hivi sasa huyu bwana hajalipa hata hiyo *insolvent* iliyobaki.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi nashindwa kuelewa kwamba, wakati hawa wanunuzi wanapokuwa wanasaini Mikataba ya kununua viwanda hivi, hivi inakuwa ni Mikataba ya kupitisha wakati, ku-*joke* au

wanakuwa wanajuana humo kwa humo na wale wanaowauzia? Iweje mtu ana-*tender* kununua kiwanda na wengine wanajitokeza kutoa *offer* zao ambazo watazitoa endapo watauziwa, mtu anapewa hicho kiwanda, anauziwa baada ya kununua anaingia mitini na wakati ambapo watu wamepewa majukumu ya kusimamia *exercise* hiyo ya kuhakikisha watu wao wanalipa lakini mtu anajifanya kama vile hakuna Serikali, hakuna watu wanaopaswa kuwajibika kumfuatilia, mambo yote yanaishia kimya kimya.

Mheshimiwa Spika, mimi nipende kukupongeza kwa *system* ambayo imeanzishwa ya utendaji kazi wa Kamati za Bunge ambapo zinatembelea sekta mbalimbali. Mimi nina uhakika kama Kamati zingekuwa hazitembelei, tungekuwa hatuna utaratibu wa kutembelea Ofisi mbalimbali na Taasisi mbalimbali ambazo zinasimamiwa na Kamati husika, mambo mengine haya hata yasingeweza kujulikana, nina uhakika huo. *(Makofi)*

Nami inanitia wasiwasi iwapo hali ni hivi, naamini kuna mashirika mbalimbali ambayo hayajatembelewa unaweza ukakuta hali ni hivyo hivyo kwamba, watu tangu walipo-*bid* wakauziwa mashirika mbalimbali ya Serikali ambayo wananchi walijinyima sana kwa miaka mingi, yakaliwa mpaka yakawa hayawezi kusimama tena, wakauziwa watu ambao tunaamini kwamba wangeweza kuyanunua, hao watu kumbe wao ile pesa ya kulipia ilikuwa ni njia ya kuondokea lakini baada ya hapo ilikuwa ni kuingia mitini.

Mheshimiwa Spika, sasa linalotia huruma zaidi ni mwekezaji huyo huyo ndiye huyo huyo aliyeuziwa *MOPROCO* kwa shilingi milioni 900 na yeye akalipa shilingi milioni 120, sasa zile zilizosalia shilingi milioni 780 akaingia nazo mitini. Sasa mimi naona kama ni *syndicate*, si suala ambalo tunapaswa tuliangalie kijumla jumla tu kupeana taarifa na kuondoka basi, ni suala ambalo linaonekana *there is a syndicate*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, ningependa kuomba kupitia Bunge lako Tukufu kwamba, Mikataba yote ambayo watu mbalimbali waliuziwa viwanda na mashirika mbalimbali, ni vizuri taarifa hiyo ikaletwa Bungeni na Kamati husika, ili tuweze kuona mwenendo na *trend* nzima ya ulipaji wa mashirika haya na viwanda vilivyonunuliwa, vinginevyo tutakulana humu kwa humu. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwamba, katika Bajeti aliyoisoma hapa, alitangaza kufutwa kwa kodi ya maendeleo na Halmashauri zikawa zimeagizwa kufuta vyanzo vingine vya mapato ambavyo kwa kweli ni kero kwa wananchi. Napenda kuwapongeza kwa hilo. Lakini kitu ambacho nimekuja kugundua na ambacho kinanitia wasiwasi ni kwamba, pamoja na uamuzi huo mzuri, nina wasiwasi maandalizi yake yalikuwa bado hayajawa tayari. Ninakuwa na wasiwasi huo kwa sababu kama tunavyofahamu, vyanzo hivyo vya mapato kwa sehemu kubwa ndivyo vilivyokuwa vinazipa Halmashauri zetu mapato ya kuendesha Halmashauri na hususan kulipa mishahara ya watumishi ambao hawapati mishahara kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana hata katika tamko lililotoka katika vyombo vya habari jana, Mheshimiwa Waziri, amezidi kusisitiza kwamba, atakula sahani moja na wale ambao bado wanaendelea kutoza kodi. Napenda kumpongeza kwa kufuatilia hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini hapo hapo mimi namsihi Mheshimiwa Waziri, ajaribu kwa haraka sana kuwanusuru Wakurugenzi wake. Kuna hatari ya Wakurugenzi kuanza kupigwa, wataanza kupigwa na watumishi pamoja na maamuzi hayo mazuri lakini ni kutokana na suala la utekelezaji wa kuwapelekea angalau *subsidy* za kuweza kuziba mapengo ambayo walikuwa wanakusanya mapato wao wenyewe kwa sababu hayajaanza kwenda na sijui kama Mheshimiwa Waziri, amekwishajiandaa kwa hilo. Halmashauri nyingi mpaka hivi sasa ulipaji wake wa mishahara ni wa kusuasua. Halmashauri nyingi bado hazijalipa mishahara ya watumishi, wengine wanadaiwa mishahara ya mwezi wa sita na wengine mwezi wa saba. Sasa mambo yakiiva huko mimi nina uhakika hawa Wakurugenzi wataanza kupigwa wala hawatamfuata au hakikisha hawatamfuata Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

Mheshimiwa Spika, sasa ningeomba pamoja na kuwa suala hili labda liliamuliwa kwa uharaka wa utashi wa kisiasa, lakini vile vile kuwepo na uharaka wa kuweza kuwanusuru watumishi wetu na wasimamizi wa Kurugenzi zetu.

Mheshimiwa Spika, ningependa mwisho niwapongeze wenzetu wa Mifuko ya Pensheni na hususan Mfuko wa *PPF,* ambao kwa kweli mimi nasema ukizungumzia mashirika ambayo yanaongeza mandhari ya Mji wetu, yanaongeza mandhari hata ya ile sura ya Mji, *PPF* ni mojawapo huwezi kuzungumza nje ya shirika hili. Tumeweza kuwekeza, kufanya *investment* katika kujenga majumba makubwa makubwa, wameingia katika mipango mikubwa mikubwa, kwa kweli watu wanapofanya kitu kizuri ni lazima tuwapongeze. Lakini pia ningependa kusema kwamba, pamoja na kazi nzuri wanayoifanya, mimi naamini kuna haja kubwa sana ya kuwaangalia wanachama pia. Isije ikawa wanafanya mambo makubwa lakini wanachama wao wananyong'onyea. Tungeomba mambo yote mawili yaende sambamba, ulipaji wa mafao ya wanachama ufanyike vizuri na hata mipango mizuri ya kuweza kuboresha hali za wanachama iweze kufanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa pamoja na kutoa haki na gawio kwa wanachama wake, kuna tatizo la wanachama kutoelewa taratibu na Sheria za Mfuko wenyewe. Hili lisipotiliwa maanani na kufanyiwa kazi, suala hili linaweza likaleta migongano mikubwa sana baina ya wanachama pamoja na Mfuko wenyewe. Kwa mfano, ni sisi wenyewe tulipitisha Sheria ya Mfuko huu lakini kuna kitu kimoja ambacho kimeendelea kuleta migongano na hasa kwa wanachama ambao wanakuwa na miaka labda 30 wanadai kupata mafao yao kutoka katika Mfuko huu, ile pensheni ya uzeeni.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi sitaki kumlaumu sana huyu mwanachama au malalamiko ya wanachama wenyewe, mimi nafikiri jambo linalotakiwa ili lipewe umuhimu na kipaumbele, ni kutoa elimu kwa wanachama na hata wale ambao sio wanachama walio nje ya Mfuko huu, ni vizuri wakapewa elimu, wakaelezwa kanuni na taratibu zinazosimamia Mfuko huu. Ninaamini watu wakielewa, kwanza, Mfuko huu utapata wanachama wengi zaidi kwa misingi kwamba, wameuelewa Mfuko wenyewe na taratibu zake, Kanuni na Sheria inayousimamia na pia migongano hii haitakuwepo kwa watu kufanya tafsiri yoyote ile kwa jinsi anavyoona au anavyotafsiri Sheria na taratibu zenyewe. Kwa hiyo, kwa msingi huo mimi napenda nizidi kuwapongeza kwa kazi nzuri lakini wasibweteke, waboreshe mambo mengi zaidi na pia wawekeze kwenye mambo mengi zaidi na hususan kwa wanachama wao ambao wanachangia katika Mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, napenda nimalizie kwa kuwapongeza waliojenga daraja la kilomita moja, ambalo limechangiwa na Watanzania wote, hata mimi mlima kahawa nimechangia. Inatia matumaini kwamba, baada ya miaka 40 tunapata daraja moja la kujisifia, inatia moyo na tunaamini kama tukienda kwa *speed* nzuri, tunaweza kujenga mengine mengi tu hata Kigamboni wanaweza wakapata daraja, Rusumo wanaweza kupata daraja kwenda Ngara, kwa hiyo, ni jitihada nzuri lakini tusibweteke tukaona kwamba, tumefanya maajabu makubwa. Naamini kama ingekuwa ni hivyo, hata Marekani ambako kuna madaraja makubwa Vyama vingine vingekuwa havichukui madaraka.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na nawapongeza. (Makofi)

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami nichangie Wizara hizi mbili. Nianze kwa kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Manaibu Waziri wa Fedha, Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu, Mhasibu Mkuu wa Serikali, Mhakiki Mali, wakusanya kodi wote na watendaji wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuipongeza sana Serikali kwa kukamilisha ujenzi wa Daraja la Mto Rufiji. Lakini mimi nianze kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Pili, kwa sababu ndiyo iliyobuni na kuanza mradi huu na nimpongeze sana Rais wetu wa Awamu ya Tatu kwa kazi nzuri aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazipongeza hatua zinazochukuliwa za kuongeza mapato ya Serikali. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, ahakikishe yanatumika kama inavyotakiwa. Pia naupongeza utaratibu mzuri wa *pension,* ambao wameuanzisha sasa lakini naomba waende ndani zaidi ikiwezekana wanaodai *pension* waanze kulipwa kwenye Kanda badala ya kutoka Mwanza aende Dar es Salaam, Bukoba aende Dar es Salam, Singida aende Dar es Salaam, tuanzishe Kanda wawe wanalipwa kule. Nawapongeza sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ndio inayofanya kazi zote za kutafuta fedha kwa ajili ya Serikali hii na inahitaji iwe na watendaji waadilifu na waaminifu sana. Lakini inasikitisha unapokwenda Hazina, unakuta Wakuu wengi wa Vitengo wanakaimu na wengine wamekaimu kwa zaidi ya miaka miwili, mitatu. Najua kwa utaratibu wa Serikali unakaimu kwa miezi sita aidha, unakuwa *confirmed* au unapewa barua kwamba wewe hufai anawekwa mtu mwingine. Sasa kwa nia njema kabisa, namwomba Ndugu yangu Mheshimiwa Waziri wa Fedha, aliangalie kwa njia ya haraka sana hili, ndio linafanya wafanyakazi wanaanza kukata tamaa. Utafiti niliofanya kuna zaidi ya Wakuu wa Vitengo au Wasaidizi wao saba au zaidi hawajawa *confirmed,* inasikitisha sana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, nakuomba sana uliangalie suala hili.

Lingine asubuhi ulipokuwa unasoma hotuba yako, ulizungumzia juu ya mikopo ya kuwawezesha watu wanaouza mazao yao nje. Ulituambia hapa umewasaidia sana lakini mimi ninakuomba urudi na kwa wazalishaji wa ndani hasa wakulima wanaozalisha mbegu za mafuta kama vile alizeti, ufuta na kadhalika. Hapa Bungeni imesemwa kwamba, mbegu zinahitajika sana lakini uzalishaji bado uko chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, nimewahi hata kuzungumza na wewe juu ya hili na unajua wazi kwamba, Mikoa hii ya Kanda ya Kati inazalisha sana alizeti kwa hiyo, tunaomba mikopo hiyo iende na kwa hawa wakulima wadogo ili wazalishe zaidi, tusitegemee mafuta yanayotoka nje ambayo hatuyafahamu. Nirudie kukuomba kwamba, kodi ya mafuta yanayotoka nje isipunguzwe bali tujitahidi tuwape uwezo wakulima wetu walime mbegu nyingi zaidi kwa ajili ya kuzalisha mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, nafahamu wazi kuna mpango ambao wewe na Wizara yako umeuandaa wa kusaidia Mikoa kame na iko mingi. Najua *ADB* wanashughulikia fedha hizi na wanasaidia upande wa kilimo, barabara, maji, nishati na mengineyo. Kwa nini mambo haya yanakwenda kimya kimya, kwa nini msiyatoe tuyafahamu? Nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, kwa juhudi zako na jinsi unavyofanya kazi na wasaidizi wako wanavyochapa kazi, mtusaidie kwa hilo.

Mimi ninakotoka wakulima wanazalisha sana lakini hatuna pa kupeleka mazao haya, tunahitaji barabara, sasa hivi Serikali ina mpango wa kuunganisha Mikoa kwa barabara za karibu. Wakati wote nimekuwa nasema sisi tunahitaji daraja la kilomita 12 watu wa Arusha, Singida, Shinyanga, Mwanza, Mara na hata Burundi, waanze kupita pale wakati wote. Tutengenezeeni hizo kilomita 12 za Mto Sibiti na daraja lake gharama yake ni karibu milioni 650 ambazo mimi najua Mheshimiwa Waziri, unaweza kuzipata. Nakuomba sana na hili ni ombi pekee, shughulikia suala hili. *(Makofi)*

Vijiji vyetu vingi hapa Tanzania tuna tatizo la umeme na hilo mimi najua kabisa uwezo wa kutafuta wafadhili Mheshimiwa Waziri anao. Nimekuomba juu ya Jimbo langu ambalo umeme tunausikia kama ndoto, naomba utimize hiyo ahadi yako na hii iende na maeneo mengine ambayo yana shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, maeneo mengi sana yana matatizo ya maji, maeneo mengine tukipata maji ya kumwagilia hili tatizo la kulialia watu kulipa kodi, michango mbalimbali litakwisha, sasa hebu tuingie kwenye hiyo miradi mikubwa. Hawa *ADB* mnaozungumza nao na wafadhili wengine wa nchi mbalimbali hebu tuelekeze nguvu hizo kwenye umwagiliaji. *(Makofi)*

Ninakotoka mimi kuna Mto ambao ukizuiliwa tunaweza kulima mpaka hekta 20,000 za mazao mbalimbali na wakati wote wa mwaka Mto huo unaitwa Malasaki. Nakuomba utusaidie ili wananchi wetu waendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, kuna mikopo ambayo imekuwa inatusaidia ya *import support,* hata wakati wa Bajeti nilizungumzia juu ya mikopo hii. Hii ndio mikopo ambayo itatuwezesha sisi wananchi wa Tanzania tuweze kuendelea, tutanunua pembejeo, tutanunua vifaa vya kutengeneza barabara ambavyo vitaleta maendeleo hapa kwetu lakini masharti bado magumu na hela zinatolewa kama chemchem inayoelekea kukauka. Sasa muwaombe wale ambao wanatufadhili juu ya hilo waongeze fedha hizi ili tupate maendeleo.

Mheshimiwa Waziri, nakupongeza sana wewe na watendaji wako wote, kuanzia Wilayani mpaka hapo ulipo. Kwa kweli sasa hivi wanajitahidi hata hiyo tunayoita rushwa sehemu nyingi imeanza kupungua, ndio maana mapato ya Serikali yanaongezeka. Tunakuomba tu uwape vitendea kazi, uwawezeshe na wale ambao ni sugu waondolewe haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, ni wewe mwenyewe ulituambia ...

**SPIKA:** Elekeza maelezo yako kwa Spika.
**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Samahani Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, alituambia hapa Bungeni sasa hivi anawashughulikia wale ambao sio waaminifu. Tunajua ameshawashughulikia lakini bado wako wengi ambao ni sugu kwa hiyo, tunaomba hao nao wafichuliwe na wachukuliwe hatua za haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile namwomba Waziri wa Mipango washirikiane na Waziri wa Fedha kwani bila kupanga hatuwezi kupata maendeleo. Wenzangu hapa ndani wamezungumza sana juu ya ubinafsishaji lakini namwomba hebu tupitie upya tuone.

Mheshimiwa Spika, nizungumzie juu ya huu umeme nikianza na huu unaotoka Songosongo, kwa vyovyote vile utakuwa wa bei ya juu kuliko hata huu ambao tunauundia Tume leo, nashauri tutafute njia nyingine. Tuna *Stigler's Gorge* kule *Seleous,* ambapo umeme wake tungeutumia ungetosheleza mahitaji ya ndani na hata kuuza nje. Tuna *Mnazibay,* Mchuchuma, naomba twende kwenye vile vyanzo ambavyo havituletei matatizo, sasa hivi ni lazima tukubali. Naishukuru sana Serikali yetu huwa ikiambiwa na wananchi wake na Wabunge wake inakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Mipango, akakae sawasawa na watu wake, waangalie miradi hii upya. Kwa kweli tunakokwenda tutawaumiza sana wananchi wetu kama maji yapo pale *Stigler's Gorge* yanamwagika usiku na mchana, kwa nini tusiende kuyatega yale? Sasa hivi tunaleta wawekezaji, nimefanya utafiti huu mradi wa Songosongo Mikataba 16 imesainiwa lakini mpaka leo matunda yake hayajaonekana, tutakuja kujuta Watanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa hayo machache, nawaomba Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, wasisahau niliyozungumza, wayafanyie kazi kwa faida ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye hoja hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba nitoe shukrani zangu na pia niwapongeze Mawaziri wote wawili, kwa hotuba zao ambazo zimeandikwa vizuri, zinatoa mwelekeo mzuri na mipango mizuri ya mwaka huu wa fedha tunaouanza. Kitu ambacho nawaomba tu wote wawili kwa pamoja, mipango hii sasa waipangie mikakati mizuri ili iweze kutekelezeka maana yake ikibaki kama mipango bila kutekelezwa vizuri, basi tutajikuta kwamba haya yaliyowekwa hapa yatatutia tamaa tu tusiweze kupata faida zake kama zilivyoainishwa.

Mheshimiwa Spika, kwanza, katika Ziwa Victoria, kuna tatizo la vyombo vya usafiri, tatizo hilo sasa ni kubwa. Vyombo aina ya feri karibu vyote vimesimama havisafirishi watu katika Ziwa Victoria, ndio kusema Ukerewe, Kome, Buchosa na kwingine kote kule sasa hivi haviendi. Tatizo hili kwa sababu ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Wizara ya Fedha inajua chanzo cha tatizo hili hasa Ofisi yetu ya *TRA* Mwanza, imeweka msimamo wa kutoza kodi au ushuru kwa watu hao wanaotumia feri hizo. Kuna ushuru wa Sh.500 kwa abiria mmoja na ushuru wa ile *gate* wa kama Sh.200 kabla hawajalipa nauli, sasa gharama inakuwa kubwa.

Mheshimiwa Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, ajaribu kutoa tamko la wazi kabisa wananchi hawa wafanyeje na Wabunge wa maeneo hayo, nina imani kabisa anafahamu Wabunge wa maeneo yote hayo hivi sasa wana wasiwasi wa Buchosa, Ukerewe na wananchi wao kule la kutoa picha kamili na maelekezo sahihi kwa wananchi na wote wanaoendesha feri hizi katika Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwamba, ni vizuri sasa tuone taratibu za mikakati ya utekelezaji kwenye mipango hii ya *speech* zote mbili. Napenda nizungumzie kwa kirefu suala la Ushuru wa Forodha, taratibu nzima za kuingiza bidhaa ndani ya nchi kutoka nje. Ingawa suala hili limeshazungumziwa na Waheshimiwa Wabunge waliotangulia, lakini bado kuna kitu cha kusema tu kwa sababu linaleta wasiwasi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa makusudi ili nilete picha kwa nini bei inakuwa tofauti namna hiyo kwa bidhaa ambayo inazalishwa nchini na bidhaa inayotoka nje, inayotoka nje inakuwa rahisi inayozalishwa hapa inakuwa ghali? Suala hili namwomba Mheshimiwa Waziri, aliangalie kwa makini kwa sababu inaonekana utekelezaji sio mzuri. Kwa nini bidhaa kama ni ile ile iwe na tofauti ya bei kubwa namna hiyo?

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, ukiangalia bidhaa kama khanga, tuna khanga zinazozalishwa hapa nchini na kuna khanga ambazo zinatoka nje ya nchi. Lakini kitu ambacho ni cha wazi ni kwamba, bidhaa hizi zinatofautiana kwenye ubora kwa sababu khanga inayotoka nje, hii ningeomba akina mama waishabikie hii, wawe wagumu kwenye suala hili kwa sababu zile khanga za kutoka nje ni nyepesi mno, maana yake ni kwamba, hazikidhi mahitaji ya kuvalika mbele ya watu nguo zile kwa sababu akivaa bila utaratibu mzuri inaonekana sio vizuri ndani kule. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachotaka kusema hapa ni kwamba, kwa vile tumeweka hii sheria ya ubora wa bidhaa, naomba Wizara hizi mbili ziwasiliane ziweze kuwa na msimamo wa pamoja ili khanga zinazotoka nje na zinazozalishwa nchini zilingane kwa ubora halafu tuangalie kama bei itaachana.

Mheshimiwa Spika, jambo hili nalisema kwa makusudi kwa sababu kuna mambo mengi yaliyojitokeza kutokana na bidhaa kutoka nje. Leo kwenye vyombo vya habari kuna suala la mafuta, pamoja na mipango ambayo Mheshimiwa Waziri ameiweka kwa ajili ya kudhibiti mafuta lakini bado inaoneka kuna matatizo na hapa Serikali inapoteza kipato kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, nimeona jambo hili niliseme kwa kumpa picha Mheshimiwa Waziri, ili alichukulie jambo hili kwa uzito unaostahili ili watendaji wake awapange kufuatana na uwezo wao katika maeneo ya kazi ili kazi hii iweze kuwa nzuri na mapato yote yapatikane na Serikali ipate mapato yake.

Mheshimiwa Spika, kuna bidhaa nyingine kama sukari na nyingine za aina hiyo ambazo zinatofautiana bei hapa nchini na huko nje. Vikija nchini vinakuwa bei rahisi pamoja na kwamba vimesafiri kwa umbali mkubwa mpaka kufika kwetu hapa lakini vinafika hapa vinauzwa bei rahisi, jambo ambalo inabidi lifanyiwe kazi liwe na usahihi mzuri ili tatizo hili lifikie mwisho tuache kulipigia kelele tena.

Mheshimiwa Spika, unapokuwa katika nchi nyingine kwa mfano, ukienda Japan mchele wa Japan utakuwa rahisi tu sababu yake kubwa ni kwamba, hawa watu wanasimamia forodha zao vizuri hakuna mchezo wa kuingiza bidhaa kutoka nchi za nje bila utaratibu wa kulipia kodi. Naomba utaratibu huu na sisi ufanisi huu tuufikie ili tufaidike na hali halisi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, napenda nizungumzie suala zima la elimu kwa walipa kodi. Suala hili bado halijafanyiwa kazi vya kutosha, bado lina mapungufu, bado linahitaji juhudi kubwa za Wizara. Kwa mfano, ukiangalia katika Hotuba ya Bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Fedha, aliyoitoa tarehe 12 Juni, 2003 akizungumzia utaratibu mzima wa jinsi atakavyokusanya mapato, alitoa mfano katika ukurasa wa 58, kuweka viwango vya malipo kwa mtu anayeshughulika na biashara hapa nchini.

Kwa mfano, ameweka viwango akaeleza wazi kwamba, mtu atakayefanya biashara isiyozidi shilingi milioni tatu kwa mwaka basi alipe kodi kama ya Sh.20,000/=, hii inakuwa wazi mtu unaelewa. Anayefanya biashara kati ya Sh.3.1 milioni - Sh.7 milioni alipe ushuru usiozidi Sh.50,000/=, hii iko wazi. Jambo ambalo najaribu kulisema hapa ni kwamba, mambo kama haya yangewekwa wazi kwa wananchi

kama ni kutangaza yatangazwe ili anayekwenda katika Ofisi zetu za *TRA* kulipa ushuru wake aende na mwanga wa kutosha na aweze kujitetea kama akiulizwa swali. Jambo hili linaleta kidogo matatizo ambayo sio mazuri.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri wa Fedha ameeleza wazi kwamba ataongeza kipato, atakusanya zaidi kutoka kwa wananchi na amesema kwamba, atakusanya zaidi ya shilingi trilioni 2.7. Lakini chombo ambacho kinafanya kazi hii bado ni *TRA,* kazi yao tunaifahamu tulikoanzia na walipotufikisha sasa na tunaheshimu na tunawapongeza kwa juhudi hizi ambazo wanazifanya. Kitu kikubwa ni kwamba, kuna machache madogo madogo ambayo yanaweza kuwaharibia jina kama hayakuangaliwa kwa makini. Suala kama hili la uelewa wa wananchi wa viwango vya kodi ambavyo wanapaswa kulipa hasa sisi tulio katika maeneo ya mijini wananchi wengi wanakuja kutulalamikia wanasema kwamba, mbona mimi nimetozwa zaidi kuliko fulani na biashara zetu zinafanana? Jambo kama hili kulijibu inakuwa ngumu lakini sababu kubwa ni kwamba, elimu kwa hawa walipa kodi haitoshi, kwa sababu anayekuwa na taarifa kamili ni yule ambaye anatoza kodi, mlipa kodi anakuwa hana taarifa yoyote.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, haya mapendekezo aliyoyatoa Mheshimiwa Waziri wa Fedha katika Hotuba yake ya Bajeti katika ukurasa wa 58 *table* ile na utaratibu ataukabidhi *TRA,* Afisa wa *TRA* atakuwa na taarifa yote hii ndani ya faili lake lakini anayelipa sasa anakuwa hana mwanga hata kidogo, jambo ambalo naliona linapaswa kufanyiwa kazi, taarifa hizi na maelezo yatolewe kwa sababu hawa ndio wadau wenyewe katika suala zima la kodi. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha, afanye juhudi hizo ili iweze kumsaidia kufanya kazi na wananchi bila ugomvi wowote. Kwa sababu suala hili ukiliangalia kwa undani zaidi unaweza kukuta hasa katika ngazi mbalimbali na uwezo wa Maafisa wake wa kodi labda inaweza kuwa moja ya sababu ambazo zinafanya mambo kama haya kujitokeza. Lakini yeye ajitahidi, apange na aone atasaidiaje wananchi ili waweze kulipa kodi zao kwa uhuru, uwazi na wawe *more willing* kuliko kutozwa kodi kwa utaratibu ambao wanatozwa bila kufahamu wanachopaswa kulipa.

Mheshimiwa Spika, siku za nyuma tulilizungumzia jambo hili la nyumba ambazo zimejengwa nusu hazikukamilika, kuna maswali yaliulizwa Bungeni humu, yanahusiana na Wizara ya Fedha, kwa mfano, hapa Dodoma kuna jengo la *THB* ambalo limeachwa nusu haijulikani nani analiendeleza. Mambo kama haya ni *resource misuse* kwa sababu kama fedha hizo zingekuwepo zingeweza kufanya kazi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, majengo kama haya yapo na sehemu nyingine kwa mfano, Mwanza lipo jengo la Ofisi ya Wizara ya Fedha yenyewe, ambalo mpaka sasa halijakamilika na lina muda mrefu na hapa Bungeni tulilizungumzia lakini mwisho tulijaribu kutafuta njia nyingine za kulitumia jengo hili na nilipeleka maombi kwenye Ofisi ya Waziri kuhusiana na kuruhusu watu wengi walitumie jengo hili, lakini kwa bahati nzuri au mbaya nasikia fununu kwamba, wanataka kulijenga tena. Hali hii inatupa wasiwasi na tunashindwa kujua ni kipi bora tukifanye lakini pesa ndogo hizi tulizonazo ni vizuri kuzitumia vizuri na ziweze kutusaidia katika maeneo ambako tuna shida nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitamke machache kuhusiana na ubinafsishaji. Kwa kifupi ningejaribu kusema wazi kwamba, mpaka sasa juhudi ambazo Wizara imezichukua, semina ambazo imezitoa kwa Waheshimiwa Wabunge, sasa angalau kuna picha kidogo na maswali ya ugumu wa kutoelewa ubinafsishaji yamepungua. Lakini kikubwa ambacho ningependa niseme na kieleweke na Waziri aone kama kinaweza kumsaidia ni kwamba, wanapoingia kwenye ubinafsishaji ningependa mambo haya yawe yanatangazwa wazi zaidi kwa kila mtu, kama mtu ana maoni atoe maoni kwa sababu maoni yakija kwa wingi nina imani kabisa kitakachofanyika kitakuwa bora kuliko ambavyo inavyofanyika sasa hivi. Hilo ni tatizo ambalo limejitokeza ndio sababu limeleta hata hoja za wananchi namna gani tuzungumzie mambo ya ubinafsishaji na kila mtu anataka aseme kufuatana na hali anavyoiona kuhusiana na ubinafsishaji.

Mheshimiwa Spika, kikubwa ni kwamba, tunajaribu kuishauri *PSRC* isisahau uzalendo. Kwa mfano, suala na hoja nzima ilivyojitokeza kuhusiana na ubinafsishaji wa *NMB, NMB* imeleta hoja na mazungumzo marefu lakini ni kwa juhudi zao wenyewe wananchi haikutolewa nafasi kutoa maoni katika jambo hili kabla halijafanyika. Naomba mambo haya yaeleweke, tuna Benki nyingi kama *TIB,* ambayo tunaiona inazidi kubadilika na kila mtu anaona sasa hali hii *PSRC* nayo iangalie kwa undani kama Watanzania kwa sababu *proprietorship* tunaipoteza kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. ALI SAID SALIM:** Mheshimiwa Spika, naomba Wizara iwe makini na kuchukua hatua madhubuti katika suala zima la kubinafsisha Mashirika ya Umma.

Pili, pia ni vyema katika kubinafsisha, hatua za dharura zikachukuliwa ili kuhakikisha kuwa rushwa haipati nafasi katika suala hili.

Tatu, naishauri Serikali kwa kupitia Wizara hizi iwalipe fidia wafanyakazi wote ambao mashirika yao yamebinafsishwa ili kuwaondolea kero.

Nne, wafanyakazi wengi wamekuwa wakilalamika juu ya kucheleweshwa mno mafao yao baada ya kustaafu.

Ni vema kwa Wizara ya Fedha kuandaa na kubuni utaratibu mpya na wa kufaa wa kulipa pensheni ili kuona usumbufu huu wa kufuatilia mafao kwa muda mrefu unaisha.

Tano na kwa kuwa Suala la Ukimwi limekuwa ni tishio kwa Taifa letu ambalo hupoteza maisha ya wananchi wetu, miongoni mwao wakiwemo wafanyakazi ambao wamesomeshwa kwa gharama kubwa, ni vyema kwa Wizara ya Fedha zikachukuliwa hatua za dhamira katika kukabiliana na tatizo hili sugu na hatari.

Katika suala la mikopo naishauri Wizara ya Fedha, irahisishe utaratibu wa kutoa mikopo kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na wao waweze kumudu kuendeleza mtaji ili baadaye waweze kujitegemea.

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, naipongeza Serikali ya awamu ya tatu kwa kazi nzuri na jitihada ya kufufua uchumi, ninashauri kama ifuatavyo:-

Serikali iwe na kitengo cha *monitoring* katika Ofisi ya Mipango ili watalaam waweze kufuatilia utekelezaji wa mipango ya Serikali kwa kipindi husika cha Bajeti. Hivi sasa hatuna *monitoring system* inayoeleweka.

Vile vile *TRA* katika baadhi ya mikoa, kama Lindi wanakatisha tamaa wafanyabiashara Mjini Lindi, wafanyabiashara takribani wote wanalalamikia viwango wanavyodaiwa na vitisho toka kwa maafisa wa *TRA*. Baadhi wameshafunga maduka na kuna hatari, kama hawa *TRA* wataendelea kuwa-*harass* wafanyabiashara, Mjini wa Lindi utakosa maduka. Serikali iliangalie hili.

Ubinafsishaji ni Sera ya CCM, ni Sera yenye lengo la kuitoa Serikali katika kufanya biashara. Lakini pamoja na ujuzi wa Sera, CCM ina mila na desturi ya kujipima na kujikosoa. Sera ya CCM siyo misaafu kwamba hazirekebishwi ni vema Serikali ya CCM ikapima ufanisi tuliopata. Taarifa niliyopata kutokana na jibu langu Bungeni, Serikali ilikuwa iuze Mashirika wa kwa Dola za Kimarekani 204 Milioni na Sh. 64 bilioni hela za Tanzania tumepata 43 bilioni, wakati dola ni 63, nusu ya kiwango bado. Serikali ijipime na ichunguze malalamiko ya wananchi kuliko kuendeleza tena mipango bila kupima hali ya hewa ilivyo.

Nashauri *NMB* isibinafsishwe sababu ina mtandao nchi nzima, lakini zaidi tumejifunza kwamba, *NMB* tuliyobinafsisha, wamefunga baadhi ya matawi ambayo ni kero kwa wananchi. Nashauri Serikali kwa sasa ipime matatizo na iache kabisa kubinafsisha *NMB.*

**MHE. SALOME JOSEPH MBATIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja hii muhimu.

Ninaomba nianze kwa kumpongeza sana Waziri wa Fedha, Manaibu wake na wasaidizi wao wote, kwa kweli kwa kazi nzuri sana wanayofanya kama timu kuhakikisha Hazina inatimiza majukumu yake bila ya mtetereko mkubwa. Katika kipindi hiki cha mwaka uliopita nchi imeshuhudia ufanisi si wa uendeshaji tu bali kukua kwa uchumi na sekta zote. Kama mapato yameongezeka, nidhamu ya fedha imeimarika na hata mafao ya Bunge, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninaipongeza sana Wizara pia kwa kuanzisha mtandao wa usimamizi wa fedha na malipo kwa kutumia kompyuta *(IFMS).* Bila ya usimamizi madhubuti kama huu, uvujaji wa fedha utapunguza nia na uwezo wa Serikali kukamilisha malengo yake. Ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuongeza kiwango na sasa kutolipa kwa mkupuo kwa pensheni pia tumeipongeza Wizara. Isipokuwa ningependa Waziri akifanya majumuisho aliambie Bunge kuhusu pensheni kwa wafanyakazi wa iliyokuwa *East African Community* ya zamani. Nini utaratibu wa watu hawa? Nina maana kuwa wao hadi sasa wanapata kiasi cha shilingi 800/= kwa mwezi. Hundi ya Sh. 800/= kwa mwezi kuifuatilia pamoja na *clearance* ya benki na kadhalika ni zaidi ya shilingi 1,000/=. Hali hii inafanya malipo haya kuwa kero na mzigo kwa walipwaji. Je, Mheshimiwa Waziri, anatuambia nini kuhusu hili, watu hawa wakamlilie nani? Tungependa kupata maelezo na maelekezo ya wapi wahusika waende au wafanye nini? Kwa nini nao wasipate shilingi 20,000/= kwa mwezi kama wastaafu wengine? Hawa si ni wananchi kama wengine.

Mheshimiwa Spika, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja.

**MHE. CHRISTOPHER S. WEGGA:** Mheshimiwa Spika, naanza kwa kuwapongeza, Mawaziri wote wawili, Naibu Waziri watatu, nawapongeza Makatibu Wakuu watatu Wizara zote mbili. Nawapongeza watumishi Wizara zote mbili kwa uhodari wao wa umahiri katika kazi zao Wizara zote mbili.

Naomba kuchangia eneo la *TRA.* Nashukuru kuwaondolea wakulima wangu wa kilimo cha miwa Kilombero, wakulima wadogo wa *(ROA)* ambao matrekta mawili ya wakulima hao yamekwama Tunduma. Nashukuru ushirikiano niliopewa na Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil P. Mramba, hiki ni kielelezo tosha kwa Waziri wetu na Watendaji wa Wizara ya Fedha. Hongera sana kwa hoja hizo hapo juu.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mpango wa kutoa mikopo kwa wakulima wadogo wadogo hatujawahi kupata mkopo mpaka sasa, wakulima wa Kilombero wananunua trekta kubwa kwa fedha yao bila mkopo wowote. Wana mtaji ambao ni zaidi ya shilingi bilioni mbili. Ukiunganisha na mashamba yao, wana umoja wao na wamesajiliwa. Tatizo hawana hati za nyumba, ili wapate mikopo hiyo, naomba Serikali iwatambue wakulima wa Kilombero *(ROA),* waweze kupata vitendea kazi kama vile trekta, pembejeo na kadhalika ili wakatwe wakati wa kuuza miwa yao Kilombero. Chama cha Wakulima wa Kilombero *(ROA)* wanaomba kupitia Mbunge wao hisa zilizoko Kilombero, Serikali isifanye kosa, wasifanye kama Mtibwa kuwapa wawekezaji wa Kilombero, asilimia 25 ni ya Watanzania wa Kilombero na Watanzania wenzao nchini. Kwa kweli suala la kutoa hisa zote kwa mwekezaji ni kumnyima haki mkulima mdogo wa miwa kukaa bila kuwa na sauti katika biashara ya miwa na sukari.

Mheshimiwa Spika, kilimo cha pamba katika Jimbo la Mikumi tumeamua kulima katika jamii ya Tarafa za Masanze, Mikumi, Wilaya ya Kilosa, tunaomba mikopo ya pembejeo na mbegu za pamba pamoja na madawa ya pamba, masharti nafuu, tuweze kulima pamba.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ZAHOR JUMA KHAMIS:** Mheshimiwa Spika, siku za hivi karibuni tulisoma katika magazeti kuhusu utozaji wa kodi kwa magari ya kigeni nchini Tanzania. Katika utaratibu huo pia unajumuisha na magari ya watu binafsi yaliyosajiliwa Zanzibar. Naomba ufafanuzi ambao Mtanzania wa Zanzibar kuwa sawa na mgeni katika mali zake ndani ya Tanzania Bara. Naomba ufafanuzi.

**MHE. REMIDIUS E. KISSASSI:** Mheshimiwa Spika, napenda kusema naunga mkono hoja zote mbili zilizopo mbele yetu. Vile vile nawapongeza Mawaziri wote wawili, pamoja na watendaji wao, kwa kazi nzuri wanazofanya. Nawatakia kila la kheri katika utendaji wao lakini napenda kuchangia machache yafuatayo:-

Kwanza, Mashirika ya Umma yanayoendelea kubinafsishwa yalazimishwe kuingia katika soko la *DSE,* baada ya muda fulani ili Watanzania waweze kununua hisa zao. Lakini vile vile zile hisa za Serikali nazo ziuzwe kupitia *DSE.*

Pili, elimu ya umuhimu wa kununua hisa kupitia *DSE* isambazwe mpaka Wilayani na vijijini kote ili Watanzania wahamasike. Ikiwezekana hisa zitengwe kikanda/kimkoa ili ushirikishwaji/umiliki uwe mpana zaidi nchini kote.

Tatu, suala la *TRA* kupanga magari yenye namba ZA, ZNZ kuwa ni kama za kigeni, lirekebishwe haraka sana na naomba kauli ya Serikali juu ya hili. Hii inaleta usumbufu na malalamiko yasiyo na msingi na Waziri wa Fedha tumeshamweleza hili.

Nne, matatizo katika Bandari ya Dar es Salaam katika kutoa mizigo bado yapo na inaelekea yanapaliliwa na baadhi ya watendaji wa *THA* na *TRA.* Wafanyabiashara wa Zanzibar bado wanasumbuliwa sana na hivi karibuni kumejitokeza kero ya ajabu sana. Kwanza, tiketi zinalanguliwa kutokana na tiketi kuuzwa mapema kwa walanguzi na vyombo vya dola vinajua. Pili kuna kitu kinafanywa eti kutia *seat number* kwenye *lounge* na kuleta usumbufu wa bure. Pia, wameanza kuzuia abiria wasipande kwenye boti na mizigo yao midogo midogo na kadhalika. Naomba hili likemewe haraka sana. Ahsante.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naunga mkono hoja zote mbili kwa asilimia mia kwa mia.

Nachukua nafasi hii kuwapongeza kwa kazi nzuri mnayofanya, hotuba zenu ni nzuri, zenye dira na mwelekeo na kadhalika. Pia nawapongeza sana Makatibu Wakuu wa Wizara zenu kwa kazi nzuri wanazofanya wakisaidiwa na Watendaji wengine Wakuu.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Fedha, kwa hatua nzuri anazozichukua kuhakikisha ongezeko kubwa la makusanyo ya Serikali kila mwezi, nakuomba endelea hivyo hivyo na ikiwezekana mapato yaongezeke zaidi kwa faida ya Taifa hili. Vile vile nakupongeza sana kwa hatua unazochukua kuhakikisha wale wachache wanaovunja maadili ya kazi zao na kujiingiza kwenye wizi wa fedha za umma, rushwa nakadhalika, wanashtakiwa au kufukuzwa kazi mara moja. Mheshimiwa Waziri, nakupongeza kwa hatua unazochukua kuhusu malipo ya *pension,* hata hivyo, bado nakuomba ujitahidi sana ili uanzishe ofisi za kanda ili wastaafu waanze kulipwa huko. Wananchi wastaafu wanakupongeza sana kwa kuwaongezea fedha za mafao ya uzeeni.

Mheshimiwa Spika, nakuomba utaratibu ulioanzishwa wa kuwakopesha wananchi wanaolima/kusafirisha mazao nje uanzishwe na kwa wakulima wa alizeti na ufuta kwani sasa hivi bado wanalima kidogo kutokana na uwezo wao mdogo. Wewe ni shahidi ya kwamba, mbegu za alizeti zina soko kubwa sana na zionaongeza kipato cha Serikali. Nakuomba uendelee na msimamo wako imara wa kutopunguza kodi ya matuta yanayoagizwa kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, nafahamu fika ya kwamba, kuna mradi unaofadhiliwa na *ADB* wa kusaidia mikoa kama maeneo ya kilimo, barabara, maji, afya na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, chini ya mpango huo namwomba Mheshimiwa Waziri, asaidie kwenye miradi ifuatayo:-

(a) Shilingi 650.0 milioni kwa ajili ya kujenga Daraja la Mto Sibiti, eneo linalounganisha Mikoa ya Arusha, Manyara, Shinyanga na Mwanza kupitia Iramba Mashariki.

(b) Fedha kwa ajili ya kuanzisha kilimo cha umwagiliaji kwenye Mto Malasagi ambao eneo la hekta 10,000 zinaweza kumwagiliwa, gharama ya mradi unakisiwa kuwa shilingi 350 milioni.

(c) Mheshimiwa Spika, nilishaongea na Mheshimiwa Waziri, juu ya kupeleka umeme Iramba Mashariki kama ifuatavyo:-

(i) Mtinko - Iambi km 35 - 830.0m;

(ii) Iambi - Nduguti km 15 - 320.0m; na

(iii) Kinampanda - Msingi km 6 - 82.0m.

Mheshimiwa Spika, eneo la Iambi (Nkungi) tumepata wafadhili ambao watatujengea:-

(i) *Nursing School* - Diploma;

(ii) Chuo cha Sekondari; na

(iii) Upanuzi wa Hospitali ya Nkungi inayotegemewa na wakazi wote wa Iramba Mashariki eneo la Hanang na Singida Kaskazini.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa *import support,* uboreshwe masharti yake maana wananchi wa kawaida hawawezi masharti yake. Pia kwa wale ambao wamebahatika kuanza kukopeshwa utafutwe utaratibu wa kupata kiwango kinachotakiwa *50.0m Yen* ili wakamilishe miradi ambayo wameshaanzisha.

Mheshimiwa Spika, kwa kumalizia naomba sana suala la viongozi wa vitengo Hazina kukaimu, haipendezi kufuatana na Kanuni za Serikali anatakiwa akaimu miezi sita tu baada ya hapo anathibitishwa au anapewa sababu za msingi kwa nini hakuthibitishwa.

**MHE. KILONTSI M. MPOROGOMYI:** Mheshimiwa Spika, naomba kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wa Fedha na Mipango na Ubinafsishaji. Naunga hoja zote mbili mkono mia kwa mia. Ningependa nitoe mchango wangu kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Kwanza, hivi sasa nchi inapoteza fedha nyingi sana katika kulipia madeni ya nje. Lakini madeni mengine kama yale ya *IPTL* ni ya kujitakia na nchi inapata hasara kubwa sana, kwamba nchi maskini kama Tanzania tunalipa Sh. 30 bilioni kila mwaka. Fedha hizi zingeweza kusaidia sana katika jitihada za Serikali na kuondoa umaskini.

Pili, hata hivyo, Serikali itaendelea kupoteza fedha nyingi tu kwenye Mradi wa *Songosongo Gas*. Mradi huu ulipoanzishwa ulitegemea kugharimu kiasi cha Dola za Kimarekani milioni 194 mwaka 1993. Gharama hii iliongezeka na kufikia Dola za Kimarekani milioni 240 mwaka 1997 na hivi sasa mwaka 2003 gharama hizo zimefikia Dola za Kimarekani milioni 300. Bei hizi zimekuwa zikipanda eti kwa sababu ya kutoa *figure* ya *escalation* ya 3%. Mpaka hapo mradi huu utakapokamilika gharama itafikia *cent* za Marekani 12 kwa *kilowatt hour*. Gharama zote hizi hatimaye zitatolewa na wananchi wa kawaida. Ikumbukwe kwamba, fedha za kujenga *Songas* ni mkopo kwa Serikali kutoka Benki ya Dunia. *Capacity charge* kama ilivyo kwa *IPTL* Sh. 2.5 bilioni, *Songas* itagharimu Sh. 5 billion kwa mwezi *on the basis of take or pay* kwa mwezi.

Miradi yote miwili ni ya kuikosesha Serikali mapato makubwa ambayo yanaikosesha nchi maendeleo makubwa. Je, Waheshimiwa Mawaziri, kwa nini tulikubali miradi hii kuliko ile ya *Mnazi Bay* na Mchuchuma, ambayo gharama yake ni *cent* za Kimarekani 5 na 4 *respectively.* Kwa nini Mikataba ya *Songas* toka 1993 mpaka leo hii haipungui 16 na yote inahakikisha kwamba, mwekezaji analindwa kwa njia zote *against all costs,* asipate *any financial exposures*, asipate *foreign exchange rises* zozote na kwamba, fedha zinazolipwa na Serikali kwa ajili ya mikopo hii zinatokana na mlipa kodi wa nchi hii?

Mikataba yote ya *IPTL* na *Songas* ni mibaya. *Cost of during business* kwa wafanyabiashara na wenye viwanda wanalalamikia gharama kubwa za uzalishaji zinazosababishwa na gharama kubwa ya umeme. Wawekezaji wengi wanaogopa kuja Tanzania kwa sababu ya mambo kama haya.

**MHE. MATHEW T. OLE-TIMAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia.

Mheshimiwa Spika, nampongeza mtoa mada/hoja, pamoja na safu yake nzima ya watendaji. Kazi ni nzuri na wanastahili pongezi. Hoja sina tatizo nayo, hivyo naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ubinafsishaji, binafsi sina ugomvi na dhana wala sera ya ubinafsishaji kwa sababu zipo sababu za kimsingi za kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, ninalo tatizo na nina ugomvi na utekelezaji wa sera ya ubinafishaji kwenye maeneo yafuatayo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza, ni Mikataba. Karibu sehemu kubwa ya Mikataba ya wawekezaji ina utata mkubwa, ni kwa nini? Je, ni uwezo hatuna au ubinafsi umetutawala? Mfano, Mikataba ya Madini au uchimbaji madini ya mrahaba wa 3%, ni wapi kwingine duniani wanafanya hivyo?

Pili, ni maslahi ya wafanyakazi. Karibu sehemu kubwa ya mashirika yaliyobinafsishwa wafanyakazi wamelalamika na wanaendelea kulalamika kwa sababu maslahi yao hayajazingatiwa na kupewa umuhimu unaostahili mfano, *NBC, TES* na kadhalika. Unafanya kazi miaka 30, Shirika likibinafsishwa unapewa mshahara wa mwezi mmoja, kwaheri.

Tatu, ni kuhusu ubinafsishaji na wawekezaji wa ndani. Zoezi la ubinafsishaji unawapendelea zaidi watu au wageni kutoka nje, zaidi ni wawekezaji wa Afrika Kusini, kwa nini? Ni lini tutawawezesha Watanzania kuchukua mashirika hayo, kwa mfano, *DAHACO?*

Nne, ni kuhusu uvunaji wa maliasili, madini na wanyamapori. Eneo hili la uvunaji wa maliasili limetawaliwa na wageni kwa maana ya uchimbaji wa madini na uvunaji wa wanyamapori. Mwenyezi Mungu, katujalia utajiri mkubwa wa maliasili badala ya kunufaika nazo tunaona ni busara tuwakabidhi wageni kwa kuwekeana Mikataba isiyo na maslahi kwa Taifa letu, kwa nini? Je, ni uwezo au utaalam hatuna au ubinafsi umetutawala?

Mheshimiwa Spika, sote tujiulize, ni kwa nini tukubali mrahaba wa 3% tu kwa madini yetu? Kwa nini tukubali tani na tani za udongo kutoka kwenye machimbo ya madini yetu usafirishwe nje ya nchi? Pia, ni kwa nini wawindaji wa kigeni wapewe vitalu vya uwindaji kwenye ardhi ya vijiji bila ridhaa ya wenye ardhi kisheria ambao ni wanakijiji? Je, ni uwezo/utaalam hatuna au ni ubinafsi umetutawala?

Mheshimiwa Spika, hatuwezi kufungua tu milango ya uchumi na kutangaza kufuata mfumo wa soko huria au uchumi wa soko bila kupunguza umaskini kwa watu wetu. Raslimali zetu za asili yaani madini na wanyamapori ni lazima Watanzania wafaidike nazo kabla ya wageni kufanya vinginevyo, ni kuwasaliti umma wa Watanzania ambao wengi wao wanaogelea kwenye dimbwi la umaskini uliokithiri wa kutokuwa na huduma muhimu za afya, maji, shule/elimu, barabara usafiri na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali iangalie uwezekano wa kupitia upya Mikataba ya wawekezaji hususan Mikataba inayohusu uvunaji wa maliasili (madini na wanyamapori).

Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil P. Mramba, kwa kuendelea kuimba wimbo wa mafanikio makubwa ya kiuchumi yanayotokana na ukusanyaji wa mapato ya ndani na nje. Ni kwa nini maisha ya wananchi wa kawaida vijijini bado ni duni kwa kukosekana kwa huduma muhimu za jamii ambazo ni maji, afya, elimu, barabara na kadhalika?

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Spika, nawapongeza Mawaziri wote kwa hotuba nzuri. Napenda kupata ufafanuzi toka kwao: -

- Pamoja na kwamba Afrika Kusini haiongozi katika kununua mashirika yetu, si hatari kiusalama kuendelea kuwauzia mashirika nyeti kama *TBL* na *ATCL?* Kama wakiamua kugoma, mapato ya Serikali yatakuwaje?

- Kuna tatizo la wastaafu wa *PPF* kutolipwa mafao yao eti kwa kuwa hawajatimiza miaka 55 na hata kile kidogo walichokuwa wanapata kimesimamishwa na hawapati lolote. Hili ni tatizo kubwa na ni kero kubwa sana kwa watu wengi ambao uwezekano wa kupata ajira ni mgumu kupata na kiwango cha maisha kimepungua sababu ya UKIMWI. Kwa nini Serikali isiwalipe tu wale waliostaafu mashirika ya umma?

- Kuna minong'ono iliyozagaa kuwa *NIC* inafilisika na haiwezi kuwalipa wateja wake. Nini hatma ya watu wenye Bima zao na wanaoidai? Nini tamko la Serikali kuhusu hili sakata na je, kwa nini kuna haja ya kuendelea kuweka Bima za Magari kwa lazima kupitia *NIC?*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. LEKULE M. LAIZER:** Mheshimiwa Spika, napenda kuipongeza Wizara ya Fedha, kwa utaratibu mzuri wa fedha uliowekwa sasa. Ongezeko la mapato limeonyesha ufanisi wa kazi nzuri kwenye Wizara. Wizara hii ndio Wizara mama na inayotegemewa kwa maendeleo ya Watanzania wote.

Ukaguzi wa fedha ndio msingi wa kuimarisha ufanisi uendelee kwani wizi wa fedha ni kama UKIMWI kwa maendeleo na kuathiri mipango mizuri iliyowekwa na Wizara. Naomba watumishi wachache ambao ni wezi, wasiruhusiwe kuharibu utaratibu na ufanisi wa Wizara hii. Kwa kuwa nchi yetu imekuwa mfano, basi iendelee bila kuharibiwa na watu wachache.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa malalamiko kwako kuhusu jambo ambalo lilifanywa na Wizara hii mwaka 1994. Napenda kuelezea jengo ambalo limejengwa Namanga karibu na geti la kuingilia ndani eneo la Kituo cha Namanga. Jengo hilo limejengwa na Bwana Mungai, baada ya kuombwa sana na Serikali ya Wilaya ili liwe la *VIP* pale Namanga kutokana na kwamba, wageni maarufu wanapopokelewa hakuna eneo la viongozi la kupumzikia au wale wanaoingia na kutoka waweze kupata mahali pa kukaa. Mwananchi huyo hakutaka kujenga jengo hapo bali aliombwa sana, tena mara nyingi, *DC* alimfuata na Viongozi wa Chama kumsihi akubali kujenga *VIP* pale.

Mheshimiwa Spika, jengo hili limejengwa pale kiwango cha kumalizika. Mhusika ambaye ni Bwana Mungai amenunua *furniture* zinazohitajika. Mwaka 1996 Wizara ya Fedha, ilimsimamisha mwananchi huyo kujenga jengo hili kwamba, liko katika eneo la Serikali. Ni kweli eneo hilo ni la Serkali, hakuna ubishi, lakini ombi la kujenga pale limetoka Serikalini. Tangu jengo lianze kujengwa, Serikali ilikaa kimya bila kumsimamisha mhusika kwamba ameingilia eneo lao mpaka jengo kukamilika!

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ilimwomba mwananchi huyo ajenge nyumba hiyo na baada ya kumaliza akasimamisha basi Serikali ichukue jukumu la kumfidia ili itumie jengo hilo kwa matumizi waliyotaka au kwa matumizi mengine yoyote wanayotaka. Jengo hili limekaa miaka 7 bila kutumika na kwa kuwa liko kwenye eneo la Serikali, basi mhusika afidiwe.

Mheshimiwa Spika, kuna wakati Serikali ilitaka kufidia, lakini sijui mpaka sasa kikwazo ni nini? Kuliko jengo hilo likae mpaka liharibike, afadhali litumiwe na Serikali kuliko kuwa gofu. Jengo hilo limekuwa kero pale Namanga? Kwa kuwa wananchi wanaelewa kwamba, Bwana Mungai aliombwa, sasa malalamiko yamezidi kutolewa.

Mheshimiwa Spika, wakati wa majumuisho, nami napenda kupata jibu kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kwani malalamiko kuhusu jengo hili yamezidi kiwango.

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Spika, ninaomba Benki mpya ya Wavuvi kuonyesha njia sahihi za kupata mikopo kwa sababu ya utata wa dhamana hata na uwezo wa kulipa na ujuzi wa wavuvi. Dhamana huwa inaleta matatizo ya kupata urahisi wa mikopo.

Mheshimiwa Spika, *CRDB* ilipokuwa ni Benki ya Maendeleo na Ushirika, ilikopesha wavuvi wengi sana Mkoani Kigoma, wavuvi wengi waliweza kurudisha kwa wakati uliopangwa lakini kwa sasa utaratibu huo haupo na kama upo unaonyesha nyuma ya dhamana.

Mheshimiwa Spika, *NMB* iimarishwe kwa sababu imeanza kukopesha watumishi na Serikali hasa walimu, waganga na watumishi wa ngazi za chini.

Mheshimiwa Spika, miundombinu hafifu ni chanzo cha umaskini kwa Mikoa ya Kanda ya Magharibi. Serikali kutopeleka umeme wa uhakika ambao ni mgao kama chakula cha wafungwa kwa Mkoa kama vile Kigoma, umaskini hauwezi kuondoka.

Vile vile barabara isiyokuwepo ya *shortcut* kati ya Itigi - Tabora - Kigoma, bado ni shida kubwa na Serikali ianze mikakati ya haraka ya kupata au kukubali deni kubwa kutoka mahali popote pale kutoka *World Bank.*

Pia, mipango ya Daraja la Mto Malagarasi ni muhimu sana kupata wahisani na kulikamilisha kwani linahitaji pesa nyingi sana. Mipango ya kuleta maendeleo siyo kuhusu suala la umeme na barabara ya *shortcut* Kanda ya Magharibi, itazamwe kama vile macho yameanza kutazama Kanda ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, ni vema Serikali ishughulikie mipango ya kila kanda ili kuondokana na umaskini uliokithiri hasa hasa wa miundombinu.

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza sana Waziri wa Fedha, kwa Hotuba yake nzuri.

Ninaipongeza sana Serikali kwa uamuzi wake wa kufuta Kodi ya Maendeleo na Ushuru wa Mifugo kwa nchi nzima. Kwa niaba ya wapiga kura wa Jimbo la Kondoa Kusini, ninaishukuru sana Serikali kwa uamuzi huu.

Katika Hotuba ya Bajeti, Waziri wa Fedha, aliahidi kuwa Serikali Kuu itafidia mapengo yatakayojitokeza katika Halmashauri zote nchini ili ziendelee kutimiza majukumu yake. Taarifa kutoka Wilaya zote nchini zinathibitisha kuwa ahadi hii bado haijatekelezwa na matokeo yake ni kwamba, hivi sasa Halmashauri nyingi zimeshindwa kujiendesha, hasa zile Halmashauri zilizokuwa zinategemea kwa asilimia kubwa Kodi ya Maendeleo na ushuru wa mifugo ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa. Athari katika Wilaya ya Kondoa ni kama ifuatavyo:-

(i) Halmashauri imeshindwa kuchangia miradi ya wafadhili; na

(ii) Halmashauri imeshindwa kuwalipa watumishi wake wakiwemo Watendaji wa Vijiji na Kata.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja zilizo mbele ya Bunge lako Tukufu.

Awali ya yote, napenda nichukue fursa hii kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu wahusika, pamoja na Watendaji wote ambao kwa pamoja wameshiriki katika kuandaa hotuba hii kwa umahiri mkubwa. Hongera sana.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee nitoe pongezi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwezesha kutekelezwa ndoto za kujenga daraja maarufu la Mkapa.

Mheshimiwa Spika, niruhusu niwapongeze wananchi wa Mbinga kwa kuanzisha Benki ya Wananchi *(Mbinga Community Bank)*. Napenda niishukuru Benki Kuu ya Tanzania, kwa kushughulikia maombi yetu kwa mwendo wa radi. Naomba kwa niaba ya wakazi wa Mbinga, Mheshimiwa Waziri, apokee salamu zetu.

Mheshimiwa Spika, tatizo letu limekuwa ni kukosekana kwa huduma za mikopo kwa wakulima wetu kuanzia mwaka 1997 hadi leo hii. *NMB* kwa kipindi chote hiki haitoi mikopo kwa sababu ya kukosekana kwa umeme.

Mheshimiwa Spika, hofu yetu kubwa ni gharama kubwa za umeme kwa sababu kwa kuanzia imebidi pawepo na jenereta mbili za umeme. Hali kadhalika Kampuni ya Simu za Mkononi ya *Celtel* ina mtandao hadi Mbinga, lakini huduma hiyo imeathirika kwa sababu ya kukosa umeme.

Mheshimiwa Spika, kama utaratibu wa Mipango yetu hautaangaliwa upya, nchi hii inaweza ikajikuta pabaya kutokana na hali inayojionyesha kuwa na upendeleo wa maendeleo katika maeneo fulani fulani.

Mheshimiwa Spika, ni jukumu la Wizara hizi mbili kuishauri Wizara ya Nishati na Madini, kupeleka umeme katika Wilaya ambazo hazina umeme na hasa Wilaya ya Zamani kama Mbinga.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba fedha zitakazotolewa za Mfuko wa Pembejeo na kadhalika, zitakazopelekwa kwa wakulima wa Mbinga sasa zipitie *Mbinga Community Bank.*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. DR. BATILDA SALHA BURIAN:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, naomba kuanza kwa kutoa pongezi zangu za dhati kabisa kwa Waheshimiwa Mawaziri hawa wawili, yaani Mheshimiwa Basil Mramba, Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, pamoja na Manaibu Waziri, kwa kazi nzuri na hotuba nzuri walizowasilisha humu Bungeni. Pia, naomba nimpongeze Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Mipango, Dr. Bukuku na Makatibu Wakuu wa Fedha, pamoja na Wataalam wote kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, napenda kuanza kwa kusema moja kwa moja kwamba, ninaunga mkono hoja hizi mbili. Pamoja na kuunga mkono hoja, naomba kuchangia katika maeneo machache kama ifuatavyo:-

Napongeza jitihada za *TRA* za kuwa na mikakati ya kufikisha huduma za kodi zote *(One Stop Centre)* katika Mamlaka za Wilaya ifikapo mwaka 2004. Mimi napendekeza jitihada hizi zisifanyike *in isolation,* bali kuwe na utaratibu wa kuunganisha huduma mbalimbali ili kupunguza gharama, lakini pia kuongeza ufanisi zaidi, kwa mfano, kodi ya *TRA*, kodi ya kiwanja, Bima na kadhalika, ingeweza kulipwa kupitia Ofisi za Posta. Hivyo, mashirikiano ya kisekta ni muhimu sana kati ya Sekta ya Mawasiliano, Mipango na Fedha.

Jambo lingine ni kuongeza kasi ya uanzishwaji wa *One Stop Center* kupitia *TIC.* Nadhani jitihada hizi ziharakishwe ili kila Mkoa uwe na *focal center* ambayo itaweza kufanya kazi na Ofisi za Kanda. Utaratibu huu utapunguza gharama za ufuatiliaji.

*Harmonization* ya *Tax* kwa nchi za Afrika Mashariki, jitihada hizi ni nzuri. Hata hivyo, nchi yetu iangalie upya ili kupunguza asilimia ya kodi ya *VAT*. Pia Waziri wa Fedha, ningeomba atoe kauli kuhusu Tanzania kuingia tena kuwa Mwanachama wa *COMESA.*

Kuhusu utaratibu wa Michezo ya Kubahatisha, nchi nyingi zimeanza kuweka masharti magumu sana kwenye michezo hii ili ku-*discourage* watu (Wazalendo) kuzoea kutumia fedha zao katika kamari. Nchi kama Afrika Kusini, Mauritius ni mifano michache. Hivyo, nchi yetu iangalie upya, leseni za michezo

ya *slot machine* ziwe na ada kubwa ili kupunguza mashine hizo kwani wahanga *(victims)* wa mchezo huu ni vijana zaidi.

Utaratibu wa kutayarisha *Tanzania Assistance Strategy (TAS),* kwa mawazo yangu ningependa *TAS* ishughulikiwe na Ofisi ya Mipango kwani kutokana na Mfumo wao ni rahisi zoezi zima likawa shirikishi zaidi kuliko linavyofanyika sasa chini ya Ofisi ya Hazina. *Emphasis* hapa si tu kupata fedha za *development partners* lakini zaidi ni maeneo ambayo fedha hizo zitaelekezwa na *impact* itakayopatikana kutokana na mchango huo.

Kuhusu ubinafsishaji na ufuatiliaji wa Makampuni yaliyobinafsishwa, naomba Mheshimiwa Waziri wa Mipango, aelezee kwa nini viwanja vya usokotaji wa nyuzi vya Ubungo na *Tabora Spiral Mills* havifanyi kazi mpaka sasa?

Pia ningependa kupata maelezo kuhusu *Rural Telecommunications Funds.* Je, fedha hizo mpaka sasa hivi ni kiasi gani na nipewe mchanganuo wa matumizi hadi kufikia mwisho wa mwaka huu wa Fedha 2002/2003. Napongeza jitihada za kuboresha *National Website.* Naomba jitihada zaidi zifanyike kwa ushirikiano na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ili kuhakikisha kwamba, *National Website* inawafaidisha wananchi wengi hasa wa Vijijini.

Hivyo, jitihada za Wizara ya Mawasiliano katika kuhamasisha uanzishwaji wa *Community Tele-Centre* ziungwe mkono na Ofisi ya Mipango na Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba kuunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Spika, dhana ya ubinafsishaji ni ya msingi na tunaiunga mkono na hasa tukitilia maanani mwenendo na mfumo mzima wa kiuchumi wa kidunia ulivyo hivi sasa.

Hata hivyo, dhana hiyo inapokosa usimamizi ulio thabiti, inatoa nafasi kwa wajanja na watu wenye kupandikiza mchezo mchafu dhidi ya dhana yenyewe na matokeo yake ni kushindwa kufaulu kwa zoezi zima lililokusudiwa.

Katika mambo ambayo Wizara imeyaeleza kuyapa kipaumbele katika mwaka wa fedha 2003/2004 katika ukurasa wa 26 Kifungu cha 50, suala la kufuatilia madeni kwa Makampuni yaliyonunua Mashirika/Viwanda vilivyobinafsihwa halikuelezwa. Hii ina maana hakuna mikakati mahususi itakayowekwa ya kukusanya madeni hayo. Hivyo, suala linaloelezwa la kuendelea na ubinafsishaji wa Mashirika yaliyobaki ni kazi bure. Mfano, naomba Mheshimiwa Waziri, anifafanulie na kunieleza hatma ya viwanda vya *Morogoro Canvas Limited,* vilivyobinafsishwa mwaka 1998 kwa kuuzwa Shilingi bilioni 1.872 na mnunuaji akalipa Shilingi milioni 936. Pamoja na kutakiwa kulipa *balance* iliyobaki ndani ya kipindi cha miezi sita, bado mpaka leo hajalipa. Naomba kuelezwa tatizo ni nini?

Je, Mikataba inasemaje? Kwa nini mnunuzi hanyang'anywi kiwanda hiki kutokana na utapeli aliofanya? Ni vizuri mnunuzi akapewa *ultimatum* ya siku 30 za kulipa na pia alipe na *interest* ya miaka mitano. Mbaya zaidi ni ukweli kwamba, mnunuzi huyo huyo aliuziwa kiwanda cha *MOPROCO* kwa Shilingi milioni 900 na akalipa milioni 120 tu. Milioni 780 hazijalipwa hadi leo. Hivi Serikali inataka kuwaambia nini Watanzania ambao walifunga mikanda kuyaanzisha na kuyaendesha Mashirika haya huko nyuma?

Hali kama hii inatia wasiwasi kwamba, huenda mambo yako hivyo hivyo kwa Mashirika mengi yaliyouzwa. Hivyo, kuna haja ya kutolewa taarifa inayoonyesha mwenendo mzima wa ununuzi wa Mashirika yaliyobinafsishwa au kukodishwa.

**MHE. JUMA S. KIDUNDA:** Mheshimiwa Spika, Wizara hii chini ya Waziri, Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda na timu yake ya wataalam, wakiongozwa na Katibu Mkuu, inastahili pongezi kwa kazi kubwa ya kufufua uchumi wa nchi hii. Hongera sana. Pamoja na pongezi hizi, nina machache ya kuchangia kuboresha hotuba ya Mheshimiwa Waziri, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya Chuo cha Mipango kuendesha Semina na warsha za mara kwa mara kwa Maafisa Mipango wa Wilaya ili Maafisa hawa wabadilishane mbinu na mikakati bora ya upangaji wa maendeleo katika Wilaya zetu. Jambo hili ni muhimu kwa sababu Maafisa Mipango wa Wilaya hutoka Vyuo tofauti vyenye mielekeo tofauti juu ya dhana na mwelekeo wa mikakati ya upangaji katika ngazi za Wilaya na Vijiji. Kuna haja ya kuimarisha dhana ya takwimu katika Chuo cha Mipango na napendekeza kianzishwe Kitengo cha Takwimu katika mtaala wa Chuo cha Mipango. Jambo hili ni muhimu kwa kuwa taaluma ya takwimu ni muhimu sana kama sehemu kuu ya dhana na taaluma nzima ya mipango. Kwa kuanzia au pamoja na mapendekezo haya, nashauri mahusiano kati ya Chuo cha Mipango na Chuo cha Takwimu yaimarishwe ili kuboresha taaluma ya Mipango katika Chuo cha Mipango zaidi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Spika, ingekuwa vyema kwa Wizara kuwasiliana na TAMISEMI ili kuhakikisha kuwa, Maafisa Mipango wa Wilaya ni wale tu wenye vyeti vya taaluma ya Mipango. Kwa sasa kuna idadi kubwa ya Maafisa Mipango wasio na vyeti vya taaluma ya Mipango au vile vinavyoshabihiana na vile vinavyotolewa na Chuo cha Mipango. Jambo hili si sahihi kwa kuwa mipango ni taaluma.

Nampongeza Mheshimiwa Waziri na Watendaji, kwa kuchukua hatua za hakika za kukiimarisha Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini. Upanuzi wa Mabweni, Madarasa, Ofisi na Ongezeko kubwa la zana za kufundishia kama ko,pyuta unaonesha dhamira nzuri ya Wizara ya kuimarisha utaratibu wa kutafsiri mafanikio makubwa yaliyopatikana katika uchumi mkuu kwenda uchumi wa kaya. Chuo cha Mipango ni chombo muhimu katika kuwezesha mabadiliko haya. Naipongeza Wizara kwa kuliona na kulifanyia kazi jukumu hili la kukiimarisha Chuo hiki. Hata hivyo, idadi na kiwango cha taaluma bado inahitaji kuboreshwa sana? Kuna haja ya kukisaidia Chuo kupata *scholarships* nyingi za Udaktari wa Falsafa. Kitendo hiki kitawavutia wasomi wengi kwa shahada za kwanza na pili kujiunga na Chuo kwa matarajio ya kuendeleza taaluma zao kufikia kiwango cha juu na hivyo kujaza nafasi nyingi za wakufunzi ambazo ziko wazi kwa muda mrefu kwa kukosa waombaji wenye sifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, kwa Bajeti nzuri na kuongeza mapato kufikia shilingi bilioni 110. Pamoja na pongezi hizo, naomba maelezo kwa yafuatayo:-

Kwa kuwa Waziri ndiye Msimamizi na Mdhibiti wa fedha zote nchini, naomba maelezo juu ya fedha zilizotolewa na *GGM* kama fidia kwa wananchi wa Geita (Mtakuja) na zikaishia kuliwa na watumishi wa Serikali. Wakaguzi wanasemaje kuhusu hili? Ni kwa nini Serikali inajitahidi kuficha ukweli kuhusu wizi wa pesa hizi?

Kwa kuwa wananchi hawajalipwa fidia, Serikali imetenga kiasi gani ili kuwalipa wananchi wanaodai na watalipwa lini? Kwa sababu Wabunge wa Geita wameambiwa hakuna kurudi kama hawana jibu la uhakika, kwa nini wezi wasiwajibishwe au na Waziri aligawiwa kidogo? (Aseme kama alipata kitu kidogo).

Kwa kuwa kukusanya mapato ni pamoja na kuwawezesha wananchi kujiongezea kipato; Je, njia zilizofungwa na Mgodi wa *GGM* zimesababisha hasara kiasi gani kwa wananchi wa Kata za Bukwando, Nyakagamba, Busanda, Chigunga, Katoro, Kaseme, Rwangasa na Nyarugusu? Kwa nini njia hiyo isifunguliwe kupitia Samina, Magema hadi *Cop Cot,* ambayo haipitii mgodini ili kuwawezesha wananchi kuzalisha haraka haraka na kuongeza ushuru au mapato Serikalini? *GGM* wako tayari kufungua ile, wanangoja agizo la Serikali tu. Kwa nini Serikali haisaidii?

Mwisho, naomba Waziri afuatilie fedha za *OC* kama zinafanya kazi yake, kwa mfano, Walimu hawalipwi madai yao wakati *OC* zinapelekwa. Naomba atueleze kuna matatizo gani na madai ya walimu? Madai haya ni kero na yeye anafahamu. Sasa sielewi kwa nini hawalipwi madai yao? Ni kero mno! Tafadhali naomba Mheshimiwa Waziri, aingilie kati.

Mwisho, naomba maelezo ya fidia kwa wananchi wa Geita hususan Kijiji cha Mtakuja na barabara ya Geita - Ilogi, Vijiji vya Buyagu, Nyakwanzaja, Kamera na Ikina. Naomba watu hawa walipwe, vinginevyo tunawaruhusu warudi kwenye maeneo yao na shughuli za uchimbaji zisimame.

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda, kama ifuatavyo:-

Nchi yetu miaka ya nyuma ndio iliyokuwa inaongoza katika uzalishaji wa zao la mkonge duniani. Kwa sasa nchi ya Brazil ndiyo inayoongoza katika uzalishaji wa zao la mkonge duniani. Brazil inazalisha mara saba zaidi ya tunavyozalisha mkonge katika nchi yetu, nchi ya Mexico inazalisha mkonge mara tano zaidi ya tunavyozalisha sisi na nchi ya China inazalisha mara tatu zaidi ya tunavyozalisha sisi. Mbinu wanayotumia katika nchi hizo kuzalisha zaidi na kukikuza kilimo cha zao la mkonge ni kuwawezesha wakulima wadogo wadogo kushiriki katika kilimo cha zao la mkonge. Kwa kutumia mfumo wa kushirikisha wananchi katika kulima zao la mkonge nchi ya Brazil katika *State* ya Bahia wakulima wadogo wadogo wamewezeshwa na Serikali yao ya Brazil kujenga viwanda vya kusindika bidhaa zitokanazo na zao la mkonge.

Mheshimiwa Spika, haya ni mafanikio makubwa na mazuri sana. Napendekeza Serikali ipeleke *delegation* Brazil kwenda kujifunza jinsi ambavyo wakulima wadogo wadogo wa mkonge katika nchi ya Brazil walivyoweza kufikia hatua ya kujenga viwanda vya kusindika bidhaa zitokanazo na zao la mkonge.

Mheshimiwa Spika, nashauri *delegation* hiyo ijumlishe viongozi kutoka Serikalini, Halmashauri za Wilaya, Bodi ya Mkonge, *Sisal Association* na Kamati ya Bunge ya Kilimo, Ardhi, Maji na Maendeleo ya Mifugo. Nashauri hivyo kwa sababu viongozi wao wakipata elimu kutoka *State* ya Bahia, watasaidia kuhamasisha wananchi kujiunga na kilimo cha mkonge.

Mheshimiwa Spika, aidha, naomba Mheshimiwa Waziri, anieleze sababu na msingi zilizopelekea kushindwa na kukataa kutoa hatimiliki kwa Kampuni ya *Katani Limited* kwa kipindi cha zaidi ya miaka sita sasa tangu Kampuni hiyo ilipotimiza masharti yote waliyotakiwa kuyatimiza katika Mkataba kabla ya kubinafsishiwa mashamba hayo.

Mheshimiwa Spika, Kampuni hii inamilikiwa na Wahisani 87 wa Tanzania. Hawa wanahisa 87 ni mabingwa wa zao la mkonge duniani na imewashirikisha wakulima wadogo wadogo wa zao la mkonge 2,250. Naomba Mheshimiwa Waziri, anieleze ana mikakati gani ya kuwawezesha hawa wakulima wadogo wadogo kuendeleza uzalishaji wa zao la mkonge kwa shabaha na lengo la kufikia hatua iliyofikiwa na wakulima wadogo wadogo wa *State of Bahia* ya Brazil?

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza hapo juu, naomba nielezwe sababu zilizokwamisha kutolewa kwa hatimiliki kwa *Katani Limited*, lakini wakati huo huo Serikali imetoa hatimilliki kwa wawekezaji katika Sekta ya Madini ingawa uchimbaji madini sio endelevu ikilinganishwa na zao la mkonge ambalo ni endelevu kwa maana linaweza kupandwa mpaka mwisho wa dunia kwa kuzingatia kanuni za uendelezaji wa zao la mkonge.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, mchango wangu leo naelekeza pande zote yaani Wizara yenyewe ya Fedha na upande wa Mipango na Ubinafsishaji. Kwa kuwa fedha hazitoki bila mipango, naona ni haki kulaumu Ofisi hii ya Mipango maana haijapanga lolote la maana katika Jimbo langu la Moshi Vijijini. Nasema haya kwa sababu kuanzia mwaka 1964, Serikali kwa makusudi ya kisiasa iliondoa kisingizio kuwa ni eneo lililoendelea, hivyo ni sahihi kupiga *mark time* ili wenzetu wa Kusini au Singida au Pwani waweze nao kupiga hatua ya maendeleo ili tufanane sote Watanzania.

Mheshimiwa Waziri kinachotokea sasa ni kibaya sana. Mimi sikuwa na tatizo sana kuhusu msimamo wa Serikali wa wakati huo, lakini kinachoendelea sasa ni kwa ile *marking time* inaonekana

kuendelea na kilichotokea mbele ya ushahidi wa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mheshimiwa Cynthia Hilda Ngoye ni kwamba, Jimbo la Moshi Vijijini ni la mwisho sasa Tanzania kama vile ukiangalia elimu, ndio eneo lililoshika mkia Tanzania na ripoti inaonyesha Shule saba mbaya sana zinatoka Moshi Vijijini, jambo ambalo zamani ilikuwa ikiongoza. Hii ni kutokana na kutofikiria nyuma kwamba huyu tuliyemsimamisha nae anahitaji sana kutembea. Mheshimiwa Waziri, atakubaliana na mimi kuhusu maendeleo yalivyokuwa huko nyuma? Hata ukiangalia mipango ya maji ya bomba pamoja na wananchi hao kuchangia, hakuna kinachoendelea. Hata michango ya wananchi hao kuhusu barabara ya lami hadi lami yenye thamani ya Sh.350,000,000/= ambayo ni jumla ya pipa za lami zaidi ya 3,500 inaoza bure na Serikali ipo, visima vya maji vilivyochimbwa huko Mtakuja, Chekereni na Mabogini Jimbo la Moshi Vijijini vimeachwa hivyo hivyo na vimeharibika na fedha za umma kupotea.

Napongeza jitihada zinazofanywa sasa huko kwenye Wilaya ya Hai na Rombo ni za kutia moyo. Sijui kuna makosa gani waliyofanya kwa Serikali hii hawa wananchi wa Moshi Vijijini, kama lipo niko tayari kupiga magoti na kuomba msamaha kwa niaba yao.

Baada ya kutoa maelezo haya ya utangaulizi, naiomba Serikali kupitia Wizara hii ya Fedha, kurejea ahadi yake kwamba, *marking time* ilikuwa ya muda tu ili Serikali sasa ifungue daraja lake la maendeleo la huko Moshi Vijijini ili tuweze kupata elimu kama zamani. Afya mahospitalini na madawa kama zamani, barabara nzuri kama ilivyokuwa imependekezwa kwenye mipango yetu ya maendeleo hata mpango wa MMEM ufike huko kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, naeleza haya kwa uchungu maana Mawaziri wote niliowauliza kuhusu hoja hii, walinijibu hivyo hivyo kuwa Serikali hiwezi kukubali kuleta maendeleo haya huko. Hata ukisoma kwenye *Hansard*, mchango wa Mheshimiwa Lamwai, alisema kuwa, mnapoangalia kigezo cha maendeleo kimkoa haitoshi na alitoa mfano wa Kibosho Tarafa iliyopo huko Moshi Vijijini kuwa ni eneo lenye watoto wenye kwashakoo na umaskini kuliko eneo lolote lingine Tanzania.

Nisikuchoshe ila naomba utupie macho na tuwasaidie maana wametengwa mno. Nategemea ushirikiano hata kahawa ya huko inachekesha ukiliinganisha na nyingine. Ahsante.

**MHE. MWADINI ABBASS JECHA:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kuichangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri hasa katika Mradi wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri amesema kwamba, zoezi la Sensa ya Watu na Makazi lilikamilika mwezi wa Septemba, 2002 na kwamba, taarifa ya jumla ilikamilika mwishoni mwa Desemba, 2002 na kusambazwa Wilayani, Mikoani, Wizarani na katika Taasisi mbalimbali na wadau wengine.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano, ni miongoni mwa wadau muhimu wanaostahili kupatiwa taarifa ya jumla ya zoezi zima la Sensa ya Watu na Makazi. Miongoni mwa majukumu ya Waheshimiwa Wabunge, ni kushirikiana na asasi na wadau wengine katika kuwaletea maendeleo, sio tu kwa wananchi waliomchagua, lakini kwa ajili ya maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Kwanza, naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri iwapo anakubaliana nami kwamba, Waheshimiwa Wabunge wanastahili kupatiwa ripoti hiyo na iwapo wanastahili ni lini atawapatia Waheshimiwa Wabunge ripoti hiyo ili nao wawe katika nafasi nzuri ya kupanga maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla?

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kuunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia. Awali ya yote niwapongeze Wizara hii, kwa kuanzia na Waziri Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda, Watendaji na wataalam wote wa Wizara kwa kutayarisha hotuba hii yenye uelewa.

Mheshimiwa Spika, shughuli zote mbili za ubinafsishaji na uwekezaji huenda sambamba na hutegemeana sana. Ucheleweshaji wa Vitengo hivyo husababisha Serikali kukosa mapato au soko la uhakika ambalo lingeweza kutuletea faida zaidi. Pale tu inapoonekana kwamba hili limeanza kuzorota ni vyema Serikali ikaanza mara moja kutafuta soko au kutengeneza kwani kama hatutachukua hatua haraka,

basi itabidi iuzwe kwa bei ya hasara kama vile *ATC* na kadhalika au kukosa soko kama vile *TABOTEX* (Tabora).

Kwa maana hiyo, Serikali isisite kuwekeza au kubinafsisha, kwani hizo ndizo Sera za CCM, hatuwezi kukwepa lawama na tutakapoacha tutalaumiwa na vizazi vijavyo. Kwa mfano, hata kama mtaji umempa mtoto wako akashindwa kuendesha ni bora utafute mtaji umpe mtu baki ili atakapokiuka utampekeka Mahakamani au hatua zozote. Bado nasisitiza umuhimu huo ufanyike mapema. Pia ufanyike ukaguzi wa mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyoanza hapo juu, ningependa nitoe shukurani kama ifuatavyo:-

- Kutokana na elimu duni ya wananchi kutokana na mambo mawili (ubinafsishaji/uwekezaji), ni vyema elimu hii ikashuka hadi chini, Wilaya, Mkoa na kadhalika.

- Elimu ya Makampuni, Mashirika, viwanda ambavyo havifanyi kazi vizuri, wafanyakazi wa maeneo hayo waelezwe mapema kabla ya kutangaza na wapewe takwimu, wawashirikishe Vyama vya Wafanyakazi na Uongozi mzima.
- Viandaliwe vipeperushi kwa lugha nyepesi ili viwafikie mpaka Vijijini.

- Semina mbalimbali kwa ngazi zote hususan viongozi wa Wilaya/Mikoa na kadhalika pale uwezo utakapokuwepo.

- Kwa wale waliowekeza kwenye Mashirika, Makampuni na wameshindwa kuyaendesha, yachukuliwe na Serikali kwa kuvunja Mkataba na wafikishwe kwenye Vyombo vya Sheria.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo kubwa ni ubovu wa Mashirika yetu, ni vyema Shirika la *TRC* lingekuwa katika hali nzuri kabla ya kununua vifaa vingine ambavyo vitavutia wawekezaji hususan, mabehewa na mahitaji muhimu, kwani wao pia wanapokuja na kufikia migogoro huogopa. Hivyo, ni vyema tumalize mapema kabla ya soko, kama nilivyogusia hapo juu.

Mheshimiwa Spika, naomba niunge mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dr. Abdallah O. Kigoda, Mbunge na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, kwa hotuba yake nzuri, yenye maelezo ya wazi kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara hiyo.

Aidha, napenda kuwapongeza Watendaji Wakuu wa Wizara hiyo na Asasi zake wakiongozwa na Dr. Bukuku, Katibu Mkuu, kwa kumsaidia Waziri katika kuandaa hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, napenda kutoa ushauri ufuatao:-

Kwanza, hotuba ya Waziri ukurasa wa 24, Kamati inayohusika ya Uwekezaji na Biashara na siyo Mitaji ya Mashirika ya Umma. Waziri arekebishe wakati wa kufunga hoja.

Pili, Wizara ijaribu kushauri Mashirika ya *PPF, NSSF, LAPF* na kadhalika, yaagalie uwezekano wa kushirikiana na kujenga *Conference Centre* Dar es Salaam. *Conference Centre* inahitajika sana Dar es Salaam. Hoteli kubwa zilizoko zina vyumba *(Meetting Rooms),* visivyo na hadhi ya kushughulikia mikutano kama *SADC.*

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, wakati Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini iliposomwa, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, aliilieleza Bunge lako kuwa, katika Mikataba ya kati ya Serikali na Makampuni ya Madini, ikiwemo Kampuni ya *Geita Gold Mine* kuna kipengele ambacho kinazipa mamlaka Halmashauri za Wilaya/Miji/Jiji husika, kudai kodi kutoka Makampuni hayo zisizozidi Dola za Marekani 200,000 kwa mwaka.

Huko nyuma, Wizara ya Nishati na Madini, ilishatamka hapa Bungeni kuwa Mikataba ya Serikali na wenye migodi hao ni siri. Kwa sababu hiyo, sisi Wabunge wa Geita, pamoja na Halmashauri yetu, hatukujua chochote kuhusu kipengele hicho kwa sababu ya usiri wa Mkataba huo.

Hii ilipelekea Halmashauri ya Wilaya ya Geita, ishindwe kudai kodi hizo kwa miaka minne sasa yaani kuanzia mkataba uliposainiwa Septemba 1999 hadi leo Agosti, 2003. Kwa sababu hiyo, ninaomba maelezo ya kina kuhusu yafuatayo:-

(i) Ni kodi zipi (zitajwe) ambazo Halmashauri itoze Makampuni hayo?

(ii) Yapo Makampuni yaliyo chini ya msamaha wa Kodi *(Tax Holiday)* kama vile *STANCOM (T) Limited*, Tumbaku - Tabora ambayo hulipa *land rent* na *property tax.* Kuna sababu zipi zinazoifanya Kampuni ya *GGM* isilipe *land rent* na *property tax?*

(iii) Wizara inatamka nini juu ya Halmashauri ya Wilaya ya Geita kudai malimbikizo ya kodi katika Kampuni ya *GGM* ya miaka minne iliyopita kama Mkataba unavyojieleza?

Mheshimiwa Spika, kuna maelezo kuwa Mkataba kati ya Serikali na *Ashanti Goldfields* ya Ghana ulisainiwa Septemba, 1999 kwa masharti hayo ya Mkataba na kwamba kipindi cha *Tax Holiday* cha miaka mitano kingeishia mwaka 2004. Mwaka 2001 Kampuni ya Ashanti iliuza asilimia 50 ya *shares* zake kwa Kampuni ya *Anglo-Gold* ya Afrika ya Kusini na jina sasa la Kampuni likabadilika na kuitwa *Geita Gold Mines (T) Limited.* Sasa swali; je, mabadiliko haya yanahusu pia masharti ya Mkataba wa kwanza ambapo *Tax Holiday period* ingeisha mwaka 2004 na kwamba sasa kipindi hicho kimesogezwa hadi 2006?
Je, ikitokea *GGM* wakauza *shares* au Kampuni hiyo kwa nyingine Serikali inasemaje kuhusu masharti ya Mkataba wa awali? Ninaomba majibu ya Serikali.

**MHE. BENEDICT K. LOSURUTIA:** Mheshimiwa Spika, ninachukua nafasi hii kumpongeza Waziri, pamoja na wataalamu wake, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii. Naomba nichangie kwa mambo yafuatayo:-

Kwanza, suala la Pato la Taifa. Inaelekea kuwa nyenzo ambazo zinatumika kukadiria Pato la Taifa bado hazijakamilika na hili ni jambo la hatari kwani lugha ya kupanda Pato la Taifa huenda sambamba na matarajio ya wananchi. Naomba Serikali ikamilishe zoezi hili.

Nashauri Serikali ifungue Idara za Takwimu kwa kila Wilaya. Muundo ni ule ule, naomba uendelee kurekebisha hali hii ili wananchi walio wengi waweze kufaidi keki ya Taifa.

Nampongeza tena Waziri kwa kufanikisha Sensa ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii mia kwa mia.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, pongezi kwa Waziri, Katibu Mkuu na Wakuu wote wa Idara katika Wizara ya Fedha. Pia natoa shukrani na pongezi kwa Waziri, Katibu Mkuu na Wakuu wote wa Idara katika Wizara ya Mipango.

Mheshimiwa Spika, *Tender Board* za Wilaya ziko chini ya Wizara gani? Sheria ya *Tender Board* na ununuzi wa vifaa inatamka Waziri gani mwenye Mamlaka ya uundaji na usimamizi wa *Tender Board* za Wilaya?

Mheshimiwa Spika, miradi mingi sasa hivi inakwenda na kushughulikiwa zaidi Wilayani. Hivyo, wasimamizi wakuu na wafuatiliaji wakuu ni Waheshimiwa Madiwani. Je, Wizara inayo habari kwamba, Waraka uliotolewa kuwa Mheshimiwa Diwani yeyote anapotaka kutembelea mradi wowote kwenye Kata yake eti lazima apate kibali cha Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo?

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha kwa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ungeanza pamoja Julai hadi Juni. Hii ingeepusha masuala mengi yaliyojitokeza hivi sasa ambayo Halmashauri ilibidi zikae tena kufanya marekebisho ya kodi zake na vyanzo vya mapato kwa ajili ya gharama ya uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, *PSRC* imemaliza kazi zake, naipongeza. *PSRC* kwa mujibu wa sheria, kazi yake ni kubinafsisha, kuuza na kuingia ubia. Mashirika ya aina hiyo sasa yamekwisha, yamebakia ya kukodisha kama vile *TRC, TANESCO, DAWASA*, Simu na Vyombo vya Fedha.

Mheshimiwa Spika, nina maoni mawili. Kwanza, kusitisha zoezi hili la ubinafsishaji na kuangalia mafanikio ya Mashirika haya yaliyobinafsishwa kwa miaka mitatu na *PSRC* ifutwe.

Pili, *PSRC* haikupewa madaraka ya kukodisha, bali ni kuuza, kuingia ubia. Sio kukodisha! Neno kukodisha limezuka miaka ya karibuni ili *PSRC* kujipa kazi ya zaida.

Mheshimiwa Spika, *chain* ya mipango ikoje Kitaifa, Kimkoa na Kiwilaya? Mkoa unapanga vitu gani? Wilaya hata ikipanga mfano barabara, shule, maji, fedha zinazotolewa na Serikali hazifuati mipango ya Wilaya. Inatuma fedha jinsi inavyoona Wizara ya TAMISEMI, Elimu, Ujenzi hutoa fedha kulingana na mgao unavyopangwa na Wizara. Je, yapo mahusiano?

Mheshimiwa Spika, Wahasibu waangaliwa marupurupu yao ili wasizibie Idara zao? Ipo haja Wizara kufikiria upya marupurupu ya wahasibu ili wawe na motisha.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa naomba kutoa shukrani za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika hoja ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji. Tumezingatia hoja zilizotolewa na yale ya kufanyia kazi tutayafanyia kazi. Lakini kabla sijaanza kugusia baadhi ya hoja naomba niwatambue Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa maandishi.

Nao ni Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Profesa Henry Robert Mgombelo, Mheshimiwa Juma Kidunda, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Mwadini Jecha, Mheshimiwa William Shellukindo, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Mbarouk Mwandoro, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Ole Timan, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mheshimiwa Dr. Masumbuko Lamwai, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, Mheshimiwa Mwanamkuu Kombo na Mheshimiwa John Elieneza Singo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni kwanza ni Mheshimiwa Njelu Kasaka, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi. Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mheshimiwa Alhaj Hassan Mpeme, Mheshimiwa Lucy Nkya, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa Mutamwega Mgaywa, Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Lwakatare, Mheshimiwa Mgana Msindai na Mheshimiwa Stephen Kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kumshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi kwa mchango wake alioutoa kutokana na hotuba tuliyoitoa hivi leo. Napenda kukiri kwamba hivi sasa ofisi yangu kwa maana Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji mimi nikiwa kama Waziri nimepata ushirikiano mkubwa sana kutoka Kamati hii ya Fedha na Uchumi katika masuala mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo ambalo tumelipatia ushauri wa kina sana ni katika eneo ambalo tunalizungumza kwa muda mrefu, nalo ni eneo la ubinafsishaji ambalo Waheshimiwa Wabunge wa Kamati hii wengi walitembelea mashirika tuliyobinafsisha. Wamerudi wamekuja kutueleza mafanikio, matatizo na mimi naahidi Kamati hii na Waheshimiwa Wabunge kwamba Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji itazingatia kwa makini sana ushauri wote uliotolewa na Bunge hili. Kwa hakika kabisa kabla ya kufika mwaka 2005, yale mashirika yote ambayo yanaonekana yakiwa na tatizo hili au lile tutashirikiana na Wabunge kwa karibu zaidi wote kwa pamoja tumalize matatizo hayo ili tuendelee na suala zima la kukuza uchumi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Njelu Kasaka na Kamati yake walitaka Chuo cha Mipango, Maendeleo Vijijini kihusishwe na mpango wa *PADEP.* Sisi tunasema kwamba Chuo cha Mipango kimeshirikishwa na mpango wa kilimo wa *PADEP.* Chuo kimeshiriki katika kuandaa na kutoa hadidu za rejea kwa ajili ya mfumo wa utekelezaji wa *Participatory Land Evaluation and Production Sector* kama Mjumbe wa Kamati ya Kudumu. Vile vile Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi imesisitiza uboreshaji wa Ofisi ya Takwimu, kazi ya ukarabati itafanywa kwa awamu kuanzia mwaka huu wa fedha na taratibu za kumpata kandarasi zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, vile vile Kamati ya Fedha na Uchumi imezungumzia suala zima la ufuatiliaji wa mashirika ya umma yaliyobinafsishwa. Lazima tukubali kwamba katika eneo la ufuatiliaji bado tunayo changamoto ya kufuatilia. Mimi nakubaliana kabisa na hoja ya Kamati ya Fedha na Uchumi kwamba tunataka tuweke jitihada kubwa katika kufuatilia mashirika yale yaliyobinafsishwa kwa maana ya kuyaona kwamba yanafanya kazi kama yalivyokusudiwa kwa maana ya wawekezaji wale kumaliza madeni ambayo wanadaiwa hivi sasa. Pia kwa maana ya kuona kwamba ni misaada gani tunaweza kuitoa kama Serikali hata ile ya Kisera kuhakikisha kwamba baadhi ya viwanda visivyofanya kazi vinafanya kazi. Kwa hiyo, mimi nakubaliana kabisa na Kamati ya Fedha na Uchumi kwamba pamoja na Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kuwa mfuatiliaji mkuu pamoja na sekta husika za mashirika yaliyobinafsishwa kuendelea na ufuatiliaji huo bado tunahitajika kufanya kazi kubwa zaidi ili kuweza kumaliza hili zoezi la ubinafsishaji ambalo kimsingi sasa limeisha tukibakia na mashirika makubwa machache hasa mashirika makubwa ya miundombinu ambayo tunatarajia kuyafanyia ukodishaji.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi vile vile alizungumzia suala la *PSRC* kuajiri wakusanyaji madeni. *PSRC* kwa kweli haina uwezo wa kufuatilia madeni kutokana na kukabiliwa na majukumu mengi ya ubinafsishaji. Kwa hiyo, kutokana na hali hiyo inachukua wakusanyaji wa madeni na hadi sasa kwa kweli kuna kiwango kikubwa tu cha madeni kimekusanywa kupitia utaratibu unaofanywa hivi sasa. La msingi ni kuboresha zaidi taratibu hizo ili kuwafikia wote wale wanaodaiwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi vile vile imesisitiza tuboreshe mazingira ya uwekezaji wa biashara nchini. Katika hotuba yangu nimeelezea programu maalum inayoitwa *Business Environment Strengthen for Tanzania Basis* ambayo kazi kubwa itakuwa ni kuhuisha kanuni na taratibu na zile sera ambazo zinakwamisha wafanyabiashara ili kuondoa kasoro na vikwazo ambavyo vinazidisha gharama ya kufanya kazi kwa upande wa sekta ya biashara.

Mheshimiwa Spika, vile vile napenda kumpongeza Mheshimiwa Hamad Rashid Mohammed, Mbunge kutoka *CUF* ambaye ndiye Waziri Kivuli wa Mipango. Kwanza kwa kuunga mkono hoja zote mbili ya Waziri wa Fedha na hoja yangu. Napenda kumwambia tu kwamba mpango wa muda wa kati ambao unaendana na kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025, unatarajiwa kukamilika mwaka huu wa fedha wa 2003/2004 ili utekelezaji wake uanze mwaka 2004 na 2005.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile Mheshimiwa Hamad alisema kwamba Wizara inatumia vigezo vyake vya kupimia umaskini kinyume na vile vya Kimataifa. Si sahihi kwa sababu ni kweli kabisa kuwa Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji inajenga vigezo vyovyote vile kwa kufuatilia hali ya uchumi na ustawi wa jamii kama vile vya Kimataifa na ndiyo maana katika kujenga vigezo hivyo tunashirikiana na Chuo Kikuu na Taasisi za Utafiti za ndani na nje ya Nchi.

Mheshimiwa Spika, vile vile Kambi ya Upinzani waliuliza kwa nini mwekezaji wa *NBC Limited* hajalipa fedha za ununuzi wa hisa za *NBC.* Ukweli ni kwamba mwekezaji amekwishalipa jumla ya shilingi bilioni 12 ambazo zimeingizwa katika *NBC* kama mtaji. Fedha hizo zililipwa mwaka 2000, mwaka 2004 wawekezaji hao wanatakiwa walipe shilingi bilioni moja, mwaka 2005 wanatakiwa walipe shilingi bilioni moja na mwaka 2006 wanatakiwa pia vile vile walipe bilioni moja. Kwa hiyo, jibu sahihi ni kwamba wawekezaji hawa wamelipa shilingi bilioni 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waziri Kivuli vile vile alizungumzia suala la zoezi la ubinafsishaji linaendeshwa bila kuzingatia ushirikishwaji wa wadau mbalimbali na kwa nini kunakuwepo na usiri mkubwa katika zoezi hili. Katika kutekeleza zoezi hili Serikali kupitia *PSRC* inawashirikisha wadau mbalimbali katika hatua zote za kubinafsisha Shirika. Utaratibu huo unaanzia kwenye Kamati ya Wataalam ambayo inaundwa na wawakilishi kutoka shirika lenyewe linalobinafsishwa, Wizara mama, Wizara ya Fedha, Wizara ya Sheria na Katiba, Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji, Wizara ya Ardhi na *PSRC.* Maandalizi ya Kamati hii yanapelekwa kwenye Tume ya *PSRC* na baada ya hapo mapendekezo ya Tume hupelekwa Wizara mama ambayo pia hupitia mapendekezo hayo na hatimaye kupeleka mapendekezo kwenye Baraza la Mawaziri kwa uamuzi wa mwisho. Sasa kutokana na mlolongo huo ni dhahiri kwamba suala la ushirikishwaji wa wadau mbalimbali linazingatiwa na suala zima la usiri halipo.

Mheshimiwa Spika, Msemaji wa Kambi ya Upinzani vile vile aliulizia kwa nini wafanyakazi wa *Tanzania Elimu Supplies* wanacheleweshewa malipo yao baada ya shirika lao kupelekwa *LART* kwa ajili ya kufilisiwa. Kisheria wafanyakazi hawa wanastahili kulipwa mafao yao ya msingi *(Statutory Benefits).* Fedha za kuwalipia *statutory benefits* zimeshapelekwa. Mgogoro ni kwamba wafanyakazi wanadai malipo ya ziada nje ya utaratibu ambayo nitakuja kuyazungumzia vizuri wakati tutakapozungumzia suala zima la mafao ambalo linapigiwa sana kelele. Hata hivyo Serikali sasa hivi inawasiliana na wafanyakazi hao wa *TES* na tunategemea kwamba tutapata maelewano ya hivi karibuni.

Mheshimiwa Spika, mchango mwingine ambao tumeupokea ni uliotoka kwa Mheshimiwa Alhaj Ahmad Hassan Mpeme, Mbunge wa Mtwara Vijijini. Mheshimiwa Mpeme alizungumzia sana suala la ni jinsi gani tunaweza kupambana na umaskini na umaskini tunaweza kuupa msisitizo gani na tuna sababu gani kwamba huo umaskini upo. Lakini katika mchango wake Mheshimiwa Mpeme alielezea vizuri yeye mwenyewe taratibu za nini tunaweza kufanya tukapunguza umaskini wetu. Kwanza amezungumzia ukosefu wa uwezo wa miundombinu, lakini vile vile aliongelea suala la elimu, pia alisisitiza kwamba ipo haja ya Serikali kushirikisha wananchi katika uzalishaji mali, lakini vile vile kutafuta chachu ya kuwavutia wawekezaji hasa katika maeneo ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, amezungumza vizuri vile vile kwamba suala la kilimo lipewe kipaumbele hasa kilimo cha umwagiliaji maji na baadaye alitoa pongezi kwa sera zetu za uwekezaji hususan kwa kumalizwa daraja la mto Rufiji. Mimi napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mpeme kwamba umaskini tulionao na mipango yetu tuliyoipanga hasa mkakati wetu wa kupunguza umaskini kama tutaufuatilia kwa miadi yote na kama tutaufuatilia kwa kufanya kazi na kama Serikali itaendelea kuwezesha wakulima hawa, nina uhakika kabisa kwamba suala la umaskini litaweza kupungua kwa kiwango fulani. Lakini kama ninavyosema siku zote ni lazima tubainishe umaskini wa kipato na lazima tubainishe umaskini usio wa kipato.

Mheshimiwa Spika, katika suala la umaskini usio wa kipato tumepiga hatua kidogo hasa katika kuendeleza sekta za elimu, afya, maji na baadhi ya miundombinu ingawaje kwenye suala la umaskini wa kipato bado tuna kazi kubwa ya kufanya. Lakini kwa kuondolewa kwa kodi hizi na Serikali kutoa ruzuku katika mambo ya pembejeo inaweza kusaidia kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, alizungumza kwa jazba sana ilifikia kipindi mpaka alisema anataka kulia, hapana, usilie. Labda nimweleweshe mambo fulani Mheshimiwa Dr. Nkya.

Kwanza, *Morogoro Shoes* na *Morogoro Leather Companies,* hivi vilifilisiwa chini ya usimamizi wa Wizara ya Viwanda na Biashara mwaka 1992. Wakati ule hata *PSRC* na mambo ya ubinafsishaji hayajaanza. Lakini kwa taarifa tulizozipata ni kwamba wafanyakazi wote wale waliotoka katika viwanda hivi walilipwa mafao yao ya kisheria *(statutory benefits).*

Mheshimiwa Spika, matatizo yanajitokeza pale ambapo wafanyakazi hawa wanataka kulipwa mkono wa kheri au wanataka utekelezaji wa Mikataba ya Hiari na tunasema siku zote kwamba wafanyakazi wanapotakiwa kulipwa mkono wa kheri ile *golden handshake* ile itatokana na tija na faida iliyopatikana katika shirika husika. Sasa kama shirika limefikia kiwango cha kufilisika, kwa vyovyote vile suala la *golden handshake* litakuwa ni tatizo kubwa sana. Ndiyo maana tunasema kwamba ni vizuri tukakubali kabisa kwamba mpaka hivi sasa hakuna madai yoyote ya mafao ya kisheria ambayo Serikali bado haijayalipa.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile kuna masuala ya pensheni na *PPF* na haya tunayazungumzia siku zote kwamba katika viwanda vile wakati utawala ukikata malipo yale ili kwenda kuyapeleka kwenye vyombo mahsusi vya Pensheni makato yale yalikuwa hayapelekwi. Sasa kwa sababu yalikuwa hayapelekwi kutokana na taratibu zile za zamani na kutokana na *mismanagement* ya viwanda hivi vingi deni hilo bado limebakia na linakuwa ni mzigo kwa Serikali. Sasa hivi kuna mabilioni ya shilingi ambayo Serikali inajaribu kuyaangalia yakiwa katika hali ya pensheni ambayo zinatakiwa kulipwa kwa wafanyakazi. Kwa hiyo, mimi ningependa kumshauri Mheshimiwa Dr. Nkya aongee vizuri na wale wafanyakazi kwamba madai yanayodaiwa ni ya kisheria au ni haya ya mkono wa kheri.

Mheshimiwa Spika, vile vile amezungumzia tatizo la baadhi ya viwanda kutokuanza kazi na mimi napenda kumwambia kwamba viwanda vingi ambavyo vimebinafsishwa tunataka au tusitake sasa tumegundua kwamba tuna tatizo la teknolojia duni tuliyoikuta katika viwanda vile. Viwanda kwa mfano vya korosho kama alivyosema Mheshimiwa Lydia Boma, hatuwezi kabisa tukasema kwamba teknolojia ya viwanda vile vya kubangulia korosho ni ya kisasa. Teknolojia ile sasa hivi ina miaka zaidi ya 30 mpaka 40, kwa kweli ni teknolojia ya zamani. Kwa hiyo, hata pale ambapo wawekezaji wanataka kuchukua viwanda hivi suala la kwanza la kuangalia ni vipi wataendana na mabadiliko ya kuleta teknolojia ya kisasa na taratibu hizi zina gharama zake na zinahitaji vile vile kufanyiwa utafiti mkubwa kuona kwamba ni teknolojia gani inaweza kuendana na hali ya sasa.

Mheshimiwa Spika, *Tax Holiday* zimefutwa, zilifutwa nafikiri toka Septemba, 1997. Kwa hiyo, suala la *Tax Holiday* sasa hivi halipo. Hili tumeshalizungumza katika Bunge hili kwamba tumezifuta. Lakini ningependa kumshauri Mheshimiwa Dr. Nkya aelewe kwamba uchumi unakwenda haraka haraka sana, tulianza na uchumi funga *(Closed Economy)* tukaja na uchumi huria (soko huria). Sasa hivi linakuja suala la utandawazi maana hili ni suala ambalo hatuwezi kuliepuka hata kidogo na ni suala ambalo linaweza kutokea labda miaka miwili au mitatu ijayo. Wakati huo tutasema kwamba kumleta mtu kuja ku-*promote Coca cola* kutoka nchi za nje itakuwa si kitu cha ajabu kwa sababu mipaka itafunguliwa na ushuru wa forodha utakuwa *lined.* Kwa hiyo, anaweza kuja mwekezaji kutoka Kenya na watu wake akaanzisha kiwanda hapa. Huo ndiyo utandawazi ambao Mheshimiwa Rais aliuzungumzia juzi katika hotuba yake. Kwa hiyo, sisi kama viongozi, sisi kama Wabunge ni lazima tuelimishane kwamba suala la utandawazi kwa vyovyote tutakavyofanya hatuwezi kuliepuka.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Karamagi, Mbunge wa Bukoba Vijijini, namshukuru sana amezungumzia suala la ubinafsishaji. Nakubali kwamba kweli suala la ufuatiliaji kama alivyolielezea na kama alivyosema Mheshimiwa Njelu Kasaka inabidi tulifanyie kazi na ni changamoto. Lakini kama kweli tunataka kuepukana na dhana ya upotoshaji kuhusu sera ya ubinafsishaji tunaweza tukasema kwa wazi kabisa kwamba hata katika mashirika yaliyobinafsishwa na tulishasema hapa Bungeni kwamba mashirika mengi kwa kweli yamebinafsishwa kwa Watanzania ukilinganisha na wageni kutoka nje. Takwimu hizo tumezitoa, gharama tulizitoa, sasa tunavyozidi kuendelea kwamba ubinafsishaji ni kuuza nchi, ubinafsishaji hausaidii au ubinafsishaji unatupeleka wapi. Nadhani linaweza likawa kama suala la upotoshaji. Lakini kama alivyosema Mheshimiwa Karamagi tutaendelea kuhamasisha wananchi, nia ya Serikali kwa nini imechukua sera ya ubinafsishaji, Serikali inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mutamwega Mgaywa na yeye pia amezungumzia ubinafsishaji. Mimi nilifikiri kwa sababu yeye ni msomi, anasafiri sana, akiwa Bungeni hapa anatwambia alikuwa India juzi, Uchina, sasa nafikiri kwa upeo wake angetusaidia sana katika kuelezea hoja hizi za ubinafsishaji. Ubinafsishaji maana yake si watu waweke fedha mfukoni, zipo njia nyingi tu. Kwa mfano, Serikali kugharamia elimu, afya, maji, barabara na tumetoa mifano hapa kabla Kiwanda cha Bia hakijabinafsishwa kilikuwa kinatoa kodi kwa Serikali shilingi bilioni 15, sasa kinatoa zaidi ya shilingi bilioni 55. Fedha hizi zinakwenda Hazina na zinatumika kuleta maendeleo nchini kwetu. Lakini si Kiwanda cha Bia tu kuna Kiwanda cha Blanketi na Saruji. Kwa hiyo, nadhani ni vizuri tukayazungumzia matatizo ya ubinafsishaji yale yaliopo kweli kweli badala ya kuzungumza matatizo ambayo yanaweza kuwa ni upotoshaji.

Mheshimiwa Spika, mimi namshukuru sana Mheshimiwa Mutamwega, Mbunge wa Mwibara kwa kusema kwamba anaipongeza Serikali, sisi tunashukuru sana kwamba anaipongeza Serikali amekiri kwamba tupongeze Serikali lakini asisahau Serikali hii inaongozwa na Chama cha Mapinduzi na inatekeleza sera za Chama cha Mapinduzi. Sasa tunaposema kwamba utekelezaji ni wa sera za Chama cha Mapinduzi ni kwa sababu tunafuata Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Ilani ambayo tumeiuza kwa wananchi wakaiweka Serikali hii madarakani. Kwa hiyo, nadhani hilo kwake litakuwa si tatizo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lydia Boma, ameelezea suala la kuboresha miundombinu. Mimi nakubali lakini Mheshimiwa Lydia Boma atakubaliana nami kwamba akipima maendeleo yaliyotokea akiangalia miaka kumi nyuma kwa maana ya shughuli zilizokuwa zikiendeshwa katika Mikoa ya Kusini ataona sasa kuna uboreshaji mkubwa wa miundo mbinu.

Mfano, uwekezaji katika daraja la Rufiji, barabara hizo zinafanyiwa kazi na mimi nakumbuka kabisa kwamba Serikali kupitia Wizara ya Nishati na Madini ilisema kabisa kwamba italivalia njuga suala la umeme ambalo kweli ni kero katika maeneo hayo.

Kwa hiyo, nina hakika kwamba Serikali itajitahidi sana kuhakikisha kwamba wawekezaji wanavutiwa Mikoa ya Kusini. Hata Mheshimiwa Rais alipofungua daraja la Mto Rufiji alisema kwamba anatoa ufunguo ambao una haki ya kutumiwa na yeyote katika nchi yetu. Maana yake anasema Wawekezaji sasa wataanza kwenda Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, viwanda vya korosho tumevizungumza. Serikali inalifuatilia kwa karibu zaidi, lipo tatizo la teknolojia, tunaandaa utaratibu wa kuona kwamba ni vipi viwanda hivi tunaweza kuvipa vivutio zaidi ili viweze kuchukuliwa. Lakini kwa yeyote yule atakayechukua viwanda vile moja ya jambo la msingi atakalofanya ni kuboresha teknolojia ya viwanda hivyo, lakini nawasisitiza Wabunge ambao wengi nimekuwa nikishirikiana nao kutoka Mikoa ya Kusini wanapopata tu wawekezaji katika maeneo hayo basi waje tuongee nao ili tusaidiane kati ya Wabunge na Serikali katika kuinua viwanda vya kubangulia korosho.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Lwakatare namkubalia kwamba Kiwanda cha *Morogoro Canvas* bado mwekezaji yule anadaiwa. Ni kama anadaiwa shilingi milioni 900 lakini ukumbuke kwamba kiwanda kile kilikwishalala kwa muda wa miaka minne yaani hakikufanya kazi kwa miaka minne.

Mheshimiwa Spika, ilibidi mwekezaji atafute fedha kubadilisha teknolojia ile lakini sisi tunavyofahamu ni kwamba bado Serikali inamfuatilia kwa karibu sana ili alipe salio la fedha ya kununulia kiwanda kile. Si *Morogoro Canvas* peke yake au *MOPROCO,* vipo viwanda vingi tumeshatoa taarifa nyingi tu hapa Bungeni kwa Waheshimiwa Wabunge kuona ni fedha ngapi zimetolewa katika viwanda kadhaa na nini viwanda hivyo vinadaiwa.

Sasa hivyo vyote tunavifuatilia na kutokana na ushauri wa Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi kama nilivyosema mwanzoni tutalifanyia kazi kwa bidii ili watu hao walipe fedha hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Mheshimiwa Mgana Msindai, nitashirikiana na Waziri wa Fedha kuona kwamba tunaboresha vyanzo ambavyo havina matatizo. Kuna Mchuchuma, *Mnazi Bay, Stigler's Gorge* ingawaje *Stigler's Gorge* vile vile lazima tuangalie suala la mazingira kwa sababu inasemekana kwamba *Stigler's Gorge* itakapoendelezwa inaweza kabisa kuharibu mbuga za wanyama za

*Selous* na kadhalika. Kwa hiyo, kuna wanaharakati wa mazingira nao vile vile inabidi wasikilizwe. Lakini Mchuchuma kuna *Mtwara Corridor* inafanyiwa kazi na sasa hivi kama mnavyofahamu kuna taratibu za kuunganisha umeme kutoka Mufindi, kwa hiyo zipo jitihada zinaendelea kuendeleza vyanzo hivi.

Mheshimiwa Spika, namkubalia Mheshimiwa Stephen Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini kwamba tunapoingia kwenye ubinafsishaji tuwe wazi zaidi. Nimeeleza taratibu zinazofanyika. Kwa hiyo, tutaendelea kurekebisha, tutaendelea kurekebisha pale ambapo matatizo yote yale yameweza kujitokeza.

Mheshimiwa Spika, ipo michango mingine ambayo nimeipata kutoka kwa Waheshimiwa. Sasa muda ni mfupi lakini labda nimgusie Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga amesema idadi ya watu ya Dar es Salaam ni ndogo kutokana na matokeo ya sensa kwamba wamepatikana watu milioni 2.4. Sasa napenda kumhakikishia Mheshimiwa Dr. Mahanga kwamba idadi ya watu kwa Mkoa wa Dar es Salaam iliyopatikana ya milioni 2.4 kwa kweli ni idadi sahihi.

Kwa mfano, Wilaya ya Kinondoni jumla ni watu 1,083,913, Mjini wakiwa ni watu 1,027,225; Ilala 634,924 na Mjini 588,897; Temeke 768,451 na Mjini ni 719,933, wakati Vijijini ni 48,500. Sasa tunaweza tukaona kwamba idadi ya watu milioni 2.4 ni ndogo kwa sababu kuna factors nyingine ambazo lazima tuzitilie maanani. Dar es Salaam kama Mji Mkuu unazungukwa na Wilaya na Vijiji mbalimbali kama Kibaha na kadhalika.

Sasa wapo watu wengine kwa kweli wanafanya kazi Dar es Salaam kwa muda wao wote na siku ile tulipozungumzia masuala ya sensa tulisema kwamba mtu atahesabiwa pale alipoamka.

Kwa hiyo, inawezekana kwamba ile presha inayovuta watu Mjini kufanya shughuli zao na siku ile kwa sababu tulisema tuhesabie katika maeneo inaweza kuondoa ile picha ya kuona kwamba Dar es Salaam kuna watu wengi kumbe ni wale wanaotoka Kibaha asubuhi, jioni wanarudi. Lakini tunazo hapa takwimu ambazo tutakuwa tayari kuchangia tuzione na Mheshimiwa Milton Mahanga.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Kidunda amezungumzia suala la kuboresha Chuo chetu cha Mipango na hilo kwa kweli tunalifanya kwa ukamilifu zaidi. Amesema tufanye utaratibu wa kutoa *Scholarships* kwa kweli Wizara yetu imekwishatoa *Scholarships* za Udaktari wa Falsafa tano tangu mwaka wa fedha wa 2002/2003.

*Scholarships* hizo moja katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Kilimo Morogoro, Chuo Kikuu Huria na tunashirikiana na *UNFPA* kuendeleza taaluma hiyo ya ngazi ya shahada.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shellukindo alisema kwamba tulikosea ile si Kamati ya......

**SPIKA:** Kumbuka una mtoa hoja mwenzako naye anasubiri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MIPANGO NA UBINAFSISHAJI:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Shellukindo alisema Kamati ile ni ya Uwekezaji na siyo ya Biashara na siyo Mitaji na Mashirika ya Umma. Kwa hiyo, tunasahihisha hilo kwamba ni Kamati ya Uwekezaji na Mitaji.

Mheshimiwa Spika, mawazo yaliyotolewa ni mengi, tutayafanyia kazi, tutawajibu Waheshimiwa Wabunge kama tulivyotoa ufafanuzi wetu kwa hoja tuliyoitoa mwanzoni.

Mheshimiwa Spika, Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa sababu utaratibu huu ndiyo leo naanza, nadhani tungemaliza kwanza. Nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Njelu Kasaka, kwa niaba ya Kamati ya Fedha na Uchumi na Hamad Rashid Mohamed kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kwa mawazo yao mazuri na baadhi yake nitayarejea baadaye. *(Makofi)*

Lakini vilevile nichukue fursa hii kuwashukuru wale waliochangia kwa kuzungumza hapa Bungeni na wale waliochangia kwa maandishi. Waliochangia kwa maandishi ni Mheshimiwa Mathew Ole-Timan, Mheshimiwa Samwel Chitalilo, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa William Shellukindo, Lekule Laizer, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Dr. Milton Makongoro Mahanga, Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Abu Kiwanga, Mheshimiwa Salome Mbatia, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud, Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Prof. Henry Mgombelo, Mheshimiwa Benedict Losurutia, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Mwadini Abass Jecha, Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mheshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Juma Kidunda na Mheshimiwa Dr. Batild Burian. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, waliochangia hoja hii kwa kuzungumza hapa Bungeni ni Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mheshimiwa Alhaji Ahamadi Mpeme, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Nazir Karamagi, Mheshimiwa Muttamwega Mgaywa, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Mgana Msindai na Mheshimiwa Stephen Kazi. Wote hawa wametoa mawazo mengi na mengine mapya kabisa nawashukuru. Sitaweza kuwajibu wote, lakini nitayafanyia kazi yale ambayo nitashindwa kuyajibu.

Mheshimiwa Spika, labda nianze na Mheshimiwa Njelu Kasaka. Kwa kweli mengi ya mawazo ya Kamati ya Fedha na Uchumi tuliwahi kuyasikia sisi katika Wizara ya Fedha na tunayathamini, na naweza nikasema tu kwamba tutayafanyia kazi kikamilifu na vilevile mengi ya mawazo ya Kambi ya Upinzani. Lakini jinsi nitakavyokuwa nayapitia baadaye nitapata fursa ya kuyagusia hayo kwa topic ili kusudi wote tuweze kupata majibu kadri itakavyowezekana.

Mheshimiwa Spika, labda nianze na wale waliochangia kwa maandishi. Mheshimiwa Thomas Ngawaiya alikuwa na wasiwasi kwamba eti kuna sera ya kuhakikisha kwamba Jimbo la Moshi Vijijini linarudi nyuma, kwa sababu hajaona maendeleo ya maana kwa muda mrefu ukilinganisha hata na Wilaya nyingine za Mkoa wa Kilimanjaro. Ningependa kumhakikishia kwamba mimi kama mshikadau sijawahi kusikia sera yoyote yenye lengo la kurudisha Wilaya yoyote nyuma katika Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ni kweli kwamba Wilaya zinapishana kwa sababu mbalimbali na ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge huwa tunatumia njia rasmi za kupitia kwenye Bajeti na njia za ubunifu wa Mheshimiwa Mbunge mmoja mmoja kujaribu kuona namna ya kusukuma Wilaya zetu mbele. Kwa hiyo, ningependa kukuhakikishia kabisa Thomas Ngawaiya mimi kama mshikadau wa Jimbo lako, ingawa hata siku moja sina nia yoyote mbaya na Jimbo lako, kwamba kitu cha namna hiyo hakipo katika Serikali wala katika sera za Chama cha Mapinduzi, kwamba eti Wilaya fulani itarudishwa nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, alikuwa na wasiwasi kwa nini Serikali haiteremshi viwango vya kodi ya *VAT* na mimi nakubaliana naye. Serikali inajua kabisa kwamba itabidi viwango vya *VAT* viteremke. Yeye anapendekeza viteremke sasa kutoka asilimia 20 hadi asilimia 16 au asilimia 17 au asilimia 18. Ukiteremsha viwango vya *VAT* kwa asilimia 1 tu tunapoteza kwenye Bajeti shilingi bilioni 70. Nilifikiria sana hilo jambo, nadhani tukaona kwamba kabla ya kuteremsha hivyo viwango tusubiri mambo mawili.

Jinsi ukusanyaji wa mapato utakavyokuwa katika mwaka huu. Baada ya marekebisho makubwa ambayo tunafanya kwenye kudhibiti ukwepaji ulipaji kodi, kama nilivyoeleza kwenye bajeti. Vile vile baada ya kuona wenzetu katika Afrika ya Mashariki watakuwa katika ngazi gani. Kwa mfano, kwenye

bajeti ya mwaka huu Kenya imezidi kuteremsha kodi ya *VAT* imefikia nadhani asilimia 16, sisi tungeliteremsha hiyo kodi ya *VAT* tungefika labda asilimia 19, kumbe tungelikuwa nyuma kabisa ya Kenya. Kwa hiyo, tumesema tusubiri, tukishasaini ule Mkataba wa Ushuru wa Afrika Mashariki ambao tunausaini mwezi Novemba, 2003, hali itajulikana zaidi katika soko zima la Afrika Mashariki, na ndipo sisi tutakapofikiria mwakani kushughulikia hili tatizo la viwango vya *VAT.* Kwa hiyo, siyo kwamba hatujui au tumeghairi, tunaelewa. Lakini tuliogopa tusije tukafungua milango yote mwishowe tukashindwa kuzuia upepo utakaokuwa unaingia kupitia kila mlango na kila dirisha.

Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga ana wasiwasi juu ya hatua tunazochukua kwenye ukwepaji wa mafuta ya petroli kwamba pengine tutashindwa. Hata gazeti moja leo limezungumza kwamba labda hatua tunazochukua zitaongeza rushwa na kwa hiyo hazitafanikiwa. Mimi siamini wala sidhani kwamba hilo litatokea. Kinyume chake Serikali inaweza ikajikuta inapata zaidi ya bilioni 50, bilioni 70 kuliko ambavyo tungeliacha hali kama ilivyokuwa hapo mwanzo. Wanaochochea chochea ni wale ambao sasa hali ya nyuma itawezekana tena kama ilivyokuwa. Kwa mfano, gazeti moja la leo ni walalamikiwa ndiyo wanaotoa hoja hizo. Lakini sasa Serikali imeamua kuwa macho, na kama nilivyoeleza tunatumia njia za kisayansi pamoja na kompyuta kudhibiti uingizaji, kudhibiti bei, kudhibiti mafuta yanayokwenda nje, kudhibiti mafuta yanayokuja kwa barabara na kudhibiti kila mwanya tulioujua sisi kwenye mafuta.

Mheshimiwa Spika, hoja ninayokubaliana nayo ni kwamba tutafute watu waaminifu wa kusimamia system hiyo. Lakini hilo ni kweli kwa kila jambo. Jambo lolote hata likiwa nzuri namna gani lisiposimamiwa na watu waaminifu litaharibika tu. Kwa hiyo, challenge yetu kubwa ni kupata watu waaminifu wa kusimamia hiyo system. Kwa hiyo ushauri tunaouchukua ni huo labda kutafuta watu waaminifu na siyo labda ni lazima na mimi nitafanya hivyo. Nitatafuta watu waaminifu na nitashukuru kuendelea kupata habari. Nitashukuru sana kuendelea kupata habari kwamba hapa tunaona kuna kasoro na hapa tunaona mambo yasiyo ya kawaida na sisi tutachukua hatua mara moja. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge mimi nitashukuru sana kupata habari kutoka kwenye Majimbo yenu kwamba hapa udhibiti wa mafuta hauendi vizuri ili kusudi wakati wote tuendelee kuuboresha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna wasiwasi juu ya rushwa na hata Kambi ya Upinzani ilizungumza juu ya ajira katika Shirika la Mamlaka ya Kodi na kadhalika. Mimi ningependa kusema tu kwamba nakubaliana na wale wanaosema kwamba Shirika hili ni nzuri na linafanya kazi nzuri, lakini lina watu wachache wanaoliharibia sifa yake. Hiyo ndiyo kazi ya mwaka huu ya hao watu wachache na nitashukuru sana kupata hao watu wachache. Hivi leo kwenye kuchangia tayari kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja ameishaniambia pale kwangu kuna mtu huyu, ana nyumba kubwa kwenye Wilaya jirani na nyumba ndogo anapofanyia kazi. Sasa anaishije huyu tunamwona maisha yake siyo sawasawa. Kuna Jimbo moja wiki chache zilizopita nimepewa mpaka jina la mtu, mtu huyu anaitwa fulani, ndani ya muda mfupi amejenga nyumba tatu, anafanya hivi, anafanya hivi na anavyofanya akavitaja kila kitu na namna anavyofanya. Sasa kazi yangu mimi nikufuatilia. Siku chache zilizopita tuliambiwa kuhusu magendo mnayozungumza.

Kwa mfano, *Bagamoyo Route,* kuna *Route* siku hizi inaitwa *Bagamoyo Route. Bagamoyo Route* haifanywi na watu wadogo wakawa wanatueleza, wanatueleza, tumelala porini, tumekamata magari na tumeyataifisha na kweli hayakuwa ya watu wadogo. Magarihayo yalikuwa yanafanya magendo ya sukari. Hayakuwa ya watu wadogo na wala hayakuwa ya wafanyabiashara sawasawa ni ya watumishi viongozi. Kwa hiyo tunavyozidi kupata habari za hawa watu wabaya na wanafanya nini sisi hatutasita kabisa kuchukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa William Shellukindo alitupa ushauri kuhusiana na *STABEX* kwamba baada ya mazungumzo yote haya, basi labda sasa Serikali ingetoa kauli ya mwisho kwa namna fulani au *secular* au tangazo na kadhalika tutazingatia ushauri huo.

Mheshimiwa Salome Mbatia alizungumzia juu ya pensheni ya waliokuwa watumishi wa Afrika ya Mashariki. Tatizo la watumishi hawa ni kwamba liko Mahakamani, na kwa sababu wana kesi Mahakamani hatuwezi kuwashughulikia mpaka kesi yenyewe iishe. Lakini kama ni kweli kwamba waliokuwa Serikali ya Tanzania pensheni yao sasa imefika shilingi 20,000/= na wao wapo kati ya 800 na 1000 basi hili jambo itabidi nilichukue na nilifanyie kazi ili nijaribu kulielewa zaidi. Kwa sababu kwa

kweli hivi ni viwango vya chini mno ili nione kama hawa ndiyo wenyewe ama ndiyo hao wenye kesi au ni namna gani tuweze kuona la kufanya.

Mheshimiwa Spika, lakini kama nilivyosema pensheni ilipofika shilingi 20,000/= mkupuo umekwisha. Tunachofanyia kazi sasa na Waheshimiwa Wabunge wengi waliochangia kwa maandishi wameniandikia ni kuona jinsi ya kushughulikia wale ambao kwa kujua au kwa kutojua wengi wananiandikia sasa wanasema hawakujua walichukua mkupuo. Kuna watu waliishakula mkupuo bila kujua, na bado wako hai wanasema sasa tutafanyeje na hatujafa. Kwa hiyo, jambo hilo ndilo tulilonalo la kuangalia tufanye nini na watu hawa. Mimi nina matumaini kwamba ikifika bajeti ijayo naweza nikatoa kauli juu ya jambo hilo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Lekule Laizer amesema pale Longido kuna jengo la mtu mmoja anaitwa Mungai ambalo lina matatizo ya siku nyingi. Mimi nafahamu tatizo hilo. Labda kilichobaki ni Serikali kuchukua ushauri wako na kuangalia namna ya kumaliza tatizo hili. Kwa sababu tatizo hili ni la toka Awamu ya Pili mtu aliyeingilia barabara sasa anataka fidia.

Mheshimiwa Bernadine Ndaboine aliuliza nani huyu mwenye madaraka ya kwenda kumfungia mtu Akaunti katika Benki kama namna fulani ya kufuatilia mambo ya kodi. Sheria inatoa kibali kwa Mamlaka ya Mapato kukamata Akaunti ya mtu kwenye benki ambaye amekuwa akikwepa kulipa kodi kwa njia iliyo sugu. Hata kwenye Muswada wa Fedha kesho kutwa nitaleta mapendekezo mengine ya kukamata Akaunti za Mawakala wa Ndege ambao wakishauza tiketi hawarejeshi kodi Serikalini, huo Muswada unakuja kesho kutwa. Kwa sababu tumegundua kwamba ukilinganisha idadi ya tiketi zinazokatwa na makusanyo kutoka kwenye Sekta hiyo ni kidogo sana. Wako watu wanaokata na ile kodi lakini kodi hiyo hairejeshwi Serikalini. Kwa mapendekezo yanayokuja yanafanana na haya. Mtu wa *TRA* atakwenda kwenye Akaunti ya Wakala yule kukamata hiyo Akaunti kuchukua fedha za Serikali zilizomo kwenye Akaunti yake na kumuachia za kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maana Serikali ni kitu kikubwa kama wewe unajidai ni mjanja, Serikali ina ujanja zaidi tena ina nguvu. Kwa hiyo, wewe tii amri hakuna mtu atakayekuchokoza. Lakini ukifanya ujanja ziko sheria za kumwezesha mtoza kodi kuingia kwenye Akaunti yako na kuchukua haki yake huko na kukuachia haki yako kwenye Akaunti yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Abu Kiwanga nakushukuru kwa ushauri wako, na ushauri wako Mheshimiwa Abu Kiwanga unajitokeza kwenye Marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato ambayo tunatarajia kuyaleta baadaye katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Mariam Mfaki kwa kuomba kwamba watu wapate elimu zaidi juu ya biashara ya hisa, na tunakusudia kuendelea kuwaelimisha watu jinsi ya kufanya biashara ya kununua na kuuza hisa. Vilevile alikuwa anataka kujua na hili Waheshimiwa Wabunge wengi wameliulizia sasa itakuwaje kwa hizi Halmashauri ambazo zilikuwa na mapato fulani, sasa mapato yale yamevurugika kutokana na maamuzi yetu juu ya kufuta baadhi ya kodi, sasa itakuwaje.

Mheshimiwa Spika, nataka kuwahakikishia tu kwamba hesabu zinafanywa sasa hivi, hivi tunavyozungumza wataalam wa Wizara ya Fedha, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa wanafanya mahesabu ili kujua namna ya kuweza kufidia hizo Halmashauri. Lakini niseme wazi kwamba tusiogope sana, kwa sababu gani zaidi ya nusu ya malipo ya Halmashauri ni fedha ambazo zinatoka Serikali Kuu miaka yote. Zaidi ya nusu zinatoka Serikali kuu, mpaka fedha za Walimu zote ni Serikali Kuu, fedha za madawa zote ni Serikali Kuu, fedha za maji zote ni Serikali Kuu na fedha za Elimu zote ni Serikali Kuu hakuna mengi yaliyobaki. Kwa hiyo msiwe na wasiwasi tembeeni kifua mbele, wakati sisi tunafanya hesabu, halafu tutatoa mambo sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na tena hapo hapo nimesikia hata kwenye baadhi ya Halmashauri wanasema ooh huu uamuzi wa kufuta kodi na ushuru umeshutukizwa na hata hapa nimesikia kwamba umeshutukizwa. Ni miaka miwili tunafanya utafiti huu mpaka tukajua kwamba hata zile fedha ambazo tungefuta ni kiasi gani ile tujue. Lakini mnajua mambo haya ukitaka kuwa perfection unafanya jambo mpaka huwezi kujua doti iko wapi, nukta iko wapi, T imeshakatwa itachukua miaka 10. Katika mambo

yanayohusu kero za wananchi huwezi kuchukua miaka mingi, Lazima uende haraka haraka, na kama mbele ya safari tukigundua kwamba hapa na pale kuna mashimo ya kufukia tutayafukia pamoja si uamuzi wetu. Mimi lazima niseme sikuwa *perfection* lakini kwa uhakika uamuzi huu haukustahili kusubiri tena zaidi, maana madhara yangekuwa mabaya zaidi mbele ya safari kuliko hivi tulivyofanya sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi nafikiri kwamba ikifika mwakani, mashimo mengi tutakuwa tumeishayafukia. Lakini hakuna jambo lolote litakalokuwa balaa, balaa hakuna, uamuzi huu hautaleta balaa yoyote. Waheshimiwa Wabunge walikuwa wanauliza hapa. Je, sasa itakuwaje. Kwenye *Finance Bill* Serikali inachapisha orodha mbili. Orodha ya kwanza ya kodi halali na ushuru halali na faini halali. Orodha ya kwanza, kodi halali na ushuru halali. Sasa wakati ule nilisema tulipunguza toka 60 zikafika 7, sasa ni 6 halali. Hapo hapo tunachapisha orodha haramu, kwa hiyo kila tunaposema hili sawa, tunasema lakini kikomo hiki, hili sawa lakini usizidi hapa, hili sawa lakini hili hapana. Kwa hiyo, hiyo orodha haramu ndiyo ya kwenda nayo kwenye Jimbo. Ukawambie watu wako waielewe kama sala ile orodha haramu. Ndiyo watu wataelewa maana ya uamuzi huu tuliofanya, bila kuwasomea ile orodha haramu hawataelewa. Nitafafanua zaidi kesho kutwa. Mheshimiwa Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa atatoa secular ya kufafanua kwa undani na kuweka utaratibu mkali kwa mtu ambaye atashindwa kuelewa hiyo orodha haramu. Ni marufuku kutokuielewa hiyo orodha haramu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, na papo hapo kwa kumujibu Mheshimiwa Semindu Pawa ni kweli kwamba mwaka wa Fedha wa Serikali za Mitaa sasa utaanza mwezi Julai mpaka mwezi Juni sawa na mwaka wa Fedha wa Serikali ili tuweze kwenda sambamba katika masuala haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, yapo masuala mengine aliyoyatoa Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte nafahamu suala lako na wengine wengi. Lakini ningetaka niseme kwa wale walioniandikia orodha hiyo ni *representative* na nitaishughulikia.

Mheshimiwa Spika, kuna Waheshimiwa Wabunge waliokuwa na wasiwasi sana juu ya Zanzibar. Nifafanue kidogo biashara na Zanzibar. Ukweli ni kwamba namna tunavyotoza ushuru wa bidhaa baina ya Tanzania Bara na Zanzibar ni tofauti. Sisi kuna baadhi ya bidhaa hapa Tanzania Bara ambazo zina *Suspended Duty* Zanzibar hazina. Bidhaa inayoingia Tanzania Bara kabla ya kuonyesha ushahidi wa kulipiwa *Suspended Duty* Zanzibar, hapa Tanzania Bara inatakiwa ilipiwe ile *Suspended Duty* kwa sababu ndiyo sheria. La pili, kuna bidhaa ambazo kule Zanzibar hazitozwi aina fulani ya ushuru, lakini huku Tanzania Bara zinatozwa ushuru huo zinapoingia kupitia Dar es Salaam. Hiyo ndiyo inayoleta hizi tofauti na milologo mirefu ya kudaiana ushuru na vyeti na kadhalika. Lakini tunavyozungumza sasa hivi, tunazungumza na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa lengo la kuhuisha matatizo haya ili kuondoa kero zilizopo. Mazungumzo yamekwishaanza na tumaini langu ni kwamba tutaelewana mbele safari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu hili namba za magari kutoka Zanzibar. Ningependa niwahakikishie kwamba hakuna tatizo. Tatizo ni kwamba sheria hapa Tanzania Bara namba za magari zilikuwa zinaandikwa Kimkoa *MS Moshi,* TA Tanga, KG Kigoma, DO Dodoma na kadhalika. Zanzibar hawakuwa na utaratibu wa Kimkoa. Kwa hiyo, tulipojaribu kuingiza utaratibu huu mpya, Zanzibar ukawa umeleta mshikeli kule. Kwa hiyo, tumekubaliana sasa kwamba watarekebisha taratibu za kwao za kisheria ili namba hizi magari tunazozitumia sasa hivi hapa Tanzania Bara ziwe ni namba za Muungano na magari yote yaandikishwe mahali pamoja. Kwa hiyo hakutakuweko tena gari la kigeni ni la Jamhuri ya Muungano. Kuhusu hili jambo tumekwishakuelewana ni taratibu tu zinasubiriwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa nirudie tena kuzungumzia juu ya wale waliozungumzia juu ya pensheni kulipwa kikanda. Hili limezungumzwa na Mgana Msindai nakubaliane naye kwamba tutalifanyia kazi, na ni jambo nzuri kwa kusema kweli. Vilevile ningependa kumhakikishia kwamba yale yote aliyozungumzia juu ya mafuta na kadhalika na kadhalika tutayashughulikia, pamoja na wale wafanyakazi *TRA* kufikiriwa mishahara ndani ya *TRA* tutalifikiria.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla ningesema Serikali inajua kwa sababu tunafundisha watumishi wengi wa Uhasibu, ni lazima tuangalie mafao yao na mishahara yao na mambo mengine. Lakini lazima

tufanye hivyo kwa kuangalia vilevile Serikali nzima. Jambo hili tunalo na ni tumaini langu kwamba tutalipatia jibu. Mimi ninashukuru sana kwamba mnaona umuhimu wa kuwa na treatment maalum kwa ajili ya watumishi ambao kwa kweli wanafanya kazi nzuri kama hawa *TRA.* Ningependa kuzungumzia hili la ferry, naelewa kwamba kuna tatizo la ushuru wa ferry limezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wengi. Mheshimiwa Samwel Chitalilo na wengine na Stephen Kazi sasa hivi kuhusu ushuru wa ferry kwenye Ziwa Victoria. Ni kweli kuna hali isiyoridhisha ya usafiri wa meli na vyombo vya majini katika Ziwa Victoria, na wiki iliyopita tunasikia kumetokea hata baadhi ya wananchi kuugomea.

Lakini nilichonacho kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, ni kwamba hali hii ni lazima irekebishwe na tuna nia ya kuirekebisha kwenye sheria ya *Finance Bill* kesho kutwa. Ili kusudi ukishaita chombo chako ni *ferry* ijulikane nauli yake ni nini, iwe ni ya Serikali au ya watu binafsi. Ukisema ni meli ilijulikane nauli yake ni nini, iwe ni Serikali au ya watu binafsi. Hiyo inakuja kesho kutwa ili kuondoa utata ulioko ambapo watu wengine wanatoza ushuru usiotakiwa kisheria kwenye vyombo vyao, na hivyo kusababisha manung'uniko kwa watu ambao kwa kweli siyo ya lazima.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kesho kutwa nitapata tena fursa wakati wa Muswada wa Fedha ya kufafanua baadhi ya mambo kama yatajitokeza. Lakini ningependa kusema kwamba sasa tumepania kufanya kazi. Kwa sababu matokeo ya kufuta kodi, maana yake ni kutafuta fedha kwa kila hali na kusimamia kwa kila hali. Kazi hiyo ndiyo tunaomba mtupe lakini lazima tupate fedha kwanza ndiyo ukweli wenyewe. Kwa hiyo naomba mnielewa kwamba hata ile ya kukusanya hizo fedha ili mzipate muweze kukaa hapa Bungeni na kunidhibiti pia lazima zitokane na mimi kupewa fedha ili niweze kukusanya mapato zaidi na kuweza kuendesha shughuli za Serikali katika nchi hii. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba kutoa hoja kwamba mkubali kama nilivyoomba ili sote turudi kufanya kazi na tuendelee kudhibitiana mbele ya safari.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaingia kwenye Kamati ya Matumizi kwa kuwa hii ndiyo ya mwisho sasa katika Mkutano huu, napenda kutoa ufafanuzi ufuatao. Pengine ingekuwa vizuri ningeutoa mapema zaidi. Lakini kwa utaratibu niliouweka wa kuwapatia nafasi Wasaidizi wangu Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti, nilikuwa sipo kutoa ufafanuzi huu. Nao ni kwamba katika utaratibu mpya tuliouweka wa Kamati za Kudumu za Bunge aliousifia Mheshimiwa Wilfred Lwakatare. Tumeweka mgawanyo wa wazi kazi baina ya Kamati za Kudumu na Kamati ya Bunge Zima. Kazi ya kusimamia utekelezaji wa Serikali ni mnukuu Mheshimiwa John Malecela. Narudia Kazi ya kusimamia utekelezaji wa Serikali ni ya Kamati za Kudumu za Bunge siyo ya Kamati ya Matumizi. Kazi ya Kamati za Matumizi ni kuidhinisha matumizi ili Serikali ikafanye kazi. Ndiyo mgawanyo huo. Kwa hiyo, ni vizuri tukazingatia hilo.

Hilo linanifikisha kwenye lingine la pili, nalo linatokana na kanuni Na. 58 (1). Inasema hivi: "Bila ya kuathiri masharti ya kanuni ya 4, kanuni ndogo ya (2) Spika atawajibika kuhakikisha kuwa utaratibu bora unafuatwa Bungeni na uamuzi wake kuhusu jambo lolote la utaratibu utakuwa ni mwisho. Namwiiga Mheshimiwa Malecela tena narudia: "Na uamuzi wake kuhusu jambo lolote la utaratibu utakuwa ni wa mwisho". Sasa leo asubuhi Mheshimiwa Chambiri anaona kwamba kuna Katibu anasoma Muswada mara ya kwanza yeye anasimama anataka nimpe nafasi wala sijui anasimama kufanya nini. Nikamzuia. Baadaye nimeshamwita Mheshimiwa Waziri anasimama tena, anataka nimpe nafasi. Ndio nikasema kama kweli Mheshimiwa Mbunge unataka kupata mwongozo wa Spika kwa nia njema mwarifu mapema kwamba nitaomba mwongozo wako kuhusu jambo fulani (a) aweze kujiandaa na (b) aweze kukuona tu, *to catch the speaker's eye.*

Sasa mimi najua alichokuwa anasimama kufanya. Alikuwa anataka kubishia utaratibu niliouweka wa kwamba Wizara hizi mbili zitajadiliwa kwa pamoja leo. Lakini kanuni inasema: "Uamuzi wa Spika utakuwa ni wa mwisho". Sasa kujaribu kubishia uamuzi wa Spika ni kujitafutia matatizo. Sina maelezo zaidi. Nimalizie kwamba kwa nini tuliweka mgawano huo. Katika Kamati za Kudumu usimamizi wa utekelezaji wa Serikali ni mzuri zaidi, kwa sababu gani kuna siku 60 katika mwaka za kufanya kazi hiyo. Hapa kila Wizara ina siku moja tu na sisi tuko wengi hatuwezi kusimamia Serikali katika siku moja Waheshimiwa Wabunge karibu 300. *(Makofi/Kicheko)*

Ya pili, kule kwenye Kamati za Kudumu Mheshimiwa Waziri anakuwepo sio peke yake kama alivyo sasa anakuwepo na Maafisa wake wote waliokaa nyuma ya kioo kule wanakaa naye ndani ya Kamati wanamsaidia kujibu maswali, unapata ufafanuzi na maelezo yote unayoyataka. Ndani ya Kamati za Kudumu hawabanwi na kanuni ya kusema mara moja na usirudie. Unasema mara nyingi, unauliza maswali utauliza mara nne, tano mpaka uridhike. Kama tunavyojua pamoja na kwamba Kamati zimepangiwa Wabunge wachache wachache lakini kanuni zinasema Mbunge yoyote ana haki ya kwenda kwenye Kamati yoyote ambayo anataka kushiriki katika mazungumzo yake. Kwa hiyo, narudia basi kwamba Kamati ya Matumizi kazi yake ni kuidhinisha vifungu tu. Kusimamia utekelezaji wa Serikali ni Kamati za Kudumu ambazo zinapewa siku 60 kwa mwaka. Kwa mujibu wa habari nilizozipata waliojiandaa eti kumbana Waziri kuhusu ubinafsishaji wakati wa Kamati ya Matumizi hawatapata nafasi. Katibu ameshatamka Kamati ya Matumizi kwa hiyo tusimame. *(Makofi/Kicheko)*

Fungu 66 - Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji ..Shs.8,181,637,000/=

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA**: Mheshimiwa Mwenyekiti,

**MWENYEKITI:** Ndani ya fungu hilo unazungumzia kifungu gani au programu gani?

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Nazungumzia mshahara

**MWENYEKITI:** *Okay* sawa, programu ya 10

**MHE. DR. MILTON M. MAHANGA:** Katika kifungu hicho Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kabla ya kupitisha kifungu hicho wakati Mheshimiwa Waziri anajibu hoja yangu ya uwezekano wa kurudia sensa ya Mkoa wa Dar es Salaam alitoa sababu kwamba inawezekana tunaona watu ni wengi kwa sababu wanatoka Kibaha. Lakini katika utafiti mdogo ambao umefanyika wa takwimu za Wenyeviti wa Mitaa na kuangalia ni watu gani hawakupatikana nyumbani wakati ule siku ile ya kuhesabu na ukuaji wa mijini ambao inaonyesha kwamba ni asilimia 400.2 kwa Dar es Salaam unaonyesha kwamba ni hali ndogo. Sasa nilitaka Mheshimiwa Waziri akubali kuufanyia utafiti kidogo suala hili na kama inabidi kweli *sensa* ya Dar es Salaam irudiwe kwa sababu idadi ile ni ndogo kwa vigezo vyote.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UBINAFSISHAJI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maelezo ya Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwewnyekiti nilitoa sababu na hili ni suala la takwimu na utafiti na ndiyo maana nilimwambia baada ya kikao hiki tunaweza tukakutana tukaona ni jinsi gani tunaweza kuliainisha hili suala vizuri. Hili ni suala la takwimu hatuwezi kulitolea maamuzi hapa ya aina hiyo. *(Makofi)*

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

FUNGU 66 - Ofisi ya Rais Mipango na
Ubinafsishaji..........................Shs. 16,700,081,700/=

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**WIZARA YA FEDHA**

Fungu 22 - Deni la Taifa ... . Shs. 405,103,791,000/=
Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali Shs. 62,501,069,500/=
Fungu 45 - Mkaguzi Mkuu wa Serikali Shs. 4,373,198,400/=

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 50 - Wizara ya Fedha ...................Shs.123,540,193,800/=

**MHE. PASCHAL C. DEGERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali moja. Programu ya 10, kifungu cha 250100.

Nilipokuwa nachangia kwa maandishi nilimwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha afikirie kipindi cha kuwalipa wastaafu pensheni yao. Hivi sasa wastaafu wanalipwa kwa miezi sita, sita. Sasa wastaafu wengi wanalalamika kwamba miezi sita ni muda mrefu sana wa kuweza kusubiri pensheni yao na waliomba kwamba angalau walipwe kwa kila robo mwaka. Hoja yao ni kwamba wana matatizo mengi na pili ni kwamba hoja iliyotolewa mwanzo ya kuweza kuweka kipindi cha miezi sita ni kiwango kidogo cha pensheni. Hivi sasa kiwango kidogo kimeboreshwa kwa miezi mitatu inawezekana wakaweza kujilipa gharama na kuweza kupata fedha kidogo ya matumizi. Sasa nilikuwa namwomba atoe msimamo wa Wizara ni nini kuhusu ombi hilo?

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo sio tatizo. Kwa hiyo mara wataalamu wangu wakiweza kuweka utaratibu tunafikiri sasa maadamu viwango ni vikubwa zaidi, viwango vya pensheni vimekuwa vikubwa tunaweza tukalipa miezi minne minne, hamna tatizo. *(Makofi)*

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, programu ya 10 mshahara wa Waziri. Naomba kabla hatujaidhinisha mshahara wake naomba maelezo mafupi.

Mwaka jana nilikuwa nimezungumzia kuhusu jengo la Benki ya Posta hapa Dodoma ambalo ni mali ya Serikali lakini jengo lile halijakamilika lakini linaoza. Nikashauri wakati ule kwamba jengo lile kama likikamilika linaweza kabisa Wizara mbili ndogo ndogo zikahamia Dodoma. Kama kweli tunayo dhamira ya kuhamia Dodoma mimi nina hakika fedha sio tatizo. Tatizo ni ukosefu wa dhamira ya kisiasa kuhamia Dodoma. *(Makofi)*

Juzi Rais alionya, alisema wale ambao wanasita kuhamia Dodoma waelewe kwamba bado ana miaka zaidi ya miwili ya utawala wake. Sasa naomba Waziri anisaidie kwamba katika voti 31 ya Ofisi ya Makamu wa Rais zilitengwa shilingi 476,000,000 kwa ajili ya ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Rais Dar es Salaam. Na vile vile voti 53 Ofisi ya Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto zimetengwa shilingi 200,000,000 kwa ajili ya kuongeza ofisi. Sasa jumla ya hapo ni 676,000,000. Lakini kukarabati au kumalizia jengo la Benki ya Posta Dodoma sio zaidi ya shilingi 500,000,000. Je, si busara kwamba fedha hizi ambazo zimewekwa kwa ajili ya kukarabati hizo Ofisi kule zikatumika kujenga Ofisi za kudumu Dodoma. *(Makofi)*

Nakata Waziri akubali kwamba fedha hizi ambazo zimewekwa kwa Ofisi hizo hizo zitumike kumalizia jengo la Benki ya Posta Dodoma ili Wizara hizo ziweze kupata makao ya kudumu Dodoma. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Benki ya Posta Tanzania yenyewe haifurahi sana kuwa na hilo jengo, kwa sababu linawaharibia mizania ya vitabu vyao. Kwa hiyo, hilo la kwanza.

La pili, sina uhakika kama vyombo vya usalama vitakubali wazo la Ofisi ya Makamu wa Rais kuwa mahali hapo. Kuna ngazi katika Taifa ambazo Ofisi zao zinawekwa mahali panapokubalika kiusalama. Lakini jengo hilo tunalo katika majadiliano na mashauriano kati ya Ofisi yangu na Ofisi ya

Waziri Mkuu kwa lengo la kujua tufanye nalo nini. Hivi sasa majadiliano yale yanaendelea tupate habari zote ili tuweze kufanya uamuzi ambao ni wa busara. Kwa hiyo, hoja yake inaongezea tu jambo ambalo liko mbioni katika kufikiriwa tulifanyie nini.

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nadhani suala la usalama hapa sio hoja kubwa. Tukizungumzia Ofisi ya Makamu wa Rais maana yake ni Mawaziri wawili wa Nchi wale pamoja na Wakurugenzi wao. Wao wanaweza kabisa wakahamia Dodoma wakati tunangoja hilo jengo ambalo lina usalama zaidi kwa ajili ya Makamu wa Rais kama Ofisi binafsi ya Makamu wa Rais. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Jaribu tena Mheshimiwa Waziri. Ooh Mheshimiwa Waziri Mkuu muokoe. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe maelezo ya kuongezea kwa yale ambayo amekwishayatoa Waziri wa Fedha.

Kwanza nataka kuwahakikishieni kwamba dhamira ya kuhamia Dodoma ipo na inazidi kupamba moto. *(Makofi)*

Kwa upande wa jengo hili la Posta mimi mwenyewe nimelitembelea wala sio mara moja. Kwa kweli tatizo kubwa ni kwamba ni jengo la Posta. Kwa hiyo kama tunalitaka mimi nakumbuka wakati huo tulipolitembelea walisema wanahitaji kitu kama shilingi 800,000,000 kulinunua katika mazingira yale iliyopo. Kwa hiyo ulinunue kwa shilingi 800,000,000 halafu uje ulitengeneze lifikie hali ya kuwa Ofisi. Kwa hiyo, ndiyo kwa sababu hiyo tukaona ni afadhali tutafute majengo mengine. Tunaweza kuendelea kuzungumza na watu wa Posta kama wangelitukubali kutupa kwa kweli Serikali ingelifurahi sana ilikamilishe ili iwe sehemu ya Ofisi. Hivi sasa Mheshimiwa Mwenyekiti, hata jengo la Chimwaga kama mlivyoona mwaka huu tumetenga shilingi 500,000,000. lengo letu ni kujaribu kwa kiwango kadri inavyowezekana ili ikiwezekana baadhi ya Wizara hata zianzie Chimwaga. Kwa hiyo dhamira iko pale pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa hili la Ofisi ya Makamu. Nadhani Ofisi ya Makamu kama ilivyo kwa kweli ni Ofisi ya Muungano itachukua muda sana kuhamia hapa na hizo fedha ni za kufanya ukarabati ili paweze kuishi. Kwa sababu kwa vyote vyote vile Ofisi ya Makamu wa Rais kwa sababu inaunganisha pande zote mbili za Muungano haitaweza kukwepa kukaa Dar es Salaam kwa muda mrefu kidogo. Kwa hiyo, ndiyo sababu tu ya hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hayo ndiyo maelezo. *(Makofi)*

**MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, programu ya 10 mshahara wa Waziri. Wakati wa kuchangia kwa maandishi Mheshimiwa Waziri wa Fedha nilimwuliza suala ambalo sasa hivi ni tatizo katika Wilaya ya Geita. Suala la fidia. Wananchi walihamishwa, pesa zikatolewa kwa ajili ya kuwalipa wananchi, sehemu kubwa ya fedha ikaliwa na Watendaji katika Ofisi ya Serikali. Sasa wananchi wana hali mbaya na wanalalamika kwa nini hawapewi fidia na hivi sasa sisi Wabunge tumeambiwa tusirudi bila jibu. Sasa namwomba Waziri sasa hivi tumefikia mwisho. Tumekuwa tukieleza tangu mwanzo tumefikia mwisho tunaomba tuwe na jibu la uhakika, sasa hivi kusudi twende nalo. Kama hakuna jibu atusaidie tuishije huku na usalama wa majimbo yetu yatakuwa namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Waziri atusaidie katika hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri Mkuu tena okoa jahazi. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili lilijitokeza sana wakati wa mjadala wa Wizara inayohusika. Lakini kwa vile hatukupata muda wa kulizungumza huku nilipata wasaa wa kukutana na Waheshimiwa Wabunge wa eneo hilo, Mheshimiwa anayeuliza swali akiwepo mmoja wapo, niliwaahidi kwamba jambo hili Serikali italishughulikia na nikasema mimi mwenyewe nikisaidiana na Waziri wangu wa Nishati na Madini nitalichukua jambo hilo kuhakikisha kwamba tunapata ufumbuzi wake kwa haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa usibishane na maelezo. Mimi nilikuwa naku-test ebu endelea. *(Makofi/Kicheko)*

**FAUSTINE K. RWILOMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa test yako ambayo niliona kwamba inataka kupinga Kanuni kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo hili ni kubwa labda nimwombe Mheshimiwa Waziri Mkuu ikiwezekana atupangie tarehe ya kuja kule kwa sababu hivi sasa tukienda kule sisi hatutapokelewa kwa kuelewa kwamba jibu linatolewa. Kwa sababu ni muda mrefu Serikali imekuwa ikisema tutatekeleza. Hata Mkuu wa Mkoa alikuja, akaJa na kauli ya Serikali kwamba subirini miezi miwili nitatekeleza. Rais alikuja akasema tutawalipa. Sasa hili jibu nina wasi wasi linaweza likaenda hivyo hivyo sasa isije ikawa imetuharibu na tusipokelewe kabisa. *(Makofi)*

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini kabisa kwamba kauli ninayotoa hapa itamwezesha Mheshimiwa Mbunge kupokelewa jimboni kwake. Kwa hiyo kwa kauli hii naomba wananchi wa Geita wampokee Mheshimiwa. Jambo hili tutalifanyia kazi. (Makofi)

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti,

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Missanga amefuta basi Mheshimiwa N'hunga wa mwisho.

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukushukuru kwanza kwa kunipa nafasi hii ili kuuliza kidogo kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Waziri wa Fedha alipokuwa anajibu kuhusu hoja ya Zanzibar alisema kwamba mazungumzo yanaendelea. Mheshimiwa Mwenyekiti?

**MWENYEKITI:** Hoja ya Zanzibar gani?

**MHE. JUMA SULEIMAN N'HUNGA:** Inayohusu mambo ya kodi kuwa sawa baina ya Zanzibar na Tanzania Bara. Moja katika kero kubwa ya Muungano hasa kwa upande wa Zanzibar ni hii. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano alipokuwa anagombea na kuchaguliwa kipindi hiki alisema kero hizi zitakwisha sio zaidi ya miezi sita. Nimefurahishwa sana na kauli ya Mheshimiwa Waziri aliposema kwamba mazungumzo yanaendelea. Lakini ningeiomba atoe kauli kwamba mazungumzo hayo yatakwisha lina ili kero hii imalizike. Nauliza hayo kwa sababu kila siku moja inayokwenda hali ya uchumi wa Zanzibar inakuwa mbaya sana. Hivi sasa Serikali ya Zanzibar pengine inamudu kulipa mishahara tu matumizi mengine haimudu. Sasa nilikuwa naomba kauli ya Mheshimiwa Waziri katika Bunge hili ya kumaliza suala hili kwa haraka. Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. ABDISALAM ISSA KHATIB):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa Fedha kama mazungumzo yanaendelea. Kutokana na kauli zilizotolewa za uchangiaji Waheshimiwa Wabunge mmojawapo akiwa Mheshimiwa Mohammed Rajab Soud tarehe 1 Julai ulifanyika Mkutano, Kamishna Jenerali wa *TRA* pamoja na Waziri wa Biashara Zanzibar pamoja na baadhi ya wafanyabiashara ambao aliwachagua yeye Waziri wa Biashara Zanzibar walikaa pamoja kuzungumza. Kwa hivyo mazungumzo bado yanaendelea kama alivyosema.

*(Fungu lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

**MATUMIZI YA MAENDELEO**

| | | |
|---|---|---|
| Fungu 23 - | Mhasibu Mkuu wa Serikali | Shs. 1,487,394,000/= |
| Fungu 45 - | Mkaguzi Mkuu wa Serikali | Shs. 1,617,029,300/= |
| Fungu 50 - | Wizara ya Fedha ........... | Shs. 21,145,067,800/= |

*(Mafungu yaliyotajwa hapo juu yalipitishwa na Kamati bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (MIPANGO NA UBINAFSISHAJI):** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba baada ya Bunge lako Tukufu kukaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia kifungu kwa kifungu Makadirio ya Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji kwa mwaka 2003/2004 na kuyapitisha yote bila ya mabadiliko yoyote. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Makadirio hayo sasa yakubaliwe. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Ofisi ya Rais (Mipango na Ubinafsishaji Kwa Mwaka 200/2004 yalipitishwa na Bunge)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa Taarifa kwamba baada ya Bunge lako Tukufu kukaa kama Kamati ya Matumizi na kupitia kifungu kwa kifungu Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Fedha na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa mwaka wa 2003/2004 na kuyapitia bila ya mabadiliko yoyote. Sasa naomba kutoa Hoja kwamba Makadirio hayo yakubaliwe.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA USHIRIKA NA MASOKO:** Mheshimiwa Spika, Naafiki

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Fedha Kwa Mwaka 2003/2004 yalipitishwa na Bunge)*

**KUAHIRISHA BUNGE KABLA YA WAKATI**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kwa mujibu wa kifungu cha 21 (6), naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liahirishwe sasa saa 1.27 dakika 23 kabla ya muda wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maelezo binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa kanuni ya 40 ya kanuni ya Bunge Toleo la mwaka 2003 naomba niwasilishe mbele ya Bunge maelezo binafsi kuhusu suala la umeme kutoka Masasi mpaka Lindi.

Mheshimiwa Spika, mwishoni mwa miaka ya 1980 *TANESCO* iliamua kuunganisha umeme toka Masasi mpaka Lindi ili kutumia umeme wa ziada uliokuwa unazalishwa na jenereta ya Masasi yaani *Excess Electricity.* Mpango huu ulilenga pia kuvipatia umeme vijiji vilivyopo kando kando ya barabara ya Lindi/Masasi.

Kwa upande wa Wilaya ya Masasi vijiji hivyo ni pamoja na Chikukwe, Chigugu, Chikundi, Mwena, Nangoo na Nanganga.

Mheshimiwa Spika, uamuzi huu wa busara ulipokelewa kwa shangwe na wanavijiji husika kwa kuona sasa watapiga hatua katika kujipatia maendeleo yao hasa ikizingatiwa umuhimu wa nishati hii katika shughuli za kiuchumi.

Katika kutekeleza mpango huu viongozi wa Chama na Serikali pamoja na *TANESCO* walihamasisha wananchi kuwa wajitoleee kukata mikorosho pamoja na mazao mengine ya kudumu katika baadhi ya sehemu ili kuruhusu nyaya za umeme kupita. Wananchi walifanya kama walivyoelekezwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mkoa wa Lindi uwekaji wa nyaya za umeme ulikwenda kwa kasi ya kuridhisha. Mpaka sasa umeme umepatikana katika maeneo mengi ya vijiji kati ya Lindi na Nyangao ambacho ni kijiji kilichopo mpakani kati ya Wilaya ya Masasi Mkoani Mtwara na Wilaya ya Lindi Vijijini Mkoa wa Lindi. Kwa sababu zisizojulikana uwekaji wa nyaya za umeme kwa upande wa Mkoa wa Mtwara umekuwa ukifanyika kwa kasi ndogo sana. Kwa muda wa karibu miaka 15 umewekaji wa nyaya za umeme umefikia mpaka Ndanda kiasi cha kilomita 40 kutoka Masasi.

Pamoja na hayo, umeme unapatikana kwa sasa hivi Masasi na kwa kituo hicho cha mwisho yaani Ndanda. Sehemu za katikati zote yaani Vijiji vya Chikukwe, Chigugu, Chikundi na Mwena havijapatiwa step down transformers hivyo hawapati umeme. Katika maeneo yote niliyoyataja wanalilia umeme huu na katika sehemu hizo kuna wateja wasiopungua 400 kwa kila Kijiji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ndanda kwenda Nanganga kupitia Nangoo ni umbali wa kilomita kama 18. Vijiji vya Nangoo na Nanganga ni vikubwa sawa na Miji midogo ambapo kuna uhakika wa kupatikana wateja zaidi ya 500 kwa kila Kijiji.

Sehemu hizi zote zilikuwepo katika mpango wa awali wa kupatiwa umeme na pia *TANESCO* wanafahamu kwamba wateja wapo wa kutosha katika maeneo hayo na wana uwezo wa kulipia umeme huo.

Mheshimiwa Spika, jambo la kusikitisha ni kwamba, katika sehemu ya Kijiji cha Chikukwe*, TANESCO* wameweka step down transformer ndogo kwenda kuwapatia umeme Masista wa Kanisa Katoliki na kuwaacha Wananchi wa kawaida ambao ndio wengi na ndio waliojitolea kukata mikorosho na miembe yao kwa ajili ya kupatiwa umeme.

Mheshimiwa Spika, matakwa halisi ya kuwezesha umeme kupatikana katika sehemu hizo ni kama ifuatavyo: -

(i) *Step down transformers 4* kwa ajili ya Chikukwe, Chigugu, Chikundi na Mwena.

(ii) Waya, nguzo na viunganishi kwa sehemu iliyobaki yaani Ndanda hadi Nangoo kwa kilometa 8 na Nangoo hadi Nanganga kilomita 10

(iii) Gharama ya mradi huu inakadiriwa kuwa Shilingi milioni 200 mpaka 300. *TANESCO* wanafahamu gharama halisi.

Mheshimiwa Spika, Wananchi hawaelewi sababu zinazoifanya Serikali ishindwe kukamilisha ahadi yake kwa muda wa zaidi ya miaka 15 sasa bila kutoa maelezo yoyote. Wananchi hawaelewi ni kwa vipi wao wanahangaika na kulalamika kwa kukosa umeme wakati wanaona unapita katika maeneo yao bila wao kufaidika.

Wananchi pia wanasikitika kwamba wamejitolea nguvu zao kukata mikorosho na miembe iliyokuwa inawaletea faida kubwa bila kupata manufaa yoyote kwa maana ya kutelekezwa kwa ahadi ya kupatiwa umeme. Wananchi hawaelewi kwa nini katika sehemu nyingine nchini mipango ya kupeleka umeme imeanza siku za karibuni na tayari imekamilika wakati wao bado wanalalamika na suala hilo mpaka sasa halijakamilika.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla Wananchi wanaamini kuwa Serikali yao pengine inawadharararau na au kutokuwathamini, kwani hawaelewi ni kwa vipi katika kipindi cha miaka 15 Serikali imekosa Shilingi milioni 300 za kukamilisha mradi huu wa *TANESCO.* Kama fedha zisingekuwepo ni vema basi mradi wenyewe usingeanzishwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la ufuatiliaji, zaidi ya jitihada za ufuatiliaji wa suala hili zinazofanyika nje ya Bunge hili toka mwaka 2000 nilipochaguliwa kuwa Mbunge wa Masasi nimelifuatilia suala hili kwa Mawaziri husika mbalimbali na katika vikao mbalimbali vya Bunge lako Tukufu. Mwanzoni mwa mwaka 2000 ndani ya Bunge hili niliuliza swali kuhusu matatizo haya na Serikali ilijibu kuwa suala hili litashughulikiwa baadaye Serikali ikipata fedha.

Katika Mkutano huu wa Bunge unaoendelea wakati wa kujadili Hotuba ya Bajeti ya Serikali kama ilivyowasilishwa na Waziri wa Fedha, hoja hii tena ilikuja. Hoja hii inaweza kupatikana katika Hansard ya Kikao cha Sita tarehe 18 Juni, 2003 katika ukurasa wa 74 - 77.

Pia, nilileta hoja hii wakati wa majadiliano ya Hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini, nayo inapatikana katika Hansard ya Kikao cha 31 cha tarehe 27 Julai, 2003 ukurasa wa 172 - 173.

Mheshimiwa Spika, mwisho, kwa kuwa suala hili limechukua muda mrefu na kuwasababishia Wananchi wa Masasi mateso makubwa ikiwa ni pamoja na kurudisha nyuma jitihada zao za kujiletea maendeleo, nawasilisha maelezo haya ili Serikali iseme wazi na kujibu ni lini umeme utapatikana na utawaka katika Vijiji vya Chikukwe, Chigugu, Chikundi, Mwena, Nangoo na Nanganga.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kunisikiliza. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri mhusika amenihakikishia kwamba, atakuwa tayari kutoa maelezo ya kujibu hoja yako kesho kutwa tarehe 6 Agosti, 2003. Kwa hiyo, nafasi yake itakuwa kwenye *Order Paper* ya kesho kutwa.

Waheshimiwa Wabunge, tunayo hoja mbele yetu inayohitaji kuamuliwa, nayo ni kuahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Saa 1.37 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne Tarehe 5 Agosti, 2003 Saa Tatu Asubuhi)*